Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA KUMI NA SITA

**Kikao cha Thelathini na Saba – Tarehe 24 Julai, 2009**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Naibu Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua*

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 272

**Halmashauri ya Wilaya ya Dodoma Kukabidhiwa Jengo lake**

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA (K.n.y. MHE. FELISTER A. BURA)** aliuliza:-

Kwa kuwa Halmashauri ya Manispaa ya Dodoma inatumia majengo ya iliyokuwa Shule ya Sekondari ya Aga-Khan kama Ofisi zake:-

Je, ni lini Halmashauri itakabidhiwa jengo lake linalotumiwa na Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika ?

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, napenda kuchukua fursa hii, kutoa shukrani nyingi sana kwako wewe mwenyewe binafsi na kwa Waheshimiwa Wabunge wenye taaluma ya afya, ambao wamemhudumia Naibu Waziri, Mheshimiwa Hezekiah Chibulunje, wakati alipopata matatizo hapa Bungeni. Natoa shukrani nyingi sana pia kwa Wabunge wote, ambao wamekwenda kumpa pole na kumwombea dua ili aweze kupona mapema. Mheshimiwa Naibu Waziri, sasa hivi anaendelea vizuri, yuko katika mapumziko na Mungu akijalia, tutakuwa naye hivi karibuni.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa, eneo lenye majengo yanayotumiwa na baadhi ya Wizara za Serikali hapa Dodoma ni mali ya Halmashauri ya Manispaa ya Dodoma, kwa mujibu wa Hati Miliki Na. 12814 iliyotolewa tarehe 2 Desemba, 1958. Eneo hilo ambalo lilijulikana kama *Town Hall Plot*, majengo

yake yalianza kutumiwa na Wizara za Serikali kwa nyakati mbalimbali kutokea mwaka 1973, baada ya kuvunjwa kwa Serikali za Mitaa na yameendelea kutumiwa na Wizara za Serikali hata baada ya kuanzishwa tena Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Hivi sasa majengo hayo mali ya Manispaa ya Dodoma pamoja na jengo jipya lililojengwa kwenye eneo hilo na iliyokuwa Wizara ya Ushirika na Masoko, yanatumiwa kama Ofisi za muda za Idara ya Ushirika, iliyoko chini ya Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika; Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko; Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana; Wizara ya Katiba na Sheria na Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua haki ya Kisheria, ambayo Halmashauri ya Manispaa ya Dodoma inayo juu ya Miliki ya majengo hayo, pamoja na hali ya kutokuwa na ofisi zake za kufanyia kazi. Pia kwa kuzingatia kuwa, kwa muda mrefu Wizara za Serikali zimekuwa zikiyatumia majengo hayo, pamoja na kuongeza jengo jipya kwenye eneo hilo, Wizara yangu itaandaa mazungumzo kati ya Halmashauri ya Manispaa ya Dodoma na Wizara za Serikali zinazohusika ili kupata utaratibu wa namna ya kupata usuluhisho wa tatizo hili.

**MHE. FELISTER A. BURA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu, naomba kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza :-

Kwa kuwa Halmashauri ya Manispaa ya Dodoma imeshateseka kwa muda mrefu sana kwa kukosa ofisi ; na kwa kuwa ofisi wanayotumia ni jengo la iliyokuwa Sekondari ya Aga- Khan; na kwa kuwa jengo lile siyo lao hawawezi kuongeza chumba hata kimoja na baadhi ya ofisi wanatumia vyumba vilivyokuwa vyoo, ambavyo hakuna madirisha hakuna nini:-

(i) Je, serikali haioni kwamba inawatesa Watumishi wa Halmashauri ya Manispaa ya Dodoma ?

(ii) Ni lini Serikali itazungumza na Halmashauri na kutenga fedha kwa ajili ya kujenga Ofisi ya Halmashauri ya Manispaa ya Dodoma ?

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Felister Bura, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, moja ni kwamba, Serikali inatambua tatizo ambalo Wafanyakazi wa Halmashauri ya Dodoma wanalipata, kwa kutokuwa na majengo yao na hasa baada ya kuwa tumekiri kwamba, wana eneo ambalo kwa haki kabisa ni la kwao, ambalo walilipata mwaka 1998; na pale kwenye *Plot* ile *Town Hall* bado ina kibao chake kile kwamba, jengo lile limezinduliwa Julai, mwaka 1959 na Sir Richard Turnbull, ambaye alikuwa Gavana wakati ule. Tunatambua tatizo ambalo lipo na tutashughulikia haraka iwezekanavyo, usuluhishi wa kupata *Plot* hii au majengo yale ambayo yalikuwa ya Halmashauri ili waweze kurudishiwa na tukishafanikiwa hilo, maana yake ni kwamba, sasa hatutakuwa na tatizo la kutenga pesa kwa ajili ya ujenzi wa Ofisi mpya.

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Wizara ya Miundombinu imekuwa ikifanya kazi ya kujenga majengo na kuyauza na kukusanya pesa na kujenga mengine; na kwa kuwa Halmashauri zetu nyingi katika nchi yetu ya Tanzania kwa kweli hazina ofisi nzuri zinazopendeza ukilinganisha na hadhi ya Halmashauri katika nchi yetu ikiwemo Halmashauri ya Wilaya ya Songea:-

Je, Mheshimiwa Waziri sasa yuko tayari katika ule mpango wa kujenga, kuuza na kupokea pesa, baadhi ya pesa wanazozipata baada ya kuuza majengo haya wanaweza sasa kutengeneza programu rasmi ya kujenga ofisi kwa ajili ya Halmashauri zetu ikiwepo Halmashauri ya Wilaya ya Songea ?

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mhagama kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia TBA, inatenga pesa kila mwaka kwa ajili ya mpango wake mahususi wa kuwajengea nyumba watumishi wa Umma. Imetenga pesa mwaka uliopita na imetenga tena katika mwaka huu wa fedha, lakini katika Halmashauri za Wilaya mbalimbali, ujenzi huu unaweza ukafanywa pia na TBA kama Mkandarasi, lakini kwa kutumia pesa ambazo wenyewe Halmashauri wamezitenga kwa ajili ya ujenzi huo. Wizara ya Miundombinu kupitia TBA, itakuwa tayari kufanya kazi hiyo kama ambavyo imetimiza kazi hiyo maeneo mbalimbali, kwa mfano, katika Mkoa wa Manyara na katika Halmashauri za Mkoa wa Manyara.

Na 273

**Ujenzi wa Daraja la Kigamboni**

**MHE. SAVELINA S. MWIJAGE (K.n.y. MHE. ANIA S. CHAUREMBO)** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali ina mpango wa kujenga Daraja la kusaidia uvukaji eneo la Kigamboni Wilaya ya Temeke; na kwa kuwa wananchi wanategemea sana utekelezaji wa ujenzi kuanza mara moja:-

(a) Je, Serikali inasema nini kuhusu kuanza kwa ujenzi huo?

(b) Je, ujenzi huo utagharimu kiasi gani cha fedha?

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ania Saidi Chaurembo, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli Serikali ina mpango wa kujenga Daraja la Kigamboni ili kupata ufumbuzi wa kudumu wa usafiri wa Wananchi wa eneo la Kigamboni Wilaya ya Temeke.

Kwa kuwa ujenzi wa Daraja kubwa la Kigamboni unahitaji fedha nyingi kuliko uwezo wa Serikali, Serikali imeamua kufungua milango na kukaribisha Wawekezaji kutoka Sekta Binafsi ili kuwekeza katika ujenzi na uendeshaji wa Mradi huu kwa kushirikiana na Shirika la Taifa la Hifadhi ya Jamii (NSSF).

Mheshimiwa Naibu Spika, mchakato wa kumtafuta mbia kutoka Sekta Binafsi chini ya utaratibu wa Public Private Partnership (PPP), umeshaanza kwa kuorodhesha *(shortlisting)* makampuni yaliyoonesha nia ya kuwekeza katika Mradi huu. Aidha, NSSF inaendelea kuandaa nyaraka za zabuni za kumpata Mshauri *(Transaction Advisor)*, atakayesaidia NSSF kuandaa nyaraka za zabuni ya kumpata mbia toka Sekta Binafsi.

Gharama za ujenzi wa daraja hili zitajulikana baada ya zoezi la kumpata Mkandarasi wa kujenga Daraja hili kukamilika.

**MHE. SAVELINA S. MWIJAGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwa kuwa, matatizo ya Daraja la Kigamboni ni sawasawa na matatizo ya Daraja la Bujugo na Kashalo:-

Je, ni lini Serikali itawaonea huruma watu wa Kashalo na kuwasaidia angalau kivuko au daraja ili waache kutumbukia mara kwa mara kwenye Mto ule?

**NAIBU SPIKA**: Mheshimiwa, wala siyo sawasawa; Kigamboni ni bahari na Kashalo ni mto tu. Haya Mheshimiwa Waziri majibu. *(Kicheko)*

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Savelina Mwijage kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni bahati mbaya sana sikumbuki kwa ukamilifu, ratiba ambayo tumeiweka kwa ajili ya eneo hilo la Bujugo, lakini namuahidi kwamba, tukimaliza *session* hii, nitampatia majibu kwa maandishi.

Na 274

**Tatizo la Uratibu kwenye Mifuko ya Jamii**

**MHE. AZIZA S. ALLY** aliuliza:-

Kwa kuwa Mifuko ya Jamii Tanzania inakabiliwa na tatizo la uratibu; na kuwa kuwa haki ya mafao ya Wafanyakazi wa Tanzania zinatofautiana sana kutokana na Mifuko hiyo kuundwa kwa Sheria tofauti na kuwa kwenye Wizara tofauti na hivyo kusababisha mafao ya Wastaafu kutofautiana:-

(a) Je, Serikali haioni kuwa Mifuko hiyo kuwa na Sheria tofauti ni tatizo kubwa?

(b) Je, Serikali inasema nini kuhusu kuleta Sheria Bungeni ili Mifuko hiyo iwe na Sheria moja ili mafao ya wafanyakazi yasitofautiane kati ya wale wa Serikali Kuu na za Mitaa na wale wa Mashirika ya Umma?

**WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Aziza Sleyum Ally, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania ina Mifuko sita ya Hifadhi ya Jamii. Mifuko hiyo imeundwa kwa Sheria za Bunge na ipo katika Wizara tofauti kama ifuatavyo: NSSF upo chini ya Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana; PPF upo chini ya Wizara ya Fedha; PSPF upo chini ya Wizara ya Fedha; LAPF upo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Serikali za Mitaa; GEPF upo chini ya Wizara ya Fedha; na NHIF upo chini ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu wa kila Mfuko kuwa na Sheria yake, umesababishwa pamoja na mambo mengine, mafao yanayotolewa na Mifuko hiyo kutofautiana. Baada ya Serikali kubaini tatizo hili, hatua za kutafuta ufumbuzi wake zimeanza kuchukuliwa. Hatua hizo ni pamoja na kuandaliwa kwa Sera ya Taifa ya Hifadhi ya Jamii ya Mwaka 2003. Sera hiyo pamoja na mambo mengine, inabainisha matatizo na changamoto zinazoikabili Sekta ya Hifadhi ya Jamii na utaratibu wa kutafuta ufumbuzi wake. Aidha, kutungwa kwa Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti na Usimamizi wa Hifadhi ya Jamii Na. 8 ya Mwaka 2008 ni sehemu ya utekelezaji wa Sera hiyo. Sheria hiyo inampa uwezo Mdhibiti na Msimamizi wa Hifadhi ya Jamii, kuboresha na kusimamia suala zima la mafao ya Mifuko. Sheria mpya inaelekeza Mifuko yote kurekebisha Sheria zake ili ziendane na Sheria ya Usimamizi na Udhibiti wa Hifadhi ya Jamii. Ni matarajio ya Serikali kuwa, katika mchakato wa kurekebishwa Sheria zinazounda Mifuko yote ya Hifadhi ya Jamii, tatizo la tofauti za mafao litazingatiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, pendekezo la kutungwa kwa Sheria moja ya Hifadhi ya Jamii, litawasilishwa kwa Mamlaka ya Usimamizi na Udhibiti wa Hifadhi ya Jamii ili liweze kufanyiwa kazi mara tu Mamlaka hiyo itakapoanza kufanya kazi.

**MHE. AZIZA S. ALLY:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa Shirika la ILO ambalo ni la Wafanyakazi limefanya utafiti na kugundua kuwa kuna ongezeko la watu, ongezeko la soko la ajira na hali ya kiuchumi kuweza kubadilika:-

(i) Je, Mheshimiwa Waziri, haoni kuchelewa kupitishwa kwa Sheria hii hapa Bungeni na Mifuko hii kuweza kutoa ufafanuzi wake vizuri kunacheleweshа wafanyakazi kupata fedha au mafao yao katika kiwango kimoja?

(ii) Mheshimiwa Waziri amesema kuwa mchakato upo, mwaka jana tulipitisha Sheria ya 2008 hapa Bungeni ya kusema Mifuko hii iweze kutoa mchanganuo wake ili kila Mfuko uweze kuwa sahihi. Je, Mheshimiwa Waziri anatueleze Mifuko hii mpaka sasa imefikia kiwango gani cha kutoa mchanganuo ili Mifuko hiyo iweze kuwa sawa kwa sababu kama mfanyakazi ataona Mfuko mmoja anaochangia mafao yake haufai, aweze kuhamia katika Mfuko wa pili?

**WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Aziza Ally, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli utafiti wa ILO umeonesha kwamba, watu wameongezeka, idadi ya wafanyakazi imeongezeka, lakini vilevile wameonesha kwamba, hata ule mtandao wa kutoa hizi Hifadhi za Jamii hautoshelezi. Sasa kinachopaswa kufanywa ni kwamba, baada ya huyu Mdhibiti Mkuu kuingia madarakani, hayo ni maeneo ambayo yeye atakuja kuyashughulikia ili kuona jinsi ambavyo anaweza kuhakikisha kwamba, Mifuko hii kwanza inaendana na sheria zile watakazokubali wao wenyewe. Pili, Sheria ile ambayo pengine inatarajiwa kuundwa baada ya Mifuko hii kuwa chini Mdhibiti na Msimamizi Mkuu wa Hifadhi ya Jamii moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mifuko imefikia wapi katika mchanganuo huo? Mifuko haiwezi kuanza kazi ya mchanganuo kabla ya Sheria kubadilika. Kwa hiyo, kwa sasa hivi kila Mfuko unatawaliwa na Sheria yake. Nataka tu nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, uundaji wa Mamlaka hii ya Udhibiti na Usimamizi wa Hifadhi ya Jamii umekwishaanza. Tumeshatangaza nafasi za Mkurugenzi Mkuu, Mwenyekiti wa Bodi, Wakurugenzi wa Bodi na hivi sasa watu wameshaomba na kinachofanyika kule Wizarani ni kuwaorodhesha hawa watu ili waweze kufanyiwa *short listing* ili wachache watakaopatikana, wafanyiwe usaili. Tunafanya kazi kwa ushirikiano na Wizara ya Fedha na Uchumi na vilevile na Benki ya Dunia. Kwa hiyo ni kitu ambacho kinasimamiwa kwa karibu sana.

Ninachomwomba Mheshimiwa Mbunge, avute subira kwani hili liko katika hatua nzuri kuhakikisha kwamba, wafanyakazi hawa hawaathiriki pale wanapostaafu.

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii wa Serikali za Mitaa (LAPF) unafanya kazi nzuri sana na unaanza kuandaa mambo ya mstaafu miezi sita kabla; na siku ambayo mfanyakazi anastaafu anapewa hundi yake na kupelekewa kwenye kituo chake cha kazi;

je, Serikali haioni kwamba hii Mifuko iende kwenye Mfuko wa Serikali za Mitaa ikajifunze wanafanyaje ili na wao waige kwa faida ya watumishi wetu? *(Makofi)*

**WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Msindai, Mbunge wa Iramba Mashariki, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli Mfuko huo unafanya kazi nzuri kwamba, kabla ya miezi sita wanakuwa wameshajumlisha kila kitu na kuandaa hundi ya anayetarajia kustaafu. Napenda nimhakikishie kwamba, mawasiliano baina ya Mifuko hii ni ya mara kwa mara; wanavyo vikao vyao rasmi na visivyo rasmi kwa lengo la kubadilishana uzoefu na hata katika mchakato wa kusimamiwa na ILO vilevile wanajumuishwa. Kwa hiyo, nina uhakika yanayofanywa na huu Mfuko wa Serikali za Mitaa, kwa namna moja au nyingine, yanaambukizwa katika Mifuko mingine.

Ukiangalia yanayotokea katika Mfuko wa Hifadhi ya Jamii wa NSSF, ambao mimi nausimamia, hali si mbaya, vilevile mfanyakazi au mwanachama anapata mafao yake mara tu anapostaafu. Kwa hiyo na Mifuko mingine, naamini kuwa iko mbioni katika kuhakikisha kwamba, wanarekebisha taratibu zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niongezee kwa kusema kwamba, haya yote yatakuja kuwianishwa pamoja pale ambapo wote watasimamiwa na mtu mmoja, ambaye ni Mdhibiti na Msimamizi Mkuu wa Hifadhi ya Jamii.

Na. 275

**Kujenga Gereza Jipya Msalato na Kuboresha Nyumba za Askari wa Gereza la Isanga**

**MHE. EPHRAIM N. MADEJE** aliuliza:-

Kwa kuwa Gereza Kuu la Isanga lipo katika eneo ambalo ni finyu na hivyo maendeleo yake na ujenzi wa nyumba za askari wake umebanwa; na kwa kuwa eneo kubwa zaidi lilikwishatengwa katika Kata ya Msalato kwa ajili ya maendeleo ya baadaye ya Gereza hilo:-

(a) Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa Gereza jipya Msalato ili kuwezesha kuhama kwa Gereza la Isanga?

(b) Je, Serikali inachukua hatua gani za kuboresha nyumba za askari wa Gereza Kuu la Isanga ambazo ziko kwenye hali mbaya sana wakati ujenzi wa Gereza jipya unasubiriwa?

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimkiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ephraim N. Madeje, Mbunge wa Dodoma Mjini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali haina mpango wa kulihamisha Gereza la Isanga kwenda Msalato kama alivyobainisha Mheshimiwa Mbunge katika swali lake la msingi.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu kupitia Jeshi la Magereza, itaendelea kujenga nyumba mpya na kuzifanyia ukarabati ambazo zimechakaa zikiwemo za Gereza la Isanga, kwa awamu kadiri hali ya bajeti itakavyoruhusu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka huu wa fedha, Serikali imetenga jumla ya shilingi 1,608,900,000 kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa makazi ya Maafisa na Askari Magereza hapa nchini.

**MHE. EPHRAIM N. MADEJE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa hali ya makazi ya Askari wa Gereza la Isanga ni duni sana; na kwa kuwa Kikao hiki kinaendelea na Mheshimiwa Waziri yuko hapa; je, Mheshimiwa Waziri atakuwa tayari kuongozana na mimi kabla Kikao hiki hakijaisha, akajionee mwenyewe jinsi ambavyo hali ni duni na kwamba makazi haya yanastahili kupewa kipaumbele katika kugawiwa fedha ili yajengwe upya?

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Ephraim Madeje, Mbunge wa Dodoma Mjini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nilishawahi kulitembelea Gereza la Isanga, lakini pia niko tayari kwenda naye Mheshimiwa Mbunge ili kupatembelea tena.

**MHE. ESTHERINA J. KILASI**: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza. Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri katika majibu yake ya nyongeza amesema kwamba, kuna pesa iliyotengwa kwa ajili ya kuboresha baadhi ya magereza; na kwa kuwa Wilaya ya Mbarali ni mojawapo yenye gereza jipya ambalo limejengwa baada ya kupata matatizo makubwa kwa miaka ya nyuma iliyopita; na nimekuwa nikimweleza Mheshimiwa Waziri kwamba, lile gereza halijakamilika kwa sababu Wafungwa wanakaa kwenye giza:-

Je, Waziri ana mpango gani kuhakikisha kwamba katika fedha zilizotengwa mwaka huu wa fedha gereza lilojengwa Mbarali linapata umeme?

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue fursa hii, kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Estherina Kilasi, Mbunge wa Mbarali kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba, Mheshimiwa Kilasi, amekuwa akiniulizia kuhusu gereza la Mbarali kwa muda mrefu, lakini kwa bahati mbaya,

kutokana na bajeti ambayo inatengwa, sina uwezo wa kutengeneza na kukarabati magereza yote kama ambavyo ningependa. Nitakachomhakikishia ni kwamba, namkaribisha aje ofisini kwangu ili tukae na kuangalia namna ya kuweza kupanga katika mwaka huu wa fedha au mwaka ujao wa fedha ili tuweze kuangalia namna ya kukarabati gereza hili la Mbarali.

**MHE. MARIAM S. MFAKI**: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ili niulize swali la nyongeza.

Kutokana na majibu ya Mheshimiwa Waziri kuhusu Gereza la Msalato ni kweli Gereza lile limekaa kama vile limesahauliwa na halionekani kama ni Gereza ambalo linaweza likaendelea kutunzwa. Kwa hiyo, naomba anipe majibu kuhusu fedha alizosema kwamba wametenga fedha za kutosha kwa ajili ya ukarabati wa magereza.

Je, kuhusu Gereza la Msalato wanaweza kuchukua hatua za haraka kwa kutumia fedha hizo walizotenga ili kulitengeneza Gereza hilo?

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kuchukua fursa hii, kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mariam Mfaki, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kabisa kwamba, Gereza la Msalato linahitaji ukarabati mkubwa na linahitaji kutengewa fedha, lakini kwa bahati mbaya, kutokana na kiasi cha fedha ambacho nimetengwa katika bajeti yangu, Gereza la Msalato kwa mwaka huu wa fedha, halitaweza kufanyiwa ukarabati. Kitu ambacho nitamhakikishia Mheshimiwa Mbunge ni kwamba, tutajitahidi kama Wizara kwa kadiri ya uwezo wetu kutokana na fedha ambazo tunatengewa, kushughulikia Magereza yote hapa nchini awamu kwa awamu.

**MHE. JAMES D. LEMBELI**: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Kwa kuwa hali ya Gereza la Isanga inalingana kabisa na hali ya Gereza la Kahama ambalo lilijengwa kabla ya uhuru likiwa na uwezo wa kuchukua wafungwa 70 na leo lina wafungwa zaidi ya 500.

Je, Serikali ina mpango gani wa kulijenga upya Gereza hili la Kahama?

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa James Lembeli, Mbunge wa Kahama Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Gereza la Kahama kwa bahati nzuri nimeshawahi kulitembelea na nilikuwa na Mheshimiwa Mbunge, tulilitembelea mwaka huu na kwa kweli hali yake nimeiona na inahitaji matengenezo. Kama nilivyoeleza nilipokuwa najibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mariam Mfaki, hali ya bajeti hairuhusu kuweza kutengeneza Magereza yote hapa nchini kama ambavyo ningependa. Tutaendelea kutengeneza na kujenga na kukarabati Magereza yetu awamu kwa awamu.

**NAIBU SPIKA**: Waheshimiwa Wabunge, mfano mzuri wa kuuliza maswali na majibu ni swali hili. Tumeweza kutoa maswali ya nyongeza manne na dakika zao ni tano zile zile. Sasa mnaona Waziri amejibu kwa kifupi, kwa sababu waliouliza nao wameuliza kwa kifupi. Kwa hiyo, tumepata waulizaji wa maswali ya nyongeza wanne, kwa dakika zao zile zile tano. Sasa kutokana na hili, tunakupa pongezi sana Waziri. *(Makofi)*

Na. 276

**Kuweka Mtafsiri wa Lugha ya Ishara Bungeni**

**MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE** aliuliza:-

Kwa kuwa Watanzania wengi hivi sasa wanapenda kuangalia vipindi vya Bunge vinapooneshwa moja kwa moja *(live)*; na kwa kuwa walemavu wenye uziwi hawapati fursa hiyo kwa kuwa hakuna utaratibu wa kuwepo Mkalimani wa Lugha ya Ishara Bungeni kwa ajili ya watu wenye ulemavu wa uziwi na hivyo kuwanyima haki yao ya msingi ya kupata habari za Bunge linavyoendelea:-

Je, Serikali ina mipango gani ya haraka ya kuweka Mtafsiri wa Lugha ya Ishara kwa ajili ya watu wenye ulemavu wa uziwi?

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa George Simbachawene, Mbunge wa Kibakwe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijajibu swali la Mheshimiwa Simbachawene, napenda kuchukua fursa hii, kusahihisha maneno aliyotumia ya Lugha ya Ishara kwa maana aliyokuwa anataka ya kuwepo kwa mkalimani au mtalaam, atakayewasaidia Viziwi kufahamu masuala yanayoongelewa Bungeni. Mtalaam huyo anaitwa Mkalimani wa Lugha ya Alama na sio Lugha ya Ishara. Baada ya maelezo hayo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Simbachawene kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mojawapo ya haki za msingi za binadamu, kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni kupata habari. Hivyo basi, watu wenye Ulemavu wa Kutosikia, yaani Viziwi, kutopata habari ni kuwanyima haki yao ya msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imekwishafanya mazungumzo na Chama cha Viziwi Tanzania (CHAVITA), kuona ni jinsi gani huduma ya Mkalimani wa Lugha ya Alama inaweza kutolewa kupitia Televisheni ya Taifa ili Jamii ya Watu Wasiosikia (Viziwi), iweze kupata haki yake ya msingi ya kupata habari. Hatua ya awali ya mazungumzo hayo, ilifanikisha kumpata mkalimani huyo, ambaye alianza kufanya kazi

katika vipindi vya taarifa za habari na matukio ya wiki, ambayo yalikuwa yanajumuisha taarifa muhimu zilizokuwa zinatangazwa kupitia TBC.

Hata hivyo, mkalimali huyo hakuweza kufanya kazi hiyo kwa wakati wote, kwa sababu hakuwa ameajiriwa na TBC. Hivyo basi, mazungumzo yanaendelea baina ya Wizara yangu, TBC na Chama cha Viziwi Tanzania, kuona uwezekano wa kuajiri wakalimali watakaofanya kazi kwa muda wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa vile jamii yenye ulemavu wa kutosikia kama ilivyo kwa watu wengine, inayo uhuru wa kuchagua chombo ambacho kinaweza kutumika kupata habari mbalimbali kupitia Bunge lako Tukufu, naomba kutoa wito kwa wamiliki wa vyombo vya habari nchini, kuajiri Wakalimani wa Lugha ya Alama ili waweze kusaidia kuipa taarifa mbalimbali jamii ya watu wenye ulemavu wa kutosikia, zinazohusu sio tu shughuli za Bunge, bali pia masuala mengine ya kijamii na maendeleo ya nchi yetu kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue nafasi hii kukupongeza, jana wewe mwenyewe uliwaalika Shule ya Msingi na Sekondari kuja kujionea wenyewe hapa namna wenzetu wasiosikia wanavyoweza kupata habari. Nakushukuru sana.

**MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, nikushukuru sana kwa kunipa nafasi hii na nimpongeze Naibu Waziri, kwa majibu yake mazuri. Kwa kuwa amekiri hapa kwamba ni haki ya msingi kwa wenzetu hawa wenye uziwi kupata habari na mimi swali langu limejikita zaidi kwenye habari za Bunge.

(i) Kwa kuwa haki inayochelewa ni sawa sawa na haki ambayo inataka kupotea hivi. Je, Serikali haioni kwamba kuna haja ya haraka sana na pengine kabla ya Bunge hili kwisha ikaanza kufanya majaribio ya kumuwezesha yule muonesha Lugha ya Alama kufanya kazi hiyo haraka iwezekanavyo?

(ii) Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kwa kuwa pia suala la hao wenzetu wenye ulemavu wa uziwi ni sawa sawa na wale wasioona na habari za Bunge ni haki yao na Bunge ndio chombo chao kinachowawakilisha. Je, Bunge lenyewe halioni haja ya kuwa na Kitengo Maalum cha Mawasiliano kwa ajili ya wenzetu hao wenye ulemavu wa aina hizi mbili unazozisema?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, unaweza kuwa na majibu maana hii ni Huduma ya Tume ya Bunge.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Naibu Spika, hili la kwanza nilikwishalijibu. Ni kwamba, Wizara yangu, TBC na Chama cha Viziwi Tanzania, tunaharakisha kuajiri mtu huyu ili angalau televisheni yetu na tumeomba na televisheni nyingine ziweze kuonesha Lugha hii ya Alama, kwa watu ambao wana matatizo ya kutokusikia.

Hili lingine, nadhani Viongozi wa Bunge wamesikia, sisi kama Wizara husika tutawashauri ili angalau shughuli hiyo iweze kutendeka mara moja.

**NAIBU SPIKA:** Kwa upande wa Bunge, tunajaribu kutafuta utaratibu wa kuwasaidia hawa wenzetu wasioona kuwa na zile *braille* mashine zao na utaratibu mzima wa kuandika hotuba zao kutumia *braille.* Sasa na hili lingine tutaendelea kutafuta, lakini hili la wasioona tumelifanyia uamuzi kwamba, tutafute namna ya wao kuwa na maandiko yao ya kusikia.

**MHE. MARGRETH A. MKANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri yaliyotolewa na Naibu Waziri na kwamba anawaomba na vyombo vingine waweze kufanya suala hilo, mimi nilikuwa nauliza; je, ombi hilo haliwezi kubadilishwa kwamba ni utaratibu ndani ya sheria ya vyombo vya habari tunayoitegemea kuitunga kipindi kijacho?

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikubaliane naye kwa sababu sheria hii bado iko kwenye mchakato na yeye pia atahusika na sheria italetwa ndani ya Bunge, sisi tutalichukua na wadau mbalimbali ili tuweze kulifikiria liwe mojawapo ndani ya sheria; kwa sababu jamii iliyozungumzwa ni jamii muhimu katika nchi yetu.

Na. 277

**Fedha za Miradi ya Maji Vijijini**

**MHE. MARIAM R. KASEMBE** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali imekuwa ikitoa fedha kwa ajili ya Miradi ya Maji Vijijini - *Quick Wins*:-

(a) Je, ni vigezo gani vimekuwa vikitumika katika kutoa fedha za utafiti na za utekelezaji wa Miradi ya Maji kwenye kila Halmashauri?

(b) Je, ni Wilaya ngapi zimekwisha kamilisha utafiti huo kuanzia mwaka 2007 – 2008 na 2008 – 2009?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mariam Reuben Kasembe, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji ulianza mwezi Julai, 2007, kwa kutekeleza miradi midogo ya maji kwa madhumuni ya kuondoa kero ya kukosa huduma ya maji kwa wananchi katika muda mfupi wa kuongeza idadi ya wananchi wanaopata huduma ya maji safi na salama. Lengo

la miradi midogo, lilikuwa ni kukarabati na kupanua miradi iliyopo, kukamilisha miradi iliyokwishaanza na kufanya utafiti wa miradi mipya midogo pale inapobidi.

Kutokana na urasimu uliopo katika utaratibu wa kupata fedha za Benki ya Dunia, Serikali ilibuni utaratibu mwingine kwa kutekelezwa Miradi ya Maji inayoweza kutoa matokeo haraka *(Quickwin)*, wakati tukisubiri utaratibu wa Benki ya Dunia ukamilike. Utekelezaji wa miradi hiyo kwa utaratibu wa *Quickwin* uligharamiwa na Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji (WSDP).

Vigezo vilivyotumika kuchagua miradi ya kutekelezwa katika Halmashauri zote vilikuwa vifuatavyo: Kuwepo kwa chanzo thabiti cha maji; Kuwepo kwa Mradi unaoendelea kujengwa; Kuwepo kwa Kamati ya Maji au chombo cha watumia maji; Mradi usiwe unahitaji usanifu wa kina; na Mradi unaotekelezeka katika kipindi kisichozidi miezi sita.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, Miradi Midogo *(Quickwin)*, iliyofanyiwa utafiti ilikuwa ni ile ambayo tafiti zake hazikuhitaji muda mrefu. Halmashauri zote nchini, zilifanya tafiti hizo na kuzikamilisha katika mwaka 2007/2008 na mwaka 2008/2009.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi hicho, Wizara yangu iliendelea kutekeleza Programu ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini katika Halmashauri zote nchini. Fedha za kuandaa kutekeleza Miradi na kujenga uwezo, zimekuwa zikipelekwa kwenye Halmashauri chini ya utaratibu wa utoaji wa ruzuku ya maendeleo. Vile vile Wizara imeendelea kuziwezesha Sekretarieti za Mikoa kwa kuzipatia fedha za kutekeleza majukumu yake ya kutoa ushauri wa kitaalam kwa Halmashauri husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2008/2009, Wizara yangu kupitia Wizara ya Fedha na Uchumi, ilipeleka jumla ya shilingi bilioni 55.9, kati ya shilingi bilioni 62.4 zilizokasimiwa kwenye Halmashauri zote, kwa ajili ya kuendelea kuzijengea uwezo na kutekeleza Miradi ya Maji. Kulingana na taratibu za kuzipatia Halmashauri ruzuku ya maendeleo, kati ya Halmashauri 132 zilizopo, 127 zilitimiza masharti ya kupewa ruzuku ya maendeleo. Halmashauri 5 hazikutimiza masharti. Halmashauri hizo ni Kwimba, Masasi, Manispaa ya Shinyanga, Shinyanga na Jiji la Tanga na Halmashauri hizo zilipewa fedha za kujenga uwezo tu.

**MHE. MARIAM R. KASEMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

(ii) Kwa kuwa Wilaya ya Masasi tafiti zilifanyika na visima vilichimbwa katika Vijiji vya Mpanyani, Mraushi na Nandete lakini havikuweza kupewa maji. Je, ni lini Serikali itapeleka tena fedha za utafiti ili wananchi hawa waweze kuchimbiwa visima vingine?

(ii) Kwa kuwa katika Wilaya ya Nanyumbu kuna mwananchi mmoja ambaye anaitwa Father Francis, yeye huwa anafanya tafiti za maji na zimekuwa zikileta

mafanikio makubwa sana katika Mkoa wetu wa Mtwara. Je, ni lini Mheshimiwa Waziri ataitembelea Wilaya ya Nanyumbu ili kukutana na uongozi na huyu mwananchi kuangalia mafanikio makubwa ambayo yamesaidia kufanya tafiti za maji ili Serikali iweze kumtumia Father huyu kuokoa fedha nyingi za utafiti ambazo zinatumika na badala yake zipelekwe katika kuchimba visima?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema, tuliandaa utaratibu huo wa *Quickwin* kwa ajili ya kuhakikisha kwamba, tunatoa maji wakati tunasubiri mchakato huu wa *World Bank.* Hivi sasa tunachokifanya, kwa kuwa miradi inayofadhiliwa na *World Bank* imekwishachukua kasi nzuri; tunaisukuma miradi hiyo sasa itekelezeke. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Mbunge avute subira kidogo, kwa sababu sasa mchakato unakwenda vizuri na awe na uhakika kabisa kwamba, Mradi utatekelezeka katika Wilaya ya Masasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swali la pili la Father Francis, naomba nimhakikishie kwamba, nitatembelea Nanyumbu, lakini sio Father Francis tu nimepata pia wataalam wengine. Mheshimiwa Mramba, alikuwa ananieleza kuhusu mtaalam ambaye anatumia utaalam *(water dazing)*, ni kama utaalam wa kienyeji kutafiti maji. Wote hao nitawatembelea na tutahakikisha kwamba, tutawajumuisha katika kusaidia Serikali kutafiti maji.

**MHE. OSCAR R. MUKASA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na namshukuru Naibu Waziri kwa majibu mazuri. Kupitia Mpango wa Miradi ya Maji Vijijini *(Quickwin)*, Serikali ilitoa ahadi kwa wananchi wa eneo la Nyakanazi; Jimbo langu la Uchaguzi Biharamulo Magharibi ya kufanya mradi wa usambazaji maji kwenye eneo hilo; na kwa sababu ahadi hiyo iligusa eneo ambalo ni la kipaumbele sana kwa Wananchi wa Nyakanazi; na kwa hiyo walikuwa wanasubiri kwa hamu sana utekelezaji wa ahadi hiyo tangu mwezi Februari, 2009; ninaomba kusikia Serikali imefikia wapi kwenye utekelezaji wa ahadi hiyo? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Pamoja na kwamba, umeuliza swali ni jipya kabisa, lakini Waziri anajua mambo mengi sana, kwa ajili ya ugeni anaruhusiwa kujibiwa.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, naomba nikushukuru kwa kumruhusu Mbunge mpya kuuliza swali hili na mimi nampongeza kwa kuanza kufuatilia kwa nguvu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli nililitembelea eneo lile la Nyakanazi katika Jimbo lake kwenye mwezi Machi, 2009. Kwa niaba ya Serikali, niliahidi kwamba, tungetoa shilingi milioni 50 kwa ajili ya kusambaza maji baada ya Shirika la *Concern World Wide* kutusaidia kujenga Mradi wa Maji. Fedha hizo zilikwishapelekwa tangu tarehe 9 Juni, 2009 kwa Halmashauri ya Wilaya ya Biharamulo; kwa hiyo, ziko tayari sasa kufanya kazi ya kusambaza maji katika eneo la Nyakanazi.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri, najua wewe unayamudu maswali haya.

Na. 278

**Uimarishaji wa Bwawa la Kidawashi**

**MHE. DORAH H. MUSHI** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali imeazimia kuinua hali ya uchumi wa wananchi kupitia rasilimali walizonazo, ikiwa ni pamoja na uvuvi katika Bahari, Maziwa na Mabwawa na kadhalika; na kwa kuwa Bonde la Mto Pangani lipo kwenye Wilaya ya Arumeru na Wilaya ya Simanjrio; na kwa kuwa Bwawa la Kidawashi lililopo Simanjiro halina faida yoyote:-

Je, Serikali ina mpango gani wa haraka wa kuliimarisha Bwawa hilo liwe Bwawa kamili kuliko kuacha mkusanyiko huo wa maji bila kutumiwa kwa kazi yoyote?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Dorah Herial Mushi, Mbunge wa Viti Maalum, naomba nitoe maelezo mafupi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Kidawashi ni eneo oevu la asili, ambalo limesambaa katika maeneo ya Wilaya za Arumeru na Simanjiro. Hata hivyo, sehemu kubwa ya Bonde hilo ipo katika Kata ya Shambalai Wilayani Simanjiro na vijiji vilivyo karibu na Bonde hilo ni Kilombero, Shambalai na Oldil kwa upande wa Kaskazini na upande wa Kusini limepakana na msitu na milima.

Bwawa hilo la asili, hupokea na kuhifadhi maji ya mvua yanayotoka katika maeneo ya Wilaya ya Monduli na maeneo mengine. Maji hayo ya mvua yanachanganyika na uchafu mwingi unaotokana na shughuli za binadamu katika Miji ya Arusha na Monduli. Bwawa linakuwa na maji katika misimu ya vuli na masika tu na hata katika vipindi hivyo maji mengi yanapotea kwa kuvia chini ya ardhi *(seepage)* na maji mengine hupotea kwa njia ya mvukizo *(evaporation).*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuwepo kwa bwawa hilo la asili (Tindiga), kunasaidia kusafisha maji machafu yanayoingia bwawani kwa kuyachuja kupitia ardhini na hivyo kuongeza maji *(recharge)*, yanayotiririka katika Mto Pangani. Aidha, Bwawa la Asili la Kidawashi (Tindiga), liko katika eneo la tambarare na lina wastani wa kina cha maji cha mita 0.5 tu. Bwawa hilo linazungukwa na wananchi ambao asili yao ni wafugaji. Hakuna kilimo kinachofanyika katika eneo hili, isipokuwa eneo hutumika kwa malisho na kunyweshea mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo mafupi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dorah Herial Mushi, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa Serikali haina mpango wa kujenga na kuliongezea uwezo wa kuhifadhi maji Bwawa la Kidawashi. Kinachotakiwa ni kwa wananchi kuzingatia kanuni za ufugaji bora na kuweka miundombinu inayofaa, ikiwa ni pamoja na kutafuta maeneo yanayofaa kujenga malambo ya kuhifadhi maji yanayotosha mahitaji na kujenga mabirika ya kunyweshea mifugo.

**MHE. DORAH H. MUSHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri, naomba niulize maswali mawili ya nyongeza:-

(i) Kwa kuwa Serikali yetu imekusudia kuinua uchumi wa wananchi kwa kutumia rasilimali zilizopo kama uvuvi katika bahari, mabwawa, pamoja na maziwa. Je, Serikali ina mpango gani wa kuliimarisha Bwawa hili la Kidawashi lililoko eneo la Shambalai kuwa bwawa kamili?

(ii) Kwa kuwa bonde hili lina maeneo mazuri kwa kilimo cha umwagiliaji; na kwa kuwa kilimo hicho kitafaidisha Wananchi wa Wilaya tatu ambapo ni Arumeru, Simanjiro na Hai; je, Serikali haioni kwamba kuna haja ya kuliimarisha Bwawa hili ili liweze kuwanufaisha wananchi hawa kuliko kuzingatia tu uchimbaji wa madini? Ahsante.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema katika majibu yangu ya swali la msingi, Bwawa la Kidawashi liko kwenye sehemu tambarare; ni sehemu oevu halifai kujenga bwawa kubwa la kuhifadhi maji. Ndiyo maana hata wananchi wanaokaa maeneo yale, wako mbali kidogo na bwawa hili na hawafanyi kilimo.

Ningependa kumhakikishia Mheshimiwa Dorah Mushi kwamba, nimewasiliana na Serikali ya Mkoa, nimewasiliana na DCs wote wa Wilaya zinazozunguka bwawa hili; Simanjiro na Monduli; tunachotaka kufanya ni kwamba, kwa kuwa bwawa lile liko pale na lina mandhari mazuri, basi tutaangalia pamoja na Baraza la Mazingira ni mpango gani tunaweza kuufanya kuwasaidia wananchi wale, kuwapatia maji safi ya kunyweshea mifugo, kufuga samaki na hasa kambare ndio wengi pale. Pia kwa upande wa kilimo, wataalam wangu wataangalia jinsi tunavyoweza kutumia bwawa hilo. Kama si hapo, basi tutatafuta sehemu nyingine ili tuwasaidie wananchi wale angalau wapate sehemu za kulima.

**MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Kwa kuwa mbali na Bwawa la Kidawashi; kupoteza hayo maji kudidimia chini kuna maji mengi ambayo yanapatikana wakati wa mvua nyingi lakini maji hayo yote yanapotea baharini. Je, Serikali ina mpango gani kuyamega baadhi ya maji haya na kuweza kutumika katika umwagiliaji?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyojibu katika majibu yangu yaliyotangulia, nitawapeleka wataalam kule na nimesema nitashirikiana na Baraza la Mazingira, pamoja na Halmashauri za Wilaya,

kutazama sasa eneo mbadala ili maji haya tuweze kuyatunza yasaidie kumwagilia katika maeneo yale na sio kumwagilia tu pamoja na kunywesha mifugo.

Na. 279

**Mikoa Minne Inayolima Mahindi Nchini**

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA (K.n.y. MHE. ANNE K. MALECELA)** aliuliza:-

Kwa kuwa Tanzania imejaliwa kuwa na Mikoa mine, yaani Rukwa, Mbeya, Iringa, na Ruvuma ambayo ina uwezo wa kulima mahindi yatakayoweza kutosheleza matumizi ya ndani ya nchi nzima na hata kuweza kuuza ziada nje ya nchi:-

Je, Serikali inaisaidiaje Mikoa hiyo ili iweze kutumia ardhi yote kikamilifu na kuweza kupata mazao mengi zaidi kuliko ilivyo sasa ambapo ni sehemu ya ardhi tu inayolimwa na inakadiriwa kuwa chini ya asilimia 50?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, Mbunge wa Same Mashariki, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kuwa Mikoa ya Iringa, Mbeya, Ruvuma na Rukwa, ina hali ya hewa inayofaa kwa mazao ya chakula, likiwemo Zao la Mahindi. Kwa kutambua fursa hiyo, Serikali inatekeleza mikakati mbalimbali, yenye lengo la kuwawezesha wakulima wa mikoa hiyo, kuzalisha chakula cha kuwatosheleza na ziada kupelekwa maeneo yenye upungufu ndani ya nchi na nje ya nchi. Mojawapo ya mikakati hiyo ni pamoja na kuwapatia ruzuku ya pembejeo za kilimo ili kuwawezesha wakulima watumie pembejeo hizo kwa wingi na hivyo kuongeza tija na uzalishaji wa mazao ya chakula.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa utaratibu wa ruzuku ya pembejeo za kilimo, ulioanza kutekelezwa mwaka 2003/2004, ulianza katika Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini, ambapo jumla ya tani 39,387 za mbolea yenye ruzuku ilisambazwa katika mikoa hiyo. Katika misimu ya kilimo iliyofuata, Serikali imeendelea kuitengea mikoa hiyo mbolea ya ruzuku kwa kiwango kikubwa kuliko maeneo mengine nchini. Kwa mfano, katika msimu wa 2008/2009, jumla ya tani 57,576 sawa na asilimia 44.3 ya mbolea yenye ruzuku nchini, ilisambazwa katika mikoa hiyo. Aidha, kuanzia mwaka 2003/2004 hadi mwaka 2008/2009, wakulima wa Mikoa wa Nyanda za Juu Kusini kupitia Mfuko wa Pembejeo wa Taifa, walikopeshwa jumla ya matrekta makubwa 54, yenye thamani ya shilingi bilioni 1.6. Kupitia DADPs, vikundi vidogo vya wakulima viliwezeshwa kupata matrekta madogo ya mikopo 32 na zana mbalimbali za wanyamakazi. Mwaka 2009/10, zitanunuliwa *power tillers* 530 kupitia DADPs na kusambazwa katika mikoa hiyo. Aidha, jumla ya vituo 18 vya wanyamakazi vilikarabatiwa na kupatiwa zana kwa ajili ya

kutoa mafunzo kwa wakulima, kwa lengo la kuwawezesha kutumia wanyamakazi katika kazi za uzalishaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, huduma nyingine inayotolewa na Serikali ni kuwafundisha wakulima mbinu na kanuni za kilimo bora cha mazao kupitia utaratibu wa Shamba Darasa. Katika mwaka 2008/09, Wizara ikishirikiana na Halmashauri za Mikoa hiyo, imeanzisha jumla ya Mashamba Darasa 298. Uanzishaji wa Mashamba Darasa bado unaendelea. Aidha, katika mwaka 2007/08 na 2008/09, jumla ya Maofisa Ugani 124 wameajiriwa na kupangiwa kufanya kazi katika Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini.

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

(i) Kwa kuwa ni ukweli ulio dhahiri kabisa kwamba hali ya hewa katika mikoa hiyo inayotajwa na Serikali kama kipaumbele cha kuzalisha chakula inaruhusu kabisa mikoa hiyo kuzalisha hata ziada ya kuuza nchi za nje. Mheshimiwa Naibu Waziri pamoja na mikakati hiyo yote anayoisema; na kwa kuwa katika bajeti amekiri bado tuna upungufu wa tani karibu takribani 1,000 za chakula ndani ya nchi; je, anaweza kuliambia Bunge hili ni sababu ipi sasa ambayo inapelekea mikoa hiyo isifikie kuzalisha tani hizo 1,000 ili kuwa na ziada ya chakula?

(i) Kwa kuwa Mfuko wa Pembejeo kupitia SCULT ndio umekuwa kimbilio pekee la wakulima na hasa kule vijijini kupitia kwenye vyama vya ushirika kupata zana bora za kilimo; na kwa kuwa matrekta hayo makubwa 50 ni wastani wa matrekta 10 tu katika kila mkoa ambayo yaligawiwa mwaka jana; je, Mheshimiwa Waziri yuko tayari sasa kutoa kipaumbele kutoka matrekta 10; Mfuko wa Pembejeo sasa upeleke angalau matrekta makubwa 30 kwa kila mkoa unaozalisha chakula ili waweze kutosheleza mahitaji na kuzalisha ziada na kuongeza pato la nchi yetu ya Tanzania?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, nipende kusahihisha kwamba, upungufu utakaojitokeza ni tani 1.3 milioni na sio tani 1,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, mikopo ya pembejeo, ruzuku ambayo tunaipeleka inatokana na uwezo wa Serikali kwa hivi sasa. Kwa ujumla, tulikuwa tunapendelea mikoa hii kwa sababu ya hali ya hewa na ndiyo maana tumepeleka mbolea mwaka jana kuliko maeneo mengine na hata mwaka huu tutafanya hivyo hivyo. Tutakapopata uwezo zaidi, tutaweza kuongeza pembejeo, pamoja na kuhakikisha kwamba, maeneo hayo yanapata mikopo ya matrekta madogo na makubwa, kadiri Mfuko wa Pembejeo utakavyowezeshwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kusema kwamba, suala hili la ruzuku sio la kudumu ni suala ambalo wakulima wa maeneo yote nchini, lazima waelewe kwamba ni suala ambalo ni la muda wa kati, tunajiandaa kuanzisha Benki ya Kilimo kuendeleza kilimo nchini. Kwa sababu hatuwezi kusema kila mwaka hatuwezi, tunapeleka pembejeo sehemu fulani tu ya nchi, lazima tujue kwamba nchi hii ina wakulima asilimia zaidi ya 75

wanategemea kilimo. Hata maeneo ya Shinyanga, ambao wanalima mpunga wanahitaji wasaidiwe wazalishe zaidi ili waweze kununua mahindi ambayo ndiyo wanayotumia. Maeneo ambayo wanalima mihogo ndio wanategemea kwa chakula na kuuza, lazima wawezeshwe na wao. Hatuwezi tukategemea tu sehemu moja, kwa sababu hata wakizalisha ziada kule Iringa na Ruvuma, hawawezi wakasomesha watoto wa Shinyanga na Mwanza. Kwa hiyo, lazima tu-*balance* kwa sababu hata nchi yetu hii inaheshimika duniani kwa sababu ya usawa; lazima tuendeleze masuala haya ya pembejeo maeneo yote.

Na. 280

**Kuhamisha Makao Makuu ya Bodi ya Kahawa**

**MHE. GAUDENCE C. KAYOMBO** aliuliza:-

Kwa kuwa Makao Makuu ya Bodi ya Kahawa yapo Moshi:-

(a) Je, ni lini Bodi hiyo itafungua ofisi katika maeneo ya wakulima wa kahawa kama vile Mbinga ili kuongeza huduma karibu na wakulima wa kahawa?

(b) Je, ni lini tutaachana na utaratibu wa kupeleka sampuli za kahawa Moshi kwa ajili ya kuonjwa ili utaratibu huo ufanyike katika maeneo husika?

(c) Kwa kuwa Viongozi wa Bodi hii hulazimika kufika Dar es Salaam mara kwa mara kuhudhuria vikao mbalimbali; je, Serikali haioni kuwa ni vyema sasa kuhamisha Makao Makuu ya Bodi hii Dar es Salaam ili kupunguza gharama?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula kna Ushirika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Gaudence Cassian Kayombo, Mbunge wa Mbinga Mashariki, kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kwa kutambua umuhimu wa kusogeza huduma karibu na wakulima, Bodi ya Kahawa nchini tayari imeshatoa maamuzi ya kuongeza Ofisi za Kanda katika mikoa inayolima kahawa hapa nchini kutoka ofisi 3 za sasa hadi 6. Kanda tatu zitakazoongezwa ni Kanda ya Ruvuma, Tarime na Kigoma. Aidha, Bodi imejipanga vyema kuhakikisha kuwa, ofisi hizo zinakamilika mapema iwezekanavyo katika mwaka ujao wa fedha 2009/2010. Hali kadhalika, ili kuhakikisha huduma bora zinatolewa kwa wakulima na wadau wengine katika maeneo hayo, Maafisa Maendeleo wapya wa Zao la Kahawa wataajiriwa pia.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Bodi ya Kahawa, katika mwaka wa fedha 2009/2010, inao mpango madhubuti wa kuhakikisha kwamba, kahawa zote zinaonjwa katika maeneo yake ya uzalishaji kwa kuanzisha maabara ya kuonjea kahawa katika kila Ofisi zake za Kanda. Aidha, katika mwaka wa fedha 2009/2010, Bodi

imekusudia kuanzisha maabara za kuonjea kahawa *(cupping labs)* katika Kanda ya Ruvuma na Mbeya ili zihudumie Mikoa ya Ruvuma, Iringa, Mbeya na Rukwa. Mpango wa Serikali kwa miaka ijayo ni kuwa na maabara za uonjaji katika kila Kanda, jambo ambalo litapunguza gharama za hivi sasa kusafirisha sampuli za kahawa kwenda kuonjwa Moshi.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli gharama za kusafirisha Viongozi wa Bodi ya Kahawa kwenda Dar es Salaam kuhudhuria vikao mbalimbali ni kubwa. Hata hivyo, bado ni ndogo sana ikilinganishwa na gharama za kuhamishia Bodi Makao Makuu ya Dar es Salaam kwa sababu zifuatazo:-

(i) Bodi ya Kahawa ina jengo la kudumu la Kahawa House zilipo Ofisi za Bodi hiyo pamoja na ukumbi wa kuendeshea minada ya kahawa.

(ii) Aidha, kwa kuwa Bodi tayari ina Ofisi Ndogo Dar es Salaam, ambayo inasimamia uhifadhi na usafirishaji wa kahawa nje ya nchi, Maafisa wake hutumika pia kumwakilisha Mkurugenzi Mkuu katika baadhi ya vikao hivyo, kupunguza safari za kutoka Moshi kwenda Dar es Salaam.

**MHE. GAUDENCE C. KAYOMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana na pia nashukuru majibu mazuri ya Serikali, ingawa nina maswali ya nyongeza. Kwanza, nilipongeze Bunge lako kwa kupitisha Sheria ya Kahawa Mwaka 2001. Kwa masikitiko makubwa, sheria hiyo kwa kiasi kikubwa utekelezaji wake ni Bodi ya Kahawa. Kwa kiasi kikubwa sana, pia Bodi ya Kahawa haina fedha toka Serikalini, ilipoweka maamuzi ya kutokutoza ushuru kwa ajili ya kusaidia hizi Bodi. Ninao wasiwasi wa Bodi hizi kutekeleza majukumu yake. Maswali yangu ya nyongeza mawili ni kama ifuatavyo:-

(i) Kwa vile Serikali imekwishaamua sasa kupitia Bodi ya Kahawa kuongeza Kanda na Kanda mojawapo ni Kanda ya Ruvuma; kwa vile tumepata uzoefu kutokana na TACRI ambayo ni Taasisi ya Utafiti pale Mbinga na kile kituo kinafanya kazi vizuri sana katika Mikoa ya Ruvuma, Mbeya na Iringa; Serikali inaweza kukubaliana na mimi kuwa Makao Makuu ya Kanda hiyo yawe Mbinga ili iwe rahisi kutoka Mbinga na kuhudumia Mikoa mingine kuliko kuweka Mbeya?

(ii) Bodi hii imeamua kuajiri sasa Maafisa Maendeleo wa Zao la Kahawa jambo ambalo halijafanyika toka Sheria ya Kahawa ilipoundwa. Je, Serikali inaweza kuweka *time frame* kwamba jambo hili litatekelezwa katika kipindi cha miezi sita kuanzia sasa?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, niseme pamoja na kusema kwamba, pesa hazitoshi zinazotengwa kwa ajili ya Bodi, lakini sasa hivi kwa sababu tunafanya mabadiliko ya Sheria ya Mazao ni kwamba, masuala yanayohusu *regulatory functions* za Bodi, yatashughulikiwa na Serikali kwa asilimia mia moja.

Masuala yale yanayohusiana na kuendeleza mazao haya likiwemo Zao la Kahawa, litashughulikia na wadau pamoja na Serikali. Kama nilivyosema juzi wakati wa Bajeti ni kwamba, muungano wa wazalishaji wa kahawa wameshakubali kuchangia Bodi hii shilingi milioni 500 kila mwaka na wataanza mwaka huu. Kwa hiyo, tunategemea wataendelea kuongeza lakini tukishafanya marekebisho, nadhani fedha hizi ambazo Serikali inaendelea kuziongeza mwaka hadi mwaka zitatosha. Suala la kuhamisha Makao Makuu ya TACRI kwenda Mbinga ni suala la kitaalam zaidi, nadhani wataalam wataangalia ni vigezo gani ambavyo vilisababisha wapeleke Mbeya na si Mbinga na kama inawezekana basi watafanya hivyo.

Swali lake la pili, tunalichukua na tutalifanyia uchambuzi.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge muda wa maswali umekwisha na maswali yamekwisha. Tunao wageni kama ifuatavyo:-

Tuna wageni wa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Ezekiel Maige, ambao ni mke wake Bi. Liberata Ezekiel Maige, halafu yupo na mtoto wake Godlucky Maige; karibuni sana. Mtoto ameshakua, maana yake tumemfungisha harusi hapa hapa Bungeni.

Tuna wageni wa Mheshimiwa William Shellukindo, ambao ni Advocate Joseph Ngiloi na Dkt. Detronela Ngiloi, hawa nadhani ni mtu na mke wake; karibuni sana.

Tuna wageni wa Mheshimiwa James Lembeli, ambao ni Wenyeviti wa Kata wa CCM toka Jimbo la Kahama na Kata wanazotoka ni za Ushetu, Kahama Mjini, Malunga, Igwamanoni, Mvunze, Nyandelwa, Muhongelo na Kilango, wakiongozwa na Mwenyekiti wa CCM wa Kata Bi. Febronia Ikombe. Naomba wasime wageni wote walipo. Karibuni sana kwa kupata Mwenyekiti mwanamke.

Wageni wengine ni Mheshimiwa Reuben Katwiga, yeye ni Diwani wa Kata wa Igwamanoni na Paulina Petro, Katibu wa CCM wa Tawi la Igalilimi. Ahsanteni; karibu sana. Halafu tuna wageni wa Waheshimiwa Wabunge wa Mkoa wa Tabora, ambao ni Madiwani wa Viti Maalum Urambo, ambao ni Madiwani wa Viti Maalum Urambo, wanaongozwa na Mwenyekiti wa UWT Wilaya ya Urambo. Mwenyekiti anaitwa Martha Susu na Katibu ni Chiku Masanja; karibu sana Viongozi kutoka Tabora, tumefurahi kuwaona.

Tuna wageni wa Mheshimiwa Herbert Mntangi, ambao ni Mwalimu Clementina Mntangi, bila shaka mke wake, kuna mama wanne wa ukoo wa Mkawe, watoto wawili James na Lawrencia. Hawa watoto wako wenyewe Mheshimiwa Mntangi? Karibuni sana, nimefurahi kuwaoneni.

Tuna wageni wa Mheshimiwa Gosbert Blandes, Mbunge wa Karagwe ni Wanafunzi kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma. Hawa ni wanafunzi wa kutoka huko kwake; ni Bwana Jonas Rugakingira, Cosmas Edward na Madai Ananius. Nadhani kama wamekosa nafasi baadae wataingia.

Tunao wageni wa Mheshimiwa Anthony Diallo, wanatoka Zain Dar es Salaam na Zain Mwanza. Hawa ni B. Violet Guyumi, yupo na Halima Okashi na Aneth Muga. Wapo kwenye maonesho na Waheshimiwa Wabunge mnakaribishwa.

Tuna wageni wa Mheshimiwa George Simbachawene, Mbunge wa Kibakwe, ambao ni Viongozi wa Chama cha Mapinduzi Kata ya Ipela, wakiongozwa na Mheshimiwa Diwani Theresia Wole wa Viti Maalum. Nadhani wako *basement* kwa sababu ya ukosefu wa nafasi.

Tuna wageni wa Mheshimiwa Job Ndugai, Mbunge wa Kongwa; ni wanafunzi 35 na Walimu watano kutoka Shule ya Msingi NDC huko Kongwa; karibuni sana.

Tuna mgeni wa Mheshimiwa Dkt. Willibrod Slaa, Mbunge wa Karatu, ambaye ni Mwenyekiti wa CHADEMA Singida Kaskazini; ni Mzee Sindi K. Sinda. Yuko kule nyuma.

Tuna wageni 17 wa Mheshimiwa Wabunge Yahya Kassim Issa, Mheshimiwa Asha Jecha na Mheshimiwa Kiumbwa Mbaraka. Hawa ni kutoka Jimbo la Chwaka, wakiongozwa na Katibu wa Jimbo la Chwaka, Ndugu Suleiman Ame Vuai. Ahsante sana, karibuni sana.

Tunao wageni wa Mheshimiwa Alyoce Kimaro, ambao ni mke wake, Bi. Oliver Kimaro; ahsante sana. Amefuatana na Bi. Hawa Lembeli. Sasa hawa Lembeli si Lembeli huyu? Karibuni sana akina mama.

Tuna wageni wa Mheshimiwa Benson Mpesya, Mbunge wa Mbeya Mjini, ambao ni Madiwani watatu wa Halmashauri ya Jiji la Mbeya na naomba wasimame; ni Mheshimiwa Aneth Kapambe, Kata ya Kalobe, Mheshimiwa Sara Mwamfupe, Kata ya Mahanga na Mheshimiwa Mary Malema, Viti Maalum Kata ya Mahanga. Naomba tuwapongeze sana hasa ninyi mliochaguliwa kwenye Kata na muendelee hivyo hivyo.

Tuna wageni sita wa Mheshimiwa Diana Chilolo, ni Wajumbe wa Kamati ya Utekelezaji wa UWT Mkoa wa Singida, ambayo yeye mwenyewe Chilolo ni Mwenyekiti wa Mkoa wa huo. Sasa hawa Wajumbe wake, yupo Ndugu Anastazia Amasi, Katibu UWT, Theresia Mkawi, Mjumbe wa Baraza Kuu la UWT, Yange Kiaratu Mjumbe, Margareth Mlewa Mjumbe, Sara Nalingigwa Mjumbe na Jane Miano; karibuni sana.

Tuna mgeni wa Mheshimiwa Emmanuel Luhahula, Mbunge wa Bukombe, ambaye ni mpigakura wake toka Masumbwe ni Ndugu Samora Abdallah, ahsante sana.

Tuna wageni wa Mheshimiwa Dkt. Zainab Gama, ambao ni Viongozi wa Jumuiya ya Wanawake wa Kiislam Mkoa wa Dodoma, wanaongozwa na Bi. Mwanaisha Mwinchoum. Naomba wote wasimame walipo.

Tuna wageni 30 kutoka Kanisa la Kiinjili la Kilutheli Tanzania, ambao ni Wachungaji na Wainjilisti Dodoma. Nafikiri wamekosa nafasi. Tuna wageni ambao ni wanakwaya 45 kutoka Parokia ya Katholiki ya Kiwanja cha Ndege Dodoma. Huko ndiko ninakosali mimi, karibuni sana, kwaya yenu nasikia mnaizindua sijui lini?

Tuna wageni kumi ambao ni wajasiriamali kutoka Mkoa wa Dodoma wakiongozwa na Bwana Chaula, wako wapi? Bwana Chaula ni maarufu sana kwa kilimo, namfahamu maana mimi zamani nilikuwa nalima hapa Dodoma.

Kuna wanafunzi 50 na Walimu wao kutoka Shule ya Msingi Mbwanga Dodoma, naomba wasimame, nadhani watapata nafasi mchana. Tuna wanafunzi 10 kutoka Shule ya Sekondari Makole Dodoma, karibuni sana. Tuna wanafunzi 50 na Walimu kutoka Shule ya Sekondari Kikuyu Dodoma, wasimame kama wamepata nafasi. Ahsante karibuni sana.

Tuna wanafunzi 40 na Walimu wao kutoka Shule ya Sekondari Nkhungu Dodoma. Wanafunzi 40 na Walimu wao kutoka shule ya Sekondari ya Hazina Dodoma. Tuna wanafunzi 6 kutoka Chuo Kikuu cha Ardhi Dar es Salaam, walipo naomba wasimame. Nafikiri hawa wamekosa nafasi.

Mheshimiwa Zungu nae ana wageni; ni wanafunzi 32 wa Chuo cha Uandishi wa Habari Dar es Salaam. Karibuni sana tunategemea ninyi ndiyo mtasaidia taaluma yenu, kwa sababu sasa hivi imeingiliwa, mambo mengine yanayoandikwa huamini kama ni wanataaluma. Basi tunawategemea sana ninyi. Ahsanteni sana.

Matangazo ya Kazi; Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji, Mheshimiwa Gideon Cheyo, anawatangazia Wabunge wa Kamati yake kwamba, leo tarehe 24 saa saba mchana, watakuwa na Kikao katika Ukumbi Namba 227.

Tangazo la Kiofisi; anaomba niwatangazie Waheshimiwa Wabunge kwamba, tarehe 24 mpaka 25 kutakuwa na maonesho yafuatayo kwenye Uwanja wa Maonesho wa Bunge: Moja, kuna shughuli mbalimbali zinazofanywa na Shirika la TANESCO, ikiwa ni pamoja na Miradi ya Umeme inayotekelezwa Majimboni. Pili, kuna shughuli ya Makampuni yote yaliyo chini ya Kampuni ya *Solar Energy Association*, wanaonesha matumizi ya umeme wa jua majumbani na kuchimba visima na kadhalika. Kwa hiyo, mnakaribishwa.

Kuna tangazo la Mheshimiwa Zainab Gama, lazima ujifunze kuandika haya matangazo rasmi. Anasema kwamba, jana tulitangaza kwamba, ile ratiba ya hitima ya Marehemu Sheikh Suleman Gorogosi na Profesa Haroub Othman, tulisema ingefanyika Siku ya Jumamosi; sasa kuna mabadiliko kwamba, ile shughuli itafanyika Siku ya Jumapili saa nane mchana hapa Bungeni kwenye eneo la *basement*. Kwa sababu imeonekana Waheshimiwa wengi walipenda kushiriki, kwa hiyo, itakuwa saa nane, Siku ya Jumapili, kwa hiyo, wote mnakaribishwa.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na shughuli za leo.

**MHE. GAUDENCE C. KAYOMBO:** Mwongozo wa Spika.

**NAIBU SPIKA:** Mwongozo wa Spika, Mheshimiwa Kayombo.

**MHE. GAUDENCE C. KAYOMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, Kanuni ya 68(1).

**NAIBU SPIKA:** Soma inasemaje?

**MHE. GAUDENCE C. KAYOMBO: "***Mbunge anaweza kusimama wakati wowote na kusema maneno kuhusu utaratibu, ambapo Mbunge yeyote ambaye wakati huo atakuwa anasema atanyamaza na kukaa chini na Spika atamtaka Mbunge aliyedai utaratibu, ataje Kanuni au sehemu ya Kanuni iliyopo."*

**NAIBU SPIKA:** Kwa hiyo, Kanuni gani unataika kuisemea?

**MHE. GAUDENCE C. KAYOMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, wakati anajibu maswali yangu ya nyongeza hasa swali namba moja, majibu yake yalionesha kama vile mimi nimeomba kuhamisha Makao Makuu ya TACRI kwenda Mbinga. Mimi nilizungumzia TAKRI kama mfano bora wa Tawi lililoko Mbinga na linafanya kazi vizuri, kuhudumia Mikoa mingine na nilikuwa naiomba Serikali, ifikirie kujenga Makao Makuu ya Kanda Mbinga.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba mwongozo wako.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge, unajua Kuhusu Utaratibu, siyo huo. Wewe hapa ungetumia Kifungu namba 50 ambacho kinakwambia: "*Maelezo Binafsi ya Mbunge"*. Kwa sababu hiki kipindi kinatakiwa kufanywa baada ya kuahirisha Bunge jioni, ukishamuarifu Spika jioni unasema; wakati Waziri anajibu swali namba fulani asubuhi sikuridhika na majibu yake ama hakunielewa, basi wewe unajieleza pale. Sasa hapa si utaratibu; utaratibu haujakosewa hapa ni kwamba, yeye hakujibu vile ulivyofikiria wewe. Kwa hiyo, kifungu kizuri ambacho ulitakiwa ukitumie wewe ni kifungu namba 50

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaendelea.

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2009/2010 – Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi

*(Majadiliano yanaendelea)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, ilikuwa vizuri tuliongeza muda kwa sababu hata hivyo, idadi ya walioomba kuchangia bado ni wengi, lakini tutaweza kuwa

na kumi asubuhi hii, pengine tutaweka wawili au wanne mchana. Kwa hiyo, naomba niwaite wafuatao ambao walichangia mara moja; ni Mheshimiwa Kilontsi Mporogomyi, Mheshimiwa Ramadhani Maneno, Mheshimiwa Felister Bura, Mheshimiwa Mzee Ngwali Zubeir na Mheshimiwa Vedastusi Manyinyi. Tuanze na Mheshimiwa Mporogomyi.

**MHE. KILONTSI M. MPOROGOMYI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii na mimi nichangie hoja iliyoko mbele yetu. Kwanza kabisa, naomba nimshukuru sana Mwenyezi Mungu, kwa kunijalia uhai nikafika hapa asubuhi ya leo, nikiwa mzima mwenye nguvu na afya njema. Pili, nawashukuru wapigakura wangu wa Jimbo la Kasulu Magharibi, ambao wamekuwa wavumilivu sana na ambao nimekuwa nikifanya kazi nao kwa muda mrefu na bado wanaendelea kunipa ushirikiano mkubwa na mimi nawashukuru sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nichukue nafasi hii, kumpongeza Mheshimiwa Profesa Jumanne Maghembe, Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi. Nawapongeza Manaibu wake, wote ni wataalam kwenye taaluma hii. Nampongeza Katibu Mkuu, naye ni mtaalam kwenye taaluma hii na nawapongeza Wataalam wengine katika Wizara hii, ambayo kwa mara ya kwanza mimi nafikiri kama mtu anafanya kazi vizuri ni vizuri tukampongeza kwa kazi nzuri anayofanya. Jamani Profesa Maghembe na Manaibu wake, wanafanya kazi nzuri sana. Kazi wanayofanya ni *professional*. Watu wakifanya kazi tunawapongeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mara nyingi nimekuwa nakubali kwamba, ukipeleka watu ambao zile fani zao zinaendana na mahali wanapokwenda, basi watafanya kazi vizuri maana uelewa wao utakuwa mkubwa sana. Kwa hiyo, ninawapongeza sana Wizara hii. Kwa kawaida, siipongezi kwa furaha kubwa, lakini Wizara hii naipongeza kwa furaha kubwa maana wanafanya kazi vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli Walimu hatuna, maabara kwenye shule zetu za sekondari hazipo na hasa wale ambao hatukuwa na shule za sekondari kwa miaka mingi. Katika Jimbo langu peke yake, mimi niliingia tukiwa na shule ya sekondari moja na sasa tuna shule za sekondari karibu 25. Toka zimeanza kufanya kazi, hizi sekondari hazina maabara, hazina *computer* ili na sisi tuendane na wakati. Bahati nzuri, Mheshimiwa Waziri amejitahidi sana, ana mpango wa kuweka *computer* karibu shule za sekondari hapa nchini ili watu wetu waendane na tekonolojia. Pili, hata maabara tunazozizungumzia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ninashukuru sana kwa sababu huwa napenda kusoma. Kwa hiyo, wakati fulani kama miezi mitatu, mine, iliyopita nilimwendea Mheshimiwa Waziri Maghembe, nikamwambia Waziri hebu niambie mipango mliyonayo maana nataka kuelewa maana kila siku mna-*reproduce* yale yale? Kwa kweli alinieleza mipango aliyonayo na mimi nikaridhika na ambayo ameionesha kwenye *speech* yake. Mipango ni mizuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ziko shule ambazo kusema kweli kwenye tatizo la Walimu zina Walimu wawili au mmoja, hizi hatuwezi kutegemea zifanye kazi vizuri na kutoa watu wenye *quality* nzuri. Shule hizi zipo na bado tunazihitaji na naomba Serikali iendelee kufanya mipango ili tupate Walimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kule kwetu katika Jimbo la Kasulu Magharibi, tuna shule ambazo nyingine zina Mwalimu mmoja, wawili au watatu. Sekondari nyingine hivyo hivyo. Kwa hiyo, moja ya mambo ambayo nataka kumweleza Mheshimiwa Waziri ni kwamba, pamoja na kwamba amefika Mkoa wa Kigoma, lakini ninamwomba afike Wilaya ya Kasulu, akatembee aone zile shule zaidi ya 50 tulizojenga, jinsi zinavyofanya kazi na matatizo waliyonayo na atazisaidia vizuri zaidi. Mheshimiwa Waziri, Mkoa wa Kigoma, uangalie kwa huruma sana maana tulikuwa nyuma sana kielimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine naomba niulize katika *form* ya maswali kwamba; ni lini Sheria iliyoanzisha Mfuko wa Elimu (TEA) itafanyiwa marekebisho ya Kisheria kuhakikisha Mfuko huu unaendeshwa kwa njia endelevu zaidi?

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, Mheshimiwa Waziri wa Sayansi na Teknolojia, siku za karibuni alipokuwa anawasilisha hoja yake alisema, wataanzisha mtandao wa *computer* ambao ni mtandao wa mawasiliano. Kwenye mtandao huo, yeye ameweka *University of Dodoma* na *Unversity of Dar es Salaam*, ndizo zitakazowasiliana. Jana Mheshimiwa Rais alikuwa anazindua rasmi *Marine Cable* ya *Seacom*. Sasa imani yangu ni kwamba, kutakuwa na mwendelezo mzuri zaidi katika sehemu ya mawasiliano. Mimi ningeshauri haya mawasiliano yawekwe karibu Vyuo Vikuu vyote, kuanzia *Open University na University* nyingine zote za *private* wawe na mawasiliano. *We need these Universities to be more efficient* kuliko walivyo sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la tatu ni watoto wanaopata mimba mashuleni. Tumekuwa tunalizungumzia sana hapa. Mimi nimekutana na wale watoto, wengi waliondoka mashuleni na hawakurudi tena. Huyu mtoto tunapomwacha asirudi shule, tuna m-*commit to permanent inferiority*. Uwezo anakuwa hana. Ninamwomba Mheshimiwa Waziri, hawa watoto tuwawezeshe warudi shule ili waweze kuwalea watoto wao ili watoto walelewe katika mazingira mazuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimekuwa naendelea kupongeza, lakini naomba niseme kuwa, humu ndani ya Bunge kuna mambo mengine ambayo yanakera kwa sababu Wabunge tunakuwa hatukufanya utafiti wa kutosha kuzungumzia mambo. Jana, yuko Mheshimiwa Mbunge alizungumzia habari ya Baraza la Mitihani na mimi mnanifahamu, mara nyingi nimekuwa nikifuatilia mambo mengi sana na nakuwa nafanya aina ya utafiti kujua mambo yanavyoendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna ndugu zangu waliokuwa wameachishwa kazi wakati ule. Mimi nikasema hebu nijaribu kufuatilia nijue kama haya wanayoniambia ni kweli au ni uongo. Nikafuatilia sana, nikagundua kwamba *a good number* ya wale walioajiriwa na hapa niipongeze Wizara ya Utumishi, kwa sababu ilifanya kazi nzuri kushirikiana na Wizara ya Elimu, wakakuta kuna watu walioajiriwa kwa njia zisizo halali

ndani ya Baraza la Mitihani. Pili, wakakuta kwenye Baraza la Mitihani kulikuwa na watu wamepewa vyeo kama *Assistant Executive Director – Form Four*. Sisi tumekuwa tunazungumzia *quality of education* katika nchi hii. *Quality of Education* katika nchi hii haitaletwa kwa ku-*employ* darasa la saba na darasa la 12. Tuseme ukweli, haitaletwa na darasa la saba na darasa la 12, unampachika cheo *Executive Director.* Tunahitaji watu wenye ufanisi mzuri, watakaofanya kazi nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ilitokana na kazi nzuri ya *research* ambayo ilikuwa imeshafanyika na Bodi ikalichunguza jambo hili; ilipolichunguza ikaelewa nini kinaendelea, wakatoa ripoti zikaenda mpaka Ofisi za Juu. Kwa hiyo, kama ni kuhukumu, kumhukumu yule Katibu wa Baraza la Mitihani, pengine unamhukumu aliyefanya uamuzi, ambaye ni Mkuu wa Nchi hii. Rais hawezi kufanya uamuzi ambao ni kinyume na utaratibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye *research* yangu niligundua kwamba, kuna watu 79, kati ya hao wamo watu kutoka Mikoa mbalimbali na wala si Mkoa wa Singida peke yake. Wale walioondoka walikuwa na sababu mbalimbali, wengine walihamishwa hawakufukuzwa. Sasa nafikiri tunapokuja hapa tunazungumzia hoja, naomba hiyo hoja iwe ya mantiki, hata sisi tunaoizungumza tufaidike na hoja hizi, zisiwe za kuambiwa au zisiwe za ndugu zetu kwa sababu tunawazungumzia tu. *(Makofi)*

Nimejaribu kusoma kinachoendelea, nikajifunza kinachoendelea katika mfumo mzima kwenye Baraza. Mitihani iki-*leak* ni lazima *action* ichukuliwe. Haiwezekani mitihani i-*leak* watu wasifuatilie wakajua kwa nini ime-*leak*! Leo tumeshuhudia watu mbalimbali, vijana mbalimbali wanakwenda *University*, wanasema wamepata *First Class*, anasema *First Class* ile ameipata shule fulani, ukifuatilia hakuna cha *First Class*. *Collusion* ya watu wanaokaa katika sehemu hizo nyeti, hawaelewi hata maana yake. Wanapokaa hapo, wanavuruga kazi. Leo unasema unaweza kumwacha huyu. Mimi nafikiri Mheshimiwa Waziri, fanya kazi yako, watu wasikubughudhi, kazi unayofanya ni nzuri, Baraza la Mitihani linakwenda kufanya kazi nzuri na mimi sidhani kama tunataka majungu humu ndani. Mimi nimeleta maneno humu ndani mara nyingi, lakini maneno yale ninayoyaleta yafuatilie yana ukweli wote, simsemei mtu uongo. Ninaweza kwenda kusema kwa haki ya mbingu zilizoniumba ninalolisema hilo ndio ninaloamini na linatoka moyoni mwangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nawaambia wala hatuhitaji hoja binafsi katika hili. Hatuhitaji hoja binafsi katika hili, ila ukileta nitalipinga maana ninaelewa kinachoendelea na nimefanya *research* kweli kweli. *Reseach* nimefanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikushukuru sana, lakini nimpongeze Mheshimiwa Waziri pamoja na timu yake yote, kwa umahiri mkubwa walionao wa kufanya kazi. Kazi wanayofanya ni nzuri. Pale watu wanapofanya kazi, tuwapongeze kwa kazi nzuri wanayofanya. Watu wakikosea tuwashauri, kazi yetu sisi Wabunge ni kuwashauri na kuwaelekeza wanachotakiwa kufanya. Sisi ambao ni Maseneta humu ndani, tu-*operate* kwa *facts* tupu wala si kitu kingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi na kwa jinsi unavyoliendesha Bunge. Ninakupongeza kwa umahiri wako na nakuombea Mwenyezi Mungu, akubariki sana kwa sababu Bunge hili linakwenda kubarikiwa kwa kuwa na watu kama wewe na Mheshimiwa Spika.

Ninaunga mkono hoja mia kwa mia, ahsante sana Mheshimiwa Naibu Spika. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante kwa kutubariki.

**MHE. RAMADHANI A. MANENO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nami nakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuchangia hotuba ya bajeti iliyo mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nami nianze kuwashukuru Waziri wa Elimu, Manaibu wake wote wawili, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara hiyo husika, kwa kazi kubwa wanayoifanya katika kutekeleza Sekta ya Elimu, ambapo wote ni mashahidi katika nchi hii, sasa Sekta ya Elimu ya Msingi, Elimu ya Sekondari mpaka Vyuo inapiga hatua siku hadi siku.

Mheshimiwa Naibu Spika, nami nawashukuru Wananchi wa Jimbo la Chalinze, Jimbo langu la Uchaguzi, kwa jinsi wanavyoniunga mkono. Nami nawaahidi nitazidi kuwasemea, kuwafikishia yale ambayo ni kero kwao, hatimaye Serikali iweze kupata ufumbuzi wa kuwatatulia matatizo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, nami nianze kuipongeza Serikali hasa kwenye suala la mikopo. Hotuba ya Mheshimiwa Waziri imeonesha jinsi gani wanafunzi watakavyoweza kujikwamua au watakavyoweza kukwamuliwa kwenye suala la mikopo kutegemea viwango watakavyokuwa wamefaulu wakati wa mitihani. Niipongeze sana Serikali kwa hatua hiyo ambayo wameichukua.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nitoe shukrani zangu za pekee kwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Mwantumu Mahiza, wakati wimbi la kuunguza shule hapa nchini hususan katika Jimbo langu la Chalinze, ziliunguzwa shule tatu za Sekondari na Jimbo la Bagamoyo iliunguzwa Shule moja. Taarifa ilipokwenda Wizarani, Mheshimiwa Naibu Waziri alifika mapema na kuweza kutufariji na kuweka mikutano pale ya kuwaelimisha wananchi, pamoja na wale ambao hawalitakii mema suala la elimu na kuweza kuwaelimisha nini wanachotakiwa kufanya. Namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri na uendelee kuwa na moyo kama huo, Mwenyezi Mungu atakujalia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nianze na jambo kubwa la Walimu. Ualimu ni neno kubwa sana, halina mipaka, kwa sababu hata walimu ambao sasa hivi wanafundisha na wao pia wanawaheshimu sana walimu waliowafundisha. Kwa hiyo, unapozungumza suala la Ualimu, halina mipaka na ni neno zito sana na kubwa katika maendeleo ya nchi yoyote ile hapa Duniani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye suala la walimu, wenzangu wamezungumzia hapa, suala la nyumba. Ni kweli nyumba hawana, mishahara yao nayo ndio hivyo. Kubwa ninalotaka, Serikali watuambie walimu hasa wamewekwa kwenye kundi gani la utumishi? Mimi ninavyojua, mtu yeyote aliyeajiriwa hapo akiwa mtumishi ana haki ya kupata mambo mengi ya msingi kama mtumishi mwingine yeyote. Inapokuja kwenye suala la walimu, upo upungufu unaofanywa na Serikali na mimi nauona kama ni wa makusudi kabisa. Serikali ifikie hatua ya kuweza kuwasaidia hawa walimu, kuwatatulia matatizo ambayo nitayazungumza sasa hivi.

Mheshimiwa Naibu Spika, inapotokea mwalimu ana mke au ana mume na mtoto; mtoto akifariki au mke au mume, Serikali haina msaada wowote wa mwalimu huyu kumsaidia ksafirisha maiti hiyo ama huduma yoyote ya kumsaidia kipindi chote cha msiba uliompata mtumishi huyo. Zipo sekta za utumishi zinaoanisha kabisa, unapopatwa na matatizo kama hayo, unaweza kupata misaada kama usafiri na fedha ya kuweza kujikimu kwa ajili ya tatizo hilo lililokuwa limekupata.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye suala la walimu, hilo halipo. Sasa tuiulize Serikali, hivi ni kweli mwalimu anapokuwa amefiwa na mwenzi wake au mtoto, hana ulazima wa yeye kusafirisha maiti hiyo kule nyumbani kwao alikozaliwa ilimradi azikie pale anapofanyia kazi?

Mheshimiwa Naibu Spika, hili jambo ni la msingi sana na linatia uchungu na haya nimeyapata kwenye Jimbo langu, walimu wamekuja kunilalamikia sana na hatimaye wameanza kuanzisha Ushirika wa Kuweza Kunyang'anyana shilingi elfu tano tano kila mwezi za kuweza kutatua matatizo hayo pindi yanapokuwa yanajitokeza. Sasa niwaombe hawa Mawaziri watatu; Waziri na Manaibu wake wawili ambao wote taaluma yao ni Ualimu wafikirie sana jambo hili. Walimu wa Jimbo la Chalinze walitaka kuanzisha huo Mfuko kwa ajili ya kuzikana, niwaombe Mawaziri hao watatu, mmoja kati yao wajichague tu, ule Mfuko tunauzindua mwezi ujao, basi waje wachangie na waone kilio cha wale walimu na hatimaye wawatamkie nini kinachoendelea juu ya kuwatatulia tatizo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine, niishukuru Serikali kwa kuipandisha hadhi Shule ya Sekondari ya Lugoba kuwa Kidato cha Tano. Pia niwaombe, Shule ya Sekondari ya Chalinze tumejitahidi kupitia Mfuko wetu wa Elimu wa Wilaya ya Bagamoyo, tumeweza kukamilisha majengo yanayoweza kustahili ile shule sasa ipandishwe hadhi na kuwa Kidato cha Tano. Kubwa lililopo pale ni suala la maabara kama wenzangu walivyosema. Serikali ilitazame suala hilo la kuweza kupatiwa sasa maabara, lakini pia ombi la kuipandisha shule kufikia kiwango cha Kidato cha Tano, naomba litiliwe mkazo na kwangu utakuwa ni ukombozi mkubwa sana, kwani Wilaya sasa itakuwa na uwezo wa kuwa na shule tatu za Kidato cha Tano ikiwemo hiyo ya Chalinze.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni suala la walimu hawa wanaofundisha watoto wetu walemavu. Jimboni pale wapo walimu wanaofanya kazi hiyo na wanaifanya katika mazingira magumu sana. Vitendea kazi hakuna, lakini kazi wanayoifanya ya kuzunguka

katika Wilaya ya Bagamoyo katika Jimbo la Chalinze, jinsi gani ya kuziendea hizo shule zilizoko mbali na Kituo chao kile wanachofundishia kwa ajili ya kwenda kuwatafuta au kuwakusanya na kuwaelimisha wazazi kuwaleta watoto kwenye kile kituo cha ufundishaji. Niwaombe tu Waheshimiwa Mawaziri, wawasaidie usafiri walimu walioko pale wanaofundisha watoto wale wenye ulemavu. Wana mazingira magumu sana, sisemi muwatafutie gari, lakini hata pikipiki ikipatikana, itakuwa mmeokoa sana na kuweza kuondoa tatizo hili la watoto walemavu ili waweze kupata haki yao ya msingi na hao walimu nao wajisikie jinsi gani watakavyokuwa wanaipenda kazi yao, pamoja na mazingira magumu waliyonayo. Yapo mengine yanawezekana, hasa suala hili la usafiri. Watafutieni hata pikipiki ili waweze kuwafikia vijana wetu, waweze kupata elimu kama wanavyopata vijana wengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, nalizungumza hili kwa sababu jitihada wanazozifanya wale walimu ni kubwa na orodha ipo ya wanafunzi hawa walemavu wanavyozidi kuwafundisha na hatimaye mitihani ya darasa la saba kuweza kuifaulu. Hata mitihani ya Kidato cha Nne, wapo ambao wanaifanya vizuri sana na kuweza kufaulu kwenda Kidato cha Tano. Lote hili haliwezi kufanikiwa kama walimu hawa hawawezi kupata motisha japo ya usafiri wa pikipiki.

Naomba wenzangu tujitahidi, mnisaidie kwenye jambo hili ili suala la walemavu nalo lichukuee nafasi yake, hatimaye watoto wapate elimu iliyo bora na nzuri zaidi. Mkiwapatia usafiri, itakuwa tumerahisisha hata haya masuala mengine ya kushawishiana kuhusu migomo. Inafikia mahali kuna wakati kunaweza kukawa na *gap* la kusema sisi hatuwezi kufanya hivyo kwa sababu tumefanikishiwa na Serikali katika jambo fulani. Tunapoacha wote wanakuwa na sauti moja, ndiyo hii migogoro ambayo imejitokeza katika Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine naomba nizungumzie suala la Waratibu Elimu Kata. Kusema kweli na wao wana mazingira magumu sana, kwa sababu ipo Kata moja katika Jimbo langu ni kubwa kuliko Jimbo la Kibaha Mjini. Mratibu Elimu Kata unamwambia afuatilie suala la elimu katika shule hizo za msingi, wakati hata baiskeli hana! Kama hamna uwezo wa kuwanunulia pikipiki Waratibu Kata, basi watafutieni hata baiskeli angalau ziweze kuwafikisha huko ili na wao waweze kuipenda kazi yao iwe katika mazingira mazuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni suala la uhamisho. Ni kweli limezungumzwa hapa jana, walimu wanapohamishwa inategemea na utaratibu uliopo ndani ya Halmashauri lakini suala hili na Serikali ilitazame kwa umakini sana. Walimu hawa wanapohamishwa, inafikia mahali mazingira yanakuwa magumu sana huko walikotoka na wanakokwenda, inawachukua hata kuona ugumu wa kuhama walikohamishwa na hatimaye wengine kukata tamaa, hawaendi walikohamishiwa na wengine kuacha kazi na kuamua kufanya shughuli nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, kubwa zaidi ni mafao yao wanayostahili kipindi wanapohamishwa, wapewe mapema. Haiwezekani, jana mmetuambia hapa kwamba, mnadaiwa na walimu malimbikizo ya mabilioni ya fedha, mlikuwa wapi siku zote

hamlipi? Walipeni, mbona zipo sekta nyingine wanapodai mafao yao wanalipwa kwa pamoja? Haiwezekani, ifikie mahali kila sekta ioneshe masuala ya migomo. Tumechoka jamani na suala hili la migomo, watatulieni watumishi shida zao, waoneni hawa Watanzania pia wanayo haki ya kutatuliwa matatizo yao kama wananchi wengine wanapokuwa na haki katika nchi hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi yangu yalikuwa hayo, lakini niwapongeze sana kwa kazi kubwa wanayoifanya. Onesheni kwa vitendo, msiishie kwenye makaratasi tu na kuja hapa kupitishiwa pesa hatimaye utekelezaji wake unakuwa hafifu. Mnaofanya nao kazi hawawasaidii kama ambavyo inatakiwa. Kaeni nao, fanyeni kazi nao pamoja ili kuleta ufanisi katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Nakushuru sana. (*Makofi*)

**MHE FELISTER A. BURA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia Hotuba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi. Kabla sijachangia, nimshukuru sana Muumbaji wangu, kwa kunipa afya njema na kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu kuchangia hoja iliyopo mbele yetu. Pia niwashukuru sana akina mama wa Chama cha Mapinduzi Mkoani Dodoma, kwa kuendelea kunipa nafasi na ushirikiano mzuri ninaopata kutoka kwao.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Profesa Maghembe, Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, pamoja na Naibu Mawaziri, Mheshimiwa Gaudentia Kabaka na Mheshimiwa Mwantumu Mahiza, kwa ushirikiano mzuri, pamoja na Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, kwa kazi kubwa wanayoifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, elimu ni ufunguo wa maisha, elimu ni urithi, elimu ni mambo yote katika maisha au niseme kuwa katika nchi iliyoendelea bila elimu hakuna maendeleo. Elimu ndiyo sayansi na teknolojia, kama hakuna wananchi wenye elimu, sayansi na teknolojia tunayoizungumzia, itakuwa ni kitendawili katika nchi yetu. Kwa hiyo, tunapozungumzia Sekta ya Elimu ni Sekta nyeti kwa nchi yetu, kwa watoto wetu, kwetu sisi wazazi na kwa vizazi vijavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishukuru sana Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa uamuzi wa kujenga Chuo Kikuu cha mfano katika Mkoa wetu wa Dodoma, bila kuwasahau Viongozi wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii; waliitikia wito wa Rais na wamejenga madarasa, wamejenga mabweni na wanaendelea kujenga. Nawashukuru sana na kuwapongeza sana kwa hatua hiyo waliyofikia, lakini uzuri wa Chuo Kikuu cha Dodoma isiwe uzuri wa majengo tu, Wahadhiri nao wapatikane, vitendea kazi vipatikane, ndiyo uzuri wa Chuo Kikuu cha Dodoma utakapoonekana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kuchaangia suala ambalo lilizungumzwa sana katika Bunge hili, kwa mwaka 2006/2007, kuhusu wasichana wanaopata mimba wakiwa shuleni. Tulipata takriban shilingi milioni 100 kutoka UNICEF kwa ajili ya kufanya utafiti juu ya watoto wanaopata mimba na wanaopata mimba ni kuanzia darasa

la sita na kuendelea mpaka *form four* na hao ndiyo tunaowategemea kuwa Mainjinia, Madaktari, Mawaziri, Wabunge na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ukiangalia katika mwaka 2007, uandikishaji wa watoto darasa la kwanza ulikuwa ni asilimia 82%. Karibu nusu kwa nusu walikuwa watoto wa kike na wa kiume, *fifty fifty* wa kiume na wa kike. Watakaomaliza darasa la saba kati ya walioandikishwa mwaka 2007, wanaume inawezekana wakawa asilimia 80, lakini watoto wa kike hawa ambao waliandikishwa watakuwa wachache. Inawezekana wakawa asilimia 30 tu au 20 kutokana na mimba.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na UNICEF kutoa milioni 100 na Tume ikaundwa na hiyo Tume ilijumuisha baadhi ya Wabunge wenzetu humu ndani, hatujapata matokeo ya Tume hiyo; hatujui ilipendekeza nini kwa Serikali yetu!

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vizuri sasa Serikali ikasema Tume hiyo ilisema nini. Katika nchi jirani kama Malawi na Zambia, watoto wanaopata mimba wakiwa shule wanaruhusiwa, baada ya kujifungua wanaruhusiwa kuendelea na shule. Wenzetu Wazanzibari hapa, wala siyo mbali Zanzibar, mtoto akipata mimba akijifungua anaruhusiwa kurudi shule; hapa kwetu tatizo ni nini? Serikali ituambie tatizo ni kitu gani? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna malengo ya kufikia *fifty fifty* kwa wafanyakazi maofisini, kwenye siasa na sekta mbalimbali, tunatamani kufikia asilimia 50, lakini hawa ambao tunawategemea wawe maofisa katika ofisi zetu, ndiyo hao wanaopata mimba wana-*drop* hawaendelei na shule. Kwa kuwa sheria haiwaruhusu kuendelea na shule, wanakuwa mitaani hawana la kufanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia utakuta kwamba, wale watoto wanaopata mimba katika umri huo wa shule wa darasa la sita hadi *form four* ni wale watoto wa maskini. Wanadanganyika na vipesa vya sabuni, vya mafuta, mimi sidhani kama watoto wa wazazi wenye uwezo wana-*drop*. Akipata mimba mzazi ana uwezo wa kumsaidia akaendelea na shule, lakini mtoto wa maskini, mzazi hana uwezo huo. Kwa hiyo, hili lifikiriwe, tuwasaidie hawa watoto sheria ije na Tume iliyoundwa tupate majibu yao kwamba, walipendekeza nini kwa Serikali na kama linarudishwa Bungeni, lirudishwe Wabunge walijadili, lakini lilijadiliwa sana katika kipindi cha mwaka 2007/2008.

Mheshimiwa Naibu Spika, UMATI walifanya utafiti wakakuta kwamba, asilimia 20 ya wanawake wanaofariki dunia wakati wa kuijifungua ni watoto wenye umri wa kuanzia miaka 15 - 25 na umri huo ni wa watoto ambao wako shule. Sasa kama hali ndiyo hiyo, watoto wanafariki kwa asilimia 20 ya wale wanawake ambao wanajifungua kwa matatizo, lakini bado wanaojifungua salama hawana nafasi ya kurudi shule.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba Serikali ituambie Sheria hiyo au Tume ile ilisema nini. Muafaka ni kitu gani? Naiomba Serikali kwamba, watoto wanaopata mimba wakiwa shule waruhusiwe kusoma. Tusiwaache, hatutafikia *fifty fifty;* wanaume

hamsini na wanawake hamsini ofisini, sekta mbalimbali hatutafikia kama *drop out* hii itaendelea kuwa kubwa na hawataruhusiwa kuendelea na masomo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niongelee uwiano wa walimu na wanafunzi. Katika Hotuba ya Waziri, ukurasa wa 17 ameeleza vizuri jinsi Serikali ilivyoajiri walimu; katika mwaka 2007 - 2009 walimu 18,711. Akatuambia pia ongezeko la wanafunzi 900,000, ukiangalia wanafunzi 900,000 na wanafunzi 18,000 hao tu ambao wameandikishwa katika kipindi hicho kifupi, hakuna uwiano. Hii inaonesha jinsi walimu wanavyofanya kazi katika mazingira magumu, darasa moja watoto 70, darasa moja watoto 50. Mwalimu huyo anaishi kwenye nyumba ya tembe; mwalimu huyo tangu ahamishwe hajapewa nauli yake; mwalimu huyo ana watoto saba, anavyokula na anavyoishi anajua mwenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la walimu limekuwa kama tatizo, kwa hiyo, unakuta mwalimu anasomeshwa lakini mbele ya safari anabadilisha kazi kutokana na ugumu wa maisha, kutokana na mishahara kuchelewa, mishahara haiji kwa wakati, wanaopandishwa madaraja wanaweza wakakaa mwaka mzima mashahara wa daraja jipya wasilipwe kwa wakati. Kwa hiyo, walimu wanafanya kazi katika mazingira magumu sana. Waheshimiwa Wabunge, hata sisi tuliomo humu, bila walimu tusingefika huku tuliko. Wafikiriwe hawa watu, Wabunge wamesema sana na mimi sitaki kulizungumza sana kwa sababu limezungumzwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia niongelee mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu. Sioni sababu ya mikopo hiyo kuchelewa kwa wanafunzi. Mimi nadhani watoto wanapokuwa *selected* katika vyuo mbalimbali, pesa zao zipelekwe kwa wakati. Jamani, kuna watoto wanaotoka vijijini wazazi hawana uwezo, kama wanatoka Kigoma, wanapewa nauli ya kuwatoa Kigoma mpaka Dodoma, Kigoma mpaka Dar es Salaam. Kama wanatoka Mtwara, wanapewa nauli tu na *pocket money* ya shilingi 10,000 wakifika chuo hakuna mikopo au pesa za mikopo hazijaingia kwenye akaunti zao, wanapata tabu sana hao wanavyuo na ndio maana wanagoma wakati mwingine. Tuwasaidie mikopo yao iingie kwenye akaunti zao kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninampongeza sana Mheshimiwa Waziri, kwa kuziba pengo hili la bilioni 80.4 kwamba, utazitafuta kwa namna unavyojua na wanafunzi watapata pesa hizo kwa wakati. Basi, ionekanae katika mwaka huu wa fedha kwamba, wanafunzi watapata hizo pesa kwa wakati. Wanapata tabu sana watoto wa kike, mnawaingiza kwenye matatizo. Wanaume sijui, lakini watoto wa kike mnawaingiza kwenye majaribu makubwa, wanapokwenda chuo mwezi mzima hawajapata pesa zao. Serikali ilifikirie hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nazipongeza tafiti zinazofanywa na Vyuo Vikuu hapa nchini na taarifa ya Waziri inaonesha kwamba, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na cha Sokoine, vimeshika nafasi nzuri katika Vyuo Vikuu Afrika na Afrika Mashariki. Tatizo ninaloliona, tafiti hizi zinatusaidiaje Watanzania? Je, tunazitumia au tumewaachia nchi jirani wanatumia tafiti zetu kwa kujiendeleza? Hebu tutumie tafiti zinazofanyika

katika Vyuo Vikuu vya Tanzania kuendeleza nchi yetu, zisibaki kwenye makabrasha na kwenye makaratasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa niongelee kuhusu Chuo cha Ualimu Mpwapwa. Chuo cha Ualimu Mpwapwa hakijawahi kufanyiwa ukarabati tangu miaka 15 iliyopita. Walimu wanalala katika nyumba zenye mazingira magumu, wanaweza kulala na nyoka ndani, hujui ukuta huu una rangi nyeupe au ni rangi ya njano. Mheshimiwa Waziri, naomba uwakumbuke Walimu wa Wilaya ya Mpwapwa, wasaidie kufanya ukarabati katika nyumba wanazoishi na hata katika madarasa yao, kweli yamechakaa sio utani. Ninakuomba sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, niongelee pia juu ya *teaching allowance*. Zamani kulikuwa na *teaching allowance,* walimu wanaofundisha katika mazingira magumu; hakuna barabara, hakuna nyumba ya mwalimu, wanaishi kwenye nyumba za nyasi na pengine zinavuja.

Mheshimiwa Naibu Spika, walimu wakumbukwe, *teaching allowance* irudi na iwe motisha kwa wale ambao hawataki kwenda kufundisha vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niende haraka kwa sababu muda umekwisha. Tumejitahidi sana kujenga Shule za Sekondari za *O Level*, kila Kata imejenga shule. Ahsante, naunga mkono hoja, lakini Serikali ikumbuke kujenga shule za *A Level* katika Kata zetu. *(Makofi)*

**MHE. MZEE NGWALI ZUBEIR:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi hii asubuhi ya leo ili nichangie Bajeti ya Wizara ya Elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, nimshukuru Waziri pamoja na Manaibu wake na Watendaji wake wote, kwa kazi nzuri wanayoifanya katika Wizara ya Elimu. Vile vile niwape pole sana, kwa sababu ukiangalia Tanzania, migomo yote iko juu yao. Kwa hiyo, nawapa pole kwa hilo pia. Wapokee pole hiyo na wawe na subira katika majukumu yao ya kazi ya kila siku.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala zima ninalotaka kulizungumzia, kama jana nilivyouliza swali kwa Waziri Mkuu, nilimuuliza kuhusu sera zetu; kuna Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 1995, Sera ya Elimu ya Mwaka 1966 na Sera ya Elimu ya Juu ya Mwaka 1999. Sera hizi sasa zimekwishaunganishwa na ziko katika rasimu ambayo imeshapelekwa kwa wadau ili kuijadili na kutoa maoni yao. Katika Sera hii, napendekeza Sera hii ifikishwe Zanzibar kwa sababu nao ni wadau wa elimu ya juu, kuhakikisha kuwa Sera hii na wao wanaitumia.

Mheshimiwa Naibu Spika , tulimuuliza kuhusu Sera zetu, kuna Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 1995, Sera ya Elimu ya Mwaka 1966 na Sera ya Elimu ya Juu ya Mwaka 1999. Sera hizi sasa zimekwishaunganishwa na ziko katika rasimu ambayo imeshapelekwa kwa wadau ili kuijadili na kutoa maoni yao. Napendekeza Sera hii

ifikishwe na Zanzibar kwa sababu nao ni wadau wa elimu ya juu, kuhakikisha kuwa Sera hii na wao wanaitumia.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia Sera zetu, zinatofautiana Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar. Suala hili huwa nalisema siku zote kuwa, kutakuwa na tofauti ya Sera na Miongozo lakini mtihani uko sambamba au mitaala yenu mnafanya mmoja, lakini tatizo linakuja katika mitihani.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika matokeo ya mitihani, utaangalia hasa wapi ambapo mitihani wanafanya vibaya zaidi na wapi wanafanya vizuri zaidi. Kwa hiyo, ipo haja kuangalia hizi Sera ili kuhakikisha kuwa nazo zinalingana. Kwa hiyo, kulingana kwenyewe kwa elimu ya juu, tuhakikishe unakuwepo uwezekano mzuri, kwa sababu masuala yanayohusu Muungano, yana matatizo yake hivi sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuliangalie kwa uangalifu, tuone kama ipo haja tulinganishe Sera iliyopo Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar ili kuhakikisha kuwa uwiano unakuwepo kwa hii elimu ya juu. Hili nalipendekeza angalau liangaliwe kwa mtazamo huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ninalotaka kulizungumzia ni suala zima la Walimu wetu katika vyuo vyetu, wakati mwingine ni chanzo cha migogoro au malumbano yasiyokuwa na maana. Walimu Wakuu wa Vyuo, nadhani mara nyingi sana hawana utaratibu wa kukutana na wanafunzi kwa muda fulani, kwa hiyo, inasababisha mgongano baina ya wanafunzi na uongozi wa chuo. Ipo haja Walimu wa Vyuo au Makamu wa Vyuo waliopo katika Vyuo hivyo, waonane na wanafunzi kila mara ili kuhakikisha kuwa, yale matatizo madogo madogo wanaweza kuyatatua.

Mheshimiwa Naibu Spika, Walimu wengine wana kiburi hata kuwaona wanafunzi wao kwa matatizo yao, lakini hata na wanafuzi wengine wana kiburi kulingana na ile hadhi waliyonayo katika vile Vyuo walivyopo. Tunaomba Walimu Wakuu au Walimu wa Vyuo waangalie, waweke utaratibu mzuri wa kukutana na wanafunzi kila baada ya muda na kuhakikisha wanazungumzia matatizo au maendeleo ya kila siku ya vyuo vyao.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo ningependa kuzungumzia ni kuhusiana na Baraza la Mitihani. Baraza la Mitihani linafanya kazi nzuri hivi sasa, lakini kuna dosari ndogo ndogo tu ambazo zipo na zinataka kurekebishwa. Hata hivyo, niseme kuwa, lazima Baraza la Mitihani liwe la utafiti mzuri kama walivyoandika katika vitabu vyao kuwa wanafanya utafiti wa mambo tofauti tofauti. Jambo ambalo linanisikitisha ni kuwa, kila yanapozuiliwa matokeo ya wanafunzi, yanachukua muda mrefu kuyafanyia uchunguzi mpaka kurejeshewa matokeo ya uchunguzi. Kwa hiyo, ipo haja Baraza liwe na uangalifu, wakishatoa yule mwanafunzi hawezi kuathirika kwa muda wote ambao anakaa nje ya masomo yake. Hata hivyo, kama nilivyosema, wana mitambo hivi sasa ambayo wameiagizia nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo siyo mitambo kuagizia mipya na ya kitaalamu, hivi sasa tunataka imani na maadili ya kazi. Lazima tuwe na maadili ya kazi katika kazi

zetu, tunaweza kuagiza kila kitu kwa sababu Baraza la Mitihani, nimetembelea mitambo unaingia mwanzo wa mlango mpaka unafika mwisho wa mlango unaangaliwa; je, mitihani inavujaje? Tufanye utafiti siyo kuongeza mitambo, kuhakikisha kuwa inaboreshwa tu, lakini na maadili yawepo katika kuhakikisha kuwa, tunafanya kazi vizuri kwa mpango.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, wametoa kitabu chao kizuri na nimekisoma cha utaratibu wa usimamizi na uendeshaji wa mitihani. Kina matokeo mazuri na taratibu nzuri, lakini hawakuonesha kama kuna changamoto zinazowakabili wangeandika na changamoto zinazowakabili wangeandika wizi wa mitihani, urasimu, uchelewaji, ucheleweshaji wa mambo tofauti tofauti. Kwa hiyo, ingeonesha kuwa hiki kitabu kina hadhi zaidi na kuhakikisha kuwa, nao wanaweka mikakati ili wayakabili matatizo na changamoto za kila siku. Kwa hiyo, ipo haja kuangalia hili suala na kulifanyia kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ninalopenda kulizungumzia ni kuwa, Baraza la Mitihani hivi sasa linafanya ukarabati katika Ofisi za Mitihani Zanzibar. Ipo haja ya kufanyia ukarabati ofisi zile, kwa sababu ni zao na zinafanya kazi. Wakati huo huo wamepata kiwanja cha kujenga ofisi nyingine mpya na kuhakikisha kuwa na wao wanakuwa na ofisi zao wenyewe kuliko zile walizokuwa wanapanga. Kwa hiyo, nawapongeza sana na waongeze bajeti kuhakikisha kuwa, hilo jengo linakamilika bila kupoteza muda na viwanja havivamiwi kutokana na Zanzibar kuwa na upungufu wa viwanja vya ujenzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni kuhusiana na *Science Marine*. Hiki ni kilio cha muda mrefu sana. Suala hili tunalizungumzia mara zote katika Bunge, ni miaka mingi tu kuanzia mwaka 2006. Kwa hiyo, linachukua muda mwingi. Hivi sasa wametengewa shilingi bilioni moja, ambazo haziwezi kufanya kazi ya ujenzi wa Chuo Kikuu cha *Science Marine*.

Mheshimiwa Naibu Spika, ipo haja ya kuliangalia hili suala, kuwaongezea pesa na kuhakikisha kuwa ujenzi unaanza. Hata hivyo, yule mkandarasi wa Kichina aliyepo pale, anasema ule mkataba uangaliwe upya. Sasa unapouangalia upya, maana yake na mambo mengine yatajitokeza. Kwa hiyo, hayo mambo mengine yatakayojitokeza yatarudisha nyuma hata huo ujenzi wenyewe.

Mheshimiwa Waziri nakuomba tuliangalie upya na ushauri ulitolewa na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, ambacho kiko chini ya Taasisi ile na ikatoa mapendekezo mengi sana ya kushughulikia katika Mabenki yetu na Mifuko ya Hifadhi. Walitoa mapendekezo ambayo kama yalivyo na taasisi nyingine zinaomba katika Mifuko hiyo, kwa mfano, PPF walipendekeza kuwa wanaweza wakapunguza asilimia 18 ya mkopo wanaoweza kuutoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, NSSF wakasema asilimia 12, CRDB wakasema asilimia 12 vilevile. Wakati huo huo wakasema kuwa wanaweza kuchukua mkopo huu kwa muda mrefu, yaani miaka 10. Mpaka leo Wizara ya Elimu haijatoa jibu katika taarifa hiyo waliyoitoa. Kwa hiyo, ipo haja ya kuangalia uwezo wa Serilali, Chuo kile

hakiwezi kujengwa kama hakuna msaada. Chuo kinaweza kuanza kama Serikali itatoa shilingi bilioni sita kwa mara moja. Kwa hiyo, siyo rahisi, wanatoa shilingi bilioni moja na inawezekana isifike au isitolewi kabisa iwepo tu kwenye maandishi, kwa sababu wakandarasi wasingelalamika kuwa mpaka leo hawajapata hela zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ninalotaka kulizungumzia ni Chuo cha Mwalimu Nyerere. Amekieleza vizuri Mheshimiwa Waziri, kinafanya kazi vizuri na kipo pale tayari na hivi sasa na wao wametengewa shilingi bilioni mbili; shilingi bilioni moja kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi bilioni moja nyingine kwa ajili ya shughuli za maendeleo. Ninawapongeza sana na ninampongeza Mkuu wa Chuo hicho, Dkt. Magoti, kwa ujasiri alionao, ambapo hivi sasa anakikarabati chuo kile. Hata hivyo, kina wanafunzi wasiopungua 1300 na kitu, lakini tatizo lililoko pale ni mabweni.

Mheshimiwa Naibu Spika, Chuo kile hakina mabweni ya kutosha, wanafunzi wanaishi nje ya Chuo kile. Kwa hiyo, ipo haja kuwa, licha ya ukarabati tulioufanya, lakini hata hivyo, tuongeze mabweni ya wanafunzi ili kuhakikisha kuwa, wanafunzi wanaishi pale. Hata hivyo, kuna suala lingine; hela hiyo hiyo ijenge Chuo Kikuu cha Bububu. Hili ni suala zito, shilingi bilioni moja unaweza kuigawa kwa ukarabati wa Chuo cha Mwalimu Nyerere Kivukoni, halafu ikajenge Chuo cha Bububu. Suala hii siyo kweli, ipo haja ya Wizara au Chuo hiki kiongezewe pesa ili kuhakikisha ujenzi ule unafanyika kwa wakati muafaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nawapongeza sana kwa ujasiri walionao. Hata hivyo, suala lingine ninalotaka kulizungumzia ni kuhusu fedha za familia duni. Kipindi kilichopita cha 2009/2009, bajeti ya fedha za familia duni iliyotengwa ni shilingi bilioni tisa, lakini walichokipata ni shilingi bilioni mbili, upungufu ni shilingi bilioni saba. Hivi sasa imeachiwa Halmashauri kuhakikisha kuwa, wanaweka katika bajeti yao; je, huu uwezekano utakuwepo? Halmashauri zetu zinashindwa michango ya Vijana na Wanawake, halafu bajeti hizo hizo zichangie! Bajeti ya Michezo, sifikirii kuona suala hili linatekelezeka. Kwa hiyo, ipo haja ya Serikali kuangalia upya kuhusu hizi familia duni kuwa wanazisaidia katika bajeti zao za Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ninalotaka kulizungumzia ni kuwa, tunawapongeza sana Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, kwa kuwajali walemavu. Katika Vyuo vya Tanzania, ambavyo vinajali walemavu ni Chuo Kikuu Cha Dar es Salaam. Mwaka huu kimesajili wanafunzi wengi sana na vilevile wanawapa usafiri wa bajaji kwa ajili ya kutembelea na vifaa vya walemavu wanawanunulia. Kwa hiyo, ipo haja ya kuwapongeza kama wanafanya vizuri. Vile vile siyo hawa tu wanaofanya vizuri; na vyuo vingine vilivyobakia viige mfano huu, kwa sababu walemavu ni wenzetu, wanaweza wakasoma mahali popote siyo lazima Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na vyuo vingine wanaweza wakasoma vizuri zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hayo machache niliyokusudia, lakini dhamira yangu hasa ni Sera ya Elimu Tanzania tuiangalie. Inatudhalilisha mno kwa matokeo ya mtihani Zanzibar na kama hatukuwa waangalifu, Zanzibar tutakuwa katika hatua ya chini katika Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Kwa hayo machache, naunga mkono hoja nasema ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, mengine umeongea asubuhi kwenye radio. Mheshimiwa Vedastusi Manyinyi, atafuatiwa na Mheshimiwa Simbachawene.

**MHE. VEDASTUSI M. MANYINYI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Wizara ya Elimu, kwa bajeti yao nzuri, lakini na Serikali kuona umuhimu wa kuipa Bajeti ya Elimu kipaumbele cha kwanza, maana elimu ndio ufunguo wa maisha. Kusema kweli, yako mambo mengi yamezungumziwa upande wa elimu na yako mafanikio ya dhahiri ambayo yamepatikana kwenye elimu. Ukiangalia kwenye maeneo yote, mfano shule za awali, shule za msingi, shule za sekondari, hata vyuo vikuu, katika kipindi kisichozidi miaka mitano, ongezeko la wanafunzi limekuwa kubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii yote inadhihirisha ni kwa kiasi gani na sisi kama Watanzania, tunajaribu kwenda kwa *speed* kuhakikisha kwamba, tunaiboresha elimu na watu wetu waweze kuendana na hali halisi ya maisha. Sasa baada ya kuwa nimezungumza hayo, mimi nichangie baadhi ya maeneo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna tatizo kubwa upande wa walimu; pamoja na maendeleo makubwa yaliyopo, lakini tuna tatizo kubwa kwenye upande wa nyumba za walimu, tuna tatizo la maabara na vifaa vya maabara, watoto wetu kule shuleni wanahitaji chakula. Hayo yote ni changamoto tulizonazo, licha ya maendeleo makubwa na mazuri ambayo tumeendelea kuyaboresha kwa upande wa elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo kubwa la walimu hapa ni kwamba, tunaishukuru Serikali kuwa na vyuo vingi na kuendelea kufundisha fani ya ualimu. Leo ukiangalia wanafunzi wanaohitimu vyuo vya ualimu na wale wanaoajiriwa kwenye ualimu, ukitafuta uwiano hauwiani vizuri, kwa sababu watu wanalipa suala la ualimu kipaumbele cha mwisho; kwanza akishamaliza Chuo cha Ualimu, kazi kubwa anayoifanya ni kutafuta nafasi katika fani nyingine. Akikosa, anasema hana namna anamua kwenda kwenye ualimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, hata kama tungefanya juhudi kubwa kiasi gani ya kuendelea kusomesha wanafunzi wengi kwenye Vyuo vya Ualimu, anamaliza *degree* yake ya ualimu, anamaliza *Diploma* yake ya ualimu, lakini anakwenda kutafuta nafasi katika fani nyingine. Kwa hiyo, kumbe kazi kubwa tunayopaswa kuifanya kuanzia sasa ni kuboresha maslahi ya walimu, kupunguza na kumaliza kabisa matatizo ya walimu. Tunaambiwa Wabunge wenzangu wamechangia mambo mengi, kati ya watu wanaopata mishahara midogo ni pamoja na walimu, lakini pamoja na mishahara yao midogo wanadai fedha za malimbikizo bado hawajalipwa. Kama tulivyoambiwa, wenzangu nimesikia humu wanazungumza, mwalimu anapanda daraja lakini bado hawezi kulipwa mshahara unaolingana na daraja lake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ukiangalia haya matatizo yote ni matatizo ambayo yanasababisha kwa msomi yeyote yule kwenda kwenye ualimu inakuwa ni

kipaumbele cha mwisho. Kwa hiyo, nimwombe Mheshimiwa Waziri, ajitahidi kuhakikisha kwamba, matatizo haya anayamaliza. Malimbikizo ya walimu yamezungumziwa mara nyingi na wanasema fedha zipo lakini hazitoki. Mimi nashukuru safari hii, baada tu ya kupitisha Bajeti ya Wizara ya Fedha, tukasema fedha zianze kutumika na kama hivyo ndivyo na kwa kuwa haya malimbikizo yote yalishahakikiwa na yako tayari na Mheshimiwa Waziri amesema fedha zipo, hebu ziende walimu walipwe na wafanye shughuli zao. Jimboni kwangu Musoma wanadai fedha zisizopungua shilingi milioni 200. Mheshinmiwa Waziri, ujitahidi fedha hizo ziende na ninadhani kwa kufanya hivyo, hata watu wengine watakuwa na moyo wa kujiunga na ualimu kwa ajili ya kuendelea kuwafundisha watoto wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunalo tatizo kubwa la nyumba za walimu, pamoja na juhudi kubwa ambayo wananchi wameifanya ya kuhakikisha kwamba, vyumba vya madarasa vinajengwa. Kama pale Musoma Mjini, watoto wengi walikuwa hawaendi sekondari, leo kila anayefaulu anakwenda sekondari. Pamoja na juhudi hizo, nyumba za walimu bado ni tatizo kubwa, maabara zenyewe bado ni tatizo kubwa na vifaa vya maabara ni tatizo kubwa zaidi. Cha kusikitisha, kutokana na vifaa vya maabara kutokuwepo, pamoja na maabara, unakuta kwamba, hata walimu wenyewe wa *Science* kwa kuwa nao walijifunza *altenative to practical,* wakati mwingine inakuwa ni vigumu sana nao kutoa mafunzo haya ya elimu kwa njia ya vitendo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nimwombe Mheshimiwa Waziri tu kwamba, aangalie hizi fedha ambazo zinatengwa kwa ajili ya maabara na nyumba za walimu, ukitafuta wastani utakuta ni zaidi ya miaka 20 ijayo, bado tatizo la maabara litakuwa halijaisha na nyumba za walimu. Sasa mimi ningependa kumshauri Mheshimiwa Waziri, liko jambo dogo ambalo angeweza kulifanya; Serikali ikiamua kujiongeza mimi naamini tatizo litapungua, walimu wengi wanakataa kwenda mashuleni kwa sababu hakuna nyumba za walimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumbe wakati mwingine tunachoweza kukifanya, hebu Serikali iamue kuwa kila sekondari iliyopo, ijenge *hostel* ya vyumba 20 – 30; ambayo mimi naamini wala siyo kazi kubwa, kwa kuwa sasa hivi wengi wanaoajiriwa ni walimu, ambapo vijana zaidi ya kumi wanaweza kukaa katika *hostel* moja na wanapata pale huduma. Tunadhani kwamba, kwa kufanya hivyo, walimu wengi wataweza kwenda kule mashuleni na kutokana na hali hiyo, tatizo la ukosefu wa walimu tutalipunguza kwa kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali kadhalika, unapozungumzia vifaa vya maabara; leo ukizungumzia kujenga maabara ya kisasa ambayo imekamilika na vifaa vyake, gharama zake ni kubwa sana. Majengo yenyewe siyo chini ya shilingi milioni 40, ukija kuweka na vifaa unajikuta inakwenda mpaka hata shilingi milioni 80.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia vile vifaa kutokana na hali yetu ya uduni, badala ya kutumia *flask* za *glass* au *test tube*, wakati mwingine tunaweza kutumia vitu rahisi kama vya *plastic*. Kazi kubwa ambazo zinafanywa ni za kupima, kwa hiyo, tunadhani kwamba, Serikali leo ikiamua iangalie namna itakavyowezesha wanafunzi

wote waweze kujifunza kwa vitendo, itakuwa imewasaidia zaidi kuliko kusema vile vifaa vya kisasa tu ndio viende kule na ambavyo itachukua zaidi ya miaka 30 kabla shule zetu zote hazijaenea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, hilo ni ombi langu kwa Mheshimiwa Waziri, aone kwa kadiri atakavyoweza kufanya ili wanafunzi wetu kwa kipindi kifupi zaidi, wote waweze kufanya masomo kwa njia ya vitendo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lipo tatizo lingine ambalo mimi binafsi nimeshindwa kulifahamu sana. Maana leo unasema kila mtoto anayemaliza darasa la saba, haruhusiwi kukariri, huyu mtoto ambaye haruhusiwi kukariri leo aliyeishia darasa la saba hata kazi ya ulinzi hawezi kupata. Ni kwamba, ukiacha tu darasa la saba, kidato cha pili anaruhusiwa kukariri, anayemaliza *form four* mpaka Chuo Kikuu anaruhusiwa kurudia; kwa nini huyu mtoto ambaye tunajua kabisa kwamba tukimwacha akishashindwa hana namna nyingine ya kusukuma maisha yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri ungeweza kuliona hili, ikiwezekana hata wale watoto wanaoshindwa, waweze kuruhusiwa kukariri au kurudia darasa.

Lipo tatizo lingine kubwa ambalo linahusiana na wazabuni walio-*supply* vyakula. Wale watu walipewa kazi hiyo na wengine wakathubutu kuchukua mikopo ya benki, Mheshimiwa Waziri anajua, lakini pamoja na kazi hiyo na baada ya kuwa wamefanya hivyo, sasa wengine yapata zaidi ya mwaka hawajalipwa fedha zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ambacho inafanya sasa, inaamua kupeleka fedha shuleni moja kwa moja, wakati wale wazabuni tayari imewakopa. Matokeo yake ni kwamba, wale watu mwisho watauziwa nyumba zao na hata ukiangalia katika bajeti au kwenye Hotuba ya Mheshimiwa Waziri, hajasema kama kuna fedha zimetengwa kwa ajili ya kuwalipa wazabuni. Kwa hiyo, ningependa Mheshimiwa Waziri katika majumuisho yake, atuambie ni nini kitakachofanyika katika kuondoa tatizo hilo?

Mheshimiwa Naibu Spika, liko suala la chakula kwa watoto. Imani yangu ni kwamba, watoto wanakaa mashuleni kuanzia asubuhi saa moja na wanatoka saa nane au saa tisa, kuja kufika nyumbani ni saa kumi; yule mtoto hajanywa chai, hajanywa uji, wala hajapata chakula. Mimi nadhani hili, pamoja na kwamba tunapaswa tuwashirikishe wazazi, lakini Serikali haina namna ya kulikwepa suala hili. Kwa hiyo, tunadhani ni jukumu la Mheshimiwa Waziri, aangalie na Serikali kwamba ni kwa kiasi gani wale watoto karibu wote; si wa shule ya msingi wala wa sekondari wanaweza kupata walau chai ili waweze kusoma vizuri, maana ikishafika saa tano au saa sita, wanaanza kusinzia madarasani kwa sababu ya njaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, yapo matatizo mengine madogo, ambayo wakati mwingine Wizara inayachukulia taratibu wakati inapaswa kuyamaliza pasipokuwa na matatizo. Katika Jimbo langu la Musoma, tumekuwa na tatizo kubwa la kukosa Afisa Elimu kwa kipindi kirefu. Afisa Elimu tuliyekuwa naye aliugua aka-*paralyze*,

tukaendelea kuwa naye, lakini baada ya kuwa amestaafu mwezi wa nne, mimi binafsi nimekwenda Wizarani kuomba Afisa Elimu wa Shule za Msingi hadi leo hatujampata. Sasa matokeo yake ni kwamba, kwa kuwa hakuna mtu *responsible* kwa ajili ya kusimamia elimu ya msingi, lazima *performance* inashuka. Ambacho ni kitu kidogo tu cha kuteua mtu wa kwenda kusimamia elimu na elimu ikaweza kwenda vizuri zaidi. Kwa hiyo, ningekuomba Mheshimiwa Waziri wakati unajibu, uniambie lini tunapata Afisa Elimu kule na tunashukuru kuwa Afisa Elimu wa Sekondari tumempata, tunaomba tumpate na wa Shule ya Msingi hilo tatizo liishe.

Mheshimiwa Naibu Spika, liko suala la Chuo Kikuu Huria, labda ni-*declare interest* kwamba na mimi nina maslahi kule. Niseme kati ya Vyuo Vikuu ambavyo vinasaidia kupunguza matatizo ya elimu hapa nchini ni pamoja na Chuo Kikuu Huria. Kwanza, kina gharama nafuu, lakini vilevile kinachukua karibu nusu ya wanafunzi wa nchi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Sasa naingia katika kundi la waliochangia mara mbili; Mheshimiwa George Simbachawene, atafuatia Mheshimiwa Lucy Owenya, Mheshimiwa Anna Lupembe na Mheshimiwa Dkt. Charles Mlingwa na Mheshimiwa Maria Hewa atafikiwa.

**MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, niwapongeze na niwashukuru Wananchi wa Jimbo la Kibakwe, kwa kuonesha imani yao kwangu na wakati unavyokwenda, sina mashaka kwamba, wanaweza wakaniongezea kipindi cha pili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama kuna mambo ambayo nchi yetu inapaswa kujivunia na kuishukuru Serikali yetu ya Chama cha Mapinduzi kwa maendeleo makubwa yaliyopatikana katika Sekta ya Elimu nchini. Yamesemwa mengi na wazungumzaji waliopita, yakionesha wingi wa wasomi nchini wa *levels* zote. Kuongezeka kwa changamoto ya kila mmoja kupenda kusoma ni dalili tosha ya maendeleo na tunakokwenda ni kuzuri, hatima ya nchi yetu katika suala zima la maendeleo, bila elimu Taifa lolote linakufa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikichukulia tu Wilaya yetu ya Mpwampwa, tumepata mafanikio makubwa sana katika Sekta ya Elimu, kwa kuongeza idadi kubwa ya sekondari katika kila Kata na hata katika Kata nyingine kuwa na sekondari zaidi ya moja. Changamoto katika maendeleo yoyote yale huwa hazikosekani na niseme tu kwamba, Wizara itegemee kupata changamoto kubwa. Changamoto moja kubwa na ya msingi ni nyumba za walimu, walimu na maabara. Nimpongeze sana Waziri, Wasaidizi wake na Watumishi wote wa Wizara hii, kwa namna ambavyo wamejitahidi kuja na mpango mahususi wa kutatua tatizo la maabara. Hii itakuwa ni hatua moja kubwa na mafanikio makubwa katika elimu hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa pia wapokee changamoto ya kufanya hivyo katika kutatua tatizo la walimu. Kuna shule kadhaa zina upungufu wa walimu, nikichukulia katika Jimbo langu la Kibakwe, Shule kama ya Rudi yenye watoto mpaka *form four,* ina walimu wawili. Shule kama ya Mbuga ina walimu wawili; hali kadhalika na nyingine nyingi. Kwa hiyo, tuseme tu kwamba, hii ni changamoto lakini ziko sababu zilizopelekea hata kupungua idadi ya walimu ambapo shule nyingine zilikuwa nao. Tujiangalie, kuna mahali kidogo Wizara ipokee maoni nitakayotoa kwamba, kwa sasa tusiruhusu sana walimu kwenda kusoma, tuliowaruhusu sasa wanatosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu tulikuwa nao wa kukidhi idadi ya kuweza kutosha vipindi, lakini tukawaruhusu kwa mfululizo sana kwenda kusoma, japo ni jambo zuri lakini kwa sasa tubane kidogo ili hao waliokwenda wakikaribia kumaliza ndio tuanze kuruhusu wengine pia waende kusoma. Vinginevyo, hatutaziba *gap* ya upungufu wa walimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninalo jambo ambalo nilipenda Wizara iliangalie na hata Wizara ya Utumishi pia iliangalie; sipendi niite unyanyasaji, lakini pengine kutokutambua hasa hii kada ya elimu katika Sekta ya Ufundi. Nchini kwetu, Sekta ya Ufundi haiangaliwi ipasavyo. Tujaribu kuweka mkazo na msisitizo mkubwa katika Wizara inayohusika na Sekta hii na ku-*specify* hawa watu wa ufundi, kuona na wao wanashiriki na kwamba na wao mchango wao katika nchi ni muhimu sana kwa maendeleo ya Sayansi na Teknolojia. Mataifa yanayoongoza katika Uchumi mkubwa Duniani, wanatutawala kwa Sayansi na Teknolojia kwa sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, bila ufundi, nchi yoyote ile haitajikwamua kiuchumi. Mataifa yanayoongoza katika uchumi mkubwa duniani, wanatawala kwa sayansi na teknolojia kwa sasa,na wanaweza kukupeleka kwenye hiyo sayansi na teknolojia mbali ya kuwa na elimu, lakini elimu ya ufundi ndiyo inayoweza kutukomboa kwenye sayansi na teknolojia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyowahi kusema na nimekuwa nikisema mara kwa mara, nirudie tena kusema, mimi ni asili ya mtu aliyesoma ufundi kuanzia *O-Level Secondary School*. Nimesoma Mazengo Sekondari, nikatoka pale nikaenda *Arusha Technical College*. Mimi *bolts and nuts* nimeanza kuzisoma tangu nikiwa *form one*, lakini nilipoingia kwenye maisha nikakuta ufundi hauthaminiki. Leo hii nina jamaa zangu ambao nimewaacha wakasema sisi tunapambana kwenye ufundi, mimi nikahamia kuwa mwanasheria, lakini wameendelea kupambana kwenye ufundi na wamefikia hadi ngazi ya *Advanced Diploma* za ufundi. Kule kuna kutokuwatambua kama kuwanyanyasa hivi. Nina hoja hapa na mwanzo wa vurugu hizi za kutowatambua hawa Maafisa Elimu wa Uhandisi, ndiyo chanzo cha tatizo lenyewe kwamba, kulikuwa kuna kada ya Maafisa Elimu Uhandisi, ambapo kuna Waraka wa Utumishi Namba 11 wa Mwaka 2002, ulikuwa unaendelea kuwatambua lakini sasa hivi hawatambuliki na sijui wametupwa wapi.

Mheshimiwa Naibu Spika, wanapodai kupandishwa vyeo, hawapandishwi eti kwa sababu hawana digrii ya ufundi, lakini pia hawapati ruhusa ya kwenda kusomea hiyo digrii ya ufundi kwa sababu hatuna ufundi katika digrii ya *education*. Kwa nini

hatuwatendei haki hawa watu wenye *Advanced Diploma in Engineering* na wakati huo walikuwa na Diploma za Ufundi? Huku ni kuwanyanyasa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukisikia watu wanaojua *physics* vizuri, wanaojua hesabu vizuri ni wale waliopitia kwenye ufundi, kwa sababu msingi wa kuingia kwenye shule za ufundi ilikuwa ni kufaulu hesabu na sayansi na waliopata *division one* na *two* ndiyo waliokwenda *Technical Colleges*. Leo hii mnasema hakuna walimu wa hesabu na masomo ya sayansi si mmewaacha huku kwenye ufundi? Wanatengeneza majiko pale Gerezani Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tuwaangalie hawa watu kwani wamenyanyasika vya kutosha na mimi nimetumwa na mafundi wenzangu. Mfano, pale Iyunga Sekondari kwa sababu ya hali hii ya kuwanyanyasa, wameondoka mafundi 11. Walimu waliosomea ualimu wa ufundi, wanahangaika kutafuta vibarua mitaani. Unategemea tutapata wapi mafundi wazuri kama hawafundishwi na mafundi?

Mheshimiwa Naibu Spika, maneneo haya nayasema kwa niaba ya mafundi wenzangu walionituma ambao ni wafuatao; Ndugu Godwin Liaki, Ndugu Samweli Tendwa, Ndugu Juma S. Mwasyenene, Ndugu Dismas Mgowela, Ndugu Jack Mabango, Ndugu Peter Kambosha, Injinia Mwasomi na Ndugu Job Njogoro. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hawa ni mainjinia lakini bado hawatambuliki kwenye kada ya Maafisa Elimu; kwa nini imefutwa? Naomba hilo liangaliwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, niingie kwenye jambo lingine linalohusiana na Chuo cha Ufundi Arusha, ambacho Bunge hili lilinichagua kwa kura zote kuwa Mwakilishi katika Bodi ya Chuo kile cha Ufundi. Mwaka jana, ilipitishwa pesa ya maendeleo, shilingi bilioni mbili, lakini hadi mwaka umekwisha hazikupelekwa, kwa hiyo, hakuna kitu kilichofanyika. Kwa hiyo, tusilaumiane. Kesho nikirudi hapa msiniulize katika ile Bodi tuliyokuchagua ulifanya nini maana mimi ndiye ninayewawakilisha kule. Mwaka huu pia tunapitisha shilingi bilioni 2.6. Mimi ningependa kutoa ombi rasmi, kwa sababu Waziri unatambua kazi nzuri inayofanyika pale na nimeleta taarifa kwako baada ya kutoka kwenye Kikao cha Bodi juzi kwamba, ile maabara ya sayansi ambayo ujenzi wake unaendelea pale na matarajio ambayo unayataka, nikupongeze kwamba, unaijua vizuri Sekta ya Ufundi na umeamua kuisaidia, hebu hakikisha kwamba hizi shilingi bilioni 2.6 zinakwenda kwa wakati na ikibidi ziwe za kwanza kwa sababu kuna kazi kubwa na nzuri ambayo wewe mwenyewe unaifahamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie pia kada nyingine ambazo nazo zinanyanyaswa kwa sababu tu ya kutokutambulika. Sijui kama kuna mipango inayokuwa wazi pale Wizarani, kwa wenzetu wanao-*regulate* haya mambo ya watu wanaojiendeleza kielimu. Mfano, katika vyuo vya utafiti kama Chuo cha LITI Mpwapwa, mtu alikuwa na stashahada akienda kuchukua shahada anaporudi kwamba ame-*graduate* ana digrii, anapotaka kupandishwa cheo wanamwambia aanze sawa sawa na mtu anayeajiriwa upya. Kwa maana hiyo, ule uzoefu wake na muda aliokaa wakati wote katika utumishi

hauhesabiwi na hauangaliwi. Hii nadhani siyo sawa sawa, Wizara ya Elimu na Idara ya Utumishi, waone namna ambavyo madaraja haya ni muhimu kwa mtu anayejiendeleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano, Ndugu Gaitan Lubuva na Ndugu Christopher Ulime wa Chuo cha LITI Mpwawa, wameamua kustaafu wakiwa na stashahada wakati wana digrii zao. Wanastaafu wakiwa na cheo kile kile wakati tayari wana shahada zao. Hii yote inatokana na kwamba, kwa sababu hawapandishwi cheo na wanarudishwa kuwa sawa sawa na mtu anayeanza kazi. Nadhani siyo vizuri na pengine muangalie kwamba, huu nao ni unyanyasaji mwingine ambao unashindwa kuwatambua wanasayansi wetu, ambao ni muhimu sana katika nchi kama hii yetu maskini na inayotarajia kukua kwa kutegemea maendeleo kwa tafiti zetu na maendeleo ya sayansi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie hali ya Ofisi ya Wizara. Ukifika Wizara ya Elimu haina tofauti na Sokoni Kariakoo; mnapishana na mtoto wa chekechea, sekondari, mwalimu anayemfundisha, bosi, yaani ni vurugu mechi. Sasa najaribu kuangalia heshima iko wapi maana mwalimu aliyekufundisha, anayemfundisha mtoto wa shule ya msingi, anapishana na aliyestaafu anafuatilia mafao yake pale. Sijui *documents* zake hazijakaa vizuri, anapishana na mwalimu wake akihangaika kwenye *corridor*. Mwanafunzi naye anatafuta matokeo yake sijui yalisahihishwa vibaya, alilalamika naye anapigana kwenye *corridor* zile. Sasa heshima na nidhamu ya utumishi iko wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ningependekeza Wizara iangalie namna ya kuzitenganisha hizi Kurugenzi zilizopo katika Wizara ya Elimu, Wizara yenyewe kwanza ni kubwa. Tulipojaribu kutenganisha Wizara ya Elimu ya Juu na Elimu ya Ufundi na Sekondari, tumepata matatizo ya gharama kwa Serikali. Hilii sioni kama lina gharama kama tukitenganisha tu majengo ya zile Kurugenzi kwamba, Idara ya Elimu ya Juu iwe na jengo lake na sehemu yake, Idara ya Ufundi au Vyuo vya Elimu viwe na eneo lake na Sekondari iwe na eneo lake.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii italeta heshima, lakini kuwachanganya wote kwa pamoja, vurugu tunazoziona pale ni kama vile upo Sokoni Kariakoo. Mimi nadhani si busara na pengine inawapunguzia hata ufanisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mazingira yale ni tofauti na ofisi nyingine zote za Wizara nyingine za Serikali. Wizara hii ni muhimu, tunahitaji Waziri wetu apate *privacy* ya kutosha, apate muda wa kufikiri na kutafakari, lakini kwa vurugu zile siyo rahisi Waziri akapata nafasi nzuri ya kuweza kufikiri na kufanya mambo vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, sasa nitamwita Mheshimiwa Lucy Owenya na Mheshimiwa Anna Lupembe ajiandaye na Mheshimiwa Dokta Charles Mlingwa atafuatia.

**MHE. LUCY F. OWENYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika Wizara hii ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niwashukuru Waziri, Naibu Mawaziri, pamoja na Watendaji wote, kwa kuandaa hotuba hii. Aidha, napenda nimpongeze Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani, kwa hotuba yake nzuri, yenye *data* ambazo nina hakika Serikali itazichukua ili iweze kuzifanyia kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba mchango wangu nianze na Chuo Kikuu cha Ardhi Dar es Salaam. Chuo hiki kina matatizo mengi na kina wanafunzi wengi. Tatizo moja kubwa ni *accommodation*. Chuo cha Ardhi kina wanafunzi zaidi ya 2441, lakini *accommodation* wanaweza wakalala wanafunzi 411 tu. Kwa maana hii, wanafunzi wana chumba chenye vitanda viwili na wanalala zaidi ya wanane. Kwa hakika, hii kiafya siyo nzuri ukizingatia Dar es Salaam kuna magonjwa ya maambukizi kama vile TB, wanafunzi wakiugua inaweza ikaleta matatizo na hawataweza ku-*concentrate* vizuri darasani.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata vyoo wanavyotumia ni matatizo, vyoo vilivyopo pole vilijengwa kwa ajili ya wanafunzi wachache, lakini hivi sasa hata takwimu zinaonesha kwamba, kwa mwaka 2010/2011 watafikia wanafunzi 3000 na tayari wanafunzi hao wanaondolewa katika mabweni yale ya Mabibo. Wanafunzi hawa watakwenda kulala wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu matatizo ni mengi, pamoja na fedha wanazopewa kwa ajili ya kufanya *dissertation* ni ndogo sana, tangu zile za mwaka 1980 mpaka sasa hivi fedha ni zile zile, mahitaji yamepanda bei unakuta hata nauli imepanda. Hata bei ya kutoa *photocopy* imepanda, kwa hiyo, inawawia vigumu sana kwa wanafunzi wale kufanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu matatizo ni mengi na ninayo hapa katika karatasi matatizo yao yote, naomba niwasilishe Mezani ili Serikali iweze kuyafanyia kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, matatizo ya walimu; wenzangu wengi wameongelea kuhusu malimbikizo ya walimu. Walimu wana matatizo mengi, lakini napenda niwapongeze kwa kufanya kazi katika mazingira magumu sana, wamekuwa na malimbikizo ya madeni yao ya mishahara na fedha za matibabu. Pia nimpongeze Mheshimiwa Waziri, katika Hotuba yake ya Bajeti, ukurasa wa tisa anasema, mwaka 2008/09 kuna shilingi 7,569,230,962 na mbili na kwa ruhusa yako naomba ninukuu ukurasa wa kumi amesema kwamba: “Katika Chuo cha Ardhi walifanya ukaguzi tena mwalimu kwa mwalimu, wakakamilisha ukaguzi huo tarehe 15 Juni na wakagundua kwamba, kuna fedha ambazo zinahitajika shilingi bilioni 22.8 na tayari wamezipeleka Hazina.”

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa nina wasiwasi, nimeangalia katika Bajeti Kuu ya Waziri wa Fedha, sijaona fedha hizi ziko katika fungu lipi na Waziri ametueleza kwamba

zimepelekwa Hazina. Naomba atueleze fedha hizi ziko wapi isije kuwa ni danganya toto halafu mwisho walimu wabaki wakiendelea kudai na bajeti imepita. Naomba walimu hawa walipwe fedha zao *once and for all*, tumalizane na matatizo haya. Wakishalipwa basi fedha zao wawe wanalipwa kwa wakati ili matatizo haya yasitokee tena.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikiwa kwenye matatizo ya walimu, pia walimu hawa wamekuwa wakienda likizo kwa kutumia fedha zao, wakirudi ndiyo wanadai madeni yao. Unajua tena ukiritimba uliopo, ukishaenda likizo ukirudi ukija kudai madai hulipwi wakati unaotakiwa. Hii inakwenda sambamba na kukatwa bima ya afya kutoka kwenye mishahara yao. Mfano, kule Tanga kuna walimu wamenipigia wanalalamika bima ya afya wanakatwa, lakini wakienda kwenye maduka ya dawa bima hazipokelewi zile bima za afya, wanalipa kwa fedha zao lakini mwisho wa mwezi unakuta fedha zao zimekatwa. Naomba Wizara iangalie hili, kama siyo lazima wasikatwe mishahara yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya elimu nchini; katika Ripoti ya Mheshimiwa Waziri, inaonesha matokeo ya Sekondari yamedorora mwaka 2008, lakini hii ni pamoja na matatizo mengine ya vitabu na walimu. Mimi ninafikiri inachangiwa pia na msingi mzuri kutoka elimu ya msingi. Serikali inabidi iangalie ni jinsi gani ya kuhakikisha kwamba, elimu ya msingi wanafunzi wanafundishwa vizuri ili waweze ku-*perform* vizuri kwenye madarasa yanayofuata.

Mheshimiwa Naibu Spika, licha ya hivyo, mimi ninailaumu Wizara; Wizarani huwa wanachukua walimu kutoka sekondari wanawapeleka Wizarani. Mimi sikati ni jambo zuri kuwapandisha madaraja, lakini mfano, Shule ya Tambaza kuna Mwalimu wa GS, na Mwalimu wa *Accounts*, amehamishwa kutoka Sekondari ya Tambaza akapelekwa Wizarani, lakini hawafanyi *replacement!* Matokeo yake unakuta yale masomo yanakosa walimu na wanafunzi wanakosa haki yao ya kufundishwa. Hivyo, hata kama wanawapindisha vyeo, wahakikishe kwamba, wanaweka *replacement* kwa wale wanafunzi. *(Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie Shule za Kata. Hili ni jambo la kupongezana, naishukuru Serikali na ninawapongeza Wananchi kwa kuchangia katika Shule za Kata. Humu ndani wengi wamekuwa wakisema Ilani ya CCM imetimizwa, lakini wakumbuke kwamba, Wananchi waliojenga shule zile ni Wanachama wa CHADEMA, CUF, TLP na hata wasio na vyama. Kwa hiyo, Wananchi hawa wana haki ya kujua fedha walizochangia katika shule zile ni kiasi gani.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Hotuba ya Waziri hajatueleza kwamba ni shilingi ngapi tulitumia katika kujenga shule zile. Mimi naungana na Wananchi, kudai haki hiyo na kujua kwamba, tumechangia kiasi gani ili tujue na sisi tumechangia katika Pato la Taifa.

**NAIBU SPIKA:** Sidhani kama unapingana na hawa wanaosema ni Ilani ya uchaguzi, kwa sababu kweli ni Ilani ya Uchaguzi ila imetekelezwa na Wananchi wote na haki ya Wananchi kujua nini wamechangia pia ni haki yao wote. Kwa hiyo, Ilani siyo

tatizo, ndiyo utaratibu wa kuendesha Serikali, lakini imefanywa na watu wote na wananchi wote wana haki ya kujua ni nini wamekifanya. (*Makofi*)

**MHE. LUCY F. OWENYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, sawa. Shule za Kata zina matatizo mengi, hakuna walimu wa kutosha, hata msemaji aliyepita amesema kuna shule ambazo zina walimu wawili tu na takwimu zinaonesha kuna upungufu wa walimu zaidi ya laki moja na elfu kumi na tano. Ningependa kujua Serikali imejiandaaje katika kuziba pengo hili? Shule hizi za Kata pia licha ya kutokuwa na walimu wa kutosha, pia hazina vitabu na maabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi tupo kwenye dunia ya sayansi na teknolojia, lakini shule hizi hazina maabara, wanafunzi wanasoma, lakini vitabu hakuna. Wanasoma kwa uzoefu wa mwalimu, wakati mwingine maabara hazina vifaa, sasa hapa tunaongelea sayansi ipi, labda tuseme tunaongelea waganga wa kienyeji, maana yake bila kuwa na vifaa hawawezi kufanya vyema katika masomo ya sayansi. Kwa hiyo, Mwenyekiti wa Kamati alivyosema Serikali ijenge maabara, mimi naungana nao kwamba, ijenge maabara ikiwa ni pamoja na nyumba za walimu ili waweze kwenda kule. Kwa kutokujenga nyumba za walimu, inapelekea mtu anakuwa yupo Dar es Salaam anapangiwa vijijini na yeye si mwenyeji, unampangia aende kijijini hakuna nyumba, hakuna chochote, mnategemea mwalimu huyu kweli atakubali kwenda kijijini? Walimu wengi wanakimbia Shule za Serikali wanakwenda kwenye Shule za Binafsi na hata za Mashirika ya Dini, ambako wana uhakika watapewa nyumba na marupurupu yao yatakuwa mazuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuzungumzia suala la mimba mashuleni. Katika utafiti uliofanyika, Mkoa wa Mwanza kuna wanafunzi zaidi ya 300 wa kike ambao walipata ujauzito wakiwa mashuleni. Hii ni hatari kwa sababu tunapoteza rasilimali watu na wanafunzi wale tunawaadhibu kwa makosa ambayo wengine hawakuyatarajia na vile vile wanakosa elimu tunazidi kuwafanya warudi nyuma.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachotaka kusema hapa ni kwamba, unakuta mtoto ambaye mzazi wake hajiwezi, hataweza kwenda shule lakini kwa mtu ambaye mzazi wake anajiweza, atamlipia mwanae na mwanafunzi yule ataendelea na shule, kwa yule asiyejiweza atabaki nyumbani. Ningependa kuishauri Serikali, ianze *re-entry* kwa wanafunzi ambao wamepata ujauzito na hawawezi kuendelea, kwa sababu hawana uwezo, iwe katika shule za jirani ambako wataweza kwenda mashuleni. Zoezi hili limeweza kufanyika Zanzibar, Malawi, Zambia na Nchi nyingine, kwani hapa kwetu kuna tatizo gani. Ninaomba Serikali iliangalie hili kwa undani ili tuweze kuwasaidia wanafunzi hao.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Hotuba ya Mheshimiwa Waziri, tumejua kabisa UKIMWI ni Janga la Taifa. Ninaipongeza Wizara inafanya semina kwa Wafanyakazi wa Wizara, pamoja na Walimu kuwa wanapewa semina kuhusu somo la UKIMWI. Ningependa kujua katika wanafunzi wa Sekondari ambao wameshakua; je, kuna mikakati gani ya kuhakikisha kwamba nao wanapata Elimu hii ya UKIMWI ili nao waweze kujikinga na madhara ya UKIMWI?

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa, ningependa kumwomba Waziri, wakati Mheshimiwa Makwetta akiwa Waziri, ile 50 *percent* ya *allowance* ya walimu kutokana na mishahara yao walikuwa wanapewa *teaching allowance,* lakini sasa hivi imetolewa. Ninaomba wairudishe ili walimu hawa waweze kuona kwamba, wanapata motisha fulani wafanye kazi badala ya wao kwenda kufanya *tuition* na kukimbilia kwenye shule za binafsi na kuacha za Serikali. Wakifanya hivyo, walimu wataona kwamba, nao pia wanakumbukwa na kupewa motisha na watafanya kazi hizo vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, cha kusikitisha, Mheshimiwa Waziri wa Kazi alipokuwa anajumuisha majibu yake hapa Bungeni, alitueleza kwamba, Watanzania wengi hawapati kazi kwa sababu siyo waaminifu. Serikali inasomesha wanafunzi wengi na inawakopesha ili waje kufanya kazi. Waziri aliposema sisi siyo waaminifu, Serikali imejiandaaje kuhakikisha kwamba, Watanzania ni waaminifu badala ya kazi zetu kuja kuchukuliwa na wageni kwa kisingizo cha kwamba, sisi siyo waaminifu. Baada ya kusema hayo, naomba kuwasilisha. *(Makofi*)

**MHE. DKT. CHARLES O. MLINGWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi, nami nichangie kwa niaba ya Wananchi wa Shinyanga Mjini.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ni Wizara inayosimamia wakala wa mabadiliko chanya katika jamii, hawa ndiyo wanaomuumba mtu. Baada ya mtu kuzaliwa, walimu wanamtengeneza ili aweze kupata nafasi ya kuweza kumudu maisha katika dunia hii na kuchangia katika maendeleo ya jamii anayoishi. Kwa hiyo, hii ni Wizara muhimu sana, ukipewa dakika 15 kuzungumza na hususan ukiwa mwalimu kama mimi, kwa kawaida hazitoshi, lakini ni lazima tubanane hivyo hivyo kwa dakika hizo 15.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kwa pongezi na ushauri. Niipongeze Wizara hii kwa kuandaa hotuba nzuri, yenye takwimu zinazoonesha sura halisi ya maendeleo ya Sekta ya Elimu. Ninampongeza sana na timu yake yote. *(Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza sana Serikali, kwa ujenzi wa shule za sekondari zaidi ya 2000 zilizojengwa ndani ya miaka minne. Nimpongeze sana Mheshimiwa Rais, kwa kulisimamia hili vizuri, kwa sababu yeye ndiye aliyeongoza harakati hizi za kututoa kwenye shule 1200 tulizokuwa nazo kwa miaka 44 ya uhuru mpaka 2005 na sasa zimefikia takriban shule zaidi ya 4000 za sekondari. Haya ni maendeleo makubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kule Shinyanga Mjini nilikuwa na shule kama nne hivi za sekondari, lakini sasa kuna shule mpya kama 15, karibia 20, ni maendeleo makubwa sana na hizi ni shule za sekondari. Hii ni juhudi kubwa iliyofanywa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nijumuishe na Chuo Kikuu cha Dodoma; ni kazi kubwa sana imefanywa na Serikali na hususan Mheshimiwa Rais katika kuhakikisha kuwa, tunakuwa na Chuo Kikuu cha Dodoma. Ukiwa kiongozi ni vizuri ujue kuwa ni

muhimu ukumbukwe baada ya uongozi wako. Mheshimiwa Rais Jakaya Kikwete, atakumbukwa kwa upanuzi wa elimu ya sekondari na ujenzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma, ambacho kitakuwa ni cha aina yake. Hayo mawili peke yake, yanamtosha kustahili pongezi zisizo na ukomo katika uhai wa Taifa la Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, Vyuo Vikuu vya zamani visisahaulike wakati wa harakati za ujenzi wa Vyuo Vikuu vipya. Vyuo Vikuu vya zamani vya Dar es Salaam na Sokoine, pia vinahitaji kuangaliwa tena kwa karibu sana ili tuhakikishe kuwa, miundombinu yake ambayo sasa imechakaa sana, inarudishwa kwenye hali inayostahili kwa mwanafunzi kusoma ili apate shahada za kumuwezesha kutambulika kuwa na taaluma stahili kwa ajili ya kuchangia katika maendeleo ya Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, bado vyuo hivi vinakabiliwa na uhaba wa walimu na kwa hiyo bado vinahitaji fedha za kutosha ili waweze kufundisha walimu wao zaidi katika ngazi ya shahada ya uzamivu na uzamili ili ziweze kuhakikisha kuwa, zinabaki katika sifa za kuwa Vyuo Vikuu vinavyotoa shahada zinazostahili. Nafahamu Vyuo Vikuu vya zamani vya Serikali, hapa nchini bado vina upungufu wa walimu. Kumekuwa na jaribio la kuiachia Sekta Binafsi ili ijenge nyumba ambazo zitatumika kama maabara kwa ajili ya wanafunzi. Nafahamu mpango huu haujafaulu sana, kwa hiyo, naishauri Serikali iangalie uwezekano wa haraka wa kuhakikisha kuwa Vyuo Vikuu hivi vya zamani vinaendelea kujenga mabweni kwa ajili ya wanafunzi ili wasizagae mitaani wakihangaika kutafuta malazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vyema pia tuamue ukomo wa idadi ya wanafunzi kwa kila Chuo Kikuu, kwa sababu sasa tunafahamu Chuo Kikuu cha Dodoma kimepangiwa kuwa na wanafunzi 40,000. Hatujabainisha Chuo Kikuu cha Sokoine ukomo wake ni upi ili tuhakikishe tunakuwa na idadi ambayo italingana na miundombinu iliyopo, italingana na idadi ya walimu na ubora unaostahili ili wanafunzi wanaotoka kwenye maeneo yale, waweze kupata elimu inayostahili; vinginevyo, tunaweza kuwa tunaongeza wanafunzi wakati maabara hazitoshi, vyumba vya mihadhara havitoshi na mambo mengine yanakuwa hayatoshi. Kwa hiyo, unakuta vijana kweli wapo Chuo Kikuu, lakini wanasomea katika mazingira magumu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mtazamo wangu dira ya sasa ya elimu ni tamko la juu mno. Ninadhani kuna haja ya kuwa na dira mahususi. Mwaka jana nilisema hapa wakati nachangia Wizara hii kwamba, kuwepo na dira inayozungumzia Elimu ya Msingi, Elimu ya Sekondari na Elimu ya Juu ili katika ujumla wake, ndiyo tunakuwa na Sera na Dira ya Elimu ambayo ni jumuisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, Dira ya sasa inasomeka kama ifuatavyo; kwa ruhusa yako inasomeka: *"To have a Tanzanian who is well educated, knowledgeable, skilled and culturally mature to handle National and International challenges in various political and social economic fields by 2025.''* Kwanza, naiona hii ina dosari katika maana ya itikadi ya nchi yetu, ambayo ni kujitegemea. Nadhani kwa mawazo yangu ingesomeka kama ifuatavyo: *"To have a Tanzanian who is well educated,*

*knowledgeable, skilled and culturally mature to effectively contribute towards national self reliance in all fields of social, economic and political development."*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hii ya sasa si sahihi na ndiyo maana unaona tunahangaika tu wakati mwingine tunakosea kosea, maana dira ni ndoto ya kufika mahala, sasa ukikosea ile ndoto yako utakwenda sehemu uliyokosea. Ninadhani mnanielewa, Wizara hii ina wasomi wanaweza wakanielewa vizuri zaidi hiki nilichokisema.

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani tuzingatie hayo kwa sababu matokeo ya kutokuwa na dira zinazolenga makundi stahili, tunakosa kuelewa bayana msukumo katika kila ngazi. Kwa mfano, mimi nilidhani elimu ya darasa la kwanza mpaka la nne ingekuwa kusoma, kuandika na kuhesabu, darasa la tano mpaka la saba ni kuanza kumjenga mwanafunzi katika stadi za maisha, sekondari ni stadi za maisha na kumwandaa kuingia kwenye taaluma, elimu ya juu ni taaluma. Kwa sasa tupo kwenye mchanganyiko, nadhani ingekuwa ni vizuri katika siku za usoni, tuzingatie mambo kama hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sera zetu za Elimu pia nadhani zina upungufu kidogo katika mipango, kwa sababu leo hii tunashuhudia shule zetu nyingi bado zina upungufu katika miundombinu, rasilimali watu, fedha za uendeshaji na ndiyo maana matatizo mengi tunayoyashuhudia wakati mwingine ya kufeli wanafunzi kwenye maeneo mengine, yanasababishwa na matatizo haya. Pia nilisema mwaka jana, bado tunaishi katika Sera ya *Universal Primary Education.* Mimi nilidhani tunapaswa kuwa na *Universal Secondary Education,* kwa sababu leo hii kijana akiishia darasa la saba tunataka awe ni Mtanzania wa aina gani? Hiyo ilishapitwa na wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushiriki wa walimu hususan katika shule za msingi katika masuala ya uchambuzi na utatuzi wa matatizo mashuleni, kwa sasa mimi nafahamu walimu wa shule za msingi hawashirikishwi kikamilifu katika utatuzi wa matatizo mbalimbali yanayotukabili katika Sekta ya Elimu hususan Elimu ya Msingi. Hawashirikishwi katika mikutano mbalimbali ya kuchambua, kwa mfano, kwenye Mikoa ambayo huwa inaonekana matokeo yake ya Darasa la Saba yanakuwa siyo mazuri, walimu hawashirikishwi katika uchambuzi wa matatizo na ndio maana yale matatizo yanapobainishwa hawaanzi na ubainishaji wa matatizo ya msingi, ambayo upungufu wa walimu kama Mkoa wa Shinyanga una upungufu wa walimu 5000 wa shule za msingi, unatarajia Shinyanga ifanye vizuri kwa namna gani kwa upungufu huu wa walimu wa shule za msingi? Miundombinu ni pungufu, nyenzo nyingine ni pungufu, lakini pia hawapewi motisha. Mwalimu ni vizuri apewe motisha hata kwa kuambiwa tu kwamba, unafanya kazi muhimu sana na ninakuthamini. Hii ingeweza kuwasaidia kuwafanya walimu wetu wafanye kazi vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kumalizia, namuuliza Mheshimiwa Waziri hawa wazabuni ambao wamekuwa wakitoa huduma kwenye shule watalipwa lini hasa maana umetaja kwamba mchakato umeshaupeleka Hazina; lakini tueleze hapa lini sasa

watalipwa maana wapo watu wanadai kuanzia mwaka 2003 kama bwana mmoja anaitwa Weja yuko kule Shinyanga anadai tangu mwaka 2003 hajalipwa hadi leo?

Mheshimiwa Naibu Spika, kule kwangu nina Shule ya Rajan, tumeiombea kibali iwe na kidato cha tano na sita. Sijapata jibu hadi leo. Ningelipenda kupata jibu na naamini nitapata jibu zuri, kwa sababu namfahamu Profesa Maghembe yuko mstari wa mbele katika kuhakikisha kuwa, vijana wetu wanapata elimu stahili na ndiyo maana ameweza kuwasilisha bajeti nzuri na ambayo kwa kuhitimisha, nasema naunga mkono hoja.

**MHE. MARIA I. HEWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi hii ili na mimi niweze kutoa mawili, matatu, kuhusu Hotuba ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi.

Mheshimiwa Naibu Spika, labda nianze tu moja kwa moja kuunga mkono hoja. Pia niendelee kutoa pongezi kubwa katika Wizara hii, kwa Mheshimiwa Waziri, pamoja na Wasaidizi wake, kwa kazi nzuri wanazozifanya ndani ya Wizara hii. Kwa kweli wanafanya kazi moja nzuri. (*Makofi*)

Wizara ya Elimu kuiendesha si lelemama. Mimi ni mtoto wa mwalimu; mama na baba walikuwa walimu, nafahamu jinsi gani wazazi hawa walivyokuwa wakihangaika kuendesha suala zima la elimu. Nilikuwa nawaangalia na nyakati hizo kulikuweko na kuonywa onywa, viboko, unajua kabisa kwamba, elimu ni kazi ngumu kuipata.

Nizidi tu kukipongeza Chama changu cha Mapinduzi, kwa jinsi kilivyoweza kusimamia suala zima la elimu. Kimesimama kidete kabisa kuhakikisha kwamba, walau kwa kila Mtanzania lazima apate elimu kuanzia Chekechea mpaka elimu ya juu. Iwemo pia elimu ya watu wazima. Kwa kweli nakipongeza Chama cha Mapinduzi. *(Makofi*)

Nianze kuliongelea la kwanza; suala la madai ya walimu. Tusichoke na tusichokane Waheshimiwa Wabunge, kulipigia kelele suala hili. Walimu nadhani inataka kufika mahali tuwakatishe tamaa kabisa. Wana mambo mengi ambayo yanaelekea kuwakatisha tamaa. Wana madarasa makubwa, walimu wanakosa nyumba na wana mihangaiko mingi. Bado hata zile haki zao nazo zinacheleweshwa. Ungekuwa wewe ungekuwaje; ungeliishi namna gani; ungelifanya kazi na *morale* ya namna gani? Tufike mahali tukiri kwamba wanachodai ni halali. Jiweke nafasi yao; wewe ungelijifikiria namna gani? Bado tunawaona madarasani kwa uchache wao wanahangaika na watoto wetu, lakini rohoni anajua ninafanya hili lakini ninadai; ni kitu kigumu sana kwa binadamu wa kawaida. Mwalimu anavumilia na anatusomeshea watoto wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hebu tunapozungumza, kwa mfano, katika bajeti yetu tunasema Wizara hii tumeipa kipaumbele hata katika bajeti yetu. Tunaposema sasa tumeipa kipaumbele, pamoja na kuipa kipaumbele si ndiyo tutimize yale yote ambayo yanaisibu Wizara hii ili iweze kuyakamilisha. Hicho ndicho kinachonipelekea kusema hivyo; kuipa Wizara hii kipaumbele na mambo mengine yapewe kipaumbele yaishe.

Ndiyo maana yangu, tuone umuhimu huu wa kuipa ingawa fedha hazikidhi, lakini tushughulike na yale ambayo yanapaswa kumalizika.

Moja la muhimu ni mtu kumlipa haki zake. Hiyo ni haki yake mwalimu kuipata na wala siyo ya kusema tuzungumzie pembeni. Tuone tu na bahati nzuri Mheshimiwa Profesa Maghembe amesema, mambo yote yamekwenda vizuri na yanakaribia kumalizika na kwamba, yanasubiri yako katika dakika za mwisho yaishe. Wizara inakiri kwamba, ilipeleka timu mbalimbali kwenye Mikoa, wamefanya uchunguzi, wana orodha na bahati mbaya sana wakaawahidi mpaka mwezi wa sita au wa saba mambo yatakamilika. Watu hawa wana matumaini, kwa hiyo, niombe Wizara ilishupalie suala hili walimu walipwe haki zao. *(Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo ningelipenda nilizungumzie ni suala la wanafunzi wa kike kupewa mimba wakiwa shule ya msingi. Eeh Mungu jamani! Mimi sina kumbukumbu sahihi, lakini nadhani niko sahihi, wakati nasoma shule ya msingi darasa la kwanza mpaka la nne sikuona mtoto tunayesoma naye akiwa na mimba. Shule hizi zilikuwa mbali sana na wazazi walio wengi, pamoja na kwamba humu katika taarifa tunaambiwa kwamba, watoto wanapata mimba kwa sababu ya umbali wa shule wanakosoma. Watoto walikuwa wanatoka nyumbani kwenda shule kilimo 5 hadi 10, mtoto anakwenda shule ya msingi lakini anamaliza mpaka darasa la nne. Kutoka darasa la tano mpaka la nane wakati ule mimi nasoma, nilikuwa natoka Geita nakwenda kusoma Shinyanga mbona sikunasa mimba hapa katikati? *(Makofi*)

Leo tunatoa sababu lukuki, shule ziko mbali na wakati shule ziko kwenye Kata. Sababu nyingi tu zinatolewa hapana! Kuna sababu nyingine za kuzungumzia. Kama zipo basi ziandamane na adhabu kali ili hawa watoto waweze kumaliza shule. Mtoto wa darasa la nne anapata mimba; hivi kama siyo ubakaji ni nini? Wote wale ambao wanafanya hivyo, waelewe kwamba hawapewi mimba kwa hiari yao wanabakwa. Kama ni adhabu itakuja ijadiliwe na mjue Muswada unakuja wa Haki za Watoto. Labda hili nalo tulipigie mbiu mapema, liandikwe vipi ndani ya Muswada huu wa kumpa mimba mtoto wa kuanzia darasa la nne, la tano, la sita au la saba. Hapana; ni mbaya hii jamani. Ndiyo maana inafika mahali tunataka kuona aibu sisi wenyewe, tunapigia kelele sisi wenyewe, hawa watoto warudi na kweli warudi wasome. Atakapomaliza darasa la nne anakwenda kuzaa, baadaye inakuwaje?

Ningeliomba twende nalo hili kwa msimamo huo kama nchi nyingine zilivyoweka msimamo. Watoto hawa warudi, maana watakaporudi watang'ang'ana na watoto wao baadaye iweje? Aache mtoto arudi akasome, lakini adhabu imuandame huyu ambaye atamtaja au atakayebainika kumpa mimba mtoto mdogo, aweze kushughulikiwa ipasavyo na Muswada uje na msimamo wa namna hiyo wa kutoa adhabu kwa wale wote ambao wanakaa wanashughulika na watoto wadogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mke wa Rais, Mama Salma Kikwete, anapiga kelele sana kuhusu mimba za utotoni. Mpaka sijui hatumwonei huruma! Juzi tulikuwa naye ziarani Mwanza, anapiga kelele mama wa watu mpaka unamhurumia. Anasema mtoto wa mwenzio ni wako. Sijui wengine nadhani kiroho roho wanasema mtoto wa mwenzio ni

mkubwa tu ni wangu. Sijui kuna usiri gani unaozungumzwa humo ndani. Kwa nini hatuheshimu kauli yake huyu mama. Mama huyu jamani anahangaika kweli, anawahurumia watoto hawa wa taifa analoliongoza! Tuombe tufike mahali tuache tabia hii na kuona kwamba, hawa watoto ni stahili yao ya kusoma na wasome mpaka wafike Vyuo Vikuu ambavyo tunavisifu vinaongezeka, vitakuwa vya wavulana tu. Vinahitaji mchanganyiko, hamsini hamsini na wasichana waingie huko wasome. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, napenda kuzungumzia suala la walimu wa sayansi; hali ni mbaya. Hebu tufike mahali, siwezi kurudia masuala ya wenzangu, tuwe na shule ziweze kupeleka wanafunzi wenye vipaji, wenye uwezo wa kuweza kusoma baadaye wawe walimu wazuri wa kufundisha masomo ya sayansi. Tutakuwa na ulimwengu wa *art* tu Tanzania nzima, wanaosoma *art* watupu. Sijawahi kuona taifa la namna hiyo. Kwa hiyo, tuone umuhimu wa suala zima la kupata walimu wazuri, wenye kufundisha sayansi. (*Makofi*)

Tunaongelea maabara, tunasema shule zitakapokuwa zikijengwa na maabara zijengwe. Serikali nayo inajenga maabara. Hili mlibebe, tusifike mahali tukajenga tena shule zikawa uyoga, zisizokuwa na maabara eti Serikali imeshindwa. Tutakemea Serikali kama itafikia hatua hiyo, wananchi wakakubali wakajenga shule halafu eti Serikali huku nyuma ijivute ije ituambie bajeti haikukidhi hatutapokea, kama kweli tutakuja kukubaliana hili pendekezo likikubalika na Serikali mlibebee bango kikweli isije ikafika mahali Serikali yenyewe ikawa ndiyo kikwazo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, napenda niweze kumalizia tu suala zima la nyaraka za Serikali za Elimu ziandikwe Kiswahili. Naomba kuunga mkono hoja hii. Ahsante. *(Makofi)*

**MHE. BENSON M. MPESYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, naomba nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii. Naomba kupitia Bunge lako Tukufu, nikushukuru sana kwa uamuzi makini ulioufanya wa kutuongezea siku, vinginevyo tusingepata nafasi hii ya kuchangia, mimi nikiwa mmojawapo. Hata hivyo, tusingekuwa tumeitendea haki nchi hii, kwa sababu Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, ndiyo hasa ambayo inaongoza katika bajeti. Kuipatia fedha nyingi kiasi hicho halafu tusipate nafasi ya kuzizungumzia na kuelekeza na kushauri, tungekuwa tunawakosea Watanzania makosa makubwa sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa busara yako, umeokoa jahazi hili. Tunakushukuru sana uendelee na busara hiyo. *(Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitumie nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Manaibu Waziri wote wawili, Katibu Mkuu, Maprofesa wa Vyuo Vikuu, pamoja na Walimu wote nchini, kwa kazi nzuri wanayofanya ya kutoa elimu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la elimu ni zito sana. Tukitanguliza elimu mbele, haya mengine yote yatafuata na ndiyo hata Serikali inasema lazima elimu tuipe kipaumbele kwa mtindo wa bajeti. Kama elimu hii hatutaisimamia, itakuwa ni fujo katika

nchi. Kwa kweli Wizara hii sasa imekuwa ni pana na kubwa na ni Wizara yenye *manpower* kubwa sana, inahitaji mipango ambayo ni kamili, inahitaji mipango ambayo ni ya uhakika ili uweze kufanya kazi. Ninaamini ni moja kati ya Wizara ambazo ni kubwa sana. Kwa hiyo, sina sababu ya kuwaonea wivu Waheshimiwa Mawaziri hawa. Ninawaombea Mungu awazidishie, awape afya njema, waweze kutekeleza majukumu ya kutupatia Watanzania elimu na mambo mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika suala zima la usimamizi wa elimu, lipo suala hili la *DEOs* na *REOs;* watu hawa toka sisi tunasoma ni watu muhimu sana. Wao ni kiungo kati ya Wizara na shule na walimu. Hawa ni watu ambao tunatakiwa tuwaangalie vizuri sana kwa upande wa maslahi, kwa upande wa uwajibikaji na kwa upande wa vyombo vya usafiri. Hivi karibuni Wizara imefanya kazi nzuri sana ya kuteua baadhi ya *DEOs*. Kwanza, *DEO* au *REO* lazima awe ni mwalimu aliyebobea katika taaluma ya ualimu, anayeujua ualimu siyo mbabaishaji. Katika maeneo mengine, hawa walioteuliwa, watu wakubwa kama hao *DEOs, REOs,* hawana ofisi mpaka sasa hivi. Wanahangaika tu kwenye *corridor* za Halmashauri zetu. Nilikuwa naomba Mheshimiwa Waziri, uwaagize hawa wapatiwe ofisi. Hawawezi ku-*coordinate* masuala ya elimu, hasa katika kipindi hiki ambacho tumejenga shule nyingi za sekondari katika Kata wakiwa kwenye *corridor*. Naomba hili tuliangalie na ninyi kama makamisaa wa elimu, mnapaswa kuhakikisha kwamba, viwango havikiukwi na Halmashauri yoyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nizungumze hili ambalo ni la kwenu, nimegundua ni bahati mbaya sana nilikuwa kwenye kikao cha *RCC,* nikabahatika kuokota *salary slip* ya mwalimu mmoja *senior,* lakini ni *REO* na moja kati ya kazi alizopewa ni ku-*coordinate* na kuwasimamia *DEOs;* inakuwaje *DEO* ana mshahara mkubwa kuliko *REO* kama si *insubordination* ni nini? Mnamtegemea huyu *REO* akamsimamie *DEO? REO* wa kwangu mshahara haujavuka shilingi 500,000, vitu vya ajabu katika nchi mnavyovifanya. Akamsimamie *DEO* mwenye mshahara wa shilingi 1,260,000; hivi kinachompa nguvu na ujasiri huyu *REO* wa kumsimamia *DEO* huyu ni kitu gani? Maana jambo hili ni *very serious* na mimi ni mwalimu tena mwalimu niliyebobea nimesoma miaka minane ualimu tu.

Tunafanya nini; huku ni kuiua elimu. Huyu *REO* hawezi hata siku moja, hata kama atazungumza lakini huyu hatamsikiliza. Anakwambia kwanza huyu *junior* tu, angalia mshahara wake na mimi napata kiasi gani. Sasa tusifike mahali tukasema kwa sababu ya Wizara ya Utumishi ni nani sasa anayetakiwa ku-*coordinate* kuhakikisha utumishi hawafanyi makosa kama haya. Ninaomba jambo hili lirekebishwe haraka sana. Si vyema kabisa, vinginevyo tutakuwa tunawapaka mafuta kwa mgongo wa chupa. Unamwita *REO* lakini kwa hali halisi umemnyang'anya madaraka hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeona nilizungumze hili ili tuwekane sawa. Lingine, mimi nina wasiwasi na ninawaonea huruma walimu wenzangu, ambao mmepewa dhamana ya Wizara hii. Inaonekana katika Wizara hii, kuna kitu ambacho ni kama *passive resistance* ya namna fulani ya kutotenda mambo, sijui kuyasukuma. Mwaka jana wakati nachangia, nilizungumza hapa matatizo ya Shule ya Sekondari ya Iyunga. Shule ambayo ni moja kati ya shule kubwa, imefundisha watu wengi sana

akiwepo DeClark, aliyewahi kuwa Waziri Mkuu wa *South Africa,* amesoma pale Iyunga. Wakati wa kujibiwa uliniambia masuala ya vitabu, masuala ya maktaba yote kwa Shule ya Sekondari ya Iyunga yatatekelezwa. *(Makofi*)

Mbali na hilo, wazabuni kutolipwa kama alivyosema mwenzangu Mheshimiwa Dkt. Mlingwa pale, bado kuna masuala ya *utilities*. Tarehe 5 nilibahatika kwenye mbio za mwenge na bahati nzuri mwenge tuliupokelea pale Wilayani kwangu Mbeya Mjini, nikashuhudia jambo ambalo naomba ni-*share* na wewe, limekuja gari la *TANESCO* kutaka kukata umeme pale Iyunga Secondary, wale watoto wameji-*mobilize* kutaka kulichoma lile gari. Thamani ya gari lile haipungui shilingi milioni 300, imetokea fujo kubwa mno wanasema tumechoka hatutaki umeme ukatwe hapa, hatutaki maji yaondoke hapa. Mnajua wale ni watoto. Suala hili sasa lina mwaka mzima, wanadaiwa shilingi milioni 14 za umeme. Wanadaiwa shilingi milioni 17 za maji. Jumla shilingi milioni 31. Nilijaribu kuzungumza na mwalimu mwenzangu Mheshimiwa Mahiza, akanieleza matatizo yaliyopo na sababu ambazo zinawakwamisha. Mimi nazungumza ni nani mwenye jukumu la kumwambia Mheshimiwa Ngeleja, Waziri wa Nishati na Madini, umeme pale Iyunga Sekondari usikatwe? Ni nani mwenye jukumu la kumwambia Mheshimiwa Profesa Mwandosya maji yasikatwe pale? Ninafikiri ni mambo ya *coordination* tu. Hata kama zile fedha zinatakiwa zitolewe moja kwa moja kutoka Hazina kwenda moja kwa moja kwenye shule, lakini ni nani anafuatilia; nani amepewa jukumu hilo? Wale watoto wamenisomea risala wakasema, sasa tumefika mahali tumechoka. *Disturbance* hizi zinatuharibia taaluma yetu; kwa nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa nafikiri kwamba, hata hii hoja ya kusema tunakamata mshahara wa Waziri ni kuwaonea tu. Nilikuwa napendekeza, kisheria turuhusiwe kukamata magari ya Waheshimiwa Mawaziri ili kulipia hizi kasoro ndogo ndogo. Kwa nchi kama hii, tunashindwa tunaacha watoto wanalala kwenye giza wanahangaika kwa ajili ya shilingi milioni 31! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, namtaka Waziri wangu aseme neno tu, vijana wale wa Iyunga wajisikie kweli hawakufanya makosa kumpata Mbunge kama mimi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Waziri aseme neno roho yangu ipate kupona, aninusuru na jinamizi linalokuja mwakani. *(Makofi/Kicheko)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri ukitoka huna gari. *(Kicheko)*

**MHE. BENSON M. MPESYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, niingie sasa juu ya Chuo changu Kikuu Huria cha Tanzania. Bunge hili Tukufu lilinipa dhamana na heshima ya kuwa mwakilishi katika baraza lile. Ninaomba kwa uchungu mkubwa sana, kwanza, nimpongeze Makamu Mkuu wa Chuo, pamoja na Wataalamu wote wanajitahidi sana kufanya kazi. Hawa watu kama tunavyojua, *nature* ya Chuo Kikuu Huria inategemea walimu wa kutoka sehemu nyingine waje wakufundishie watoto wako, waje wafanye kazi ya kuwafundisha wanachuo wako, lakini wanategemea *OC* katika kuwalipa walimu wa *part time*, jambo ambalo tuliko-*copy* mawazo haya *South Africa;* Uingereza na India hakuna kitu kama hicho. Serikali inatakiwa itenge fedha kama *personal emolument* au

inakuwa na fungu ambalo linakuwa *ring first,* kwa ajili ya kuwalipa walimu hawa wa *part time*. Matokeo yake walimu hawa wanakaa na *script* wanamwambia VC sikupi hizi *script* mpaka na unilipe hela yangu uliyonayo.

Hawa *Open University* mpaka hivi sasa wamedahili zaidi ya wanachuo 26,000, wanafanya kazi kubwa sana katika taifa kama hili lenye njaa ya elimu. Kwa nini tunawaacha wanakwenda kama watu wasiokuwa na baba, kama chuo ambacho hakina mwenyewe. Kana kwamba, haitoshi mwaka 2001/2002, OC yao ilikuwa juu zaidi, wakati huo walikuwa na wanachuo pungufu ya 8,000, leo hii wanachuo 26,000; imepungua kuliko ile ya 2001/2002. Tunafanya nini? Matokeo yake sasa ni kuleta *chaos* katika elimu na katika nchi. Juzi hapa wamekuja walimu wa Mpwapwa, wamepigwa mabomu, wanataka kufanya fujo, jambo ambalo mimi ninasema ni la kuidhalilisha taaluma ya ualimu.

Nakumbuka mimi na mwenzangu Mheshimiwa Beatrice, tumekwenda kumwambia Mheshimiwa Waziri matatizo haya. Tumekwenda kwa Waziri wa Fedha tukamweleza matatizo haya. Leo walimu wale wa Mpwapwa wanakuja Bungeni, kwa sababu wanajua hakuna mtu mwingine wa kuwatetea zaidi ya Bunge. Halafu sisi tunaamrisha wapigwe mabomu walimu hawa. Kwa nini tunawafanya hivi walimu? Walimu wamewakosea nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, ni nani ambaye amefika hapa bila taaluma ya ualimu? Profesa gani amefika hapa bila mwalimu? Mkumbuke mwalimu wako aliyekufundisha darasa la pili, hata Iddi Amini, hata madikteta wamefika kwenye udikteta ule kwa sababu ya walimu. Kwa nini tunaidhalilisha taaluma ya ualimu? Walimu wanajiona ni wanyonge katika nchi yao na naomba muwaombe radhi wale walimu wa Mpwapwa, mmliokuja kuwapiga mabomu hapa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi kama mwalimu mwenzenu, nimesikitika sana, wamechukua hatua zote na wawakilishi wao wamechukua hatua za kufuatilia mmebaki maneno tu, tuingie katika utendaji sasa. Tumkamate mtu anayekwamisha tumchukulie hatua. Pamoja na hayo yote, ninaunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Sasa nitamwita Mheshimiwa Anna Lupembe na msemaji wetu wa mwisho atakuwa Mheshimiwa Stephen Galinoma.

**MHE. ANNA R. LUPEMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kutoa mchango wangu katika Wizara ya Elimu. Kwanza kabisa, naomba nimpongeze Waziri, pamoja na Naibu Mawaziri, kwa hotuba nzuri waliyotupatia katika Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Sasa hivi tunakwenda kwenye Kilimo Kwanza. Mimi nimesoma shule ya sekondari yenye mchepuo wa kilimo kuanzia *form one* mpaka *form four*. Cha kushangaza, sasa hivi sioni shule yoyote ya sekondari ambayo ina mchepuo wa kilimo. Kipindi cha nyuma kulikuwa na mchepuo wa kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba Serikali kama wametoa mchepuo wa kilimo, waurudishe kutokana na hali ya sasa hivi tuna Shule nyingi za Kata ambazo zilijengwa zinataka mambo mengi. Inatakiwa kuwe na kilimo, sayansi na *art*. Ninaomba Shule za Kata ambazo zimejengwa, basi baadhi ziwe na mchepuo wa kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakuja kwenye suala lingine kuhusu madeni ya walimu. Wabunge wengi wamezungumzia masuala ya walimu kuhusu madeni yao. Inasikitisha walimu tumewaweka kama vile watoto yatima. Tukikumbika kama huyu mwalimu ndiyo aliyetufundisha mpaka sasa hivi tuko Bungeni, leo hii tunamtelekeza kama mtoto yatima, kusema kweli Serikali haiwatendei haki walimu. Hata kile kipindi cha bajeti, nilizungumzia sana kuhusu suala la walimu. Matatizo yote na mengi anayo mwalimu, mwalimu ndiye anayeishi vijijini sana, kwenye remote area ndiyo unamkuta, porini unamkuta na mshahara wake ni shida. Anatoka porini saa nyingine anatembea kilomita 10 au 20 mpaka afike katika kijiji au Kata na atoke pale aende kufuata mshahara wake katika Wilaya, napo bado ni matatizo, tunampa shida ndani ya madeni yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, je, ni nani ambaye atakubali kuishi porini huko? Vile vile tuwashukuru hawa walimu, wana roho ya imani, wanaipenda Serikali yao, ni wavumilivu; sasa Serikali ichukue jukumu walimu wanaofanya katika nchi yetu tuwatendee haki yao, tuwalipe madeni yao. Vile vile Serikali ipange mikakati, ione kama huyu mwalimu anatakiwa na mshahara wake apelekewe shuleni. Bajeti iliyopita nilisema, mwalimu nusu ya mshahara wake anautumia kwa nauli, pamoja na hoteli au guest na chakula kwenda kufuata mshahara wake. Ina maana anapata nusu mshahara. Sasa Serikali ijipange kumwona mwalimu ni kioo cha Taifa hili, maana yake hamna mtu mwingine. Watu wote hata Profesa, Mkurugenzi wa nini, aliyekufundisha wewe ni mwalimu, ndiyo maana amekupa sura ukaonekana kuwa wewe ni Mkurugenzi katika sehemu mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, basi tumtambue huyu mwalimu, tumjali, madeni wanayodai Serikali ilipe na sasa hivi ifanye mikakati ya kumpelekea huyu mwalimu mshahara au waweke posho maalumu ya kumpa huyu mwalimu anayekwenda kufuata mishahara katika Mawilaya mbalimbali. Tuna madeni ya wazabuni, inasikitisha kwenye shule zetu za *boarding*.

Wale watoto mpaka sasa hivi wanakula chakula cha madeni, ina maana wale wazabuni wakisema kuwa basi hatupeleki chakula ndani ya mashule yetu ya Serikali ya *Boarding*, wale watoto wa shule wamekosa elimu. Tunakwenda wapi? Tutafika wapi? Utakuta mzabuni mwingine sasa hivi anadai mpaka shilingi milioni 200, shilingi milioni 300 zimefikaje mpaka kimefika kiwango kikubwa namna hiyo? Kila siku Bunge linapitisha bajeti? Ninaomba Serikali ijipange vizuri maana unakuta saa nyingine, shule zinafungwa wanasema tumekosa chakula; mtakosaje chakula? Ninaomba Serikali ijipange vizuri, haya madeni ya wazabuni yalipwe ili wale watoto wasome kwa amani. Kuna Mbunge aliyepita sasa hivi amesema kuhusu umeme na maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, *Mpanda Girls* walikata umeme na maji kutokana na madeni hayalipwi. Sasa tunaomba Serikali, ili kuwaweka hawa watoto waweze kusoma vizuri na kwa amani, walipe hayo madeni. Katika shule tunaweza kujenga labda nyumba 2/3 lakini tunasahau saa nyingine ile shule ina walimu 10 -15. Wale walimu wanakaa mitaani, walimu wengine wanapata matatizo. Hao wa mjini, shida kubwa iko vijijini. Kuna masikitiko makubwa, utamkuta mwalimu anakaa kwenye nyumba ya nyasi, anatoka pale anakwenda kufundisha. Mazingira anayokutana nayo mwalimu kweli atakuwa na morale ya kufundisha watoto? Hawezi kuwa na morale, tunaomba Serikali ijipange vizuri; walimu wajengewe nyumba, inaweza ikajengwa nyumba kubwa yenye vyumba 15 kila mwalimu akapewa chumba kimoja kimoja. Walimu wengi wanashindwa kukaa vijijini kwa kuwa hawana sehemu ya kuishi. Akienda kuoneshwa porini, anaambiwa shule hii hapa ufundishe, nyumba hii hapa ya nyasi; labda yule mtoto amelelewa vizuri kuanzia kwa wazazi wake unampeleka kwenye nyumba ya nyasi atoke pale aende kufundisha darasani; atafundisha kweli? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba Wizara iweke mazingira mazuri katika nyumba za walimu za vijijini. Mawilayani na Mikoani, *at least* kuna nyumba za kupanga nzuri, walimu wanaweza kujikimu huko, lakini tatizo kubwa liko vijijini. Tunaomba Wizara ijipange vizuri, kuna walimu walioajiriwa Julai, 2008, wamekaa mwaka mzima hawajapata mishahara yao wala hawajaingizwa kwenye *pay roll*. Tunategemea hawa walimu watafundisha vizuri kweli? Mwalimu huyo tumemwajiri ndio kwanza anaanza maisha, tunaweka mshahara wake hatumlipi mwaka mzima, tunategemea yule mtu tuliyemwajiri atakula nini; atavaa nini; au ile nyumba ambayo amepanga atalipa nini? Ninaomba Serikali ijipange vizuri walimu wa *primary* wakienda kuripoti tuwaweke kwenye *pay roll* kabisa kwa ajili kule Wizarani. Tunajua walimu wangapi wanakwenda sehemu fulani, wawekeni kabisa kwenye *pay rolls,* wakitoka pale wanajulikana yule mwalimu amekwenda sehemu fulani mshahara wake moja kwa moja analipwa kuliko tunampeleka mwalimu halafu tunamwacha mwaka mzima hapati mshahara wake. Tunaomba Wizara kama Wizara, ichukue jukumu la kuwalipa walimu wapya mishahara haraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo lingine ni kupandishwa vyeo. Walimu wamesahaulika kabisa kupandishwa vyeo vyao; tunategemea nini? Matokeo yake matatizo yanakuwa mengi, mazito na makubwa, tukija kupandisha vyeo kwa pamoja yule mwalimu sasa anadai malikimbizo yake tunashindwa kumlipa. Tunaiomba Serikali, mwalimu kama ana haki ya kupandishwa cheo basi apandishwe ili mshahara wake au yale malimbikizo yake yapatikane mapema iwezekanavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niipongeze Serikali sasa hivi inachukua jukumu la kila mwaka kupeleka walimu maeneo mbalimbali na sasa hivi walimu wameshakwenda kuripoti. Walimu wa *primary* kila wilaya bado hawatoshi, tunaomba jitihada hizo zifanyike kwa bidii zaidi. Kuna uhaba wa walimu wa sekondari kwenye Shule nyingi za Kata, sehemu mbalimbali unakuta shule moja ina walimu wawili, sasa matokeo yake Mwalimu Mkuu wa ile shule akimkuta labda kijijini pale amekwenda kijana amemaliza *form six* au *form four,* ana uelewa kidogo, wana tabia ya kuwachukua

kwa muda. Sasa wale wanaochukuliwa kwa muda, zile hela zinatoka kwa wazazi, ina maana kuwa yule mwalimu anawaita wazazi wamchangie yule mwalimu wa muda.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa unakuta tatizo wazazi wanasema huyu mwalimu hii ni Shule ya Serikali sisi kama wazazi tunamlipia wa nini? Kuna wengine wanaelewa lakini wengine hawaelewi, sasa inakuwa tatizo. Vilevile yule mwalimu anakuwa wa muda maana yake anasubiri kipindi kikifika akipata *post* yake ya kwenda Chuo Kikuu anaondoka, tatizo linakuwa lile lile. Ninaomba Wizara kama Wizara, mfanye tathmini katika shule mbalimbali, kuna shule ambazo zinachukua walimu hao wa muda, muwawekee fungu lao mpeleke katika Shule za Kata ili wale walimu wa muda wanaokwenda kufundisha katika shule zile wapewe posho, maana wanapewa posho. Ninaomba Serikali ijipange vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa siku ya leo naomba niishie hapa, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**MHE. MOHAMED H. MISSANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuomba mwongozo wako kwamba, asubuhi nilikuwa na udhuru nilikwenda hospitali, moja ya wachangiaji waliochangia hapa asubuhi, walichukua nafasi ya Mheshimiwa Waziri kujibu hoja ambazo mimi niliwasilisha jana, ndani yake ni suala la Baraza la Mitihani. Sasa ningependa kujua Kanuni gani ambayo inatumika, Mbunge kumjibu Mbunge mwenzake wakati hiyo ni kazi ya Serikali na ni kwamba, unajua bahati mbaya wenzetu hawa ambao walikuwa Mawaziri halafu wakaondoka, wanajisahau wanafikiri bado Mawaziri mpaka leo. *(Kicheko)*

Ninachoomba ni mwongozo wako kwamba; je, ukiachia utaratibu huu wa Mbunge kumjibu Mbunge mwenzake; kwanza ni utaratibu halafu Serikali itakuwa inafanya nini? La pili, Hansard hii hapa, katika aliyoyasema mengi ni uwongo, kwa mfano, katika mchango wangu mimi sijasema kabisa katika wale waliotimuliwa wako watu wa kutoka Wilaya ya Singida au Jimboni kwangu. Naomba uchukue Hansard, hakuna *statement* kama hiyo, lakini yeye kasema nimetetea kwa sababu ...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa, mbona sijakupa mwongozo maana umesema mwongozo, lakini sasa unajadili! Swali lako ni kwamba, Mbunge anaweza kumjibu Mbunge mwenzake, ndiyo unachohitaji mwongozo hayo mengine unajadili.

Sasa tuseme hivi; Waheshimiwa Wabunge, nafikiri hata Spika wakati mwingine huwa anasema hapa mkiingia kwa udani sana, nani anamsema nani mtakuta mnachuana. Tuzungumzie *issues*, tukizungumzia *issue* utakuta mnajadili tu ndiyo maana ya mjadala na mtu asi-*personalise* kitu kwamba inaposemwa, anasemwa yeye kwa sababu mkifanya hivyo mtapata shida sana kuzungumza. Utakuta mtu mwingine anajua kitu zaidi kuliko mwenzake, sasa tuzungumzie *issues* na kutoa hoja zinazokuwa na uzito zaidi. Ile hatua ya pili ya Mheshimiwa Missanga ya kwamba, sikusema hivyo; hilo ni suala lingine.

Kuhusu mwongozo ni kwamba, tunapojadili hapa msi-*personalise* zaidi, chukueni *issues*, mkichukua *issues* mtakuta kwamba mnajadili. Kuna mtu mwingine

anajua zaidi kuliko mwingine, pengine hata Waziri mwenyewe hajui. *In fact,* hiyo naweza kusema kwamba, kuhusu taarifa pia inaweza kutolewa pale, unaweza kusema kuhusu taarifa ukasema unajua jambo fulani, kuliko pengine unavyoeleza wewe. Kwa hiyo, haina tatizo katika kujadili sasa ukweli wa taarifa hiyo. Naomba ije kwa utaratibu mwingine. Kuhusu ukweli wa nini kilichosemwa, naomba uje kwa utaratibu mwingine. Nilimwambia mtu fulani, Kanuni ya 50 inatosha kuhusu usahihi wa taarifa. Sasa naomba tuendele. Namwita Mheshimiwa Galinoma.

**MHE. STEPHEN J. GALINOMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, nakushukuru wewe kwa kunipa nafasi ya kuzungumza. Pili, napenda nichukue nafasi ya mwanzo kabisa, kuipongeza Wizara hii, kwa kazi nzuri inayofanyika. Nawapongeza Waziri, Naibu Mawaziri wake, Katibu Mkuu na Timu zao zote na ili nisibabaike mwisho itakapolia kengele, naomba nitamke wazi kwamba, nitaunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema, Wizara hii imefanya kazi nzuri na hotuba yao ni nzuri. Napenda niwapongeze sana, lakini kuna mambo fulani fulani ni vizuri kuyachangia kimawazo. Ni hulka ya binadamu katika mambo kumi kwa mfano, yakafanyika vizuri yote isipokuwa moja. Hili moja ndilo litakalovuma zaidi. Sasa Wizara hii imefanya kazi nzuri katika maeneo mengi. Wengi wamezungumza mambo ya maendeleo ya shule za sekondari na kadhalika katika maeneo yao, hata kwangu ni hivyo hivyo na nikizungumzia hili itakuwa kama narudia. Sasa ninachosema ni kwamba, licha ya kazi nzuri iliyofanyika, kuna mambo fulani fulani, hasa nazingatia mambo mawili ambayo nadhani siyo mazuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, la kwanza, ambalo wamelizungumzia wenzangu ni uvujaji wa mitihani. Wamelizungumzia Wabunge wengi na mimi nisingependa kupoteza wakati kulizungumzia hilo. Labda tu nitaje kwamba, katika mazingira ya nchi nyingine, kosa au upungufu kama huo, ungestahili yule ambaye anahusika kuwajibika au kuwajibishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili kubwa ambalo ni kosa na udhaifu mkubwa sana katika Wizara hii, pia limezungumzwa na wenzangu nalo ni urasimu. Urasimu ambao si kosa la Wizara labda ni matatizo ya jiografia ya nchi yetu kwamba, kwa sababu ya ukubwa wa nchi hii na mifumo tuliyonayo, imekuwa vigumu ku-*process* madai ya walimu na wazabuni kwa wakati ikafika mahali yakalimbikizana kwa kiwango ambacho Waziri mwenyewe ametuambia katika hotuba yake. Hilo limesababisha hali ngumu sana katika Taifa hili; kama unavyojua kumekuwa na migomo isiyokwisha ya walimu, wazabuni na hata katika ngazi nyingine za elimu hadi Chuo Kikuu na kadhalika, zaidi ni kwa sababu ya vyombo hivi havikutekeleza kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nitachagia suala moja tu, kwa sababu lina maelezo marefu kidogo, nisingependa kuingia somo lingine. Nizungumzie habari ya urasimu; kama nilivyosema urasimu ndiyo uliosababisha mambo haya yote ya migomo na kadhalika, kiasa kwamba hivi tunavyozungumza, ninafahamu kwamba, kuna mgomo umewekwa kiporo kwa kuweka pingamizi la Mahakama. Sasa kwa nini imetokea hivi;

sote tunajua. Jambo ambalo napenda kulizungumzia ni kule kugatua madaraka juu ya mambo haya ya elimu *in particular* kwa Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kimsingi, naona ni jambo zuri na linajibu tatizo hili la urasimu, kwa sababu kwa njia hiyo tutaweza kutumia mchakato, tukapeleka madai kama ni ya walimu au wazabuni katika sehemu zinazohusika na majawabu yakapatikana. Vile vile ili tuelewe zaidi juu ya kazi hii, ugatuaji huu utakavyofanya kazi kwa elimu ya sekondari kwenda Wilayani, ningependa tulitazame kwa makini zaidi na katika kulitazama nilipenda nianze na Wizara yenyewe. Bila shaka, wanaelemewa kwa sababu walimu ni wengi, kwa hiyo na madai ni mengi. Vile vile wazabuni, ni kweli shule nyingi na kwa hiyo hawakuwa na utaratibu wa kuhakikisha kwamba mambo haya yanafanyika kwa wakati wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vizuri Serikali au tuseme Wizara katika kugatua, nasikia ni jina la siku hizi la kupeleka madaraka Mikoani. Katika kupeleka madaraka huko Mikoani au Wilayani ni vizuri yaende pamoja na rasilimali zote za fedha, watu na kadhalika. Kwa maana hiyo, kwa kuwa Wizara hii itapunguziwa kazi, nadhani wataalamu waliokuwa wakishughulikia au tuseme wanaoshughulikia suala hili pale Wizarani, itabidi wafuate au waende na hayo majukumu huko Wilayani. Nimebahatika kuona makubaliano kati ya TAMISEMI na Wizara ya Elimu, kuhusu mgawanyo wa madaraka katika ngazi mbalimbali. Mkoani, yaani REO, ana kazi zake zimeainishwa pale lakini jambo ambalo linajitokeza kwa nguvu sna ambalo nafurahi kwamba, angalau kuna Wabunge wawili wamelisemea, pale ambapo unamkuta DEO ana mshahara mkubwa zaidi kuliko REO, DEO anapata shilingi 1,230,000, hii ni scale ya TGST I, ambapo REO wake anapata *scale* ya chini zaidi na kwa hiyo italeta mara moja tatizo la nidhamu. Wewe fikiria, una mshahara mdogo; REO utamsimamiaje DEO wako mwenye mshahara karibu mara mbili ya mshahara wako? Hii nafikiri ni lazima irekebishwe, vinginevyo ni kama tu kuhamisha vurugu zinazotokea sasa hivi kutoka *center* kwenda Mikoani. Hilo ni tatizo moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la pili ninaloliona, REO si rahisi kuweka *focus* katika suala la *secondary schools* Wilayani kama mfumo wa Mkoani hautabadilika. Kule Mkoani kuna kitu zamani kilikuwa kinaitwa *cluster* na sasa kimebadilishwa kinaitwa *sector*. Huu ni mkusanyiko wa idara mbalimbali chini ya *Assistant* RAS mmojawapo na sasa hivi REO amewekwa pamoja na Bwana Afya au tuseme *Regional Medical Officer*, nadhani na idara mbili, tatu nyingine. Hawa maana yake ni kwamba, hakutakuwa na *focus* ya huyo REO kufanya usimamizi wa shule za sekondari kama anavyotakiwa. Kwa hiyo, ningeshauri kwamba, mfumo huo ubadilishwe ili RAO awe peke yake kama ilivyokuwa zamani na kama ilivyokusudiwa katika Sheria inazozitawala kazi za REO, yaani Sheria Namba 25 ya Mwaka 1978.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maana hiyo, mimi nashauri REOs wapandishwe vyeo vyao au tuseme mishahara yao waweze kuwaongoza vizuri DEOs. Hapa niseme kule Mkoni REO asichanganywe na Regional Medical Officer na hapo hapo ningependekeza kwa nguvu sana kwamba, utaratibu uliopo sasa wa mitihani urekebishwe kusiwe na uvujaji wa mitihani.

Serikali za Mitaa ambazo ndizo zinapelekewa hili jukumu, sipendi nifikiri kwamba ni suala la Mnyamwezi kupewa mzigo mzito, baada ya kushindikana huku juu sasa tunaona afadhali Mnyamwezi aende akauchukue. Mimi nafikiri liko tatizo kwa sababu Serikali za Mitaa jinsi zilivyo sasa hivi ni tegemezi kwa Serikali kwa ruzuku ya asilimia 90 – 98. Kwa hiyo, kama ugatuaji huu hautaandamana na ugatuaji wa rasilimali fedha, rasilimali watu, Serikali za Mitaa zitapata shida sana. Kwa hiyo, nadhani kwa kuwa kengelele ya kwanza imeshalia na sijafika popote, niseme tu kwamba, nimekwishaandika. Wakati fulani nilikata tamaa kwamba pengine sitapewa nafasi ya kuzungumza, kwa hiyo, nilikwishaandika mambo si haya tu lakini mengi mengine na nimeshaleta. Natumaini yataingia katika mchango wangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nisisitize sana suala la urasimu kwa sababu kama nilivyosema, ndiyo uliosababisha mambo haya magumu tunayoyaona sasa na ndiyo haya tunayojaribu kuyakimbia kule center. Ili ugatuaji uwe na maana ni vizuri Serikali ihakikishe kwamba, tunakopeleka majukumu haya tunafanya mambo vizuri, vinginevyo itakuwa ni kusambaza matatizo ambayo tayari tumekwishayashuhudia.

Kwa maneno hayo machache, naunga mkono hoja kabla kengele haijalia. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Galinoma.

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. MARIAM REUBEN KASEMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua nafasi hii, kuleta mawazo na mchango wangu kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, elimu ni ufunguo wa maisha na ni haki ya kila mtu kupata elimu hiyo na itakuwa imesaidia sana endapo elimu inayotolewa kuanzia Elimu ya Awali hadi Sekondari itakuwa bora zaidi ili kuwa na msingi imara ili kuwa na Taifa lenye watu walioelimika ili kulijenga Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi sasa nchi yetu inatoa elimu ya kutosha lakini bado msingi wa elimu si bora na matokeo yake ni kama ifuatavyo. Mwaka 2007, theluthi mbili ya watahiniwa wa Kidato cha Nne walipata Daraja la Nne na 0 katika mitihani yao ya kumaliza Elimu ya Sekondari. Hali hiyo pia ilitokea katika matokeo ya mitihani ya Kidato cha Nne kwa mwaka 2008. Matokeo haya mbaya yanatokana na msingi mbaya wanaopata wanafunzi katika Shule za Msingi kwani shule nyingi zimekuwa na Walimu wachache na wanapoenda Sekondari pia hazina Walimu wa kutosheleza mahitaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, mahitaji ya elimu nchini kwa takwimu za Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, Tanzania Bara ina upungufu wa Walimu 115,000, ambao itachuku miaka zaidi ya 15 kuziba pengo hilo. Katika shule zetu nchini, hazina mgawanyo sawa wa Walimu kwani kuna shule zina Walimu wengi hasa mjini ambako vijijini unakuta shule ina Walimu wawili. Kwa kuwa mtihani unaofanywa ni mmoja, ni

dhahiri kuwa kuna maeneo yanasonga mbele na maeneo mengine hayataendelea kwa kukosa Walimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi langu katika bajeti hii, Wizara ioneshe mkakati wa kuziba pengo kubwa la Walimu wanaohitajika. Pili mkakati wa uboreshaji wa mishahara na marurupu kwa kada ya Ualimu ili watu wengi wawe na ari ya kujiunga na kada hii, ili kuwa na ongezeko la Walimu ili kuziba pengo lililopo. Tatu karo na michango mingi kwa wanaosomea kozi ya Ualimu katika ngazi ya Stashahada na Cheti, iondolewe ili watu wengi waweze kujiunga na kozi ya Ualimu. Nne naiomba Serikali iweke mpango unaopimika kwa ajili ya kutoa elimu kwa watoto wenye ulemavu sawa na watoto wa kawaida. Kwani sasa sehemu kubwa ya gharama za kuwasomesha watoto wenye ulemavu imebaki mikononi mwa taaisisi zisizo za Kiserikali kama Mashirika ya Dini.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la MMES limeleta mafanikio makubwa lakini bado Wizara ina changamoto kubwa ya kuongeza bajeti ili ruzuku katika Halmashauri ziongezeke ili zisaidie ujenzi wa madarasa katika Shule za Msingi, kwani Halmashauri nyingi zimejikita katika ujenzi wa Sekondari na kuacha Shule za Msingi zikiwa na upungufu mkubwa wa vyumba vya madarasa na nyumba za Walimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

**MHE. ANNA R. LUPEMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, Walimu wamekuwa na kero na matatizo mengi ambayo yanawaathiri katika kutenda kazi zao. Kero hizi ni pamoja na kutolipwa haki zao kwa wakati hasa pale ambapo wamekwishatimiza wajibu wao. Hivyo kupelekea malimbikizo ya madai ya fedha zao kwa muda mrefu.

Kwanza, ni malimbikizo hayo yanatokana na madai ya mishahara isiyolipwa kwa wakati (ajira mpya) kwa mfano Walimu walioajiriwa Julai, 2008 hawakulipwa mishahra yao kwa kipindi cha karibu mwaka mzima hata baada ya kulipwa mishahara ya kwanza malimbikzio yamebaki kuwa ni madeni huku fedha zilizotengwa na Bunge kuwalipa zikirudishwa Hazina baada ya mwaka wa fedha kumalizika.

Pili, marekebisho ya mishahara baada ya kupewa vyeo vipya, pamoja na malimbikizo baada ya kupanda daraja. Kwa sasa Walimu wengi wanapata mishahara ambayo siyo stahili yao kutokana na kutorekebishiwa mishahara kwa wakati. Hali hii inakatisha tamaa Walimu ambao wanajikuta wakitumikia kwa mishahara midogo na huchangia kwa Walimu kutoroka kwenda kufundisha kwenye shule zisizo za Kiserikali.

Tatu, fedha za matibabu, likizo gharama za masomo pamoja na uhamisho.

Nne, kuweka kiporo madeni ya Walimu kwa miaka mingi siyo tu kunashusha molari wao wa kazi bali pia kunaonesha jinsi kipaumbele cha Taifa kwa elimu kinatajwa kwa maneno tu na si matendo.

Tano, kumekuwa na kero kubwa ya Walimu wenye uzoefu tofauti kurundikwa katika cheo kimoja.

Sita, pamoja na jitihada kubwa za ujenzi wa madarasa kupitia MMES zinazoonekana, jitihada za ujenzi wa nyumba za Walimu zifanyike kwa bidii Walimu wana hali ngumu huko vijijini.

**MHE. JUMA H. KILLIMBAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Mungu kupata fursa hii. Nampongeza Mheshimiwa Prof. Jumanne Maghembe (Mb), Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, Mheshimiwa Mwantumu Mahiza (Mb), Naibu Waziri na Mheshimiwa Gaudencia Kabaka (Mb) Naibu Waziri, kadhalika Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara kwa mwaka wa fedha 2009/2010.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianzie na Elimu ya Sekondari. Juhudi za wananchi katika ujenzi wa Sekondari kila Kata Jimboni kwangu, zimekuwenda vizuri sana takriban Kata zote zina shule moja na kuendelea za Kata. Naomba Serikali ituletee Walimu wa kutosha ili wakidhi mahitaji ya shule, Walimu wa mchepuo wa sayansi wanahitajika pia.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia Wizara isaidie ujenzi wa mabweni kwa wasichana hasa Shule za Sekondari zile za Kata ambao zipo maeneo ya miji, mfano, Sekondari ya Ndago, Kizaga, Lulumba, Shelui na Kyengege, maeneo haya yanapitiwa na barabara kuu na ni hatari kwa wanafunzi wa kike.

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa Maabara, nao ni muhimu sana katika shule hizi za Sekondari. Naomba Wizara itilie mkazo suala hili ili wanafunzi waweze kupata elimu bora kwa vitendo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Wizara itoe msukumo ili kuhakikisha upungufu uliozuia kuanzisha Shule za A – Level (Kidato cha Tano na Sita) za Lulumba na Kingumo zilizopo Wilayani Iramba kwamba ushughulikiwa na shule hizi zianze kupokea wanafunzi kuanzia mwaka huu wa fedha 2009/2010.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara isimamie kwa ushirikiano na TAMISEMI kuhakikisha mgawo wa Walimu wa Shule za Msingi unakuwa sawa sawa badala ya sasa ambapo baadhi ya shule za mjini kuna Walimu wengi na za vijijini kuna Walimu wachache.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. RITA L. MLAKI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchangia hoja ya Wizara ya Elimu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, inasemekana kuwa vitabu vingi vyenye thamani ya 70 bilioni viko kwenye ma-*godown* ya *Publishers* ambavyo vingeweza kutumika shuleni na pia Wizara ya Elimu ilikwishavipitisha hivyo vitabu, je, kwa nini Wizara isiombe fedha zaidi ili ivichukue viweze kutumika shuleni tukizingatia kuwa watoto shuleni hawana

vitabu? Pia Serikali inawaambia nini Ma-*publishers* hao ambao tayari wameshatengeneza vitabu hivyo?

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. JACOB D. SHIBILITI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru wa nafasi uliyonipa, nianze kwa kumpongeza Waziri, Manaibu Waziri, Katibu Mkuu na Wakurugenzi wa Wizara kwa hotuba nzuri, mimi ninaahidi kuunga mkono kwa asilimia mia moja na pia katika shukrani zangu niwahusishe taasisi za elimu zinazosaidia umma wa Watanzania kusaidia kutoa umaskini kwa njia ya elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya yote, ni kuipongeza Serikali kwa kuona umuhimu wa Mashirika ya Dini kuendelea kutotoza ushuru kwa bidhaa waagizazo nje kwa ajili ya huduma za jamii kama vile Elimu, Afya, Maji na kadhalika. Ni jambo la busara sana. Hata hivyo, ushauri uliotolewa wa Serikali na wana harakati wa huduma za jamii yaani mashirika na taasisi za dini kuona kuwa wajanja wachache wasitumie mwanya huo wa msamaha kujitajirisha badala ya huduma kwa jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, lipo tatizo la shule za binafsi hapa nchini hutumia neon St. na hutoza *fee* kati ya shilingi 800,000 hadi 1,000,000, fomu hutolewa au kuchapishwa kati ya 3,000 na hutawanywa nchi nzima wakati nafasi katika shule hiyo au hizo ni kati ya 160, je, hii si hujumu kwa wananchi wanaohitaji huduma hiyo? Mmeliona hilo, hapo sijaweka vitabu ambayo navyo huelekeza mahali pa kununua na kadhalika. Jambo hili lifanyieni kazi, matabaka yataongezeka huku wanatumia mgogo wa msamaha wa kutolipa ushuru.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya Shule za Msingi zinaridhisha kwa majengo/vyumba vya kujifunzia bado tatizo la nyumba za Walimu. Juhudi ziongezwe ili Walimu, wapate mahali pa kuishi na kufanya kazi yao vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, upande wa Shule za Sekondari, wakati wa ziara ya Waziri Mkuu wa zamani, Mheshimiwa Edward Lowassa, aliahidi yeye kusaidia Shule ya Sekondari iliyoko kijiji cha Lubuga Wilayani Misungwi lakini pia ahadi ya Mheshimiwa Waziri wa Elimu wa wakati huo aliahidi kuchangia lakini ahadi hizo hazijatolewa hadi leo, je, ahadi hizo zilikuwa za binafsi au Serikali kama ni Serikali kwa nini hamjatekeleza?

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii imekuwa ikiniadhidi gari kwa ajili ya Ukaguzi, ni miaka minne sasa hakuna mafanikio. Napenda kufahamu sababu za msingi za kuendelea kunyanyaswa watumishi wa Ukaguzi Wilayani kwa kunyimwa gari wakati jiografia ya Wilaya inasumbua sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ifanye utaratibu wa kudumu wa kushughulikia mapunjo ya Walimu na madai yao. Jambo hili halitoi picha nzuri kwa nchi yenye amani, upendo na utulivu. Jitihada za pekee zifanyike ili suala hili liishe kabisa na Walimu waendelee na kazi yao bila manung’uniko.

Mheshimiwa Naibu Spika, vyuo vya ualimu, ni vyombo muhimu sana. Juhudi za kuviimarisha vyuo hivyo iendelee kupewa kipaumbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna matatizo ya uhaba wa Walimu, bila vyuo vizuri, hatutapa Walimu wenye sifa za kufanya kazi. Hivyo, tuongezeni juhudi katika vyuo hivyo ikiwemo kuongeza vyuo vingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sera ya Vyuo Vikuu, huenda inahitaji marekebisho. Wapo wanavyuo ambao wanapofeli mwaka wa mwisho hukosa chochote baada ya kusoma miaka mitatu au mine. Ni vema badala ya kupata digrii basi utaratibu wa vyeti au Diploma ufanywe ili mwanachuo huyo asiondoke bila fani yoyote. Hata hivyo, naendelea kufanya utafiti, nimwombe Waziri kama nitapata mchango wa kuchangia katika kuboresha sera basi nitaiwasilisha Wizarani.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho namtakia kazi njema Waziri, Manaibu Waziri na Mungu awasaidie.

**MHE. AZIZA SLEYUM ALLY:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kufahamu, Wizara ya Elimu ina shule ngapi za kihistoria katika nchi tangu kipindi cha ukoloni na kama shule hizo mpaka sasa zipo na zipo katika hali nzuri au mbaya?

Mheshimiwa Naibu Spika, Tabora tuna shule za kihistoria ambazo viongozi wengi walisoma hapo. Pia ni shule ambayo ilijengwa/zilijengwa tangu ukoloni, shule ya wanawake na shule ya wanaume. Zamani walikuwa wakisoma watoto wa machifu tu. Je, Wizara haioni kuwa kuna haja ya kuenzi historia ya elimu katika nchi hii na kuzienzi shule hizo ili historia hiyo isifutike kabisa maana shule hizo mbili ni shule ambazo ziko katika hali mbaya sana na zinatia aibu kabisa *Tabora Girls & Boys*. Nadhani kuna umuhimu wa kuziangalia kwa ukaribu zaidi pamoja na Shule za Sekondari kuzihamishia TAMISEMI ingekuwa ni vema katika baadhi ya shule hizo za kihistoria kuziangalia kwani viongozi wengi wamesoma hapo. Je, wangekuta wao ubovu huo na wao wangekuwa hapo walipo? Kumbuka utokako na hujui uendako. Naomba baadhi ya shule hizo katika nchi hii za tangu za ukoloni, tuzienzi na kuziangalia kwa ukaribu zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Chuo Kikuu cha Tumaini *(TUDARCO)* hata huko Iringa, *Tumaini University,* kimepandisha kiwango cha ada kwa asilimia 60, ambapo ni kutoka Sh.1.5m hadi kufikia Sh.2.5m. Je, ni chombo gani cha Serikali kinachosimamia upandaji holela wa ada vyuoni hasa vyuo vya watu binafsi?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa elimu ya Vyuo Vikuu ina wadau wengi kama Bodi ya Mikopo, wafadhili, wazazi na wanafunzi, je, chuo kinapoamua kupandisha

ada, huwashirikishaje wadau wengine, ili wajiandae na ongezeko la gharama? Je, ongezeko hilo linazingatia nini? Je linaenda sambamba na bajeti ya Serikali? Serikali iko tayari kuingilia kati upandaji holela wa ada vyuoni ili kunusuru usumbufu wanaoupata wanafunzi vyuoni hasa hicho cha Tumaini?

Mheshimiwa Naibu Spika, je, Sheria inayomzuia kijana kukariri Darasa la Saba, bado ina mantiki?

**MHE. LUCAS L. SELELII:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja ya bajeti hii na kuwapa shime kuendelea na kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri pesa kwa ajili ya vitabu kwenye Shule za Msingi na Sekondari zitolewe kwa kuangalia idadi ya wanafunzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa mpango wa MMEM na MMES, ulipokelewa vema na wananchi na kwa kuwa fedha za ku-*support* nguvu ya wananchi hazitiririki kama yalivyo matarajio ya wananchi, je, mpango huo umekwama?

Mheshimiwa Naibu Spika, je, kutakuwa na njia gani mbadala kuokoa majengo yasiyowekwa tayari na wananchi?

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauuri Itafutwe dawa ama ufumbuzi wa kudumu wa migomo ya wanafunzi wa vyuo vya elimu ya juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, wimbi la wizi wa mitihani na kugushi vyeti, limeshamiri sana hasa katika miaka ya karibuni. Nashauri watu wa jinsi hii, wachukuliwe hatua kali za kufungwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mkakati gani wa kuondosha upungufu wa Walimu kwenye Shule za Msingi na Sekondari? Je, ule mpango wa *crash programme*, umetuletea faida yoyote? Je, upungufu wa sasa ni asilimia ngapi?

**MHE. CAPT. JOHN DAMIANO KOMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Waziri Maghembe na Manaibu wake Gaudentia Kabaka na Mwantumu Mahiza, kwa kazi nzuri sana wanazofanya, *keep it up!*

Mheshimiwa Naibu Spika, shule za binafsi zimetoa mchango mkubwa sana hapa nchini. Ndizo zinazoongoza katika matokeo mazuri ya kufaulu kwa wanafunzi kuanzia msingi hadi Sekondari na vyuo. Gharama za kuendesha shule hizo ni ghali hasa mishahara ya Walimu, vitendea kazi hasa vya Maabara, vitabu na majengo. Ukweli, ni huduma ambayo haina faida yoyote zaidi ya kujitolea. Kwa kuwa shule hizi zinasomesha Watanzania na kwa kuwa jukumu la kusomesha Watanzania, ni la Serikali, nashauri Serikali itoe ruzuku kwa shule hizo ili kuwakwamua wamiliki wa shule hizo katika kuziendesha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna malalamiko mengi kuhusu Wakuu wa Vyuo vya Walimu binafsi, wanagushi vyeti ili waweze kuwaingiza wanachuo feki ili wasome vyuoni mwao. Naomba uchaguzi uimarishwe na ikibainika vyuo hivyo vifutwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, vifaa vya maabara kwa ajili ya matumizi ya Shule/Elimu, viondolewe kodi ili kiwango cha elimu kiweze kuwa bora maana vifaa hivyo vitapatikana kwa gharama ndogo kuliko ilivyo hivi sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. CHARLES N. KEENJA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Chuo Kikuu cha Tiba na Sayansi za Afya, Muhimbili kimechukua eneo kubwa kwenye eneo la Mlonganzila, Kata ya Kibamba, baada ya migogoro mingi na mikutano, wananchi wanaohusika wanasubiri fidia ili wakipishe chuo, je, fedha za kulipia fidia zimetengwa chini ya kifungu kipi?

**MHE. GAUDENCE CASSIAN KAYOMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Manaibu wake wawili pamoja na Katibu Mkuu na Naibu wake kwa juhudi wanayofanya kutekeleza majukumu makubwa ya Wizara hii ambayo ina changamoto nyingi hasa za uhaba wa Walimu. Mchango wangu ni kama ifuatavyo:-

Kwanza, Walimu wanasafiri mwendo mrefu, wanalipa nauli na mara nyingine kulala nyumba za wageni ili kufuata mishahara na pengo kufanya shughuli za utawala Wilayani. Nifahamuvyo mimi, mfanyakazi anapaswa kupata mshahara wake mahali alipo. Mwajiri anao wajibu wa kumfikishia fedha hizi pale alipo. Mwajiriwa haipaswi kugharamia mshahara wake. Ombi langu ni kwamba Serikali ni budi itafute njia ya kupunguza makali haya kwa kurejesha gharama hizo. Pengine inafaa ikadiriwe kiasi fulani cha fedha labda Sh. 50,000 na kuongezwa kwenye mishahara yao.

Pili, Wilaya ya Mbinga ina uhaba mkubwa wa:-

- Walimu kwa Shule za Msingi na Sekondari;
- Mpaka sasa ukiondoa *Kigonsera Secondary School* hakuna *High School;*
- Shule zote zilizojengwa hazina Maabara (Jimbo la Mbinga Mashariki), naomba msaada hapo; na
- Shule zote hazina maktaba na mahali pa kula mchana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Walimu wa Shule za Msingi, napendekeza ifuatavyo ili kutatua tatizo hilo.

(i) Kwa vile tunazo Sekondari mbili pale Mbinga na tunajenga Sekondari ya tatu, watu wa Mbinga wanaomba *day Secondary. School* iwe Chuo cha Ualimu kama ilivyokuwa awali. Shule hii ina miundombinu yote ya kuwa Chuo kwa sababu ilikuwa hivyo. Naomba maandalizi yaanze ili chuo kifunguliwe Julai 2010.

(ii) Shule ya Sekondari ya Kigonsera haina Walimu wa sayansi na hivyo kusababisha kufutwa kwa *combination* za sayansi. Huu si mwendo mzuri. Naomba shule hii ipatiwe Walimu ili itimize majukumu yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawatakia kazi njema katika mwaka huu wa fedha.

**MH. KAIKA S. TELELE:** Mheshimiwa Naibu Spika, hongera sana kwa hotuba nzuri. Maisha ya kuhamahama kutafuta maji na malisho ya mifugo kwa jamii za kifugaji, ni kati ya sababu zilizorudisha nyuma jamii hizo kielimu. Ombi langu kwa Serikali hususan Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ijenge shule za bweni *(hostels)* katika maeneo ya wafugaji (za Msingi na za Sekondari) katika Kata na Tarafa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Shule za Sekondari za Serikali, ni chache mno katika maeneo ya wafugaji, kipaumbele cha asilimia 75 kitolewe kwa wanafunzi jamii ya kifugaji wakati wa "*selection*" ili kuongeza idadi ya wanafunzi wa jamii hizo katika Sekondari. Mfano *Embarukaway Secondary School* iliyoko Tarafa ya Ngorongoro; ndio Sekondari pekee katika Hifadhi ya Ngorongoro yenye Kata sita na watu zaidi ya 6,000,000!

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali pia iangalie kwa jicho la huruma mazingira magumu ya Wilaya za wafugaji na upana/umbali wa shule na makazi ya watu, miundombinu duni au mwamko wa wananchi katika masuala ya maendeleo ikiwemo suala zima la elimu sio wa kuridhisha na kadhalika. Mambo haya yote hayamvutii mtendaji yeyote wa elimu hususan Walimu kufanya kazi katika maeneo ya wafugaji yenye mazingira magumu kama Ngorongoro na Longido (ambayo pia ni Wilaya za mpakani/pembezoni. Pengine motisha kwa Walimu watakaopelekwa katika maeneo hayo ingesaidia, lakini pia kuwapatia mafunzo ya Ualimu wazawa wa maeneo hayo yenye mazingira magumu ili wafundishe katika maeneo hayo, hiyo ni njia nyingine. Vile vile kufundisha kwa mkataba wa miaka 3 – 4 baada ya kupangiwa shule na kabla ya kuruhusiwa kuomba uhamisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, kujenga shule za bweni katika maeneo ya wafugaji aidha mazingira magumu ya Wilaya za wafugaji ikiwepo (upana na umbali wa shule kutoka maeneo ya makazi), miundombinu duni na mwamko duni, havivutii watendaji hasa Walimu kufanya kazi katika maeneo haya hasa maeneo ya Ngorongoro na Longido. Serikali iangalie uwezekano wa kutoa motisha na kutoa kwanza mafunzo ili warudi kufundisha katika maeneo hayo na iwekwe mikataba kati ya miaka 3 -4 kabla ya kuomba uhamisho.

**MHE. RUTH B. MSAFIRI**: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Ninayo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Somo la Sayansikimu, lirejeshwe katika mitaala ya elimu tangu Shule za Msingi hadi Sekondari. Hivi sasa, Watanzania wanashambuliwa na

magonjwa mengi kutokana na kutojua lishe bora ikoje? Sisi tulijifunza somo hili, nakiri tumefaidika sana. Angalia afya zetu na familia zetu ni nzuri. Kipo chakula kwa ajili ya wajawazito, watoto (rika mbalimbali), cha wafanyakazi wa kutumia nguvu (kama vile kuli) cha wafanyakazi wa ofisi, wazee, wagonjwa na vijana wanaokua. Hivi sasa somo hili halipo, kweli tuna hali mbaya. Familia hazijui zile chakula cha namna gani kwa wakati gani kwa sababu gani? Naishauri Serikali irejeshe somo hili. Yako mengi, nafasi haitoshi kuelezea ubora wa somo hili. Walimu wangu wote wa somo hili ni wapishi wakuu, Ikulu. Je, wakistaafu tutapata wapishi wa Ikulu nje ya nchi?

Mheshimiwa Naibu Spika, lugha ya Kiswahili, ni yetu ya Taifa, lakini haitiliwi nguvu. Kama kweli nchi yetu tungeamua tujipange kuendeleza lugha yetu ya Kiswahili bila aibu. Tusomeshe Kiswahili tangu awali hadi Vyuo Vikuu. Tutafsiri lugha zote kubwa katika Kiswahili, watu wetu waandaliwe kuwa Walimu katika Afrika Mashariki na Afrika ili Tanzania isikike kuwa nchi ya Kiswahili kweli kweli. Mimi kwa sasa naona Kiswahili bado hatujakipa nguvu ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, udhibiti wa mimba kwa watoto wa kike mashuleni. Mimba zinawarejesha watoto wetu wa kike nyuma. Wanaowasababishia mimba ni wanaume wa rika mbalimbali, wakiwemo watu wa karibu nao. Suala hili tulivalie njuga. Katika kulishughulikia walau kwa kuanzia, Serikali itusaidie kuunga mkono juhudi za kujenga hosteli kwa wasichana na baadaye kwa wavulana kote nchini.

**MHE. DR. ABDALLAH O. KIGODA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Aidha, naipongeza Wizara kwa kazi nzuri. Mambo ya kuzingatia ni haya yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, tutatue upungufu wa Walimu katika Shule za Msingi na Shule za Sekondari. Nia ni kuzalisha *quality* na sio *quantity*.

Mheshimiwa Naibu Spika, shule nyingi za Sekondari, Handeni zina Mwalimu mmoja au wawili tu. Katika mazingira haya, ni vigumu elimu ikawa na *value addition*. Tunaomba Walimu Shule za Sekondari za Komkonga, Kwanhonge, Mazingira, Mkata na Mwamsisi, Walimu hawa tutapata lini?

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapongeza utaratibu wa Wizara wa kuwasomesha ualimu wanafunzi waliomaliza Kidato cha Nne ambao *at least* wawe wamefaulu kwa kiwango cha *point 23*. Jimbo la Handeni tumeleta maombi ya vijana hao zaidi ya 100. *Up dated status* mpaka sasa ikoje? Ni waombaji wangapi watafaidika na utaratibu huu mzuri kutoka Handeni kwa mwaka 2009/2010?

Mheshimiwa Naibu Spika, bado tuna tatizo kubwa la Maabara kwa Shule za Sekondari – Handeni. Nyingi tu, hili ni tatizo la kiTaifa. Kwa mwaka 2009/2010, *allocation* ya Handeni katika eneo hili ikoje, *let alone* ujenzi wa nyumba za Walimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Mawaziri, Katibu Mkuu, Makamishna, Wakurugenzi na watumishi wote wa Wizara hii, kazi mnayofanya ni kubwa ya kuwawezesha Watanzania kupata elimu kuanzia Elimu ya Awali, msingi, Sekondari na vyuo vya aina zote vikiwepo vya utumishi, ualimu, Vyuo Vikuu na kadhalika. Kazi yenu inahitaji moyo wa kujituma, uaminifu, uvumilivu, unyenyekevu na kadhalika. Nawapongeza sana kwa kutambua kwamba ninyi sifa hizi zote mnazo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kwamba Elimu ya Sekondari, imerudishwa iwe chini ya TAMISEMI, bado kuna jukumu kubwa la kuisaidia TAMISEMI mpaka hapo watakapopata wataalam wa kutosha na uzoefu wa kazi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza sana Serikali kujenga kwa kusaidiana na wananchi kujenga Sekondari kila Kata na kule ninakotoka (Iramba Mashariki), tumemaliza ujenzi na mpaka tumejenga Sekondari kwenye vijiji kwa mfano Kata ya Nkinto baada ya kujenga kwenye Kata tumejenga Sekondari kijiji cha Mafongo Mwanga, kijiji cha Nkalakala, Ihundi, kijiji cha Kinampanda, Nduguti Kijiji cha Minganga, Iguguno Kijiji cha Tumuli, Kinangiri Kijiji cha Kihonda na kadhalika. Kazi hizi ni nzuri na za kupongeza. Hata hivyo, matatizo yaliyoko ni shule hizi hazijakamilika kwa sababu ya ukosefu wa Walimu, maabara, maktaba, nyumba za Walimu, majengo ya utawala, upungufu wa matundu ya vyoo, ukosefu wa maji, vyombo vya usafiri na kadhalika. Naiomba Serikali kusimamisha ujenzi wa shule mpya bali tutafute fedha za kutosha kukamilisha shule za sasa. Mpaka sasa wananchi wetu wametumia nguvu zao, michango ya kujenga maboma sasa Serikali iweke nguvu zake pia.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la Walimu ni la nchi nzima, kuna shule zina Walimu wawili au watatu, kiwango ambacho hakiwezi kutoa elimu ya kutosha kwa wanafunzi wetu. Pia bado kuna uhaba mkubwa wa vitabu vya aina mbalimbali, vifaa vya maabara na majengo yake, vifaa vya michezo na kadhalika. Ukosefu wa umeme, kuwawezesha wanafunzi kujisomea, uhaba wa hosteli wa kuwezesha wanafunzi wetu hasa wa kike kuepuka kukaa mitaani ambako wengi wanapata matatizo ya kupata mimba.

Mheshimiwa Naibu Spika, Iramba Mashariki, tuna tatizo kubwa la wafugaji wanaohamahama hivyo kuwakosesha vijana kupata Elimu ya Msingi na Sekondari. Pia naomba kukukumbusha kwamba Iramba Mashariki kuna wenzetu Wahadzabe ambao sasa hivi wanapenda sana watoto wao wasome kwenye shule ambazo zina mabweni yaani wakae huko huko wakipata malazi na chakula mwaka wa fedha wa 2006/2007, 2007/2008 na 2008/2009, Serikali iliniahidi kutoa fedha kwa ajili ya kujenga hostel, Shule ya Sekondari Mwangeza, shule iliyoko kwenye Kata ambako Wahadzabe wanaishi ili vijana wao wakae shuleni na kusoma lakini mpaka leo Serikali haijatoa fedha kwa ajili ya ujenzi wa hosteli. Kwa mchango wangu huu, naikumbusha Serikali itimize ahadi yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana Serikali ikubali kuwaajiri kwa mkataba Walimu wastaafu wa Shule za Sekondari na msingi, ili kupunguza uhaba wa Walimu. Pia naomba mgao wa Walimu uwe mkubwa zaidi kwenye shule (Wilaya) za vijijini. Pia

sasa hivi umezuka mtindo wa Walimu wa Shule za Sekondari wakiajiriwa tu na kupewa shule wanakwenda kusoma kabla ya kumaliza miaka mitano.

**MHE. RAYNALD A. MROPE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Prof. Jumanne Maghembe na Manaibu wake wawili, Katibu Mkuu pamoja na watumishi waandamizi. Wapo katika Wizara ambayo ni ngumu yenye matatizo lukuki. Hata hivyo, niwapongeze Mawaziri kwa kujitahidi kuiendesha Wizara hii vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, yapo maeneo kadhaa ambayo Wizara itajitahidi sana katika kutatua matatizo yake nayo ni kama yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya elimu nchini, sio ya kutia moyo sana kwa shule zetu nyingi za Sekondari za Kata kutokana na kukosekana kwa Walimu wa kutosha hasa shule za vijijini. Hali hii ikiendelea hasa kwa Mikoa ya pembezoni Mtwara, Lindi, Pwani, Ruvuma, Rukwa na Kigoma, matokeo yake yatakuwa mbaya sana kwa kuwa na watoto waliomaliza Form IV na VI ambao haelewi kitu. Watashindwa kabisa kupambana *(compete)* na wenzao wa Kenya na Uganda na ujinga bado utakuwepo nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, madai ya Walimu yamekuwa, ni kero kubwa sana ingawaje Waziri Mkuu amesema hivi sasa Serikali itaingilia kati ili yalipwe, nashauri kuwa kauli hii iheshimiwe na walipwe. Hata Walimu wapya nao wanapata matatizo kwa kutolipwa mishahara yao mara wanapoanza kazi. Naomba Wizara isimamie masuala haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, masuala ya maslahi ya Walimu katika promosheni na kupandishwa vyeo yarekebishwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya ufundishaji nayo siyo nzuri kwani hatujaona jitihada za kukagua Walimu kama ilivyokuwa zamani. Kuna sehemu nyingi ambako Walimu hujifanyia wapendavyo na hivyo kufanya matokeo ya mitihani kuwa ya chini kabisa ambapo wanaoumia ni watoto wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningeweza kuendelea kutoa maoni yangu lakini naona Waziri ni msikivu na yeye mwenyewe ni mwanataaluma. Anahitaji kufikiria haya na waliosema wenzangu ili watoto wetu waelimike hasa na sio ili mradi wamemaliza vidato. Natumaini masuala ya Maabara katika Sekondari, yakikamilika hali itabadilika kwani kutakuwa na uwezekano wa kupata wanasayansi wa zuri tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. BERNADETA K. MUSHASHU:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nimpongeze Mheshimiwa Waziri, Manaibu Waziri wote wawili, Katibu Mkuu na wataalam wote waliohusika katika kuandaa hotuba hii. Hotuba ni nzuri sana, inaleta matumaini.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongeza kwa mafanikio makubwa mliyofikia, hasa katika ujenzi wa shule na mlivyojitahidi kulipa na kupunguza madeni ya Walimu. Malipo yaliyofanywa, ni makubwa kuliko kipindi chote cha nyuma.Llakini pamoja na jitihada zote hizo bado madeni ya Walimu ni makubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati tunapitia vitabu vya Halmashauri, tukiwa tunakagua Hesabu za Halmashauri/Serikali za Mitaa, tumebaini kuwa Halmashauri nyingi bado wana madeni makubwa ya Walimu. La kusikitisha, ni kuwa Halmashauri nyingine hawaonyeshi madeni haya, ingawa yapo na ni makubwa, hata Halmashauri hizi hazijui ukubwa wa tatizo na wao ndio chanzo cha kuwafanya Walimu wagombane na Serikali. Ili Walimu waweze kufanya kazi zao vizuri, ni lini madeni yao yanayozidi shilingi bilioni 30 yatalipwa kwa ujumla wake?

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Elimu hadi leo wanadaiwa madeni makubwa ya watu waliotoa huduma kwa asasi zake hususan shuleni, huduma zilizotolewa katika mwaka 2007 na 2008. Wazabuni waliotoa chakula na vifaa vya kufundishia, wanasikitika, wengi uwezo wao ni mdogo, kitendo cha kutowalipa kwa muda mrefu kinawasikitisha, wengi waliochukua mikopo benki, wanashindwa kurejesha, riba imeongezeka sana na baadhi wamefilisika. Ni lini basi madeni ya wazabuni ya mwaka 2007 na 2008 yatalipwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongeza kwa utaratibu wa sasa wa kulipa kila mwezi kwa mwaka 2009. Lakini nasema haiingii akilini, kwa nini mlipe madeni ya mwaka 2009, wakati ya mwaka 2007 na 2008 mmeyaficha kabatini, lini yatalipwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, Elimu ya Sekondari imehamishiwa TAMISEMI, baada ya kuona Wizara la Elimulimekuwa kubwa sana, Walimu wengi sana, hivyo huduma hizo zimehamishiwa kwenye Halmashauri na hata Maafisa Elimu wameshateuliwa. Napendekeza, ili mpango huu uanze vizuri, maandalizi ya kina yafanyike, wataalam walio Wizarani wahamie TAMISEMI na kwenye Halmashauri, ofisi ziandaliwe za kutosha kila Halmashauri na miundombinu mingine, tofauti na sasa ambapo Afisa Elimu wa Elimu ya Sekondari amepewa chumba kimoja katika Halmashauri vilevile Sheria ya *Local Councils,* haitambui Elimu ya Sekondari kama jukumu la Halmashauri. Ni lini Sheria hii italetwa *under Certificate of Urgency* ili irekebishwe, mambo yaende sawa?

Mheshimiwa Naibu Spika, ili nchi yetu iendelee, ili tutekeleze Kilimo Kwanza, ili tuendeleze teknolojia, inabidi tufundishe sayansi tena kwa vitendo, tofauti na sasa tunavyodanganyana na kufundisha kwa nadharia tu. Shule zimeongezeka, shule nyingi hazina Maabara na vifaa vya kufundishia sayansi, je, ni lini Serikali itaziwezesha shule hizi kufundisha sayansi kwa vitendo?

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, naunga mkono hoja.

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza namshukuru Mheshimiwa Waziri wa Elimu Mheshimiwa Jumanne A. Maghembe (Mb), Manaibu Mawaziri, Mwantum Mahiza, (Mb) na G.M. Kabaka (Mb), kwa kazi nzuri

wanayofanya katika kukuza elimu ya nchi hii. Pia nawashukuru watendaji wote wa Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Elimu, ni Wizara muhimu sana kwa sababu ndio Wizara inayozalisha wasomi, wanasayansi na watendaji wa Wizara zote nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo la elimu, ni kumfanya mtu aweze kujikomboa katika mazingira anayoishi. Inavyoonekana, Wizara ya Elimu haiwatayarishi vijana wa nchi hii kuwapa elimu itakayowafanya wajitegemee wanapomaliza masomo yao. Kinachoonekana kwa wanafunzi wengi wanasoma kwa ajili ya kufauli mitihani tu na hii inawafanya wanafunzi wenyewe, Walimu wao na mara nyingine hata wazee wao kujihusisha kupata mitihani kabla ya muda wake ili wafaulu vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi nyingi zilizoendelea duniani kielimu, kisanyansi, kiuchumi na kiufundi wanafunzi wao wanajifunza kwa lugha zao za asili kwa mfano, China, Korea, Urusi na kadhalika. Sisi Tanzania tunajifunza kwa lugha ya pili, Kiingereza, badala ya Kiswahili tulichokizoea. Kujifunza kwa Kiingereza kinawafanya wanafunzi kwanza kufikiri kwa Kiswahili hatimaye kupeleka fikra hizo kwenye Kiingereza, jambo hili huwafanya baadhi ya wanafunzi kukariri bila kuelewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mikopo kwa ajili ya elimu ya juu, ni tatizo kubwa. Haja yangu, siku zote Serikali inapaswa kuwasomesha wanafunzi walio katika shule za Serikali bure. Hii ni kwa sababu kwanza huu ni wajibu wa Serikali kufanya hivyo. Lakini wazee wa wanafunzi wengi ni maskini sana kiasi kwamba hawana uwezo hata wa kujikimu wao wenyewe. Serikali ikijipanga vizuri, ikakusanya mapato vizuri, inaweza kuwasomesha wanafunzi wote wa elimu ya juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imejenga shule nyingi za Sekondari za Kata. Wanaosoma kule ni watoto wa wakulima, wanyonge watoto hawa ndio wanaotegemewa kuingia Vyuo Vikuu vya nchi hii. Jambo la kusikitisha ni kuwa shule hizo hazina vifaa wala Walimu wa kutosha. Ni kwa vipi vijana hawa wataweza kufikia elimu ya juu wakati wenzao wa shule za mijini wana Walimu na vifaa vya kutosha? Tunaiomba Serikali iokoe elimu ya wanafunzi wa Kata kwa kuwapatia Walimu na vifaa ili waweze kusonga mbele kielimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna msongamano mkubwa wa wanafunzi katika shule na mabweni kulingana na uwezo wa shule hizo. Aidha, baadhi ya majengo wanayoishi wanafunzi, yamechakaa na ni hatari kwa afya zao. Serikali haina budi kuyakarabati majengo na kupunguza idadi ya wanafunzi ili kuepuka msongamano na hatimaye maafa.

**MHE. MICHAEL LEKULE LAIZER**: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuunga mkono hotuba ya Waziri wa Elimu. Wizara hii ni muhimu sana kwani Wizara zingine zinategemea wataalam na wasomi kutoka Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika maeneo ya Wilaya zetu, elimu imetofautiana. Ninapenda kuzungumzia elimu kutoka eneo la wafugaji. Katika shule za wafugaji, elimu ni duni kutokana na upungufu wa Walimu kwenye shule za vijijini na kusababisha taaluma kuwa chini sana tofauti na maeneo mengine. Jambo hili inawezekana kurekebishwa kwa kutafuta Walimu kwenda kwenye maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali waweke utaratibu wa kuwapa motisha kwa Walimu wanaofundisha kwenye shule za vijijini zenye mazingira magumu. Inafaa utaratibu huu uharakishwe ili kuharakisha kuongeza taalum kwenye eneo husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo lingine kwenye shule za wafugaji, ni suala la mimba. Wazazi hawataki wasichana wasome kutokana na kupenda kupata mahari. Kupokea mahari kwa watoto wa shule, inasababisha wazazi kutochukua hatua ya kuwasomesha watoto wa kike. Ombi langu kwa niaba ya wananchi toka jamii ya wafugaji, Serikali wakubali wasichana hawa warudi shuleni baada ya kujifungua kwani wanawapoteza wasichana wengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi lingine katika Wilaya ya Longido. Hali ya ukame ni jambo ambalo limesababisha njaa kubwa. Kutokana na ukame huo, wanafunzi wameshindwa kulipa ada na baadhi wako nyumbani. Wanafunzi hao wanakosa masomo kutokana na hali ya uchumi kuwa mbaya. Naomba Serikali kuwaruhusu waendelee na masomo.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuzungumzia madai ya Walimu. Ni kweli kuna madai ya Walimu ambayo ni ya kweli, ambayo ni haki walipwe lakini jambo la mgomo siyo suluhu kwani Serikali haijawahi kukataa kulipa madeni na bado madeni yataendelea kuwepo ni afadhali kuwe na utaratibu wa kulipwa madeni bila kugoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni Walimu wenyewe kuandika madai ya uwongo na Serikali kupata wasiwasi mkubwa na kuleta hofu na Serikali kulazimika kuchukua muda mrefu wa kuhakiki madai kama ni ya kweli. Uwepo utaratibu wa kudai bila kuwa na mgomo kwani hasara kubwa inapopatikana huathiri taaluma.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, kwa kuwa Wilaya ya Longido ni mpya, naomba gari kwa ajili ya ukaguzi kwani mazingira ya Wilaya ni magumu ndio maana hakuna ukaguzi unaofanywa kwa wakati. Naomba sana ombi la gari kwa ajili ya hali ngumu ya Wilaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, maslahi ya Walimu yanazunguka katika Wizara nne tofauti. Ajira na kupandishwa madaraja iko Wizara ya utumishi, Sera na utendaji kuhusu kazi zao, ziko Wizara ya Elimu na Ufundi, usimamizi wa kazi zao uko TAMISEMI na malipo yao yako Wizara ya Fedha. Naomba sana Serikali ione suala hili maana mimi naona ndiyo sababu madai ya madeni na madaraja yao yako sio vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naona Serikali imeharakisha sana kupeleka TAMISEMI, usimamizi wa elimu na ufundi. Naona Wizara hiyo haina *capacity* tosha ya kusimamia Wizara hii kubwa sana, ingekuwa vema kujenga *capacity* kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. SIRAJU JUMA KABOYONGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongeza Waziri, Manaibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote Wizarani, kwa matayarisho mazuri ya hotuba ya bajeti.

Aidha, naipongeza Serikali kwa kuhimiza na kusimamia vema utekelezaji wa ujenzi wa Shule za Sekondari ambazo zimejengwa hapa nchini. Lakini ujenzi wa shule hizi, umedhihirisha matatizo yafuatayo ambayo yanahitaji ufumbuzi wa haraka:-

Mheshimiwa Naibu Spika, upungufu mkubwa wa Walimu, uhaba mkubwa wa vitendea kazi mbalimbali kama vile madawati, vitabu na maabara, uhaba mkubwa wa nyumba za Walimu na kadhalika. Ni lazima Serikali iweke mikakati ya makusudi ya kukabiliana na matatizo haya pamoja na mengine haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ucheleweshaji wa mishahara na malipo mengine ya Walimu, hili ni tatizo sugu na linaathiri kwa kiasi kikubwa uwezo wa Walimu kutoa huduma ya kufundisha. Naishauri Serikali ilitafutie ufumbuzi wa kudumu tatizo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, mikopo ya wanafunzi wa Vyuo Vikuu, kumekuwa na malalamiko ya mara kwa mara na wakati mwingine migomo ya wanafunzi ili kuishinikiza Wizara ya Elimu kutoa mikopo hiyo. Ni vema Wizara ikawaelimisha wanafunzi wa vyuo vya kuhusu stahili zao chini ya Sheria ya Mikopo na pia kuweka utaratibu wa wazi katika kutathmini na hatimaye kutoa mikopo.

Aidha mamlaka ya mikopo, ni budi iwekewe utaratibu mzuri wa kuhakikisha kwamba mikopo yote inayotolewa kwa wanafunzi, inafuatiliwa na kutolipwa baada ya wahusika kumaliza masomo na kuanza kazi. Hali kadhalika napendekeza Serikali itafute vyanzo vingine kwa ajili ya kutunisha mfuko wa mikopo kwa wanafunzi wa Vyuo Vikuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Chuo cha VETA Tabora, ujenzi wa Chuo hiki umekamilika kwa kiasi kikubwa. Kinachosubiriwa sasa ni kufunga mitambo na mashine mbalimbali mara tu zitakapowasili nchini na Tabora. Naishauri Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, isimamie kwa karibu sana utekelezaji wa hatua ya ufungaji wa mitambo na mashine kwa kuhakikisha kwamba zina wasilishwa nchini na Tabora haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, matatizo ya Wazabuni wa vyakula katika Shule za Sekondari. Hili ni tatizo la muda mrefu katika Shule zetu za Sekondari. Naiomba Serikali/Wizara ya Elimu na Ufundi, ihakikishe kwamba tatizo hili linapatiwa ufumbuzi wa haraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, uanzishwaji wa Vyuo Vikuu Tabora. Makanisa ya Katoliki na Morovian yako mjini Tabora. Kanisa Katoliki lina mpango wa kufungua tawi la Chuo Kikuu cha St. Augustine mjini Tabora. Kwa kuanzia, Baba Askofu anaiomba Serikali iruhusu matumizi ya muda ya baadhi ya majengo ya Chuo cha Ualimu mjini Tabora. Maombi haya bado yanatafakariwa Wizarani. Naishauri Wizara iyakubali maombi haya kwa sharti kwamba matumizi ya majengo hayo yatakuwa ni kwa muda tu, yaani siyo kwa kudumu.

Aidha, Kanisa la Morovian linatarajia kuanzisha tawi la Chuo Kikuu chake kilichopo Mbeya. Uongozi wa Mkoa na Wilaya umekwisha toa maeneo ya ujenzi na vyuo hivi vikuu mjini Tabora.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutumia nafasi hii, kuyapongeza mashirika haya ya dini (Katoliki na Moravian), kwa uwazi wao wa uanzishwaji wa Vyuo Vikuu mjini Tabora. Aidha, naishauri Wizara itoe kila msaada wa vibali vinavyohitajika ili vyuo hivi viweze kuanzishwa bila vikwazo visivyokuwa vya lazima.

**MHE. MOHAMMED A. ABDULAZIZ:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Lindi, ni mmoja wa Mikoa iliyo nyuma kimaendeleo. Pamoja na hali hiyo, bado Serikali imekuwa na mwenendo wa kusuasua katika kuusaidia Mkoa kupata maendeleo ya kielimu. Ni jambo la kusikitisha kwamba zaidi ya miaka mitatu, ahadi zimekuwa zikitolewa kuhusu ujenzi wa Chuo cha VETA Lindi pamoja na kwamba hela zimeshatengwa lakini hakieleweki nini kinakwamisha ujenzi wa Chuo hicho. Nahitaji wakati wa majumuisho, nipate maelezo ni lini Chuo cha VETA Lindi kitajengwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la Walimu bora, ni jambo la msingi kwa maendeleo yetu yote. Upo ushahidi kwamba baadhi ya Vyuo vya Ualimu vya binafsi vimekuwa na tabia ya udanganyifu na kuwapa vyeti vya Ualimu watu ambao hawana sifa za kuwa Walimu. Chuo cha Elimu Kange kilichopo Tanga, ni moja ya vyuo ambavyo kama kweli tungekuwa *serious*, kilistahili kufungwa kutokana na tabia yake ya kuingiza Walimu feki katika mfumo wetu wa elimu. Napenda kufahamu msimamo wa Wizara kwa vyuo vya aina hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bodi ya Mikopo, Bodi hii imekuwa inalalamikiwa sana kutokana na usumbufu wanoupata wanavyuo. Mara nyingi wanavyuo wanapofuatilia mikopo yao, inaelezwa kuwa fedha zao zimeingizwa Benki lakini wanafunzi hao wakifuatilia benki, fedha hizo hazionekani. Swali, je, fedha hizo huwa zinakwenda wapi? Je, Wizara imefanya uchunguzi wa kubaini dosari zinazosababisha usumbufu huu? Je, inachukua hatua gani kurekebisha kasoro hizi ili kuwaondolea wanachuo usumbufu usio wa lazima?

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kazi nzuri inayofanywa na Katibu Mtendaji wa Baraza la Mitihani, bado suala la wizi wa mitihani limeendelea na kutia aibu na dosari kubwa kwenye maendeleo ya sekta ya elimu. Ubora na uzuri wa Katibu Mtendaji hautoshi kama timu inayomzunguka ni ile ile. Serikali ingehakikisha watumishi wote

wanaohusika na suala la mitihani wanaondoka ili kuvunja mtandao uliodumu kwa muda mrefu hapo Baraza la Mitihani.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nampongeza Waziri, Naibu Mawaziri, Katibu Mkuu na wataalam wote wa Wizara, kwa kuandaa na kuwasilisha hotuba hii mbele ya Bunge lako Tukufu. Pamoja na hayo, napenda kuchangia katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Wazabuni kutolipwa hadi leo Mbeya – Iyunga Sekondari. Mwaka jana 2008, nililalamikia Serikali kuchelewa kuwalipa wazabuni wa Iyunga Sekondari – Mbeya. Serikali iliahidi kulipa madeni yote ya Wazabuni, hata hivyo, hadi leo bado Wazabuni hao wanaidai Serikali zaidi ya Sh.200 milioni. Nataka kujua tatizo ni nini na litaisha lini?

Aidha, Sekondari hiyo ya Iyunga inaidaiwa na *TANESCO* zaidi ya Sh.10 milioni ikiwa ni ankara ya umeme. Hivi ninavyoandika mchango wangu, shule imepewa *"notice"* na *TANESCO* ya kukatiwa umeme. Wizara inachukua hatua gani kutatua tatizo hilo mara moja ili kutoingiza shule kwenye giza?

Mheshimiwa Naibu Spika, Maafisa Elimu wa Mikoa (REOs) kuwa na mishahara midogo kuliko Maafisa Elimu wa Wilaya (DEOs). Katika hali ya kawaida, ungetegemea kwamba Maafisa Elimu wa Mikoa wangekuwa na mishahara mikubwa kuliko Maafisa Elimu wa Wilaya. Hata hivyo, hali haiko hivyo, Maafisa Elimu wa Mikoa wanapata mishahara midogo kuliko Maafisa Elimu wa Wilaya, inashangaza! Naomba kujua kwa nini hali iko hivyo? Hivi huyu *REO* atapata wapi nguvu, "*confidence*" ya kumsimamia huyu *DEO*? Nashauri hali irekebishwe na taaluma izingatiwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, madeni ya Walimu na migomo yao, kuna usemi unaosema na Katiba yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Ibara ya 23 (2) inasema:-

*"Kila mtu anayefanya kazi anastahili kupata malipo ya haki".*

Mheshimiwa Naibu Spika, naamini Walimu hasa wale wa Shule za Msingi na Sekondari wanafanya kazi katika mazingira magumu sana, wakati huo huo wanacheleweshewa malipo yao sana hali hii ndiyo husababisha vurugu na migomo katika Shule za Msingi na Sekondari. Kwa kuwa wajibu huendana na haki, basi ni vizuri Walimu walipwe haki zao mapema. Wakati mwingine unajiuliza, kwa nini matatizo haya yanajitokeza kwa Walimu tu?

Mheshimiwa Naibu Spika, moja ya tatizo linalosababisha ucheleweshaji wa malipo ya Walimu, ni urasimu na mlolongo uliopo katika kushughulikia madai hayo. Madai ya Walimu huanzia kwa *DEO*, *REO,* Wizara ya Elimu, Utumishi, Wizara ya Fedha na Uchumi! Huu ni mlolongo usio na tija hata kidogo na bado kila hatua ina urasimu (*bureaucracy*) mkubwa sana! Nashauri mlolongo huo upunguzwe na kuwepo na jitihada za kupunguza urasimu, kila eneo ambapo madai hayo yatapita pawekwe "*time*

*frame*" Maafisa watakobainika kuchelewesha malipo hayo wachukuliwe hatua za kinidhamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa Sekondari za Kata na Maabara. Kwanza napongeza jitihada za Serikali katika ujenzi wa Sekondari za Kata. Hata hivyo, kwa maoni yangu, nadhani tumejenga Sekondari nyingi sana. Tunachotakiwa kufanya sasa ni kujenga mabweni hasa kwa watoto wa kike. Jambo muhimu zaidi ni ujenzi wa maabara, si busara kuendelea kujenga shule zaidi wakati shule zilizojengwa hazina maabara. Hivyo, nashauri sana kwamba sasa uwe wakati wa kujenga maabara, nguvu za Serikali na wananchi zielekezwe huko ikiwa ni pamoja na kuendelea kuimarisha shule zilizopo, kujenga nyumba za Walimu na kuboresha mazingira ya shule zilizojengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bodi za Shule za Sekondari, Shule za Sekondari kama ilivyo kwa taasisi nyingi za Serikali, husimamiwa na Bodi. Hata hivyo, ubora wa wajumbe wa Bodi hizo, ndio ulionifanya niandike hili leo. Wenyeviti wengi, kama siyo wote, wa Bodi za Sekondari, ni wale waliomaliza Kidato cha Nne (4) na wengine hawakufanya vizuri. Kinachoshangaza zaidi ni kwamba baadhi ya Wajumbe wa Bodi hizo ni wale wenye elimu ya Darasa la Saba! Sina hakika kama watu wa aina hiyo wanaweza kushauri namna nzuri ya kuziongoza shule. Najua tumefungua shule nyingi sana lakini suala la ubora wa wajumbe wanaoteuliwa kuunda Bodi hizo, ni budi liangaliwe kwa umakini mkubwa sana. Ahsante.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. RAJAB H. JUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, naomba kuunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, kwa hotuba yake nzuri ambayo inatia moyo. Zaidi ya kuunga mkono hoja hii, nashauri mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mfuko wa Mikopo ya Elimu ya Vyuo Vikuu kwa wanafunzi wanaoingia vyuoni, uongezewe hela zaidi ili wanafunzi wengi wapate kufanikiwa na mkopo huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ilipe mishahara na mafao yote wanayodai Walimu ndani ya mwaka huu wa fedha wa 2009/2010.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali iongeze nguvu katika utafutaji na upatikanaji wa vifaa vya masomo ya sayansi yaani vifaa vya maabara *(laboratories)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali iongeze nguvu zaidi katika zoezi la ujenzi wa nyumba za Walimu nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja.

**MHE. FRED T. MPENDAZOE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda kuunga mkono hoja.

Kwa dhati, nampongeza Waziri Maghembe na Manaibu wote kwa utendaji wao mzuri. Hawana makuu na wanapenda kusikiliza wanapopelekewa matatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana kukumbushia Serikali juu ya ujenzi wa Chuo cha VETA Wilaya ya Kishapu kwani Halmashauri imetenga eneo kwa ajili ya ujenzi huo. Je, ujenzi utaanza lini?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Wizara ifuatilie suala la majengo yaliyopo Kampuni ya Almasi ya Mwadui ambayo imeyatoa kwa ajili ya kuyakarabati yatumike kama Sekondari na mabweni.

Mheshimiwa Naibu Spika, Walimu wengi wa Shule za Msingi, Wilaya ya Kishapu walijiunga na *Blue Financing Ltd*. wakakopa. Kampuni ya *Blue Financing Ltd*. haijawapa mikataba lakini inaendelea kuwakata kiasi kikubwa zaidi ya makubaliano. Suala hili nililileta Wizarani, akalipokea Naibu Waziri Mheshimiwa Kabaka, Walimu wanaiomba Serikali iwasaidie kwani wanadhulumiwa sasa.

**MHE. HALIMA O. KIMBAU:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza kwa dhati kabisa Mheshimiwa Waziri kwa hotuba ya Wizara na kwa maana hiyo napenda kusema naunga mkono hoja kwa 100%.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo, ninayo machache ya kuchangia juu ya uhaba wa Walimu. Nashukuru kusikia kwamba, Mheshimiwa Rais wetu wakati wa ziara zake huko Marekani amewahi kuomba kupatiwa msaada wa Walimu wa Sayansi. Ni mategemeo yangu, hili tutafanikiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naendelea kuomba tuone kama tunaweza kupata Walimu wa masomo mengine na hata wa hayo masomo ya sanyansi. Isitoshe kupata Walimu kutoka nchi za jirani hata kwa kuajiri kwa mikataba wakati wenyewe tukiendelea kujiandaa kupata Walimu kutoka humu ndani ya nchi yetu. Bila hivyo bado watoto wetu wataendelea kupata taabu kupata elimu stahili. Matokeo yake na nchi itashindwa kupata warithi, wataalam wa baadaye.

Mheshimiwa Naibu Spika, huduma za Walimu, mimi napongeza jitihada ya Serikali kwa jumla. Napenda tu kusema, naiomba Serikali iendelee na jitihada hizo za kuwapatia Walimu mahitaji yao haswa wale walio vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, narudi kwa wanafunzi. Mimi napata tabu sana ninapofika kwenye baadhi ya shule zote za msingi na za Sekondari kutokana na umri wa watoto na umbali wanaotembea. Kinachonipa taabu pale ninaposikia watoto hawa hawapati chochote shuleni kwa maana ya chakula hata uji angalau. Hii naamini inawaathiri watoto hawa. Matokeo yake baadhi yao wanasinzia hata masomo mengine

wanashindwa kuyapokea. Hebu tusisitize kuona aidha Serikali za Kata na Serikali za Vijiji na wazazi kuona hawa watoto wetu wanapata huduma ya angalau uji.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, nahimiza Kamati za Shule kuwa karibu sana na kukutana mara kwa mara kwa maendeleo ya shule na wanafunzi. Vikao vya wazazi ni muhimu kwani ushirikiano huo ndio utatupa uwezo kwa wote kuweza kutatua matatizo yaliyo ndani ya uwezo wetu.

Mwisho kabisa, napenda kupongeza sana jinsi Wizara yako inavyojibu maswali mazito mazito yanayohusu Wizara hii. Napenda kukiri kwamba sijawahi kuuliza swali lolote.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni mategemeo yangu ushauri wangu utaupokea na kuufanyiwa kazi. Ahsante, narudia kuunga mkono hoja.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE**: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri, kwa hotuba yake nzuri, yenye ufafanuzi wa kina kuhusu Wizara yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, naunga mkono hoja hii kwa asilimia 100. Pamoja na kuunga mkono hoja hii, naomba kuchangia maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Elimu ya Msingi na Sekondari na elimu ya juu, kwa kuwa mwaka huu kuna upungufu mkubwa wa chakula katika baadhi ya Mikoa ukiwemo Mkoa wa Dodoma na Wilaya ya Mpwapwa ikiwemo na kwa kuwa upungufu huu wa chakula utasababisha mahudhurio mabaya ya wanafunzi na kwa kuwa Serikali inajiandaa kupeleka chakula maeneo yenye upungufu wa chakula, je, Serikali itakubaliana na mimi kwamba shule nazo zingepata chakula ili kuboresha mahudhurio na pia kuboresha taaluma katika Shule za Msingi na Sekondari?

Mheshimiwa Naibu Spika, je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza idadi ya wanafunzi/wanachuo katika Vyuo vya Ualimu hasa vile vinavyofundisha Walimu wa Diploma ili kupata Walimu wengi na kuwapeleka kwenye Shule za Sekondari ambazo zina upungufu mkubwa wa Walimu na kusababisha kushuka kwa taaluma katika shule hizo?

Mheshimiwa Naibu Spika, je, Serikali ina mpango gani wa kujenga Maabara katika Shule za Sekondari za kutwa za Kata ili wanafunzi waweze kusoma masomo ya sayansi kinadharia *(theory)* na ki-vitendo *(practicals)?* Je, Serikali imetenga fedha kiasi gani katika bajeti ya mwaka 2009/2010 kwa ajili ya kujenga maabara hapa nchini, Mkoa wa Dodoma na Wilaya ya Mpwapwa? Je, Serikali imetenga fedha kiasi gani kwa ajili ya ujezi wa hosteli Shule za Sekondari za kutwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, je, Serikali ina mpango gani wa kutenga fedha za kutosha kwa ajili ya chakula, umeme na maji katika Shule za Sekondari za bweni ikiwemo Shule ya Sekondari ya Mpwapwa *(Mpwapwa High School).* Hivi sasa kuna

tatizo kubwa la uhaba wa chakula, umeme na maji kukatwa hali ambayo husababisha shule kufungwa kabla ya wakati wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, je, Serikali ina mpango gani wa kutenga fedha za kutosha kwa ajili ya ukarabati wa majengo ya shule ya Sekondari ya Mpwapwa *(Mpwapwa High School)?* Je, ni fedha kiasi gani zimetengwa mwaka wa fedha wa 2009/2010 kwa ajili ya ukarabati wa Shule ya Sekondari ya Dodoma, Kilakala ambazo zinahitaji ukarabati mkubwa na kujenga uzio *Mpwapwa High School,* Dodoma Shule ya Sekondari na Kilakala Sekondari.

Mheshimiwa Naibu Spika, je, Serikali imetenga fedha kiasi gani kwa ajili ya malipo ya madai ya Walimu 2009/2010?

Mheshimiwa Naibu Spika, je, ni sababu gani zinazosababisha wanachuo wa Vyuo Vikuu kugoma na kufanya maandamano? Je, Serikali imeweka mikakati gani ya kudhibiti hali hiyo? Je, Serikali imetenga kiasi gani kwa ajili ya mikopo ya wanafunzi wa Vyuo Vikuu?

Mheshimiwa Naibu Spika, je, Serikali ina mpango gani wa kuzifanyia ukarabati nyumba za Walimu wa Shule ya Sekondari Mpwapwa na Chuo cha Ualimu cha Mpwapwa? Kwa kuwa nyumba hizo zina hali mbaya sana na hazijafanyiwa ukarabati zaidi ya miaka 10. Je, Serikali ina mpango gani wa kuwapatia gari kubwa Shule ya Sekondari ya Mpwapwa na basi la Chuo cha Ualimu cha Mpwapwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Shule za Sekondari za kutwa zimekabidhiwa Serikali za Mitaa/Halmashauri za Wilaya, Miji, Manispaa na Majiji, je, Halmashauri za Wilaya zimejianda vipi kuzipokea shule hizo na hasa kuhusu bajeti? Je, Serikali imetenga fedha za kutosha za uendeshaji wa shule hizo ili kupunguza matatizo ya uendeshaji wa shule hizo?

Mheshimiwa Naibu Spika, je, Serikali ina mpango gani wa kuwapatia Maafisa Elimu katika Wilaya zote ikiwemo Wilaya ya Mpwapwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii kwa asilimia 100.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND**: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, ninampongeza sana Waziri, Mheshimiwa Profesa Jumanne Maghembe (Mb), Naibu Waziri, Mheshimiwa Mwantumu Mahiza (Mb), Naibu Waziri, Mheshimiwa Gaudentia Kabaka (Mb), Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara na wale wa Taasisi zote zinazohusika. Hakika Wizara hii ni kubwa na yenye changamoto nyingi sana lakini Mheshimiwa Prof. Maghembe (Mb) amemudu kwa umahiri mkubwa. Mungu azidi kumpa afya njema na hekima tele, pamoja na wasaidizi wake na wale viongozi wa taasisi zote.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfumo wetu wa elimu unahitaji kutizamwa upya ili kuingiza masomo ya malezi na maadili. Umuhimu wa kufanya hivi, ni kuwaandaa vijana

wetu wawe raia na viongozi wenye maadili.  Viongozi na raia wasio na maadili hawawezi kamwe kuifikisha nchi yetu kwenye malengo ya dira ya maendeleo 2025.

Mheshimiwa Naibu Spika, maamuzi mazuri yoyote ni lazima yazingatie maadili *(ethical decisions).* Maamuzi yasiyozingatia maadili, huleta matokeo hasi *(negative impact)* kwa jamii nzima. Inapotokea hali hii, tunatumia muda wetu mwingi kuhoji na kubishana juu ya maamuzi yanayotiliwa mashaka ya kimaadili.

Aidha, utandawazi *(globalization)* na TEKNOHAMA, vinavuruga kwa kiwango kikubwa utamaduni wa watu wetu hususan vijana. Tukiruhusu vijana wetu wakaharibiwa na tamaduni mbaya, tumekwisha kama Taifa. Changamoto za kukabiliana na tishio hili, zinahitaji mambo ya msingi ya utamaduni wetu yatunzwe. Mkakati mmojawapo ni kuwafundisha wanafunzi wetu mambo haya shuleni.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninashauri kwa msisitizo kabisa *(strongly)*, mfumo wetu wa elimu uandae vijana wetu kuwa raia na viongozi wenye maadili baadaye. Uaminifu, uwajibikaji, kuheshimu sheria na kadhalika, ni sifa zinazohitajika kwa raia wote na viongozi wao ili nchi yetu ipate maendeleo na amani, hili halikwepeki. Vijana wawezeshwe kielimu ili waweze kung’amua sababu ya kuishi, tabia njema na kujiheshimu. Vijana walelewe katika kujiamini.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo, ninaomba sasa nimwulize Mheshimiwa Waziri kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa mabadiliko katika dunia hii ya utandawazi hayaisubiri nchi yoyote, je, Wizara haioni kuwa kuna haja ya kuingiza somo la malezi kwenye *syllabus* ya Elimu ya Msingi, Sekondari hadi Chuo Kikuu? Ninaomba majibu wakati wa majumuisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaunga mkono hoja kwa asilimia 100.

**MHE. SULEIMAN O. KUMCHAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri na timu yake yote kwa kazi nzuri na ngumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia ukweli kwamba Mkoa wa Mtwara upo pembezoni mwa nchi yetu, tunaiomba Wizara ya Elimu itoe kipaumbele kwa kupeleka Walimu katika Shule za Sekondari za Mkoa wa Mtwara. Suala la Kipaumbele katika Mikoa ya pembezoni linatokana na kauli ya Mheshimiwa Rais ya kutaka Mikoa ya pembezoni ipewe kipaumbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuthibitisha tatizo hili la uhaba wa Walimu katika Mkoa wa Mtwara, naorodhesha Shule za Sekondari ambazo zina Walimu wachache katika Jimbo langu.

(1) Shule ya Sekondari ya Makong’onda yenye Kidato cha Nne, ina Walimu wanne.

(2) Shule ya Sekondari ya Namombwe yenye Kidato cha Nne, ina Walimu watano.

(3) Shule ya Sekondari ya Namalenga yenye Kidato cha Nne, ina Walimu watatu.

(4) Shule ya Sekondari ya Mkululu yenye Kitado cha Tatu, ina Walimu wawili.

(5) Shule ya Sekondari ya Mbuyuni yenye Kidato cha Tatu, ina Walimu watatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Hiyo ni mifano michache, ni kati ya shule nyingi za Sekondari ambazo zinakosa Walimu wa kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimefurahi kusikia kuwa idadi ya Walimu wa Sekondari itaongezeka. Tunaomba basi Mikoa ya Kusini ipewe kipaumbele kupelekewa Walimu, nyumba za Walimu, Maabara na vifaa vya kufundishia na kujifunzia ili kupunguza tofauti kubwa ya elimu kati ya Kusini na Mikoa mingine.

**MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR:** Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Naibu Waziri wake wote, Katibu Mkuu, watendaji wote, kwa kazi nzuri wanayoifanya, kwa ushirikiano mzuri pamoja na kutuletea hotuba nzuri yenye mwelekeo mzuri wa utekelezaji katika Wizara hii, napenda kuunga mkono hoja hii kwa 100%.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchangia yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi – VETA, napenda kupongeza Serikali, kwa uamuzi wake mzuri wa kuendeleza *VETA* hapa Tanzania. *VETA* ni mamlaka muhimu sana katika maendeleo ya jamii hasa kwa vijana. Kwa kuwa *VETA* inafanya vizuri, ni vyema vyuo hivi viongezeke katika sehemu kubwa ya Tanzania ikiwemo Zanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, napendekeza wanafunzi wamalizapo elimu yao kutoka *VETA*, wawezeshwe kwa kupatiwa vifaa na fedha hata kama ni mkopo ili waweze kujiajiri wenyewe pamoja na kuwezesha kuajiri vijana wenzao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa vijana wengi wa kike hawajahasisishwa vema kujiunga na *VETA*, nashauri Serikali itoe elimu zaidi na uhamasishaji kwa vijana wa kike ili waweze kujiunga na *VETA*.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimba kwa wanafunzi, kwa kuwa Serikali inajitahidi kutoa elimu kwa wanafunzi juu ya kujikinga na majanga mbalimbali yakiwemo upataji mimba, lakini vijana wengi wanajiingiza mapema katika tendo la ndoa na hatimaye kupata mimba za utotoni kitu ambacho ni kinyume cha maadili kwa wanafunzi. Kwa kuwa ni uwazi usiofichika kwamba baadhi ya Walimu wameshiriki katika kupotosha maadili ya Ualimu na kusabisha upatikanaji wa mimba kwa wanafunzi, naishauri Serikali iweze kuendelea kutoa elimu kwa wanafunzi wote kwamba si vema kujiingiza katika tendo la ndoa mapema na kuwachukulia hatua kali wale wanaofanya vitendo hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mbali na wanafunzi kupata mimba, nashauri Serikali kuwaruhusu wanafunzi kuweza kuendelea na masomo yao baada ya kujifungua kwa sababu wengi wao hupata mimba si kwa riadha zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa 100%

**MHE. LUCY F. OWENYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kujaza nafasi zilizo wazi.
Kamishna wa Elimu pale Wizarani anakaimu zaidi ya mwaka, siyo nafasi hiyo tu pia nafasi ya Kitengo cha Redio, Mkurugenzi wa Anuai *(Director of Diversity)*, naomba nipate majibu ya kina kuhusu Kanuni za Elimu za utumishi zinasemaje kuhusu hili la kukaimu karibia mwaka na kutokujaza baadhi ya nafasi katika Wizara hii?

Mheshimiwa Naibu Spika, masuala ya Walimu yamehamishiwa TAMISEMI, ni jambo zuri lakini Wizara ya Elimu imeangalia suala hili ni jinsi gani TAMISEMI imejitayarisha kupokea Walimu? Serikali ianglie, isihamishie matatizo kwenye Wizara nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, uhaba wa Walimu na hali ya elimu nchini. Matokeo ya Elimu ya Sekondari mwaka 2008 yamezidi kudorora na hii inatokana au kuchangiwa sana na kutokuwa na msingi mzuri tangu Elimu ya Msingi ikiwa ni pamoja na uhaba wa Walimu. Tayari takwimu zinaonesha Tanzania tuna upungufu wa Walimu 115,000. Je, Wizara imejipangaje kuziba pengo hili?

Mheshimiwa Naibu Spika, watoto wenye ulemavu, Serikali iweke mpango wa kuwapatia watoto hawa elimu sawa na watoto wa kawaida. Hata katika shule karibia zote zilizojengwa za Kata, hawajaweka miundombinu mizuri kwa ajilii ya watoto wenye ulemavu. Lazima Serikali itenge fungu maalum kwa ajili ya watoto hawa kwa sababu ni haki yao kupata elimu kama ilivyoanishwa katika Katiba.

Mheshimiwa Naibu Spika, malimbikizo ya madai ya Walimu. Hii imekuwa ni kero kubwa hata inawafanya Walimu kushindwa kufanya kazi zao kwa ufanisi. Hivi Serikali inategemea kwa kutowalipa Walimu haki zao, watakuwa na moyo wa kufanya kazi? Serikali ihakikishe inalipa madeni ya Walimu na malimbikizo ya shilingi bilioni 7.2 kwa Walimu wa Shule za Msingi na shilingi milioni 76.6 kwa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi. Mheshimiwa Rais aliagiza uhakiki ufanywe upya kwa Walimu kila mmoja kubaini fedha ambazo zinadaiwa na Walimu wa msingi shilingi bilioni 30 na Wizara ya Elimu na Ufundi shilingi bilioni 18. Madai yaliyokusanywa kutoka Mikoa yote kwa Shule za Msingi, Sekondari, Vyuo vya Ualimu na Wakaguzi ni Sh.53,617,640,798.20, je, ni lini fedha hizi zitalipwa kwa Walimu hawa?

Mheshimiwa Naibu Spika, nyumba za Walimu. Serikali imejitahidi kujenga madarasa kupitia MMEM na MMES lakini hakuna jitihada za kujenga nyumba za Walimu. Serikali inampangia Mwalimu akaripoti kijijini, Mwalimu yule ni mgeni katika eneo lile, bado afike huko hakuna nyumba ya kuishi. Hii ni sababu mojawapo ya Walimu wengi kutoripoti katika vituo vyao na kukimbilia shule za watu binafsi au shule

za Mashirika ya Dini. Nashauri Serikali ihakikishe kila shule yenye majengo mawili ya madarasa kuna nyumba moja ya Mwalimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, shule nyingi hasa hizi za Kata, hazina maabara wala vifaa kwa ajili ya masomo ya sayansi. Sasa hivi duniani, kila kitu ni sayansi na teknolojia. Ukosefu wa vifaa hivi, ni moja ya sababu inayochangia wanafunzi wengi kutokufanya vizuri au kufeli katika masomo ya sayansi. Nashauri Serikali iweke masharti ya kuhakikisha inajenga maabara na vifaa vyake.

Mheshimiwa Naibu Spika, ada za Shule za Sekondari. Serikali inatueleza ada ya Shule za Sekondari ni Sh.20,000 lakini tumekuwa tukilipa mpaka 200,000. Tunaomba Serikali itujulishe ndani ya Bunge, ada kamili ni shilingi ngapi ili wananchi/wazazi waelewe, tuondokane na tofauti hizi.

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwapongeza Mheshimiwa Jumanne Maghembe (Mb), Naibu Mawaziri, Waheshimiwa Mwantumu Mahiza na Gaudentia Kabaka, Katibu Mkuu na Naibu Katibu Mkuu na watendaji wao wote wa Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kwa kushukuru Wizara na Serikali kwa ujumla kwa mchango wake mkubwa wa kielimu katika Wilaya yetu ya Namtumbo kwa kutoa mchango wake wa miradi ya Shule za Sekondari mpya 17 katika Kata 12 za Serikali Wilayani Namtumbo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali pia imekuwa ikituletea fedha za kujenga nyumba za Walimu lakini bado tunaomba ongezeko la nyumba za Walimu wa Sekondari kwani bado hazitoshi na shule zingine kati ya hizi mpya hazina nyumba za Walimu kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia hatuna maabara katika shule zetu. Tunachoomba Serikali ikazanie ujenzi wa maabara katika Shule za Sekondari hizi mpya. Sisi Namtumbo, wanafunzi wanaomaliza *Form Four*, ni aghalabu kuwapata waliofaulu masomo ya sayansi vizuri au kutofaulu kabisa na hivyo kuwapunguzia fursa nyingi zinazohitaji waliofaulu masomo ya sayansi. Tunaomba Namtumbo iangaliwe kama Wilaya ya pembezoni na mpya na inayohitaji sana kusaidiwa kielimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunashukuru Serikali inapoendelea kutupatia Walimu kila mwaka wanaomaliza masomo yao. Tunaomba sana, bado hawatoshi kulingana na idadi ya wanafunzi na madarasa yaliyopo na Walimu waliopo, tunaomba muendelee kutuletea Walimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jimbo letu ni kubwa sana, lina Sq km (20,375) na Kata zake zimesambaa katika maeneo yenye umbali usiopungua km. 70 kutoka Kata hadi Kata. Hivyo, inawawia vigumu sana Idara ya Ukaguzi Elimu, kutembelea shule sababu Idara ya Ukaguzi haina gari kabisa. Hii inasababisha kushindwa kusimamia vizuri

viwango vya elimu vinavyotakiwa na hivyo kusababisha kudhoofisha elimu Wilaya ya Namtumbo. Tunaomba gari la Ukaguzi Idara ya Elimu Namtumbo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, shule zetu za Kata ili kuwa tulivu tumezijenga pembezoni kabisa ya vijiji na kuna umbali kidogo, tunachoomba msaada wa Serikali kujenga hosteli za wanafunzi ili wawe tulivu katika kupata elimu na kuepuka upewaji mimba watoto wetu wa kike.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. GRACE S. KIWELU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kupata nafasi ya kuchangia katika Wizara hii muhimu sana katika Taifa letu.

Pia nichukue nafasi hii, kumpongeza Waziri na Manaibu wake pamoja na watendaji wa Wizara hii kwa kuandaa bajeti hii na leo hii imewasilishwa ndani ya Bunge letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, elimu ndiyo urithi pekee ambao umebakia wa kuwapatia watoto wetu hapa duniani. Kwa maana hiyo, elimu inayotolewa, inatakiwa iwe elimu bora ambayo itawasaidia katika maisha yao ya kila siku. Hadi elimu iwe bora, ni lazima vitu hivi muhimu viwepo:-

(1) Mazingira ya elimu yawe bora, hii ni pamoja na kuwa na madarasa ya kutosha, madawati yapatikane ya kutosha, watoto wetu wakae kwenye madawati waache kukaa chini.

(2) Kuwe na vifaa vya kutosha vya kufundishia, vitabu vya kutosha kwa wanafunzi.

(3) Kuwe na Walimu wa kutosha wa masomo yote katika shule zetu ambao watatoa elimu bora na kuhakikisha watoto hawapotezi vipindi vyao kila siku.

Mheshimiwa Naibu Spika, matatizo yanayoikumba sekta hii ya elimu katika shule zetu. Tatizo la Walimu katika nchi yetu ni kubwa sana na hili limesababisha wanafunzi wetu kutokufanya vizuri katika mitihani yao kwa sababu ya kukosa elimu bora. Pia kumekuwa na tatizo kubwa zaidi kwa Walimu wa sayansi katika shule zetu na hii ni hatari kama hatua za haraka hazitachukuliwa kunusuru hali hii. Tatizo hili limekuwa kubwa kwa sababu tulipoanza zoezi la ujenzi wa madarasa ya MMEM na MMES ambao umeongeza idadi ya wanafunzi, hatukuzingatia suala zima la Walimu na ndiyo maana leo tatizo hili limekuwa kubwa sana. Hivyo, Serikali iweke mpango madhubuti wa kufundisha Walimu wapya na bora ili kukidhi mahitaji mapya, tuachane na yale mafunzo ya miezi miwili yaliyokuwa yanatolewa ili kukidhi uhaba huo wa Walimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la maabara katika shule zetu za Serikali. Kama maabara hazitapatikana katika shule hizi tujue Tanzania tutakosa wanasayansi na hii itakuwa hatari. Tunahitaji Madaktari, Wahandisi na waongoza ndege. Kwa mahitaji hayo,

ni lazima tuchukue hatua za haraka za ujenzi wa maabara hizo katika shule zetu hii ikiwa ni pamoja na vifaa husika kwenye maabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, hosteli za wasichana. Hili ni tatizo kubwa ambalo limesababisha watoto wetu wa kike kuacha masomo kwa kupata mimba. Hivyo, tunaomba hili nalo litiliwe mkazo, wananchi wamejitahidi, wamechangia kwenye madarasa na wengine mabweni na kutokana na hali ya uchumi ilivyo sasa, wananchi wameshindwa kuendelea na zoezi hilo la kuchangia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu nyumba za Walimu, ili Walimu wetu wafundishe kwa amani, ni lazima wawe na uhakika wa mahali pa kuishi yeye na familia yake. Kuna upungufu mkubwa wa nyumba za Walimu na hii imesababisha Walimu kufanya kazi katika mazingira magumu hasa wale walioko vijijini ambako hakuna nyumba za kupanga, hakuna umeme na tunajua Walimu wanafanya kazi nyingi za ziada baada ya masaa ya kazi. Hivyo, tunaomba hili nalo lipewe kipaumbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, madai ya Walimu, malalamiko yamekuwa mengi ya madai yao ambayo yanawaathiri katika kutenda kazi zao. Kero hizi ni pamoja na kutolipwa haki zao kwa wakati hasa pale ambapo wamekwishatimiza wajibu wao, hivyo kupelekea malimbikizo ya madai ya fedha zao kwa muda mrefu ambayo ni:

(a) Mishahara isiyolipwa kwa wakati kwa ajira mpya;

(b) Marekebisho ya mishahara baada ya kupewa vyeo vipya; na

(c) Fedha za matibabu, likizo, gharama za masomo na fedha za uhamisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na jitihada zinazoonyeshwa na Serikali, bado tatizo hili ni kubwa. Tunaomba juhudi za ziada katika madai haya ya Walimu yamalizike sasa ili Walimu wetu wawe na moyo na waipende kazi yao. Maana bila Walimu, sisi Wabunge tusingekuwa humu ndani ya Bunge hili. Kipaumbele cha Taifa cha elimu bila kujali maslahi ya watoa elimu kitakuwa hakina maana.

Mheshimiwa Naibu Spika, upandishwaji wa madaraja, pia yako malalamiko toka kwa Walimu kuhusu upandishwaji wa madaraja. Tatizo hili limekuwa sugu tangu pale Serikali ilipoamua kuhuisha muundo wa utumishi wa Walimu kwa kupunguza ngazi katika muundo huo na kuweka katika mfumo wa Alfabeti. Hivyo, kumekuwa na kero kubwa ya Walimu wenye uzoefu tofauti kurundikwa katika cheo kimoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri hatua za dhati na za haraka zichukuliwe ili kuondoa kero hizo (dosari) kwa Walimu wetu ili kupunguza malalamiko ya Walimu wetu. dosari hizo ni:-

(1) Baadhi ya Walimu wanaostahili hawajaorodheshwa;

(2) Baadhi ya Walimu wamerekebishwa vidato badala ya madaraja;

(3) Baadhi ya Walimu wenye sifa zinazofanana wamepewa madaraja tofauti;

(4) Waliopandishwa hawajapata barua zao;

(5) Wengine wamepewa madaraja ya juu kuliko wanayostahili; na

(6) Wengine hawajapewa malimbikizo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kueleza hayo, nashukuru kwa kupata nafasi hii, pia nawatakia kila la kheri katika utekelezaji wa bajeti hii muhimu sana katika Taifa letu.

**MHE. MKIWA A. KIMWANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nami napenda kutoa mawazo yangu katika Wizara ya Elimu na hoja iliyopo mbele yetu.

Kwanza, napenda kumpongeza Waziri, Mheshimiwa Maghembe pamoja na Manaibu Waziri, Mheshimiwa Mahiza na Mheshimiwa Kabaka, kwa kazi ngumu wanayoifanya ya kuwafutia ujinga vijana na Watanzania kwa ujumla. Kwa sasa elimu ya Tanzania inaanza kupanda japo si kwa kiwango kikubwa baada ya kupata shule za Kata, watoto wengi wanafuta ujinga kwa kisasi kikubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi sina tatizo na shule za Kata ila ni wasiwasi wangu kuhusu Walimu ambao hawatoshi katika shule hizi, kwani unaweza kukuta shule moja ina Walimu wawili waliosomea taaluma hiyo na wengine ni wanafunzi wahitimu wa Kidato cha IV tu na hawajapitia taaluma hiyo. Malalamiko hayo niliyapata katika Kata ya Nyaruguzu huko Busanda Geita, katika shule ya Nyarugusu Sekondari kwani hiyo ni hatari sana kwani tunaweza kujenga Taifa la wasomi mambumbu. Hivyo basi, mimi nashauri kuwa Wizara iweze kuzipatia shule hizi Walimu wenye taaluma na wa kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Walimu waishio katika mazingira magumu wasaidiwe kwa kuwapa motisha kwani bila hivyo, tutafundisha, Walimu na baada ya kuhitimu wanakataa kufundisha kwenye maeneo hayo ambayo hayana huduma muhimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tabia ya wazazi kuchangia kulipa mishahara ya Walimu ambao ni wahitimu wa Kidato cha IV ambao hawajasomea fani ya Ualimu, au tuiite posho. Hii ni kumbebesha mzigo mzazi huyo kwani kachangia jengo, kabeba maji au mawe, kasaidia kuezeka na sasa achangie posho za Walimu ambao sio rasmi achangie mshahara wa Mlinzi wa shule na mambo mengine mengi. Hapo ndipo mzazi anaona mzigo mzito na ndipo hasa wazazi wasio na uwezo huona ni kero na hatimaye watoto kubaki bila kwenda shule.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nifahamishwe, hivi kama mzazi akichangia fedha pia anatakiwa achangie nguvu? Kwani Shule ya Sekondari Busanda, wanawake huchota maji kwa karibu kutwa nzima lakini hawapewi malipo ya kazi hiyo, je, hii ni

halali na ni kwa nini waambiwe wamejitolea? Tayari kachangia na maji kasomba, naomba mlitazame suala hili na mlipime kwa mapana yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia napenda kusema kuwa, naomba tutenganishe Ualimu na siasa. Kwani Mwalimu mkuu wa Magu Sekondari amekuwa mwanasiasa zaidi kuliko kazi yake. Nimepokea malalamiko mengi toka Magu nilipokuwa na ziara yangu ya Mkoa. Mwalimu huyo anawalazimisha wanafunzi wawe wana CCM, eti kwa kuwa yeye ni kiongozi wa juu katika Chama hicho, hiyo si halali kabisa ni bora achague moja Ualimu au siasa. Kwani anapotambua mtoto fulani mzazi wake anaitikadi tofauti, mtoto huyo ataona joto ya jiwe. Nasisitiza, Mwalimu huyo achague Ualimu au siasa, kungali na mapema. Tunaomba uchunguzi ufanyike dhidi yake, ili kuweka hali kuwa shwari.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kusema kwamba kwa kumjali Mwalimu kwa kiwango cha hali ya juu kwa kumpa mshahara wake kwa wakati husika, kumpa mshahara wa kukidhi mahitaji kulingana na maisha ya Mtanzania, anapoishi pafanane na Mwalimu, apewe malimbikizo yake yote ili awe na ari ya kufundisha, hapa tutafaulu kielimu na kuona mtambo ambao ni Mwalimu unafyatua vifaa vya uhakika, ambapo vifaa hivyo ni wanafunzi bora na wa uhakika. Kama kasoro ndogo ndogo mtaziondoa na kukemea wale wote wanaokwenda kinyume na sera na kuwanyanyasa wananchi, wanafunzi na hata Walimu wenyewe, watachukuliwa hatua kali, naamini tutasogea mbele na baada ya muda mfupi tutapata mafanikio ya kutosha na tutajivunia Taifa letu. Muhimu, panapo matatizo parekebishwe na pale ambapo panahitaji kukemewa pakemewe. Tusileane, tuwajibishane, tuonyane na tuambiane wazi, naamini tutasogea kiasi kikubwa.

**MHE. OMAR ALI MZEE:** Mheshimiwa Naibu Spika, elimu ni msingi wa maisha, bila elimu hauna maisha, lakini elimu bila Mwalimu ni tatizo la msingi na tatizo kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, shule nyingi zinakabiliwa na upungufu wa Walimu, Walimu ambao hawana vivutio katika kufundisha kwao, hawana nyumba bora za kuishi, wanakabiliwa na matatizo ya mishahara na madai mengi ya mafao yao, Walimu ambao hawana motisha na wengi wao hawapendi kufanyakazi vijijini kutokana na hali duni ya maisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Shule za Msingi na Sekondari zimeongezeka, hii ni hatua nzuri kwa Serikali lakini wingi wa maboma na wanafunzi bila vitenda kazi haitoshi, shule moja ya Sekondari kuwa na Walimu watatu (3) ni tatizo kubwa. Walimu wa Hisabati, Sayansi nao ni tatizo, hivyo, lazima sasa kujipanga kukabiliana na tatizo hilo pamoja na vifaa vya maabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, Vyuo Vikuu vimeongezeka lakini kumekuwa na tatizo kwenye mikopo ya wanafunzi, ingawa tunapoambiwa kuwa tatizo la mikopo litapatiwa ufumbuzi lakini kama tatizo la mikopo litashindikana basi tatizo la migomo litaendelea kuwepo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Elimu ya Msingi na Sekondari zimehamishwa TAMISEMI, sehemu ambayo imekuwa ikishugulikia na mambo mengi, kama vile mambo ya maji, afya, kilimo, miundombinu na mambo mengi mengineyo, sasa tunawaongezea Halmashauri mzigo mwingine. Je, tunatarajia kutoa elimu bora au tunatarajia nini? Bajeti ya Elimu ya Sekondari imepungua sana ikilinganisha mwaka 2008/2009.

Mheshimiwa Naibu Spika, vyuo vya ufundi ni kimbilio la wengi, naipongeza Wizara kwa kutenga fedha za kutosha pamoja na vyuo vya Walimu kuvitengea pesa za kutosha ili waweze kukidhi malengo na matarajio waliojiwekea.

Mheshimiwa Naibu Spika tatizo la uvujaji wa mitihani, lazima lipatiwe ufumbuzi wa kudumu kwani uvujaji wa mitihani unaipatia hasara Serikali na waliohusika wachukuliwe hatua ili iwe fundisho kwa wengi.

**MHE. EMMANUEL J. LUHAHULA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Manaibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na watendaji wote, kwa kuandaa hotuba na hatimaye leo kuwasilishwa Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu katika Wizara hii, naomba Serikali ianze kwa kutoa ufafanuzi, hivi utaratibu huu wa kujadili Wizara hii siku moja sio mpango wa kudhoofisha elimu? Hivi huu ni uungwana Wizara inayoanzia chekechea hadi Vyuo Vikuu ijadiliwe siku moja, haraka ya nini? Je, Serikali inaogopa kitu gani, tunataka kuua elimu nchini?

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Shinyanga, una upungufu mkubwa sana wa Walimu ambapo kwenye takwimu inaonyesha upungufu wa Walimu 5,003. Hata hivyo nashukuru Wizara kwa kutusaidia sana hasa Wilaya ya Bukombe kuwapatia vijana waliomaliza Kidato cha Nne na Sita kupata nafasi za kujiunga na vyuo. Tangu mwaka 2006/2010, vijana wa Bukombe wapatao 235 wamefanikiwa kupata nafasi za masomo. Tatizo lililopo, hakuna anayerudishwa Bukombe. Kwa ujumla, vijana hawa wanatamani kurudi kufundisha Bukombe ili kupunguza tatizo la ujinga. Ni vizuri Serikali iangalie vijana wanaotoka Bukombe warudishwe kwani wao ni rahisi kukabiliana na tatizo la miundombinu. Najua Serikali mtasema Utaifa. Naona ni vizuri tuondoe tatizo la upungufu wa Walimu kwa njia hiyo na baadaye tuangalie suala la Utaifa kuleta uwiano.

Mheshimiwa Naibu Spika, lipo tatizo la Walimu Daraja la IIIA ambao walikuwa wameripoti Bukombe mwaka huu Julai ambao wamerudishwa. Walimu hawa, kwa kweli Serikali haijawatendea haki, huu ni uzembe wa hali ya juu sana Serikalini.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri, atoe ufafanuzi, hawa Walimu ambao tangu tarehe 20/7/2009, wanafukuzwa Bukombe kwamba Wizara imesema waripoti Septemba inawasaidiaje, hawana nauli, hawana pa kuishi, hawana uhakika kama watarudi tena Bukombe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna tatizo la baadhi ya Wakuu wa Shule, kula hela za wanafunzi. Mfano Mkuu wa Shule ya Sekondari Ushirombo. Hata hivyo, Mheshimiwa Waziri nimeshakuandikia barua ambayo ina maswali mbalimbali, naomba unijibu kwa maandishi na kusema hapa Bungeni ili wasikie. Ombi hilo ni je watafanya mitihani? Je, watapata matokeo yao?

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la maabara, ni vizuri Serikali ijitahidi kutatua tatizo la Maabara. Hata hivyo, nampongeza Mheshimiwa Waziri, kwa hotuba yake, kwamba *ADB* wamekubali kutoa fedha za maabara. Naomba Bukombe mnikumbuke ambapo tulijitahidi kwa nguvu zetu tukajenga vyumba 69 vya maabara kwa maana ya Sekondari 23 kila moja vyumba vitatu vya maabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ifuatilie tatizo la ulipwaji bima ya Taifa kwa wateja wao. Walimu wanaathirika sana, madai yao yanapoiva lakini huduma hawazipati na wanazungushwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, zipo tetesi kuwa Chuo Kikuu Dodoma kinaendeshwa kwa udini zaidi. Inasemekana, sina ushahidi wa kutosha, wanachuo wanapumzika Ijumaa halafu wanafanya kazi Jumamosi na Jumapili. Ni vizuri msingi wa Taifa letu wa kupumzika Jumamosi na Jumapili uheshimiwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, Walimu wanapata shida sana na huduma za Bima ya Afya ya Taifa. Ni vizuri sana Serikali/Wizara ihimize Halmashauri za Wilaya kuweka mfumo mzuri wa namna ya kuwapatia huduma Walimu ili wasitumie muda mwingi kuzunguka na kutafuta huduma.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. ALOYCE B. KIMARO:** Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la vitabu vya kiada kwenye Shule za Msingi na Sekondari, ni kubwa. Wanafunzi sasa wanatumia wastani wa kitabu kimoja kwa wanafunzi 10. Pale ambapo vitabu hununuliwa, vinanunuliwa hafifu na vingine ni *photocopy*. Kuna waandishi wa vitabu na makampuni ya kutosha kuchapa na kuandika, vitabu vingi vimerundikwa kwenye maghala bila kununuliwa huku vikihitajika. Makampuni yana vitabu takriban vyenye thamani ya shilingi bilioni 80 kwenye stoo zao. Utaratibu ufanyike vinunuliwe. Siku wakiacha kuandika na kuchapa vitabu itakuwa taabu maana tutakuwa sasa tunategemea watu wa nje kutuandikia vitabu na wapo watu watapoteza ajira kwa wingi.

**MHE. HEMEDI MOHAMMED HEMED:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia kuamka nikiwa mzima pamoja na usalama wa Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nachukua nafasi hii, kukupongeza wewe Mheshimiwa Naibu Spika, Spika, pamoja na wenyeviti wote kwa umahiri wenu kwa kutuongoza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia hotuba ya Waziri wa Elimu, Mheshimiwa Jumanne, inaonesha wazi nia ya Waziri katika kufanikisha azma yake ya kumkomboa Mtanzania kielimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi sasa, nchi yetu inataka kujiunga katika Jumuiya ya Afrika Mashariki. Mheshimiwa Waziri, Manaibu wake pamoja na timu yake, imefanikisha mengi katika Wizara yao ikiwemo upatikanaji wa *computer* ambazo zitatolewa katika mashule yetu, kwa hili tuipongeze Wizara yetu hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa elimu ni msingi wa maendeleo, hivyo basi inafaa tutathmini hali ya elimu na ubora wake hapa nchini. Ni vema tuipongeza Wizara hii kwa kuwepo kwa ongezeko la Vyuo Vikuu na Shule za Msingi katika nchi yetu. Wizara imefanikisha pia kuhamasisha Watanzania ili kujua umuhimu wa elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu elimu, kwa kuzingatia ukuaji wa elimu, tunaweza kusema nchini mwetu elimu imeshuka kulinganisha na elimu tuliyokuwa nayo nyuma. Hivi sasa imefikia mwanafunzi aliyefika Darasa la Saba (7) kukosa kujua kusoma na kuandika. Hii niseme inatokana na uhaba wa Walimu na wingi wa wanafunzi kwenye shule zetu, jambo ambalo hupelekea Mwalimu kupima viwango vya wanafunzi wake, je, Wizara imejipanga vipi kuondoa tatizo hili?

Mheshimiwa Naibu Spika, mara nyingi, Walimu ndio kigogo cha barabarani katika nchi yetu, yaani kila apitaye na panga lake hupiga, Serikali bado haijathamini umuhimu wa Walimu hapa nchini. Ili tuwe na elimu, ni lazima tumuandae Mwalimu ili atoe elimu. Tutapowajali Walimu, tutapata elimu na ndipo watakapowajibika vilivyo. Kuzalisha elimu ni kumuandaa Mwalimu. Mazingira ya Walimu, kwa jumla ni mabovu, jambo ambalo limemtoa katika hadhi yake. Je, Wizara itafanya nini kuwaboresha Walimu ili waweze kufurahia kazi zao?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Somo la Sayansi. Inaonekana wazi Wizara ya elimu ina upungufu mkubwa wa Walimu wa Sayansi. Hii ina maana huko mbele tutakosa wataalam wa somo hilo. Wizara kwa kujua hili lazima mambo yafuatayo yafanyike. Wizara ihamasishe wanafunzi ili wapende somo hili hasa watoto wa kike. Pili kwa kuwa somo hili linahitaji kuwepo kwa Maabara katika mashule zetu bado hali ni duni. Je, Wizara imefanikisha malengo gani ili kuepuka balaa hili? Napenda kujua Wizara imeandaaje wanafunzi ili wapende somo la sayansi? Naipongeza Wizara kwa kuwapa *grant* kwa wanafunzi wa masomo ya sayansi hii itatoa msukumo kwa wanafunzi hao. Hongera Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Bodi ya Mikopo ya wanafunzi wa Elimu ya Juu. Bodi ya Mikopo, ni eneo muhimu la kuliangalia kwani ni eneo linalowawezesha wanafunzi kusoma. Eneo hili limekabiliwa na changamoto kubwa kwa mfano, kutokubalika kwa Sera ya Uchangiaji gharama za elimu, mawazo potofu kuwa fedha hizi ni ruzuku na sio mkopo, wingi wa maombi kuliko uwezo wake na kutokuwa na jengo la ofisi na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Bodi hii ni ya Wizara, je, Wizara katika bajeti yake, itafanya nini kuisaidia ili iweze kuwajibika katika majukumu yake. Mara nyingi migomo ya wanafunzi hupitia hapa. Hivyo basi ni vizuri Wizara ikatupa jicho la rehema ili kunusuru tatizo sugu la wanafunzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hayo, niseme tena hongera Wizara.

**MHE. KHADIJA S. ALLY AL-QASSMY:** Mheshimiwa Naibu Spika, sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kunijalia nikawa mzima wa afya nikaweza kufika hapa Bungeni na kuchangia hoja hii iliyoko mbele yetu ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza, Waziri, Manaibu wake pamoja na watendaji wake wote kwa jinsi walivyoiandaa hotuba hii ambayo imeleta matumaini. Namwomba Mwenyezi Mungu awawezeshe kuitekeleza kwa vitendo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitakuwa mwizi wa fadhila, kama sijakupongeza wewe Naibu, Spika na Wenyeviti wako wote kwa jinsi mnavyoliendesha Bunge hili kwa umahiri mkubwa, Mwenyezi Mungu akupeni afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, naanza kuchangia kwa kuiomba Serikali ijitahidi sana kuboresha masuala ya mikopo ya wanafunzi ili kuwapunguzia adha na vile vile kupunguza migomo isiyokuwa ya lazima kwa wanafunzi na kusababishia matatizo makubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeweka mikakati gani ili kupatikana Walimu wa kutosha hasa vijijini? Kwa kweli shule tumejenga nyingi lakini cha kusikitisha ni kuwa ubora wa elimu umeshuka sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na nia nzuri ya Serikali lakini bado tunahitaji kufanya jitihada za dhati kwani pamoja na kuwa Walimu hawatoshi lakini hakuna vikalio, hakuna vifaa vya kutosha, hakuna maabara ya kutosha kiasi kwamba inawafanya wanafunzi kutolipenda somo ya sayansi kwani wanafunzi wanasoma sana nadharia kuliko vitendo, jambo ambalo linapunguza ari za wanafunzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaiomba Serikali iwe na mpango madhubuti ili kuhakikisha mambo yanatekelezwa kwa vitendo isiwe ni ahadi hewa zisizotekelezeka. Nchi yoyote haiwezi kuendelea bila ya wananchi wake kupata elimu. Elimu ni msingi wa maendeleo. Walimu waondolewe kero ili waweze kusomesha vizuri. Bila ya kuwajali Walimu basi tuhakikishe nchi yetu itarudi nyuma sana kwani vijana wengi watakosa ajira kutokana na elimu duni kwani Mwalimu asiyelipwa hasira yake anaimalizia kwa mwanafunzi kwa kumnyima elimu stahili. Tuhakikishe Walimu wanalipwa stahili za mishahara yao lakini pia wapatiwe nyumba nzuri za kuishi na posho pale panapostahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na jitihada za Wizara hii lakini bado tuna upungufu mkubwa kuhusu walemavu kwani bado hatujaonesha jitihada mahsusi kuhusu

walemavu. Walemavu ni watu wa kuwajali sana kwani hali zao ni duni sana, wanahitaji waangaliwe kwa kina kwa kujengewa vyoo vinavyolingana na hali zao, kujengewa majengo ya shule ambayo hayatawapa taabu katika kufika kwao.

Mheshimiwa Naibu Spika, wanafunzi wengi wanafeli kutokana na shule nyingi kukosa elimu zinazofanana na shule nyingine, shule ni nzuri na nyingine ni mbaya lakini mitihani inatolewa ya pamoja na kusababisha wengine kufaulu vizuri na wengi kutofaulu. Naiomba Serikali katika wakati huu ambao elimu zinatolewa kwa viwango tofauti basi na mitihani itolewe tofauti ili iwatendee haki wanafunzi hao.

Mheshimiwa Naibu Spika, watoto wengi wanapata mimba shuleni kutokana na mazingira yenyewe ya shule, wanafunzi wana kuwa *free* sana kwa kukosa Walimu kutokana na hayo kunawasababishia kupata vishawishi vikubwa na kuweza kuwaharibia maisha yao vile vile jambo hili litafutiwe ufumbuzi wa kudumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishukuru Wizara kwa mipango yake kabambe ya kuweza kufanikisha kuleta *computer* kwa shule zote za Sekondari, lakini kinachonipa taabu ni kuendeshwa kwa kutumia *battery* kwani nahisi gharama zitakuwa taabu kupatikana kwani itakubwa gharama kubwa. Naiomba Serikali ihakikishe unapatikana umeme katika shule zetu ili kuondoa gharama kubwa na kuja kushindwa kutumia kompyuta hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho na kwa umuhimu mkubwa, naipongeza kwa dhati Serikali kwa kujenga Chuo Kikuu cha hapa Dodoma, Mungu ajalie kimalizike kwa salama na tuweze kupata elimu bora. Nakushuru sana.

**MHE. EZEKIEL M. MAIGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali, naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri, Naibu Maziri na Katibu Mkuu, kwa kazi kubwa wanayofanya ya kupanda, kuimarisha na kuboresha elimu nchini pamoja na misukosuko kadhaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya elimu Mkoa wa Shinyanga, ni mbaya sana. Mwaka 2007/2008, Shinyanga ilikuwa ya mwisho Kitaifa kwa mtihani wa Darasa la Saba. Sababu ni uhaba wa Walimu. Tunaomba Serikali iweke mpango maalum wa kuboresha elimu Shinyanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Kahama ina madini, lakini wananchi hawa, vijana wapatiwe elimu ya *VETA*. Tunaomba ahadi ya kujenga *VETA* kila Wilaya itekelezwe Kahama. Tunaomba Wizara irudie jitihada za wananchi kujenga *VETA* kwani tayari wamepata eneo Kata ya Bugarama.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kahama hakuna hata shule moja ya Sekondari yenye bweni, hivyo hakuna shule yenye sifa kuwa na *A-Level!* Tunaomba Serikali iweke mkakati maalum wa dharura wa kujenga bweni walau kwenye shule 5 za Mwl. Nyerere, Busangi, Mpera, Baboha na Bugaramu Wilayani Kahama.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia Wizara isaidie upatikanaji wa vifaa vya Maabara katika shule za Kahama.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MUDHIHIR M. MUDHIHIR:** Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa Chuo cha *VETA* Mkoani Lindi, umekuwa katika mchakato na maandishi tangu mwaka 2003 lakini hakuna msingi uliyochimbwa wala tofali lililofyatuliwa. Wananchi wa Mkoa wa Lindi, leo tunataka tuelezwe jina la shetani anayeliziba pumzi suala hili kiasi cha *VETA* Lindi kuwa hadithi ya Alfu-lela-ulela.

Mheshimiwa Naibu Spika, Taasisi ya Elimu Tanzania. Suala la Taasisi hii kuandaa mitaala na papo hapo kuchapa vitabu kwa ajili ya Shule za Msingi, Sekondari na Vyuo vya Ualimu, ni uamuzi uliofanywa kwa pupa yenye kutiliwa mashaka na ni uamuzi unaostahili kufanywa mapitio upya kutokana na sababu zifuatazo:-

(1) Kwa kuwa hili ni suala la kisera, mabadiliko haya yalistahili kuwashirikisha wadau wote wakiwemo Wabunge, wasomi na wachapishaji wa vitabu.

(2) Uamuzi mkubwa kama huu kufanywa na Wizara pekee, ni dalili za kupuuza ushiriki na maoni ya Watanzania tuliyoikabidhi dhamana ya elimu kwenu.

(3) Uamuzi huu ni ”*narrow*”, wanafunzi wetu katika kujifunza mambo mengi juu ya hoja moja. *Under the sun of God, how can we expect this country to be a reaching nation under such a system?*

(4) Uamuzi huu haukuzingatia mzigo wa madeni kwa wachapji wa vitabu. Wakati Serikali katika Mkutano huu wa 16 imewadhamini wanunuzi wa pamba mabilioni ya shilingi ili kuwawezesha kutokana na mtikisiko wa uchumi duniani, Wizara ya Elimu inawadidimiza wachapishaji vitabu kwa madeni ya benki kupitia mtikisiko wa kisera Wizarani! Uamuzi huu haupendezi.

(5) Uamuzi huu unavifinyanga vipaji vya wasomi nchini ambao wamekuwa wakiandika vitabu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kupewa majibu ya kina kuhusu *VETA* Lindi na uamuzi wa Wizara kuhusu Taasisi ya Elimu kuandaa mitaala na papo kuchapa vitabu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. CASTOR R. LIGALLAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, napenda kupongeza Waziri, Manaibu Mawaziri, Katibu Mkuu na Wakurugenzi, kwa hotuba yenye ufasaha na yenye kuzingatia matatizo ya Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu utahusu elimu ya Chuo Kikuu hasa kwa elimu ya sayansi (vitivo vya Sayansi) sasa hivi hali ilivyo wanafunzi wengi wanapenda sana masomo ya sanaa. Wengi hawapendi kusoma masomo ya sayansi na

katika hali hiyo hata kama tutaongeza idadi ya wanafunzi gani wengi wao wataishia kuhitimu katika Shahada za masomo ya *Arts*. Napendekeza Wizara iweke vivutio fulani vya kuwafanya wanafunzi hao wapende masomo ya sayansi. Kwa mantiki hiyo, napenda kuishukuru Wizara kwa kutafuta fedha za kujenga maabara kwa shule zetu za Sekondari. Hii itachochea ari ya kupenda kusoma sayansi tangu Elimu ya Sekondari.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa Bungeni kwa mfano kuna maonyesho ya Kampuni ya Kichina yenye kuonyesha vifaa vya masomo ya sayansi kama Biolojia, Fizikia, Kemia ambayo vingefaa sana kuwekwa kwenye Maabara za Shule za Sekondari kama *visual aids*. Serikali igharamie kununua vifaa hivi vya sayansi na ivisambaze katika shule zote za Sekondari za Kata, kwa sababu bei yake siyo kubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, matatizo ya Walimu. Kazi ya Walimu, ni kazi muhimu sana, hata jamii inafahamu hivyo. Tangu zamani Mwalimu aliheshimika sana mbele ya jamii vijijini. Walimu wametumika sana na Serikali kwa jambo lolote ambalo linahitaji utekelezaji wa haraka kama uchaguzi, sense, chanjo na kadhalika. Tatizo kubwa linalowakumba Walimu hasa wale wa Shule za Msingi, ni mlolongo wa kiutawala ambao huzaa urasimu katika kuwatekelezea shida zao. Urasimu wa kushughulikia shida za Walimu mwaka hadi mwaka huzaa malimbikizo mbayo ni vigumu kuyashughulikia kwa mara moja. Lakini kwa jinsi Walimu walivyojipanga kupitia Chama chao cha CWT, ni vizuri kuyashughulikia matatizo ya malimbikizo ya madai yao kama Serikali ilivyoahidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Vyuo vya Ufundi Stadi – VETA. Ilani ya uchaguzi ya 2005 – 2010, Serikali iliahidi kujenga vyuo vya VETA kila Wilaya. Muda uliobaki ni kidogo na sidhani kama ahadi hii itatekelezwa ipasavyo. Nashauri pale ambapo kuna Vyuo vya Maendeleo vyenye nafasi kubwa kwa maana ya eneo la ardhi, Wizara hii ishirikiane na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsi na Watoto ili waunganishe nguvu na kuviunganisha vyuo hivi. Kwa mfano, katika Wilaya yangu ya Kilombero, Chuo cha Maendeleo, kina eneo kubwa ambalo lingeweza kujenga chuo hicho cha *VETA*.

**MHE. MAGALLE JOHN SHIBUDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, nawapongeza juhudi zote za Wizara hii za kutumia vema bajeti ya Wizara hii hasa katika juhudi za kuandaa Walimu wa kukidhi uhitaji wa mazingira ya kila eneo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa kila jambo lina msukumo wake, sasa nampongeza Mheshimiwa Prof. Jumanne Maghembe, Waziri wa Wizara hii, pamoja na Manaibu Waziri wote wa Wizara hii ambao ni Mheshimiwa Gaudentia Kabaka (Mb) na Mheshimiwa Mwantumu B. Mahiza (Mb). Vile vile nampongeza sana Mheshimiwa Hamisi O. Dihenga, Katibu Mkuu. Aidha, shukrani za pekee nazitoa kwa watumishi wote wa Idara ya Ualimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa kuna maeneo ambayo wastani wa viwango vya elimu sio wa kuridhisha kumudu mazingira ya kupambana na maadui ujinga, maradhi na umaskini, mfano, Mkoa wa Shinyanga hasa Maswa, je, pana mpango gani wa Wizara wa kuibua kasi ndani ya hii jamii ya wakulima/wafugaji hivyo waende na wakati na mpango wa kujipatia elimu ya Taifa hili?

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Maswa, ingependa kuibua mpango mkakati wa kujenga Chuo cha Ualimu. Je, Wizara hii yaweza kutoa motisha gani ambao utachochea dhamira hii itekelezwe kwa hatma bora ya kupatikana Walimu wa kutosha wa kukidhi hali ya mazingira ya Mkoa wa Shinyanga vijijini? Je, Wizara inaweza kunipa kwa maandishi mwongozo na changamoto hitajika kutekelezwa kwa azma ya shabaha ya Halmshauri ya lengo la kuanzisha ujenzi wa Chuo cha ualimu – Maswa? Je, lini maelezo yenye uzamilivu makini nitapatiwa hivyo mimi Mbunge nikaongoze mjadala wa ujenzi wa Chuo hiki cha Ualimu? Naomba majibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niunge mkono hoja.

**MHE. PAULO P. KIMITI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, napenda kumpongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watumishi wote wakiwemo Walimu kwa kazi nzuri wanayoifanya kwa nchi yetu hii. Naunga mkono hoja hii ya Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri anisaidie katika kufafanua yafuatayo kwa faida ya Wabunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, ni kumtaka Mheshimiwa apitie malalamiko ya Walimu kama yalivyowasilishwa na Chama chao (CWT) na kama walivyosambaza nakala za malalamiko kwa Wabunge jana na leo ili tujue hatua ambazo Serikali imechukua na zipi zinaendelea kuchukuliwa. Msingi wa ufafanuzi huu, utasaidia kupunguza kasi ya migomo inayoandaliwa mara kwa mara.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, namwomba Mheshimiwa Waziri, asaidie maombi yangu ya miaka ya nyuma kuhusu Chuo cha Walimu – Kantalamba Sumbawanga, kiwapatie nafasi nyingi vijana toka Rukwa ili wengi wao wabaki kufundisha Mkoani huko huko. Sijua Waziri anasemaje juu ya suala hilo?

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, kuiomba Wizara ipandishe hadhi ya Chuo hicho ili kitoe Diploma pamoja na Cheti ili tuweze kujitosheleza kwa Walimu - Mkoani na Kitaifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nne niliomba miaka mitatu iliyopita, Wizara ikubali kujenga Chuo cha VETA cha mjini Sumbawanga na siyo kutumia kisingizio cha Chuo cha Mpanda ndicho kionekane cha Mkoa. Hapana, hicho ni cha Wilaya na hata hivyo kilikuwa ni chuo cha wakimbizi, hivyo VETA hawajajenga kituo Mkoani Rukwa, licha ya kukarabati chuo hicho cha Mpanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, Vyuo hivyo vya Ufundi *(VETA)*, ni vizuri vikaweka mkazo katika kutoa fani mbalimbali zinazolingana na mazingara ya maeneo yao. Mfano Rukwa – iweke mkazo wa kilimo; ufugaji uvuvi na uchimbaji madini, kazi nyingine za ufundi ziwe za ziada. Lakini wanafunzi wote wapewe masomo ya ujasiriamali ili waweze kupata taaluma za kuweza kujiajiri wenyewe badala ya kusubiri kuajiriwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sijui mpango wa kuwapatia vijana wanaohitimu Vyuo vya VETA vifaa vya kuanzia kazi za kujiari, umefikia wapi!

Mheshimiwa Naibu Spika, mengine yaliyofafanuliwa na Waziri, nayaafiki, kinachotakiwa ni kusimamia utekelezaji wa yote yaliyoainishwa kwenye hotuba hii nzuri na yenye matumaini makubwa katika kuimarisha elimu nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. CHARLES N. MWERA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hotuba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi. Nichukue nafasi hii, kumshukuru na kumpongeza Waziri, Naibu Waziri, watendaji wote wa Wizara hii ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili nchi iendelee na kukua kiuchumi, ni lazima watu wake wawe na elimu ya viwango mbalimbali. Tulipopata uhuru, Mwalimu Julius S. Kambarage Nyerere pamoja na Serikali yake, ilitangaza Elimu ya Msingi kuwa ya lazima kwa kila Mtanzania. Kwa juhudi zake, Mwalimu Nyerere, mpango huu ulizaa matunda mazuri kwa Taifa, baada ya muda Watanzania wengi wakawa na Elimu ya Msingi, matokeo ambayo yalipelekea kupata Walimu wengi ambapo mpaka sasa wamekuwa Walimu wazuri. Tunatambua mchango wao Walimu hao, ambao kwa kiasi kikubwa sasa wana elimu ya Kidato cha Nne baada ya kujiendeleza. Wakati umefika kwa Watanzania, Elimu ya Sekondari kuwa ya lazima kwa kuwa kila Kata hapa nchini ina Sekondari, hili linawezekana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishukuru Serikali kufundisha somo la Kilimo na Mifugo katika shule zetu za Serikali ili mara mwanafunzi anapohitimu, atakuwa na elimu ya kilimo na mifugo. Tunahitaji kuwa kilimo cha kisayansi na wakulima lazima wawe na elimu angalau ya Kidato cha Nne wenye mafunzo ya kilimo. Hao vijana ambao watakuwa wamehitimu Elimu ya Sekondari katika shule zetu za Kata, watasaidia sana kuinua uzalishaji wa mazao kijijini. Kwa vile Elimu ya Sekondari itakuwa ni ya lazima, naishauri Elimu ya Sekondari iwe ya bure. Taifa lina rasilimali ya kutosha kulipia wanafunzi kuanzia Kidato cha Kwanza hadi Vyuo Vikuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama Serikali itasimamia vizuri na kukusanya mapato yanayotokana na migodi ya madini ya Dhahabu, Almasi, Tanzanite, nchi yetu si maskini, tatizo ni usimamizi mbaya wa rasilimali za nchi tulizonazo kama vile mbuga za wanyamapori, maziwa, mlima Kilimanjaro, ambapo watalii wengi hufika nchini kuangalia mbuga zetu hizi. Hakuna sababu ni kwa nini Watanzania wasipate elimu bure, kimsingi si bure maana wananchi wanalipa kodi na ulipaji huo usiwe kama hisani, iwe ni jukumu la Serikali kwa wananchi wake. Nchi za Kenya na Uganda, zina mpango wa kutoa Elimu ya Sekondari bure kwa wananchi wake wakati ambao angalau wao (Kenya na Uganda) kiwango cha elimu yao kipo juu na wananchi wao wengi wana Elimu ya Sekondari.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba wananchi wameshiriki kikamilifu katika ujenzi wa Shule za Sekondari za Kata hapa nchini. Tatizo kubwa linalokabili shule hizi, ni ukosefu wa Walimu pamoja maabara. Upungufu huu wa Walimu unawakatisha tama wananchi kuchangia maendeleo ya shule maana hawaoni manufaa ya shule hizi kwa vile hazina Walimu wa kutosha, matokeo yake wanafunzi hawafaulu kuendelea na elimu ya Kidato cha Tano na Sita, hushindwa kufaulu vizuri ili kupata sifa ya kujiunga na vyuo mbalimbali kama Ualimu, Uganga, kilimo na kozi mbalimbali. Naishauri Serikali ifanye yafuatayo:-

(a) Kuajiri Walimu kutoka nchi jirani za Kenya na Uganda, ili kuweza kusaidiana na Walimu wachache tulionao katika shule zetu, hasa za Kata.

(b) Kupeleka wanafunzi wengi vyuoni ili watakapohitimu wachukue nafasi za hao Walimu wengi kutoka Kenya na Uganda kama Serikali itakuwa imekubaliana na ushauri wangu wa kuajiri kutoka nje (Kenya, Uganda).

(c) Mishahara ya Walimu iboreshwe mara kwa mara.

(d) Pamoja na kuipandisha mishahara ya Walimu, wanafunzi, wanaojiunga na Vyuo vya Ualimu, wawe ni wale waliofaulu vizuri kwa kupata Madaraja ya Kwanza, ya Pili na Tatu katika Elimu ya Sekondari *(O Level)* na *High School* wawe wale waliofaulu kwa ufaulu wa Daraja la Kwanza, Pili na Tatu na kwa kuwa mishahara itakuwa mizuri wanafunzi watapenda Ualimu na watajiunga wengi katika Vyuo vya Ualimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mikopo kwa wanafunzi, naishauri Serikali, wanafunzi wote wapewe mikopo bila ya kuangalia makundi ya wanafunzi katika madaraja mbalimbali, kila Mtanzania awe na haki ya kupata mkopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa kuna shule nyingi za binafsi za wali, Shule za Msingi, Shule za Sekondari na Vyuo Vikuu ambazo kimsingi zimetoa mchango mkubwa katika kutoa elimu hapa nchini na sisi tunatambua mchango huo. Lakini pamoja na umuhimu wa mchango huo, kuna baadhi ya shule ambazo Walimu wa shule hizo hawana sifa ya Ualimu, kwa maana hiyo wanafunzi hawapewi elimu stahili. Naishauri Serikali kuwa, ukaguzi wa mara kwa mara katika shule hizo za binafsi, pamoja na kuangalia karo hizo katika shule hizo, ufanyike.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kujenga shule nyingi katika Kata zetu, naishauri Serikali kujenga mabweni hasa katika maeneo ambayo kuna mapigano ya mara kwa mara ili kuwachanganya wanafunzi na kupunguza uhasama baina ya koo na koo. Katika chaguzi za kuingia Kidato cha Kwanza, wanafunzi wapangwe kwenda kusoma katika Kata za mbali. Ahsante sana.

**MHE. DR. LUKA J. SIYAME:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, napenda kutoa pongezi za dhati kwa Mheshimiwa Waziri, kwa hotuba yake nzuri yenye kuelezea kwa kina masuala ya Wizara yake.

Napenda pia kuwapongeza Naibu Mawaziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu, Kamisha wa Elimu, Wakurugenzi na Wakuu na Makamu Wakuu wa Vyuo Vikuu na Taasisi mbalimbali zilizoko chini ya Wizara hii bila kusahau Walimu wa ngazi zote nchini kwa kazi yao iliyotukuka.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii katika kipindi cha miaka miwili, hadi sasa imepitia kipindi cha mabadiliko makubwa ikiwa ni pamoja na kuunganisha Wizara ya Elimu ya Juu na Elimu ya Msingi na Sekondari na suala la kugatua uendeshaji na usimamizi wa Shule za Sekondari kwenda kwenye Halmashauri. Katika hali ya kawaida, michakato hii ingeweza kuleta mchanganyiko wa hali ya juu kwa uongozi na watendaji wa Wizara. Kinyume chake, mambo hayakuwa hivyo bali kwa ujasiri mkubwa Wizara imeweza kukabiliana na hali hiyo kwa juhudi na maarifa na dalili za kuanza kutengemaa kuonekana kupitia hotuba ya bajeti ya Wizara hii ya mwaka 2008/2009.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hali hii, yapo masuala ya msingi ya kuyatolea maagizo:-

(1) Ukubwa wa Wizara na wingi wa shughuli zake. Bila shaka kila mmoja wetu atakubaliana na wale kati yetu wanaosema Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ashauriwe kutenganisha Wizara ya Elimu ya Juu na Elimu ya Msingi na Sekondari kwa manufaa ya uendeshaji na usimamizi bora. Kurugenzi na Idara zilizopo ndani ya Wizara hii, ni nyingi na zenye majukumu makubwa mno kuwa chini ya Wizara moja.

(2) Ugatuaji wa uendeshaji na usimamizi wa Elimu ya Sekondari kwenda Halmashauri. Pamoja na usogezaji wa uendeshaji na usimamizi karibu na wananchi, bado suala hili linahitaji kutazamwa kwa uangalifu sana. TAMISEMI, tayari Halmashauri inalemewa na mzigo mkubwa wa majukumu ya kutekeleza kutokana na kubebeshwa mipango mingi ya kusimamia ikiwa ni pamoja na *DADPS*. Hivi sasa, tayari kuna mkanganyiko mkubwa kuhusu wapi Maafisa Elimu wa Wilaya upande wa Sekondari wawajibike. Kwa kifupi, TAMISEMI itakuwa *“A **Jack** of all Trade but a Master of None*”

Mheshimiwa Naibu Spika, hali hii inazidi kunishawishi kuwa ugatuaji huu utafanikiwa tu ikiwa Wizara ya Elimu ya Msingi na Sekondari na pia Maafisa Elimu ya Msingi na Sekondari na pia Maafisa Elimu wa Mikoa warudishiwe mamlaka yao ya kusimamia masuala ya Elimu Mkoani badala ya kuwa sehemu ya sekretarieti ya Mkoa kumshauri Mkuu wa Mkoa, kitu ambacho kiuhalisia ni kutengeneza kundi la watumishi ambao hawana kazi kabisa kwani mwenye kauli ya mwisho ni yule ambaye hana utaalam wa masuala ya elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mbali na hayo, napenda nirudie kupongeza Wizara hii kwa kufanikisha mambo muhimu sana katika maendeleo ya elimu nchini katika kipindi hiki, kulipa malimbikizo ya madeni ya Walimu na Wahadhiri nchini, kuboresa mfumo wa ukopeshaji wa wanafunzi wanaojiunga na Vyuo vya Elimu ya Juu kutoka Bodi ya Taifa ya mikopo ya elimu ya juu, kuwezesha uanzishwaji wa Vyuo Vikuu na Vyuo Vikuu Vishiriki vipya kwa wingi na kuvipa idhini vile ambavyo vimekidhi masharti

yalivyowekwa na *TCU* ya kupewa hati hizo, kuanzisha mpango wa mafunzo ya *E-learning* kwa shule za Sekondari ili kuweza kutatua tatizo la upungufu wa Walimu na kuimarisha Baraza la Mitihani kwa kuondoa mianya ya uvujaji wa mitihani na kuanza utaratibu wa kulipatia Baraza hilo vifaa vya kuweza kufuatilia mwenendo mzima wa shughuli zinazofanyika pale, mfano, kamera za *CCTV*.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo yote, naomba Wizara hii iendelee kulipa Jimbo la Mbozi Magharibi upendeleo maalum katika kuinua kiwango cha elimu. Hadi hivi sasa, kutokana na kuweko kwake pembezoni mwa nchi na hivyo kuwa na shule nyingi sana vijijini, lina upungufu mkubwa wa Walimu wa Shule za Msingi na Sekondari. Katika jumla ya Shule za Msingi 81 zenye jumla ya wanafunzi 46,827 na Walimu 690 ikiwa ni wastani wa Mwalimu mmoja kwa wanafunzi sabini, lakini kwa bahati mbaya Walimu hawa wengi wako maeneo ya karibu na mjini na hivyo kuacha shule nyingi kuwa na Mwalimu mmoja hadi watatu kwa watoto 300 – 480. Hali kadhalika katika jumla ya shule 13 za Sekondari zenye wanafunzi 3,357 kuna wakuu 72 waliopangwa bila uwiano mzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba katika hili Wizara iendelee kutoa kipaumbele kwa maombi ya mafunzo ya Ualimu kwa waombaji toka Jimbo la Mbozi Magharibi, Wizara katika mfano wa Walimu wapya ikiwezekana iwe inatoa *allocation* kwa shule moja kwa moja badala ya kupeleka kwa *RAS* kwani kule hakuna utendaji haki katika mgawanyo wa Walimu na pia itakapokuja kwanza kutoa kompyuta kwa ajili ya *E–learning*, Serikali iliangalie kwa jicho la huruma Jimbo la Mbozi Magharibi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza kwa dhati Mheshimiwa Prof. Jumanne A. Maghembe (Mb), Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, kwa hotuba yake nzuri sana iliyo na maelezo ya kina na takwimu muhimu. Naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Aidha, napenda kuwapongeza Waheshimiwa Naibu Mawaziri, Mheshimiwa Mwantumu Mahiza na Mheshimiwa Gaudentia Kabaka, kwa kumsaidia Waziri wao kwa bidii, ukweli na ufanisi.

Vile vile napenda kumpongeza Katibu Mkuu, Prof. H. Dihenga pamoja na Wakuu wa Idara na Mashirika chini ya Wizara hiyo na wataalam wote kwa kufanikisha maandalizi ya hotuba ya Waziri, hongereni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kilio chetu ni uhaba wa Walimu wa Shule za Msingi na Sekondari, andaeni mpango mahususi wa kukabili tatizo hili. Tunawaunga mkono na kushinikiza Serikali itafute fedha zaidi.

**MHE. DR. EMMANUEL JOHN NCHIMBI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri na Wasaidizi wake kwa hotuba

nzuri sana ya bajeti, katika eneo hili, niwapongeze pia Katibu Mkuu na watumishi wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu leo umejikita katika kutambua uchapakazi na kasi ya utendaji waliyonayo Mheshimiwa Prof. Jumanne Maghembe, Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi. Wananchi wa Jimbo langu la Songea mjini, wamenituma nimpongeze na kumshukuru Mheshimiwa Waziri jinsi ambavyo amekuwa akishughulikia haraka matatizo anayopewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru kipekee Mheshimiwa Waziri anavyofuatilia mambo yafuatayo:-

(1) Kukatwa umeme *Songea Boy Secondary School;*

(2) Kukatwa umeme *Songea Girls Secondary School;*

(3) Kukatwa umeme chuo cha Ualimu Songea; na

(4) Kutafutiwa usafiri *Songea Boy Secondary School.*

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wa Songea mjini, wanafurahi sana kuwa matatizo haya anayashughulikia Waziri mwenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia kwa mia.

**MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Chuo cha Ualimu Kabanga – Kasulu, pamoja na umri wake mrefu kiko hoi bin taabani. Tangu kuanza kwake, katika miaka ya mwanzoni mwa 1980, bado chuo hiki hakijaongezewa majengo ama ya Darasa, Mabweni na Bwalo. Majengo yaliyorithiwa kutoka Kanisa Katoliki zama hizo hadi sasa zaidi ya miaka 25 hakijabahatika kupata jengo jipya. Nashauri *Kabanga Teachers College needs a serious facility*, kimechakaa, kupaka rangi haitoshi pekee yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Chuo cha Ualimu Kabanga pamoja na Chuo cha Ualimu cha Diploma Kasulu, vinahitaji magari mapya. Magari yaliyopo ni machakavu sana. Kulingana na Jiografia ya eneo la Kasulu – Chuo cha Ualimu Kabanga kipewe sasa gari jipya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wakufunzi wa Sayansi - Chuo cha Ualimu Kasulu, Mheshimiwa Waziri jambo hili nilishamweleza, nimefanya ziara ofisini kwake kwa jambo hili. Maabara ya Sayansi iliyopo Chuo cha Kasulu, inahitaji Walimu (*instructors*) wa masomo ya Kemia, Biolojia na Fizikia pia na Hesabu. Kwa sababu Maabara ipo, leta Walimu hao ili wasaidie kuzalisha Walimu wengine hasa kwa ajili ya Shule za Sekondari za Kata.

Mheshimiwa Naibu Spika, Shule ya Sekondari Kasangazi na Bongwe Wilayani Kasulu, hizi ni shule za zamani kidogo, tumeziteua na Wizara imekubali kuzipa hadhi ya Kidato cha Tano na Sita. Tunaishukuru na kupongeza hatua hii. Nashauri, tuleteeni pesa za kutosha hata kama ni zile fedha maalum kwa Mikoa ya pembezoni i.e Kigoma, Rukwa etc. kwa ajili ya maabara, nyumba za Walimu, motisha ya mazingira magumu na vyombo vya usafiri angalu basi tupage magari mawili ya Shule za Sekondari kwa kuanzia (Kasangazi *Secondary School and Bongwe Secondary School)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tuleteeni fedha kwa ajili ya kupima maeneo ya shule hizi mbili kwa ajili ya kuwezesha upanuzu wa shule hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Elimu, itoe miongozo rasmi kwa Walimu Wakuu wote wa Sekondari, Mkoani Kigoma juu ya taratibu za kuongoza shule Mifano vituko vya kufukuza wanafunzi eti kwa kukosa michango unakera sana. Kuwe na Kanuni rasmi kwamba *Headmaster* azuiliwe kumfukuza mtoto shule kwa sababu ya michango tena mingine ya kijinga tu. Mfano, mchango wa kitambulisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, Walimu kurundikana mjini kwa visingizio mbalimbali. Mkoa wa Kigoma, kama ilivyo Mikoa mingine, Walimu wengi wa Shule za Msingi na hata baadhi ya Sekondari wamerundikana katika maeneo ya mijini. Tafadhali, toeni miongozo juu ya jambo hili. Mfano Wilaya ya Kasulu ina Walimu wengi sana katika shule zilizopo Kata ya Kasulu mjini na ile ya Murufyiti hasa vijiji vya Nyansha na Nyantale. Tafadhali toeni miongozo, Kisera ili Walimu wengi wa Shule za Msingi wapelekwe vijijini. Jambo hili tumelizungumza hata katika ngazi ya Halmashauri ya Wilaya, msukumo wa Wizara bila shaka utasaidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Walimu wa kike kupewa haki ya kufuata waume zao. Yapo malalamiko ya Walimu wa kike kuzuiliwa kufuata waume zao eti kwa sababu mwajiri wake hajaridhia. Tafadhali lieleze Bunge juu ya taratibu za kiajira kwa wanawake kufuata waume zao wanapoolewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Idara ya Ukaguzi wa Shule za Msingi na Sekondari, nashauri Wizara iimarisheni Idara hii kwa sababu ni muhimu sana.

**MHE. ENG. CHRISTOPHER K. CHIZA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongeza Waziri, Naibu Mawaziri, Katibu Mkuu na wataalamu wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukaguzi wa shule. Eneo hili linastahili kuongezewa uwezo kwa maana ya Walimu wenye sifa za kitaaluma na uzoefu. Aidha, wanastahili kupewa posho na usafiri ili wasiendelee kutegemea fadhila za Wakuu wa Shule. Nawapongeza sana Wakaguzi kwa kuwa wanakagua kama Walimu, wanafuata maadili ya Ualimu. Walimu wachache wamesahau taratibu za kazi zao hususan kuandaa masomo wanayofundisha, wengine wanafundisha kwa mazoea tu, tabia hii inarudisha nyuma ubora wa elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ufundishaji wa Sayansi. Hili halina mjadala, tunahitaji wanasayansi katika nchi hii na lazima tuwafundishe sayansi kwa nadharia na vitendo. Iko haja ya kuweka mpango mahususi wa kuanzisha Maabara, Walimu wa Sayansi, *Lab. Technicians* katika shule zote za Sekondari, binafsi na za Serikali i.e. tuwe na *Sub-programme* ya Sayansi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ufundishaji wa muda wa ziada. Ufundishaji katika muda wa ziada, maarufu kama *tuition,* hauna malengo mabaya isipokuwa baadhi ya Walimu hawautekelezi kwa malengo ya kuboresha. Nashauri mafunzo hayo pamoja na *Remedial Teaching,* yafanywe na Walimu walio na uelewa wa wanafunzi wao ili waweze kuwasaidia. Utaratibu wa Walimu kuanzisha madarasa makubwa ya jioni au wakati wa likizo siyo "*effective*" kwa wanafunzi. Baadhi ya madarasa yana wanafunzi zaidi ya 100 na Mwalimu anakuwa kama *University Lecturer*. Uwekwe utaratibu na wanaoendesha madarasa kama hayo ikiwezekana wakaguliwe kwa sababu wanalipwa.

**MHE. JOHN P. MAGUFULI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nianze kwa kuwapongeza Manaibu Waziri wote wawili, Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara, kwa kazi nzuri, naunga mkono hoja ya Waziri. Ninaomba yafuatayo yafanywe na Wizara.

(1) Shule ya Sekondari Bwanga ifunguliwe, kwani majengo yote yapo na majengo yote tulikabidhiwa na Wizara ya Miundombinu na ni majengo ya kisasa. Hivyo nakuomba Mheshimiwa Waziri twende wote mwezi ujao ukafungue shule hii na iwe *High School*.

(2) Naomba Shule za Sekondari Zakia Meghji iliyoko Mganza, iwe *High School* na hasa kwa wasichana na hasa kwa vile mabweni kwa ajili ya wasichana yapo na majengo sasa yapo ya kutosha.

(3) Ninaomba ombi langu la siku nyingi la kupatiwa usafiri kwa ajili ya Shule za Sekondari za Wilaya ya Chato. Wilaya nzima, tuna shule zaidi ya 22 za Sekondari lakini hazina hata gari moja. Naomba Wizara itusaidie hata gari moja kwa shule zote 22 waweze ku-*share* katika matumizi.

(4) Upungufu wa Walimu. Tafadhali nisaidiwe Walimu katika shule 22 zilizo katika Wilaya yangu ya Chato.

(5) Ikiwezekana tupatiwe Chuo cha Ufundi angalu kimoja na hasa kwa sababu Wilaya sasa ina *population* inayokaribia watu laki sita hivi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho naunga mkono hoja ya Wizara hii. Hongera, Hongera, Hongera sana Mheshimiwa Prof. Maghembe, Mheshimiwa Mwantumu na Mheshimiwa Kabaka, Katibu Mkuu na Wizara yote kwa kazi nzuri.

**MHE. CLEMENCE B. LYAMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, Mheshimiwa Profesa Jumanne Maghemba

(Mb), Naibu Mawaziri, Mheshimiwa Gaudentia Kabaka (Mb) na Mheshimiwa Mwantumu Mahiza (Mb), Katibu Mkuu na watendaji wote ambao wamesaidia katika kumwezesha Mheshimiwa Waziri kuandaa na kuwasilisha hotuba hii vizuri kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, elimu ni msingi wa maisha na maisha yatafurahiwa na kila mwananchi pale ambapo uadilifu baina ya watu wengi unakuwepo katika jamii. Kwa kuwa uadilifu unakuzwa katika maisha ya binadamu tangu utotoni, sasa kuna umuhimu wa pekee, katika mazingra tuliyonayo, kwa Serikali kuanzisha mitaala ya uadilifu katika shule za mzingi, Sekondari na hata Chuo Kikuu. Kwa njia hii, watoto wetu ambao ndio wafanyakazi/waajiri au waajiriwa wa kesho, watakuwa waelewa wa masuala ya uadilifu katika wajibu wao na mipaka yao ya mahusiano na kazi watakazokuwa wanazitekeleza miongoni mwa wananchi watakaojumuika nao katika maisha yao. Lengo kuu la mitaala ya somo la uadilifu liwe ni kukuza dhamira ya uadilifu katika mwenendo wa maisha ya wanafunzi, ambao ni wazazi watarajiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Ualimu, ni kazi ngumu kwa kila hali na imegubikwa na mazingira magumu yanayohitaji kujitolea na kuvumilia mambo mengi ya ki-utendeaji, naishauri Serikali iibue "*pay package*" maalum ili kuwafariji kwa adha za kila aina ambazo zinawakumba Walimu. Wizara ni budi itoe motisha maalumu ili kuwavuta wahitimu wa Shule za Sekondari na Vyuo Vikuu wavutike kujiunga na kazi ya Ualimu ili kukabili uchache wa Walimu nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi maalum kwa Mheshimiwa Waziri ni kwamba naomba Walimu wa ziada katika Shule ya Msingi Malangali, Jimbo la Mikumi, ambayo ina wanafunzi 400 lakini ina Walimu watatu tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na uhaba wa Walimu, ipo haja ya Serikali kusisitiza Waratibu wa Elimu katika kila Kata kwa kushirikiana na Walimu Wakuu wa Shule, kuchunguza muda halisi ambao Walimu katika Shule za Msingi na za Sekondari wanautumia kufundisha. Zipo dalili zinazoonyesha kuwa katika shule ambazo Walimu hawautumii vema muda wanaopaswa kufundisha, ufaulu ni wa chini na utoro wa wanafunzi ni mkubwa. Udhibiti wa muda wa Walimu kufundisha upewe kipaumbele kwa kuratibu na kueleza bayana Walimu ambao wazembea kufundisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Kata nyingi katika Jimbo la Mikumi (Wilaya ya Kilosa), Walimu wanalamika kuhusu Mfuko wa Bima ya Afya, ambavyo hauwanufaishi kabisa, hasa wanaoishi vijijini ambako ndiko kuna Walimu na shule nyingi. Naiomba Wizara iwasiliane na taasisi husika ili tatizo hili limalizike vinginevyo wanaomba wasikatwe na fedha walizochangia warudishiwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nimpe taarifa Mheshimiwa Waziri kwamba Kata za Vidunda na Uleling'ombe katika Tarafa ya Mikumi, Wilaya ya Kilosa, ni Kata zilizo katika mazingira magumu sana. Tatizo kubwa ni ukosefu wa barabara kupandisha miamba, milima mikali sana kabla ya kufika ofisi za Serikali na shule katika vijiji mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Kata hizi hata baiskeli ni chache sana kwa sababu haziendesheki kutokana na milima mikali. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri kuwa endapo Wizara itaibua mfumo wowote wa kutoa huduma maalum, motisha zozote au upendeleo fulani kwenye maeneo yenye mazingira magumu, Kata hizi nazo zitazamwe. Nimeandika barua kwa Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI ili azijumuishe Kata hizi katika Kata zilizo katika mazingira magumu kwa vile sikuziona katika orodha yake katika hotuba ya bajeti yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya mchango huu, naunga mkono hoja.

**MHE. MWANAWETU S. ZARAFI**: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hotuba hii na ninawapongeza kwa utendaji mzuri na malengo na mipango mizuri ya elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu shule maalum kwa ajili ya walemavu, ziko chache. Nashauri kwamba endapo Halmashauri yoyote itakapojitokeza kujenga shule ya aina hiyo basi Serikali isaidie kutoa msaada japo kwa vifaa vya kufundishia. Mfano Kilwa Masoko ambako Afisa Elimu wa Wilaya na watendaji wake ambao wamefanya *renovation* majengo ambayo yalikuwa ni *middleschool* ya Mtanga ili iwe Shule Maalum ya Wasioona na wasiosikia. Nategemea Wizara mtaliona hili ili kuinua kiwango cha elimu katika maeneo ya pembezoni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mkopo wa *Baypot*. Ingawaje suala la mkopo huu linaihusu Wizara ya fedha, lakini kwa kuwa Wizara ya Elimu ndiyo nguzo ya Walimu hawa, naiomba Wizara iingilie kati kuhusu mkopo huu. Mimi binafsi nimeona *salary slip* ambayo ina mkopo wa shilingi laki sita (600,000), hadi siku niliyoona Mwalimu huyo alikuwa ameshakatwa milioni tatu. Kwa kweli, ni mateso kwa Walimu waliokopa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mpango ujao wa kujenga Maabara ya Shule za Sekondari za Kata, kama ilivyonukuliwa kwamba zitajengwa awamu kwa awamu, naiomba Wizara, ili kuwasaidia watoto kupata elimu iliyobora basi ijenge walau katika kila tarafa shule mbili au tatu zinazokaribiana ili Walimu waweze kuwapeleka wanafunzi kwa mafunzo ya maabara kwenye Sekondari hizo jirani.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawatakia kazi njema. Naunga mkono hoja.

**MHE. AGGREY D.J. MWANRI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo langu la Siha, naomba kuchukua fursa hii, kumpongeza sana Mheshimiwa Prof. Jumanne Maghembe, (Mb), (Prof), (MNEC), Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, kwa hotuba nzuri na yenye uchambuzi wa kina ambayo ameitoa asubuhi ya leo. Kipekee, nawapongeza Manaibu Mawaziri, Mheshimiwa Gaudentia Kabaka (Mb) na Mheshimiwa Mwantumu Bakari Mahiza (Mb), ambao pamoja na watumishi wa Wizara ya Elimu wanafanya kazi nzuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimefurahishwa sana na mpango wa Wizara wa kuhakikisha kwamba kila shule nchini inakuwa na maabara ambazo zitawasaidia sana vijana wetu kujifunza kwa vitengo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nitumie nafasi hii, kuipongeza Serikali kwa kuongeza Vyuo vya Ufundi pamoja na kuviboresha ili viweze kutoa taaluma yenye tija kwa maisha yao. Ni kweli vyuo hivi vya ufundi vinasaidia sana vijana wengi kuondoka kijiweni na kuwa tayari kujiajiri. Ninaiomba Serikali kutafuta fedha za kuwanunulia vifaa vinavyoendana na fani zao kwa kuwakopesha kila mhitimu kukabidhiwa mara anapohitimu mafunzo yake. Mapango huu utasaidia vijana kujiajiri wenyewe kila wanapomaliza mafunzo yao. Nasubiri majibu tafadhali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuunda Idara Maalum ya Walemavu. Ni ukweli usiofichika kuwa sasa idadi ya walemavu inazidi kuongezeka siku hadi siku. Kwa kuwa Bunge liliishapitisha mikataba ya walemavu yenye lengo la kutoa, haki ya elimu, haki ya kupata ajira na haki zingine zote za msingi na kwa kuwa Serikali ina kitengo kidogo tu kinachohudumia walemavu, ninaomba sasa Serikali kuangalia uwezekano wa kuunda Idara Maalum ya Kuhudumia Walemavu ambao sasa ni wengi mno nchini. Nasubiri majibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa Maabara Shule za Sekondari, bado kuna matatizo makubwa sana la shule zetu za Sekondari hasa za Kata kukosa Maabara jambo ambalo linasabisha utoaji wa taaluma kuwa duni sana. Ninaishauri Serikali suala la kujenga Maabara kulipa kipaumbele ili taaluma inayotolewa iweze kuwa na tija kwa maisha yao na Taifa kwa ujumla. Hivyo, fedha zaidi zitafutwe kwa ujenzi wa Maabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la wasichana kukatisha masomo kwa ajili ya kupata mimba lipo na ni kubwa. Ninaiomba Serikali kuandaa mpango maalumu, wasichana wanapojifungua wapewe nafasi tena ya kumalizia masomo yao kama wanavyofanya wenzetu wa Zanzibar. Hii itasaidia wanawake kufikia 50/50 kwenye vyombo vya maamuzi na sekta mbalimbali za Serikali.

**MHE. ZULEIKHA YUNUS HAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na watendaji wote kwa hotuba yao nzuri yenye kueleweka. Naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mipango yote iliyosomwa kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri lakini bado hali ya kifedha haitoshelezi kwa sababu hizi zilikuwa Wizara mbili na sasa imekuwa moja. Kama tunavyojua, elimu ni ufunguo wa maisha kwa hiyo inahitaji sana kupewa kipamaumbele kwa mambo yote yanayohusu elimu tangu elimu ya maandalizi, msingi, Sekondari, hadi Vyuo Vikuu. Hivyo ingekuwa vizuri baada ya mwanafunzi kuanza shule ya msingi naomba uwekwe makakati wa kuanza maandalizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali kwa kufanikiwa ujenzi wa Shule za Sekondari za Kata pia nawapongeza, wananchi, jamii na Taifa kwa ushirikiano wao kwani bila ya wao, yote yasingefanikiwa. Lakini sasa pia iwekwe mikakati na juhudi ya kupatikana Walimu, vitendea kazi na kuboreshwa majengo na Walimu walipwe hayo mafao yao haraka iwezekanavyo kwani ni aibu kwa Taifa na kweli wanastahimili sana wamechoka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu elimu ya watoto walemavu, nayo izidi kutiliwa mkazo kwani bado hawafaidiki kupata matunda ya elimu na haki yao ambayo ni ya msingi kwa kila mtu. Ukiangalia shule za wenye ulemavu, vifaa na hata Walimu hamna. Pia kuna vikwazo vya majengo ikiwemo miundombinu na matatizo mengine mengi yakiwemo ya chakula. Mwezi uliopita, Mwalimu Mkuu wa shule ya Irente, alisikitika sana kupitia kwenye redio kutokana na fedha kidogo anazopewa za chakula na uendeshaji, matatizo hayo yapo karibu shule zote maalum na katika vituo vya watoto wenye ulemavu vinavyoendeshwa na Mashirika ya Dini. Naomba Wizara iwe na mpango wa kuwasaidia na ahadi zinazowekwa na Wizara zitekelezwe kwani wanasikitika sana kwa mfano kama hichi kituo cha Miyuji hapa Dodoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Vyuo vya Ufundi viboreshwe kwani vimeanza kusahaulika na humo ndio wanamotoka, Mainjinia, Wasanifu wa Majengo na mambo mbalimbali. Kuna masomo yamesahauliwa, kama masomo ya *technical drawing, polytechnic* na *art* kwa kutumia rangi za maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nashauri kuwe na silabasi zinazofanana baina ya shule za Bara na Visiwani kwa sababu mtihani wa *Form IV* wanaofanya ni mmoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, naitakia kila la kheri Wizara.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na malalamiko toka wa wananchi wa Mbezi Juu (maeneo ya Mbezi Beach) ya kwamba wana shule moja tu ya msingi inayotegemewa hadi na wananchi wa Goba. Kibaya zaidi, wanafunzi wanakaa chini, madawati yapo Darasa la Saba tu. Halikadhalika, wanafunzi wa darasa la Kwanza wameunganishwa na wa chekechea.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri, anipatiwe ufafanuzi wa kero hii na ni kwa kiasi gani suala hili linaweza kutatuliwa na Wizara.

**MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii. Kwanza, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa maandalizi mazuri ya hotuba yake pia kwa kuiwasilisha vizuri. Kazi inayofanyika katika Wizara yake, ni nzuri kwa upande wa ongezeko la Shule za Sekondari ambalo limechangia ongezeko la idadi ya watoto wanaopata elimu hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya pekee, niipongeze Serikali kwa kazi nzuri ya ujenzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma ambacho kitasaidia kuinua elimu katika nchi yetu.

Wahitimu wa fani ya Ualimu kutoka Chuo cha Dodoma, watasaidia kupunguza uhaba wa Walimu hasa wa Shule za Sekondari.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Waheshimiwa Wabunge wengi wameshachangia kuhusu masuala mengi ya msingi, sitapenda kuyarudia sana. Napenda nianzie mchango wangu kwa kuzungumzia matatizo ya uhaba wa Walimu na jitihada ambazo Wakuu wa Shule wanazifanya ili kutatua tatizo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika shule zetu za Kata, zenye upungufu wa Walimu imebidi Wakuu wa Shule kuamua kuomba msaada kutoka kwa vijana waliohitimu au Kidato cha Nne na Sita au Vyuo visivyo vya Walimu na kukosa ajira ili waweze kupunguza tatizo la uhaba wa Walimu. Kutokana na hilo, inabidi Wakuu wa Shule kutumia michango ya wazazi kuwalipa vijana hawa kiasi kidogo kipatacho shilingi 60,000 kwa mwezi. Vijana hawa wangependa wapate walau shilingi 100,000 lakini uwezo huu wa Wakuu wa Shule wameshindwa kuzipata. Napenda kuishauri Serikali iweke utaratibu wa kuongezea shule hizi ruzuku ili kuwapata vijana wengi wa kujitolea kwa mtindo huu kwani Wakuu wa Shule zetu za Kata wanakiri kabisa kwamba vijana hawa wanaojitolea, wamekuwa wakisaidia kwa kiasi kikubwa kuboresha ufaulu wa wanafunzi wetu wa Shule za Sekondari.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie pia ufaulu usioridhisha wa wanafunzi wanaochukua masomo ya sayansi. Shule ya Sekondari ya Mtwara Girls ilianzisha mchepuo wa *CGB* miaka miwili iliyopita. Kwa kweli, inasikitisha kuona kwamba matunda ya kwanza ya wanafunzi wa *CBG* kutoka shule hiyo kongwe mwaka huu 2009 ni wanafunzi watatu tu ndio waliopata Daraja la Tatu, watano walipata daraja la nne na saba waliopata sifuri. Kimsingi, wanafunzi hawa hawakutendewa haki kutokana na kuanzishwa mchepuo huu kabla ya kufanyika maandalizi ya kutosha kuwapata Walimu wa masomo ya Kemia na Bailojia. Wanafunzi hawa wa kike hawakupata mafunzo ya "*practicals"* hadi dakika za mwisho za kukaribia mitihani. Hata hivyo, wale wanafunzi wanane waliofaulu kati ya wote 15, kutokana na jitihada zao binafsi za kwenda Dar es Salaam na kupata mafunzo ya "*Practical"* na mafunzo ya ziada ya nadhari. Napenda kuishauri Serikali ifanye uchunguzi wa kina kwa zile shule zinazoomba kuanisha michepuo mipya ili kuhakikisha kama kweli shule hizi zinakidhi mahitaji ya kuwepo michepuo hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine la muhimu ni kuhusu mahitaji ya watoto walioko katika mazingira magumu. Pamoja na Wizara kujitahidi kuwalipia ada, watoto hawa wapatiwe mahitaji mengine kama madawati na madaftari vile vile sare. Naiomba Serikali ilitazame hili lakini vile vile iwe ikiacha fungu la tahadhari kwa wale ambao wanapoteza wazazi wao baada ya bajeti kuwa imepitishwa. Watoto wa aina hii, ni wengi na inasikitisha kuona kwamba watoto hawa wanarudishwa nyumbani kutokana na kukosa karo baada ya mali ya wazazi wao kudhulumiwa na ndugu na jamaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie kwa kuishauri Serikali ilifanyie kazi haraka suala la kuhakikisha kuwa watoto wanaobeba mimba wakiwa masomoni wanapata fursa ya kumaliza masomo yao. Kama takwimu zinavyoonyesha, watoto hawa ni wengi na

hivyo wakiachwa bila kumaliza masomo yao, tutakuwa tumesababisha athari kubwa kwao na kwa watoto wanaozaliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru tena kwa kuupokea mchango wangu na ninaunga mkono hoja, ahsante.

**MHE: AMEIR ALI AMEIR**: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, nimshukuru sana Mwenyezi Mungu, kwa kunijalia uhai na uzima wa afya na kunijalia kuchangia hotuba hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri, kwa uwasilishaji wa hotuba yake. Pia niwapongeze Manaibu Waziri wote, Katibu Mkuu na Watendaji walioshirikiana, kwa kuandaa Hotuba hii ya Bajeti ya 2009/2010.

Mheshimiwa Naibu Spika, Baraza la Mitihani linafanya kazi kubwa ya kutunga mitihani na kudahili wanafunzi wote nchini Tanzania. Kazi hiyo ni kubwa na inahitaji uadilifu wa hali ya juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Idara hii imekumbwa na misukosuko mingi ya uvujaji wa mitihani na usahihishaji mbovu wa mitihani.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali hii hufanywa kwa makusudi na baadhi ya watumishi wasio waaminifu na kuitia doa Taasisi hii na kuwasababishia usumbufu watahiniwa na hasara kwa Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaipongeza Serikali kwa kuwachukulia hatua zinazofaa za kuwafukuza kazi na baadaye kuwashtaki.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia ninaiomba Serikali, isiyumbishwe kwa hatua zilizochukuliwa na izidishe kasi ya kuwatafuta waliobaki bila kujali ni nani na anatoka wapi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kutoa dukuduku langu, ninaomba kuuliza kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa katika mwaka huu usahihishaji wa mitihani haukuwa wa haki na kusababisha baadhi ya wanafunzi kukata rufaa na kubainika kuwa kweli kulikuwa na kasoro. Je, hatua gani zitachukuliwa kwa wale ambao hawakukata rufaa kutokana na hali zao kuwa duni lakini wanalalamika?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mheshimiwa Waziri anijibu wakati wa kujibu hoja zake.

Mheshimiwa Naibu Spika, hakuna jambo linalonikera moyoni kama migomo ya wanafunzi, kwani sielewi inasababishwa na kitu gani na kwa maoni yangu binafsi, naona kama kuna mkono wa mambo ya siasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba suala hili lichunguzwe kwa makini na lisichukuliwe kuwa ni jambo la kawaida, kwani linailetea aibu Taifa letu na hasara kubwa kwa Taifa pia.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninashauri kuanzia sasa fomu za kujiunga na Vyuo Vikuu zieleze bayana, kwa kila mwanafunzi ajue anastahili nini na afanye nini kabla hajajiunga na anapojiunga anastahili kulipwa nini, pamoja na mambo mengine yatakayoboresha na kuzuia migomo hiyo ili kuweza kumchukulia hatua mwanafunzi. Pia Serikali ilipe mafao yanayomhusu mwanafunzi kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ichukue hatua kali kama ilivyofanya katika Baraza la Mitihani. Serikali iache kigugumizi wakati wa kutoa adhabu kwa wahusika, kwa sababu wanaofanya mgomo huwa wanaandaliwa na wanaowaandaa baadaye huwakingia kifua kwa kuwaombea msamaha na wanapofanikiwa maombi hayo, hujigamba na kujisifu hakuna Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali lazima ijiamini kwa asilimia 100 katika maamuzi yake. Huruma hailei mwana (mtoto); mtoto umleavyo ndivyo akuavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Zanzibar mgomo wowote ni haramu na atakayejaribu au kushawishi, atakiona cha moto na ndio maana hakuna mgomo Zanzibar. Serikali iige mfumo huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. SAID A. ARFI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kukupongeza, pamoja na Kamati ya Uongozi, kwa kutenga siku moja kujadili hoja ya Wizara ya Elimu, ambayo ndiyo Wizara Kiongozi kwa kutengewa fedha nyingi katika bajeti na kipaumbele cha nchi yetu cha kwanza. Kwa makusudi au kwa sababu mnazozijua, mmeamua kutokutoa fursa kwa Wabunge, kuchangia hoja ambayo inagusa ustawi wa watu na nchi yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi sikuridhishwa na uamuzi huo. N ni dhahiri uamuzi huo unawanyima Wabunge nafasi ya kuishauri ipasavyo Serikali na hususan Wizara hii, ambapo yapo malalamiko mengi kutoka kwa wananchi na wadau wa elimu. Hata hivyo, kwa uchache tu niseme kwamba, Watanzania wanahitaji elimu bora na siyo bora elimu. Lengo siyo tu idadi ya wanafunzi wanaodahiliwa, tunahitaji mabadiliko makubwa kwa kadiri tunavyoona ubora wa elimu ukiporomoka siku hadi siku. Bila kuangalia matatizo ya Wizara hii kwa uhalisia wake, tunaliua Taifa hili tukidhani tumepiga hatua katika elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie kusema, unahitajika mjadala wa Kitaifa juu ya kadhia hii na maendeleo ya elimu nchini; vinginevyo, tunajidanganya kwa maneno na maandishi matamu katika vitabu vya hotuba na machapisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, kimsingi, yapo matatizo mengi yanayohusu walimu, majengo, vitendea kazi na programu zake. Majadiliano ya kina na uwazi yanahitajika kwa mustakabali wa elimu na maendeleo yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana.

**MHE. DKT. WILLIBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchangia kama ifuatavyo:-

(i) Mwaka jana niliuliza kuwa Sera ya Serikali wakati inafuta UPE ilitangaza kuwa kila mtoto atakuwa analipiwa na Serikali $10 kama fidia ya UPE. Kamati yetu ya LAAC wakati wa ukaguzi wa mahesabu ya Halmashauri mbalimbali za Wilaya, imegundua kuwa, fedha za *Capitation* zilikuwa zikitolewa zinapitia Hazina, TAMISEMI na OC. Nashukuru hali hii sasa imerekebishwa na hivyo kuondoa utata wa uwazi uliokuwa umejitokeza. Hata hivyo, Kamati ya LAAC imegundua kuwa, fedha zinazotolewa kwa kichwa cha motto, hazijawahi kufikia $10 bali imekuwa kati ya Sh. 5,000 na 7,000. Hali hii inahatarisha ubora wa elimu na kwa maana hiyo, watoto katika Shule za Serikali hawatapa *fair play ground* katika mitihani na kuna ushahidi kuwa, shule binafsi katika mitihani zimekuwa zikishika nafasi ya kwanza (*overall)* hadi ya 20.

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, japo elimu sasa imehamia TAMISEMI lakini sera bado iko Wizara ya Elimu, je, Wizara inatoa kauli gani hii sera ya $10 kwa mtoto imebadilika ama la?

(b) Kwa kuwa kiwango hiki kinaendelea kushuka Serikali inatoa tamko gani na hatua madhubuti kurekebisha hali hiyo ili watoto wetu wasiathirike kwa kukosa elimu bora?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa uteuzi wa Wajumbe wa Bodi umeachiwa Mkuu wa Shule kama anavyoona na hakuna chombo chochote kinachodhibiti uteuzi huu:-

(a) Kwa kuwa shule zaidi ya nusu sasa ni Shule za Kata, yaani za wananchi, ambazo ujenzi wake kwa sehemu kubwa unachangiwa na wananchi na kusimamiwa na wananchi. Inapofika mahali Mkuu wa Shule anateua Bodi na mara nyingi bila hata kushirikisha uongozi wa kata husika, matokeo yake ni wananchi kususia, hasa pale wanapokuwa hawapewi taarifa ya mapato na matumizi kama ilivyoshuhudiwa na Kamati ya LAAC wakati wa *site visitation* au kufanya shughuli kwa kusuasua tu?

(b) Kwa hali ya sasa ni kwa nini Serikali isitoe tamko rasmi na uteuzi wa Bodi hizo usiwekwe chini ya Mamlaka ya Halmashuri badala ya Mkuu wa Shule kwa mchakato utakaowekewa utaratibu maalum?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna taarifa kuwa, hivi sasa Vyuo Vikuu kadhaa, vikiwemo Kairuki na Tumaini, vimeongeza ada kutoka Sh.1,500,000 hadi 2.5m. Hii

imefanyika wakati Bajeti ya Serikali imeshapita na hivyo ni vigumu Bodi ya Mikopo kupata fedha za kukidhi hoja/haja hii ya kuongezeka holela.

Ni vyema Serikali ikatoa tamko rasmi kuhusu ongezeko hili na kama wanafunzi katika vyuo husika watapewa nyongeza na Bodi kukidhi ongezeko hili, vinginevyo Serikali ijiandae kukabiliana na matokeo ya ongezeko hili. Nashukuru kuwa, sasa wanafunzi wote watapewa mkopo; lakini ni mkopo upi kwa viwango vipya au vya zamani?

Suala la Law School bado hatima yake haijawekwa wazi. Ni vyema Serikali ikaweka wazi haki wanazostahili wanafunzi wa *Law School.*

Malalamiko yanayohusiana na kuvuja kwa mitihani, hayajapatiwa ufumbuzi wa kina na Baraza la Mitihani. Kuna taarifa pia kuwa, Bunge halijapewa uzito kamili wa tatizo la uvujaji wa mitihani. Mathalani, mwaka jana, ilielezwa kuwa ni mtihani wa hisabati tu, lakini taarifa toka shule mbalimbali zinasemekana kusema kuwa, kuna mitihani mingine pia ilichapishwa na kutawanywa kwenye shule. Ni vyema, Bunge likaelezwa ukweli kwani kuficha ugonjwa, kifo kinaweza kuwaumbua. Serikali inatoa tamko gani kuhusu taarifa hizi ambazo zimezua minong’ono mingi kuhusu kauli ya Serikali kuwa uvujaji ni kwa hisabati tu?

Kuna malalamiko pia ya Uongozi kwenye Baraza. Inasemekana hata maamuzi ya msingi sasa yanafanyika bila hata kushirikisha Bodi ya Baraza. Je, Serikali imechukua hatua gani kurekebisha jambo hili kwani kuachia bila kuchunguza msingi wa malalamiko hayo athari yake ni kubwa?

**MHE. BENSON M. MPESYA**: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kwa kuelekeza mchango wangu katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nijulishwe kwa nini REOs wengi mishahara yao mwisho ngazi “H” na mshahara wao ni kuanzia Sh. 350,000 - 540,000 kwa mwezi na bado REO amepewa majukumu ya kuwasimamia DEOs ambao mishahara yao inaanzia Daraja “I” na kuendelea kwa mshahara wa Sh.1,260,000 kama Mkuu wa Idara. Kwa nini tumeamua kutowaheshimu REOs? Je, kasoro hii itarekebishwa lini ?

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo hili likiendelea hivi, linaleta kasoro kubwa sana katika usimamizi wa Sekta ya Elimu. Naomba maelezo ya kina, ndiyo maana sikuanza na kuiunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Shule ya Sekondari Iyumba – Mbeya ni kongwe na ni miongoni mwa shule kubwa nchini, lakini inakabiliwa na matatizo makubwa sana ; miundombinu mibovu, madeni ya umeme, maji, shule haina maktaba na vitabu ni haba. Mwaka jana, wakati wa Bajeti, Serikali iliahidi kupeleka vitabu na kuboresha maktaba, lakini mpaka sasa kimya. Tarehe 5 Julai, 2009, nilifanya ziara shuleni hapo, wanafunzi walitaka kuchoma moto gari la TANESCO walipokwenda kukata umeme. Bahati nzuri,

wafanyakazi wale walikimbia, mpaka sasa shule inadaiwa Sh.14,381,02864 mpaka tarehe 22 Julai, 2009. Pia kwa upande wa maji wanadaiwa shilingi milioni 17.

Mheshimiwa Naibu Spika, wazabuni wengi wamefilisika kwa kutolipwa fedha zao kwa wakati. Jambo hili limeleta shida sana na mahusiano mabaya kati ya shule na wazabuni.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba maelezo ya kina kabisa ya kutatua tatizo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania (OUT), kina hali mbaya sana kutokana na mambo yafuatayo:-

(a) OC imepungua sana na inaendelea kupungua siku hata siku na kufanya utoaji elimu uwe mgumu sana.

(b) OC hii ndiyo pia hutumika kulipa walimu wa part time, nashauri malipo ya walimu hawa yawe *ring-fenced* au zitolewe kama PE.

(C) Madeni ya chuo kutolipwa, matokeo yake ni migogoro kama iliyotokea Mpwapwa, kwa kuja Bungeni na hatimaye kupigwa mabomu na polisi. Ikumbukwe mimi na Mheshimiwa Beatrice Shelukindo, Wajumbe wa Baraza la Chuo Kikuu Huria, tulifika rasmi ofisini kwako na hatimaye kwa Waziri wa Fedha; bila shaka hatua zingechukuliwa mapema haya yote yasingetokea.

Tunampongeza sana Rais J. K. Kikwete, kwa mawazo yake ya uanzishaji wa Chuo Kikuu cha Dodoma. Hakika ni hatua kubwa sana, kwa maendeleo ya nchi yetu. Naomba nitumie nafasi hii pia kumpongeza sana Makamu Mkuu wa Chuo (VC), Prof. Idrisa Kikula, kwa usimamizi imara wa uendelezaji wa Chuo hiki. Ombi langu ni kwamba, wapo walimu zaidi ya 32, ambao wana shahada za uzamili. Ni vyema, mpango ufanywe wa kuwaendeleza ili wasomee shahada zao za uzamivu mapema na kukifanya Chuo hiki kuwa na rasilimali watu/nguvu kazi ya kutosha. Tukumbuke Chuo si majengo, bali wataalamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna ushirikiano gani kati ya CWT na Bayport? Kwa nini Chama cha Walimu hakielezi mahusiano yao na Bayport ambayo imekuwa mwiba katika kuwaibia walimu kwa riba kubwa zaidi? Kwa nini Serikali haitaki kuingilia kati suala la Bayport; mbona DECI imeingiliwa mapema au kwa sababu Bayport kuna majina ya watu wazito au vipi?

Mheshimiwa Naibu Spika, nikipata ufafanuzi wa haya, nitaunga mkono hoja. Niko *bitter.*

**MHE. DKT. BINILITH S. MAHENGE**: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Jumanne Maghembe (Mb), Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, kwa hotuba yake nzuri sana kuhusu maendeleo ya elimu nchini. Aidha, nawapongeza Manaibu Waziri wote, pamoja na Watendaji wa Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa shukrani zangu kwa niaba ya Wananchi wa Makete, kwa mambo makuu yafuatayo :-

(a) Ujenzi wa Chuo cha VETA Wilayani Makete. Tunashukuru sana kwa Serikali kusikia kilio cha Wananchi wa Makete, Wilaya ambayo ina watoto yatima wasiopungua 13,000. Mafunzo ya ufundi, yatawasaidia kupata stadi za kujiajiri wao wenyewe.

(b) Natoa shukrani kwa Serikali kupanga walimu 48 wa shule za msingi kwenda kufundisha Wilayani Makete, kutokana na maombi ya Halmashauri ya Makete.

Mheshimiwa Naibu Spika, wanafunzi wa masomo ya sayansi kupewa mikopo asilimia 100 ni uamuzi wa kupongezwa sana. Nchi zilizoendelea, zimeendelea kwa sababu zinaweka kipaumbele Sekta ya Sayansi na Teknolojia. Kwa hiyo, uamuzi huu ulikuwa unasubiriwa kwa hamu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, maelezo ya ufafanuzi: Serikali iliahidi kupitia Hotuba ya Waziri Mkuu kwamba, itatenga fedha kwa ajili ya kuzisaidia shule za Wilayani, ambazo ziko katika mazingira magumu ambayo husababisha walimu kutokwenda kufundisha katika Wilaya hizo. Hotuba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, haioneshi mkakati wowote wa kutekeleza ahadi hii. Serikali ifafanue.

Mheshimiwa Naibu Spika, Shule za Sekondari za Wilaya ya Makete, hazipati walimu wa kutosha. Tunaomba Serikali itoe kipaumbele kwa Wilaya hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. DKT. GUIDO G. SIGONDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Shule ya Sekondari ya Southern Highlands ya Mbeya ilikuwa ni kati ya Shule tatu zilizofutiwa matokeo ya mtihani wa kidato cha nne mwaka 2007.

Mheshimiwa Naibu Spika, baadhi ya hitilafu zilizogundulika ni pamoja na kuwepo walimu ambao walikuwa hawana sifa za kuwa walimu. Wengine walibainika kuwa na vyeti vya kughushi akiwemo aliyekuwa Mwalimu Mkuu wa Shule hiyo ya Southern Highlands.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kushughulikia hali hiyo, Serikali iliahidi kuwachukulia hatua za kisheria wale wote waliopatikana na makosa ya kughushi vyeti vyao vya ualimu. Je, nini matokeo ya uamuzi huo wa Serikali?

Mheshimiwa Naibu Spika, je, mpango wa Serikali wa kutoa posho maalum kwa walimu wanaofanya kazi kwenye maeneo magumu utatekelezwa lini?

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo ambayo ni magumu kwa kufanyia kazi na ambayo yako mbali na yaliko matawi ya benki, walimu huwa wanahangaika sana kufuata

mishahara yao wakati wa mwisho wa mwezi.  Halmashauri ya Wilaya ya Chunya, imeweka utaratibu wa kupeleka usafiri wa gari kuwachukua na kuwarudisha walimu tokea maeneo yaliyo magumu kufuata mishahara yao mwisho wa mwezi.  Je, Serikali haiwezi kufikiria kuandaa gari kwa ajili ya kuwachukua walimu wakati wa kufuata mishahara yao?

Mheshimiwa Naibu Spika, walimu wanaoanza kazi kwa mara ya kwanza, hupata shida sana kupata vifaa vya ndani kwa kutokuwa na fedha; matokeo yake, walimu wengine hushindwa kununua hata vitanda, viti na vyombo vya kupikia.  Nashauri Serikali, ifikirie kutoa mikopo kwa walimu wapya ili walimu hao wasiendelee kunyanyaswa.

Mheshimiwa Naibu Spika, walimu wengi wangali wanadai kulipwa bima zao zilizokwishaiva.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. DKT. IBRAHIM S. MSABAHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja na kukupongezeni kwa kazi nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, elimu ndiyo miundombinu mama ya maendeleo ya binadamu; hivyo, lazima tujitahidi kuimarisha elimu katika ngazi zote.

Mheshimiwa Naibu Spika, uimarishaji wa elimu ya msingi ujikite katika maeneo yafuatayo:-

(1) Upatikanaji wa waalimu na hasa katika shule za vijijini ambako baadhi ya watumishi hawapendi kwenda ili maendeleo ya elimu yanayopatikana nchini, yawiane kati ya mijini na vijijini.

(2) Upatikanaji wa madawati na vitabu.  Pamoja na umuhimu wa wananchi kuchangia, lakini ni muhimu Serikali yenyewe ikatoa kipaumbele kwa kuchangia fedha.

(3) Ujenzi wa nyumba za walimu.

(4) Elimu ya Sekondari inahitaji msukumo katika upatikanaji wa madawati, vitabu, walimu, nyumba za walimu na kadhalika; usomeshaji wa masomo ya computer kuanzia shule za msingi; na ujenzi wa maabara.  Katika Jimbo langu, Sekondari ya Kilangalanga pekee, ndiyo yenye maabara; shule moja kati ya shule saba za sekondari za Kata tano za Jimbo langu.  Naomba shule zangu za Soga, Mlandizi A, Mihande, Kwala, Ruvu Station na Magindu, ziingizwe katika mpango wa ujenzi wa maabara.

Ujenzi wa Mabweni ni muhimu kwa watoto, pamoja na kuwa na shule za kata, wanafunzi wengi wanatoka vijiji vya mbali; wengine hata kilomota 15 -  20.  Kwa kuwa kijijini hakuna usafiri wa uhakika, wanafunzi hawa wanapata adha kubwa ya kusafiri masafa marefu.

Kuna tatizo kubwa sana Jimboni kwangu la *management* ya shule. Iko shule moja, Mkuu wa Shule, hajawahi kuitisha Bodi ya Shule kwa zaidi ya miaka mitatu sasa, licha ya matatizo lukuki yanayoikabili shule. Shule hiyo hiyo, baadhi ya walimu, wanagombea wanafunzi wasichana na wavulana hata kufikia kupigana! Ni vituko vitupu. Ni vyema shule hizi sasa ziko chini ya Halmashauri, lakini Watendaji wa Halmashauri, hawana *confidence* ya kusimamia kikamilifu shule hizi. Wakuu wa Shule wanajiona, wamesema na kudharau Viongozi wa Wilaya na Halmashauri. Nashauri, Wizara iendelee kufuatilia kwa karibu uimarishaji wa shule za sekondari.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kukabiliana na upungufu na ubora wa watalamu; ni vyema vyuo vyetu vikaunda mfumo wa kubakisha *(retain)*, uzoefu kwa kuruhusu wakufunzi kwenda kufanya kazi Sekta ya Umma na sekta binafsi na baadae kurejea kwenye Vyuo Vikuu kusomesha. Muingiliano huu, ndio unaojenga utaalamu na uzoefu wa kweli. Kuna wataalamu wengi waliostaafu au walioondoka Vyuo Vikuu, ambao wamepata uzoefu mkubwa katika kazi mbalimbali walizofanya au wanazofanya nje ya vyuo, ambao wangeweza kurejeshwa kwa mikataba. Vyuo Vikuu vya nchi zilizoendelea, vingi vimepata sifa za umahiri kutokana na utaratibu huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawatakia kazi njema na nawapongezeni tena Waziri, Naibu Mawaziri, Katibu Mkuu na Watumishi wote.

**MHE. JOYCE M. MASUNGA**: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, nichukue nafasi hii kumpongeza Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, kwa hotuba yake nzuri. Aidha, nawapongeza Naibu Mawaziri wote na Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara hiyo. Nasema hongereni kwa kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie kuhusu maslahi ya walimu. Pendekezo langu, ningefurahi iwapo kundi hili kubwa la wafanyakazi lingekuwa na chombo kimoja, kitakachomhudumia mwalimu. Nina maana kwamba, hivi sasa mwalimu anahudumiwa na Wizara nne; Elimu; TAMISEMI; Utumishi; na Fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi langu ni kwamba, ningefurahi kama wangehudumiwa na Wizara ya Elimu na TAMISEMI tu. Wizara ya Utumishi na Fedha, wangeendelea kuwahudumia wafanyakazi wengine. Nina maana ya kuwa, Wizara ya Fedha iwape Wizara ya Elimu, fedha zote zinazowahusu walimu na hivyo hivyo Wizara ya Elimu ishughulike na suala la utumishi wa walimu tu. Hii itapunguza mlolongo wa mwalimu; mara aende Utumishi, akitoka hapo aende Wizara ya Fedha. Huu ni usumbufu mtupu. Walimu namekuwa wengi, hivyo wanatakiwa washughulikiwe kipekee kama wanavyofanyiwa Jeshi la Wananchi. Kwa vile madaraka mengi yamepelekwa katika Halmashauri za Wilaya, sasa ni vizuri kwani mzembe atajulikana na kuwajibishwa. Badala ya mgomo kutokea nchi nzima, itakuwa inatokea wilaya au mkoa, ndipo tutakapojua nani ni mzembe na atashughulikiwa kikamilifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Idara ya Ukaguzi wa Shule, nionavyo mimi, Idara hii imezorota. Nasema hivi kwa sababu mimi nilikuwa mwalimu. Enzi hizo, wakaguzi

walikuwa wanaingia mashuleni kwa kushtukiza na wanaingia darasani, watakaa nyuma ya darasa wanakusikilia unavyofundisha, kisha atakagua andalio lako, pia ataangalia madaftari ya wanafunzi. Hivyo, walimu tulikuwa tunafanya kazi zetu kwa makini, ukijua kuwa hujui saa wala siku atakayoingia mkaguzi. Kwa kifupi, mkaguzi alikuwa anaogopwa sana. Hivyo, ombi langu ni kuwa hadhi ya ukaguzi irudishwe kwa nguvu mpya, kasi mpya na ari mpya, kwa maana ya kupewa uwezo wa kutekeleza kazi zao. Hivyo, Mkaguzi wa Wilaya, apewe majukumu ya kukagua shule zote za msingi na sekondari. Ili awe na ari mpya, apewe vitendea kazi vya kisasa mfano, gari, kompyuta na ofisi inayofanana na mkaguzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, michezo mashuleni imerudi, lakini haijarudi kama zamani. Napenda kumwambia Waziri wa Elimu kuwa, kilio kina mwenyewe na mwenyewe ni Wizara ya Elimu. Inatakiwa itenge fedha kwa ajili ya michezo ya wanafunzi. Hivi nini; Rais wa Nchi Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete anajitahidi kuleta makocha tunamshukuru sana, lakini makocha hao wanatakiwa wafundishe vijana wadogo ili waelewe michezo hiyo. Kama hatutakuwa na msisitizo mkubwa wa michezo mashuleni, hawa wanamichezo watapatikana wapi? Michezo ni afya, hivyo namwomba Waziri mhusika asikwepe jukumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie maslahi ya Afisa Elimu Mkoa na Wilaya. Maboresho yaliyofanywa miaka 2000, yaliwaondolea hadhi Maafisa Elimu wa Mikoa na kuwaita Washauri wa Elimu Mikoa, hivyo kuwafanya wabakie na mishahara midogo kuliko Maafisa Elimu Wilaya. Huu ni uonevu; itakuwaje mdogo apokee mshahara mkubwa na mkubwa apokee mshahara mdogo? Naomba Mheshimiwa Waziri, anifafanulie kwani Maafisa Elimu Mikoa hawatendewi haki na hawajisikii vizuri na hamu ya kazi imepungua.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue nafasi hii, kuwashukuru sana Wananchi wa Mkoa wa Shinyanga, kwa juhudi kubwa wanayoifanya ya kujenga Shule za Sekondari.

Mheshimiwa Naibu Spika, Awamu ya Nne ilipoingia madarakani, Shinyanga ilikuwa kama ifuatavyo:-

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 2006 | - | Shule 102 za sekondari | | |
| 2007 | - | tukajenga 117 | = | 219 |
| 2008 | - | tukajenga 31 | = | 250 |
| 2009 | - | tukajenga 5 | = | 255 |

Tunaishukuru Serikali kwa kutusaidia fedha, lakini pia tunawashukuru sana Wananchi wa Shinyanga, kwa kuchangia kwa hali na mali. Aidha, ninawaomba Wananchi wa Shinyanga, tuendelee kuchangia ili tujenge nyumba za walimu ili wafanye kazi vizuri wakiwa katika nyumba nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunachukua nafasi hii, kuishukuru Wizara kwa kutuletea walimu 1,846 wa shule za msingi. Kati ya hao; walimu 15 tu ndio wamepewa Manispaa. Nasema hao walimu 15 kwa Manispaa ya Shinyanga hawatoshi, kwani tuna

upungufu wa walimu 331. Aidha, tuna walimu 44 ambao ni wagonjwa na muda mwingi huhudhuria matibabu. Mnapogawa walimu, tunaomba mkumbuke kuipa walimu wa kutosha Manispaa ya Shinyanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mwalimu anaitwa Richard Jared Mpongo, yeye ni mwalimu asiyeona, alikwenda kutibiwa India kwa taratibu zote zinazokubalika. Kilichotokea, siku ya kuondoka wagonjwa wenzake walipewa fedha za kujikimu dola 500 na Wizara ya Afya, yenye akaambiwa atalipwa na mwajiri wake. Hivyo, tarehe 30 Desemba, 2004 alilazwa hospital ya huko India na akapewa ruhusa *(discharge)* tarehe 27 Januari, 2005. Cha kusikitisha ni kwamba, Mwalimu huyu aliishi hospitalini bila hata senti tano, akawa omba omba mpaka alipomaliza matibabu na kuruhusiwa. Cha ajabu, tangu 2004 hadi hivi ninavyoandika maelezo haya, hajapewa fedha zake dola 500 ! Je, huu ni uungwana ? Nani anayestahili kumlipa ? Mwalimu huyu kwa vile haoni, ananiambia wananifanyia hivi kwa vile ni mlemavu ? Anaomba asaidiwe. Je, aende kwa nani ili alipwe fedha yake halali ya kujikimu ? Naambatanisha barua alizonikabidhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuunga mkono hoja.

**MHE. BRIG. GEN. HASSAN NGWILIZI**: Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri, kwa kuwasilisha Hotuba ya Makadirio na Matumizi na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi. Naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana na mipango ya utekelezaji wa Wizara hii, kwa mwaka 2009/2010. Ila lipo tatizo ambalo naamini ni wakati muafaka kuanza kulishughulikia, nalo ni suala la mfumo wa elimu bora ya Bara na Zanzibar. Kwa hivi sasa, Zanzibar mwanafunzi akianza Darasa la Kwanza, anaendelea mpaka darasa la kumi na moja (Form III). Bara mwanafunzi anakatisha akifika darasa la VII, labda afaulu kwenda Form I. Ipo haja ya Wizara ya Elimu SMT na SMZ kukaa chini na kujadili suala hili hata ikibidi liingizwe kwenye orodha liwe la Muungano.

**MHE. DKT. CYRIL A. CHAMI**: Mheshimiwa Naibu Spika, pongezi kwa Wizara hii, ina viongozi wachapakazi hasa Mheshimiwa Waziri, Naibu Mawaziri, Katibu Mkuu na Watendaji wengine ; binafsi najivunia sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la mkopo kuwa mzigo, litadhibitiwa na Serikali kuanza kukusanya kwa dhati *(Seriously)*, mikopo iliyokopeshwa kwa wanafunzi kuanzia 1994. Kwanza, fedha zitaingia na kupunguza mzigo. Pili, wenye uwezo wakiona wenzao waliotangulia wanatozwa au wanalipishwa, hawatakuwa na kiu ya kujiingiza katika madaraja ya kupewa mikopo mikubwa. Hili nalo litapunguza mzigo.

Napendekeza Wizara iangalie uwezekano wa kuikodisha kampuni ya kukusanya madeni haya. The Yono Auction Mart Sort of Company, ianze na sensa ya waajiri wote na hao walazimishwe kutoa taarifa za wafanyakazi wao wote waliosomeshwa na Serikali kwa njia ya mkopo. Pia, waajiri walazimike kukata mishahara ya waajiriwa hawa (kama wakatavyo za NSSF na kadhalika) na kuziwasilisha Wizarani.

Ili hili lifanikiwe, Waziri wa Elimu angeleta Muswada hapa Bungeni ili sheria ipitishwe.

Walichofanya Rwanda *(one computer one child)*, kinawezekana Tanzania kama Waziri wa Elimu utawashawishi Viongozi wa Juu, hasa Mheshimiwa Rais na Waziri Mkuu. Bosi wa programu nzima ni Profesa Mkenya, aliyeko Harvard University, aitwaye Juma. Nilipoongea naye June, 2009 alisema, akialikwa atafurahi kuja Tanzania ili atushauri namna ya kuzipata kwa gharama nafuu au kwa kupitia wafadhili.

Yako mambo mengi yanayoweza kufanywa shuleni, bila kutegemea sana fedha za Wizara. Mashule yakielekezwa, yataomba fedha kutoka kwa wafadhili mbalimbali na mambo hayo yakafanyika. Ni hayo maeneo mawili ; shule kuvuna maji ya mvua ; na ujenzi wa mitambo ya kuzalisha umeme kwa kutumia biogas inayotokana na *waste* za binadamu. Kituo cha CARMATEC kilichoko chini ya Wizara Viwanda, Biashara na Masoko, kinao utaalamu wa kueneza teknolojia hizi mbili katika mashule, endapo Waziri wa Elimu atawasiliana na Mkurugenzi kuona namna ya kulifanikisha hilo, ambacho hatuna ni fedha, lakini Waziri wa Elimu na CARMATEC wakiandika *joint proposal*, *donors* wataona umuhimu wa kuchangia.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawasilisha.

**MHE. CHARLES N. KEENJA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Mawaziri na Watendaji wa Wizara, kwa hotuba nzuri na iliyosheheni maelezo muhimu, juu ya masuala muhimu yanayohusu elimu nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza sana Serikali, kwa mafanikio yaliyopatikana katika upanuzi wa elimu katika ngazi zote, kuanzia elimu ya msingi hadi elimu ya juu na ya ufundi. Mafanikio yaliyopatikana ni makubwa sana. Hata hivyo, mafanikio hayo, yameandamana na matatizo mengi na mazito, ambayo yanaendelea kushughulikiwa, lakini yatachukua muda mrefu kuyatatua na yataathiri vibaya kufikiwa kwa malengo ya elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni lazima Serikali ijenge mazingira yatakayowezesha kutolewa kwa elimu kwa viwango vinavyotakiwa. Mazingira hayo ni pamoja na kuhakikisha, kuwepo kwa walimu wa kutosha na wenye sifa zinazotakiwa. Kuwepo mipango ya kuandaa walimu waliobobea katika masomo wanayofundisha na katika mbinu za kufundisha masomo hayo. Aidha, shule zijengewe miundombinu inayotakiwa ; vyumba vya madarasa vitakavyowezesha kuwepo kwa uwiano wa watoto wasiozidi 45 kwa chumba cha darasa, maabara na karakana kwa masomo yanayohusika na majengo au vyumba vya utawala. Shule zipatiwe vitabu na vifaa vya kufundishia vya kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, baadhi ya watoto wanaishi mbali sana kutoka kwenye shule walizopangiwa. Kwa mfano, Dar es Salaam, idadi ya watoto wa aina hiyo ni kubwa sana, kwa kuwa shule nyingi zimejengwa pembeni mwa Jiji, ambako ndiko yalikopatikana maeneo ya kujenga. Ni muhimu sana watoto hawa, hasa wasichana, wakajengewa mabweni karibu na shule zao. Mabweni hayo yanaweza kujengwa na

Serikali, jumuiya za jamii au watu binafsi, vyovyote iwavyo ni lazima shule ziweke utaratibu wa kusimamia watoto watakaoishi kwenye mabweni hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, uzoefu umeonesha kwamba, kuwapatia watoto chakula cha mchana mashuleni, kunaongeza sana mahudhurio. Jambo hili ni muhimu kwa ngazi zote za elimu. Wazazi wanapaswa kuchanga ili kuhakikisha kwamba, watoto wao wanapata chakula wawapo shuleni. Serikali haipaswi kulionea suala hili haya, kutokana na manufaa yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni muhimu sana kwa Taifa letu, kufanya tathmini ya elimu tunayotoa ili kuhakikisha kwamba, inakuwa na manufaa yaliyokusudiwa. Elimu inapaswa kumuandaa kijana kwa maisha katika jamii. Lengo hili linafikiwa kwa kiwango gani? Asilimia zaidi ya 70 ya Watanzania wanaishi vijijini na shughuli yao kuu ni kilimo. Watoto wengi wanaomaliza shule za msingi na hata sekondari, watarudi vijijini au kuzurura mjini. Tunawaandaa vipi vijana kwa maisha vijijini hata mijini? Tuliwahi kuwa na shule zilizojulikana kuwa *middle schools,* ambazo zilifundisha kilimo, ufundi na masomo mengine. Mfumo huu uliachwa na Serikali ya Tanzania huru. Hivi sasa watoto wanaotoka kwenye shule za msingi, sekondari na hata vyuo vikuu, hawana ujuzi wowote wa kazi na katika vyuo vikuu, baadhi ya watoto au vijana wanachukua masomo yenye manufaa ya mashaka kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, elimu ina gharama kubwa sana, serikali inapaswa kuamua ni masomo gani ambayo itagharimia na uamuzi huo utokane na umuhimu wa somo katika jamii. Vijana watakaotaka kusoma masomo nje ya hayo, wajigharimie. Utaratibu huu, unatumiwa na nchi kama Cuba na umewezesha Nchi ya Cuba kwa idadi ya watu kuliko nchi yoyote duniani.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuige mifano hii mizuri.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimniwa Naibu Spika, napenda kutumia nafasi hii, kwa njia ya maandishi, kuwapongeza Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, Mheshimiwa Prof. Jumanne Maghembe, Naibu Mawaziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi ; Mheshimiwa Gaundentia Kabaka na Mheshimiwa Mwantumu Mahiza, Katibu Mkuu, pamoja na Watendaji wote walioshiriki kuandaa bajeti hii nzuri, yenye mtazamo thabiti wa kuinua elimu ya Tanzania kwa ngazi zote, yaani chekechea, elimu ya msingi, elimu ya sekondari, elimu ya juu na mafunzo ya ufundi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda nitamke rasmi kuwa, ninaunga mkono hoja hii, kabla sijaanza kutoa mchango wangu, nikiwa nina imani kuwa hoja zangu zitapatiwa majibu wakati Waziri na Manaibu wake, wakitoa ufafanuzi. Mungu awatangulie ili waweze kutekeleza malengo yao barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ninaanza kuchangia hoja hii kama ifuatavyo hapa chini :-

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imekuwa kubwa sana, ninapenda kuipa angalizo Serikali kuwa, kuunganishwa kwa Wizara hii kutoka Wizara mbili na kuwa Wizara moja, ukweli uwajibikaji wake umekuwa mgumu sana kwani Wizara ina idara nyingi na zote ni muhimu sana, mfano, Idara ya Chekechea; Idara ya Shule za Msingi; Idara ya Shule za Sekondari; Vyuo Vikuu; Vyuo vya Ufundi na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na Idara hizi nyingi, bado Wizara hii imekuwa na migogoro mingi sana na kumsababishia Waziri kuwa na majukumu mengi sana; hivyo hata muda wa kuweka mipango mizuri ya kuleta ufanisi ndani ya Wizara hii umekuwa adimu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaiomba Serikali, ifikirie upya kuigawa tena Wizara hii kuwa Wizara mbili. Hakika Mheshimiwa Prof. Maghembe, pamoja na juhudi zake, hataiweza Wizara hii. Mnyamwezi mwenye kuzoea mizigo mizito hataiweza. Ninasubiri majibu ya Serikali katika hoja ya msingi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni ukweli usiojificha kuwa, msingi wa maisha ya kila Mtanzania unatoka kwa mwalimu, wakiwemo viongozi wote wa nchi hii na watumishi wa sekta mbalimbali nchini. Hivyo, kuna kila sababu ya kuwajali walimu na kuwatia moyo kulingana na kazi yao ngumu na kufanya kazi katika mazingira magumu huko vijijini, ambako hata huduma nyingi muhimu hakuna.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaiomba Serikali itazame upya, mpango wa kuwarudishia walimu asilimia hamsini ya mishahara yao, ikiwa ni posho ya kufundishia. Nina hakika, posho hii ikirudishwa, itawapa ari mpya ya kufanya kazi barabara, kwa lengo la kuinua taaluma ya elimu Tanzania. Askari wa Jeshi la Polisi wameweza kuongezewa posho yao kutoka Sh. 50,000 hadi Sh.100,000, ambao wamefundishwa na walimu hawa hawa wanaofanya kazi katika mazingira magumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninawapongeza sana walimu, kwa wazo lao zuri la kuunda Chama cha Walimu Tanzania. Pia ninawapongeza Viongozi wa CWT, kwa jinsi ambavyo wamekuwa tayari kutetea kero mbalimbali za walimu, pamoja na matatizo ya mwalimu mmoja mmoja. Vile vile ninawapongeza Viongozi wa Chama hiki, jinsi ambavyo wamebuni mbinu ya kukuza pato la CWT kwa kuwekeza kwenye majengo; mfano, Jengo la Mwalimu House lililopo Ilala Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na yote haya mazuri, napenda pia kupitia Wizara hii kushauri yafuatayo: Kusaidia kusomesha walimu wenye nia ya kujiendeleza; kujenga nyumba za makazi na kuwapangisha walimu ama kuwakopesha kwa bei nafuu hasa mijini; kuwaanzishia walimu SACCOS ili waweze kukopeshana wao kwa wao; na kuwakopesha vyombo vya usafiri na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, inasikitisha sana kuona madai ya walimu bado yanaendelea kulimbikizwa kinyume na agizo la Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ninapenda kuikumbusha Serikali, kutokuwalipa walimu madai yao kwa muda muafaka ni kutokuwatendea haki. Pia fedha

ikikaa sana kwa mwajiri, kuna tatizo la kushuka thamani na pia humfanya mwalimu kuishi maisha duni, kwa kutopewa haki yake kwa wakati muafaka. Ninasubiri majibu ni lini Serikali italipa madai haya yanayokadiriwa karibu fedha za Kitanzania bilioni 53.6?

Mheshimiwa Naibu Spika, madai hayo ni ya fedha za matibabu, fedha za likizo, fedha za safari za kikazi, fedha za mishahara na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna tatizo pia la walimu wengi kukaa kwenye cheo kimoja muda mrefu bila sababu, ama walimu kupewa vyeo wasivyostahili, walimu wenye sifa ya kufanana kutofautiana vyeo. Hili ni tatizo naomba maelezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, inasikitisha sana pale mwalimu anapopangiwa kituo cha kazi kijijini, eneo ambalo halina nyumba za kupanga. Ili walimu waweze kufanya kazi vijijini; ni vyema sana Serikali ikatoa kipaumbele cha kujenga nyumba za walimu. Hii itasaidia walimu kukubali kufundisha vijijini na kusaidia taaluma ya elimu hasa ya Sekondari za Kata kupanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni ukweli usiopingika kuwa, Wizara ya Elimu ina migogoro mingi sana; mfano, mikopo ya elimu, mishahara, madaraja ya walimu, kiwango cha elimu, nyumba za walimu, mitaala ya kufundishia na kadhalika. Hivyo basi, ninaishauri Serikali kuunda Tume ili iweze kujadili mambo yote haya upya, kwa lengo la kuboresha taaluma, pamoja na mfumo mzima wa elimu ya Tanzania. Hata hivyo; ni miaka zaidi ya 20 tangu Marehemu Baba wa Taifa, alipounda Tume ya Makwetta kupitia sekta mbalimbali za elimu. Nasubiri ufafanuzi wa Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna tatizo kubwa sana shule zetu za sekondari hasa za Kata, kukosa hosteli kwa wanafunzi hasa wasichana. Tatizo ambalo linawafanya wanafunzi kupanga mitaani na wengi wao kupata mimba na kukatisha masomo yao. Mfano hai ni Shule ya Sekondari ya Mungungira, ambayo imefungwa kwa sababu wanafunzi wamekosa mahali pa kukaa, pamoja na walimu kukosa nyumba za kuishi. Ni vyema Serikali kuona umuhimu wa pekee na kutafuta fedha haraka. Naomba maelezo ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo kubwa sana la shule zetu hasa za vijijini ni kukosa walimu, hususan Sekondari za Kata. Serikali ifanye kila liwezekanalo, kusomesha walimu wengi.

**MHE. DKT. ANTHONY M. DIALLO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, kwa kutoa bajeti. Naomba niiombe TCU wajiondoe na shughuli ya udahili wa wanafunzi wanaoingia Vyuo Vikuu. Chombo hiki ni cha usimamizi *(regulatory)*, kazi yake ni kuona vyuo vinatoa kiwango cha elimu kinachokubalika, kwa kufuata taratibu na kufuata taratibu za ukaguzi na ushauri kwa vyuo hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, TCU wanapojiingiza katika udahili wa wanafunzi watajitoaje katika lawama pale wanapokosea kutokana na mwendelezo wa makosa

yaliyofanyika katika chuo husika? Ni sawa na uamuzi wa Mahakama ya chini kujumuisha maoni ya Mahakama ya Rufaa katika hukumu yake. Ni vyema wao wakawa wana ukaguzi wa vyuo katika nyanja za *Enrollment Regulations*, ubora wa wanafunzi, ubora wa wahadhiri, ubora wa *facilities* za kutoa elimu, ubora wa utungaji na utayarishaji wa mitihani ya chuo na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili taasisi hii iwe na hadhi ya kimataifa; ni vizuri nayo ifanyiwe uthibiti *(accreditation)* na vyombo vya Kimataifa vya utoaji wa ithibati kama vile *ISO International Education Accreditation Institutions* ili kazi zao ziwe na ubora unaokubalika Kimataifa. Siyo vizuri sana kutegemea Sheria ya TCU peke yake. Kwa mfano, *Tanzania Bureau of Standards (TBS),* ilibidi ikafanyiwe *accreditation* na ISO ili kazi zao ziwe na ubora unaotambulika Kimataifa, licha ya sheria inayowaunda peke yake.

Vyuo Vikuu visivyo vya Serikali na baadhi vya Serikali, vina matatizo ya mfumo wa *quota* kwa wanafunzi watakaojiunga Vyuo Vikuu 2009/2010. Awali ya yote, naipongeza Serikali kwa kuwa na mfumo wa kuwawezesha Watanzania kupata elimu ya juu kwa njia ya mkopo na hata kwa udhamini.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfumo huu unaijengea nchi uwezo wa kudumu, kwani hata wazazi na wanafunzi wanajenga uwezo wa kuchangia. Kwa kuzingatia uwezo wa kifedha wa nchi yetu, Bodi ya Mikopo imekuwa ikibadili vigezo vya utoaji wa mikopo mara kwa mara:-

Mwaka 2005/2006 wote walioomba mikopo walipewa mikopo, 2006/2007 walioomba walipewa asilimia 60 ya *tuition fees* ya asilimia 100 na mengineyo. 2008/2009, *means testing* iliingizwa ili kusaidia kubaini asilimia anayohitaji mwombaji kwa *tuition fees* na kuanza kulipa kwa miezi miwili miwili, badala ya *instalments* mbili kwa mwaka kwa upande wa wanafunzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo 2009/2010, *Quota System* (badiliko jingine). Naiomba Serikali ishirikiane na Vyuo Vikuu kutatua tatizo hili kuliko kushinikiza uamuzi wa Bodi ya Mikopo. Watendaji wa Vyuo Vikuu wanajua hali ngumu ya fedha ya nchi yetu na wala hawakatai uamuzi wa Serikali wa kugawa kilichopo, kufikia malengo ya Serikali kwa elimu ya juu, bali utaratibu wa ugawaji unakatisha tamaa washiriki wa makuzi ya elimu ya juu nchini na kufanya elimu ya juu iwabague wale waliosoma Shule za Kata na nyingi za Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, watoto wa wakulima, asilimia kubwa wataishia kukosa elimu nzuri ya juu, huku watoto wa wazazi waliolipia vizuri sekondari, watafaidi mikopo kuliko walengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mnamo tarehe 6 Julai, Bodi ya Mikopo imetoa mwongozo mpya juu ya ugawaji wa mikopo. Mfumo huu wa *Quota System* umeletwa kama shinikizo kwa Vyuo Vikuu. Mnamo tarehe 2 Juni, *Vice Chancellors* na *Principals (*Wakuu wa Vyuo Vikuu), wakiwa kwenye kikao cha *Committee of Vice Chancellors and*

*Principals,* ambayo ni kuishauri Serikali kwa masuala ya Vyuo Vikuu kwa mujibu wa *Universities Act. No.7, 2005,* walipokea hoja ya Bodi kuwa Serikali haina fedha za kutosha na kwa sababu hiyo, inabidi nitoe mapendekezo yangu jinsi ya kutoa mkopo kwa usawa licha ya ufinyu wa bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bodi pamoja na Wawakilishi wa vyuo vyote, ilikuwa imekwishafanya vikao viwili tarehe 17 Aprili na tarehe 8 Mei, 2009, kwa kupata mawazo zaidi juu ya suala hili kabla ya kikao cha Wakuu wa Vyuo.

Mheshimiwa Naibu Spika, iliundwa pia *Task Force* ya Wataalamu, waliotoa mawazo ya kina kusaidia kuongoza Vyuo Vikuu kufanya maamuzi yake. Kwa hiyo, tarehe 2 Juni, 2009 walipokutana, maamuzi ya Wakuu wa Vyuo yaliongozwa na uchambuzi wa kina, ambao ulifikisha na kutoa uamuzi wa kuishauri Serikali iongeze fedha katika fungu la kukopesha ili wanafunzi wenye vigezo vya kukopeshwa, kadiri ya vigezo vilivyotolewa na Bodi hiyo kwa mujibu wa Sheria inayohusu Mikopo ya Wanafunzi Vyuo Vikuu, wapate mikopo. Wakuu wa Vyuo Vikuu vya Umma na visivyo vya Serikali, wote kwa pamoja walitoa hilo pendekezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimepata taarifa kuwa, Serikali ilikubaliana na pendekezo hilo. Mnamo tarehe 6 Juni, vyuo vilipata barua kutoka Bodi ya Mikopo, ikirejea hoja yake ya *Quota System*, ikionesha tayari kila chuo wanafunzi wangapi watapewa mkopo. Hii ina maana, Bodi pamoja na Wizara, walipuuza maoni ya *Task Force!*

Mheshimiwa Naibu Spika, maoni ya Wakuu wa Vyuo Vikuu ni kuwa *Quota System* bado haitatatua tatizo lililopo, kwani tatizo lenyewe ni la msingi kuwa vigezo vilivyopendekezwa vinawagawa wanafunzi katika tabaka; ambapo ni uvunjaji wa usawa wa kikatiba.

Vile vile maandalizi yake hayaridhishi, kwani hata walengwa wa mikopo hawajapewa taarifa. Walipa kodi wote, wana haki ya kujua jinsi hela za umma zinavyotumika. Yafaa kujiandaa kukabiliana na mazingira mapya ya kupata elimu ya juu kama Bodi haitakuwa kimbilio lao. Iilibidi Bodi iwape nafasi, kuelewa utaratibu mpya kwa muda wa kutosha.

Hadi sasa vijana na wazazi wao hawajui utaratibu mpya. Wanajiandaa kuja vyuoni kwa vigezo vya *division one* na *two* na kwa taaluma teule mfano ualimu, sayansi, uhandisi na kadhalika. Wananchi hawatatendewa haki kwa Bodi kushinikiza utaratibu wa *quota system.*

Mfumo mpya, hauzingatii uwezo wa kila chuo wa kupokea wanafunzi. Naliona hili litasababisha hisia za upendeleo kwa baadhi ya vyuo, licha ya kwamba, Serikali inapaswa kuweka vipaumbele vyake kwa baadhi ya taaluma.

Mfumo mpya ulikuwa haujapitishwa kama utaratibu mpya, kwa ushirikishi wa jamii. Utaratibu huu umepitishwa kidikteta na sioni kwa nini waliunda *Task Force* na maoni yao yamepuuzwa!

Mfumo mpya unavunja ile tabia ya wananchi kuchangia kadiri ya uwezo, kwani mikopo kwa baadhi ya taaluma uwezeshwaji ni wa asilimia 100 bila kujali uwezo wa mlipaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, mapendekezo mengi yalitolewa na *Task Force* ili yaweze kutafuta ufumbuzi wa tatizo la uhaba wa mikopo, kwani idadi ya wanafunzi wenye sifa za kujiunga Vyuo Vikuu inazidi kuongezeka mwaka hadi mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachoiomba Serikali kwa sasa:-

(i) Kuielekeza Bodi ya Mikopo kuendelea na utaratibu wa zamani wa utoaji wa mikopo, kwani Bodi iliomba iongezewe fedha na fedha walizoomba ndizo zilizoongezwa.

(ii) Kama Serikali ina vipaumbele vya baadhi ya maeneo, basi vifanywe bila kuathiri mipango endelevu ya vyuo vingine na bila kuonesha ubaguzi wala upendeleo.

Serikali itenge fungu maalumu kwa ajili ya baadhi ya vyuo ambavyo vinaonekana kuwa jicho la Serikali Tawala kwa kipindi husika, kuliko kuelemea bajeti ile ile iliyowapa matumaini wananchi kwa kipindi cha miaka mitatu kwamba, ukiwa na *Division* I au II utapata mkopo kwa mujibu wa sheria. Hii ni haki ya Watanzania wote wenye sifa za mkopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kusikilizwa mapendekezo yangu kwa manufaa ya Watanzania wote na Vyuo Vikuu nchini mwetu. Mpaka sasa tulikuwa tunaendelea vizuri. Ikumbukwe kuwa, hata migomo ya mwaka jana, ilitokana na utaratibu mbovu wa kugawa mikopo kwa miezi miwili miwili badala ya *instalment* mbili.

Mheshimiwa Naibu Spika, tujenge elimu ya juu kwa njia ya ushirikishi na kuongozwa na sheria tulizoweka. Tukumbuke kuwa, fedha zinazotolewa ni mkopo na si hisani. Kuweka masharti ya kibaguzi, kutoigawa nchi yetu kwa utaratibu wa kipato na kielimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha. Nitaunga mkono hoja kama maoni yangu yatazingatiwa.

**MHE. MGENI JADI KADIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, namshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kunijalia kunipa afya njema na kuweza kuchangia Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongeza Waziri, Naibu Mawaziri, kwa kazi ngumu wanazozifanya katika Wizara. Nawapongeza na wale wote walioshiriki kuichambua bajeti hii. Nawapongeza walimu wote, kwa kazi ngumu ya kufundisha katika nchi hii, wakiwa ndani ya mazingira magumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii ina Wizara mama inayotoa na inayofunza na kuelimisha katika maisha ya mwanadamu katika dunia hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Elimu ina upungufu mkubwa wa walimu usiopungua walimu 115,000, ambapo itachukua miaka 15 kuziba pengo, kwa sababu ziko shule zina walimu wawili tu, hawawezi kufundisha masomo yote na kwa kuwa mitihani yote inayofanywa ni sawa; ni dhahiri kuwa baadhi ya maeneo hawatafanya vizuri. Kwa hiyo, tunaomba Serikali izibe pengo hilo, ili elimu iboreke zaidi na bajeti ya mwaka 2009/2010 itekeleze yaliyokusudiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mishahara ya walimu iboreshwe, ili watu wengi waipende kazi hii na wale wengine wanaosomea kozi ya ualimu katika ngazi ya stashahada na cheti, wengi watajiunga na kozi ya ualimu. Vile vile kukopeshwa asilimia mia moja wanafunzi wa Chuo Kikuu, wanaosomea ualimu na sayansi.

Mheshimiwa Naibu Spika, watoto wenye ulemavu ni sawa na watoto wengine wa kawaida, hali ilivyo kwa sasa sehemu kubwa ya gharama ya kuwasomesha watoto wenye ulemavu imebakia mikononi mwa taasisi zisizo za kiserikali na mashirika ya dini.

Mheshimiwa Naibu Spika, walimu wanakabiliwa na kero na matatizo mengi, ambayo yanawaathiri katika utendaji wa kazi zao. Kwanza, kucheleweshwa kulipwa mishahara yao, kupelekea kulimbikiza madai ya fedha zao kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na jitahada kubwa sana za ujenzi wa madarasa kupitia MMEM na MMES zinazoonekana, lakini jitahada za ujenzi wa nyumba za walimu hazionekani. Serikali ilisema kuwa kuna mpango, ikijenga madarasa mawili itajenga nyumba moja ya mwalimu. Je, katika Shule zilizojengwa zimejengwa nyumba ngapi za walimu? Naomba wakati wa kujibu unipe ufafanuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, walimu wawe na mpango mahususi wa kuwakagua watoto usafi na kuwapangia madaktari kuwakagua afya zao, angalau mara tatu kwa mwaka ili kujua afya zao. Wanafunzi wa kike wanaobeba ujauzito, wajulikane mapema ili wapelekwe vituo vya afya kupata huduma za kliniki ili kupunguza vifo wakati wa kujifungua.

Mheshimiwa Naibu Spika, bado Serikali ina kazi kubwa ya kukabiliana na tatizo la mimba mashuleni. Lazima walimu na wazee, washirikiane kulea watoto wetu ili tupate Taifa lenye heshima kwa faida yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Nakutakia kila la kheri, pamoja na Waziri na Watendaji wote wa Wizara hii. Amina.

**MHE. MASOLWA COSMAS MASOLWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Waziri, Naibu Mawaziri, pamoja na Watendaji wake wote, kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kuinua elimu nchini. Aidha, nakipongeza Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Sokoine, kwa kushika nafasi ya kwanza na nne kwa ubora katika Kanda ya Afrika ya Mashariki na Kati.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya pongezi hizo, sasa nichangie kidogo katika maeneo machache kama ifuatavyo:-

Taasisi ya sayansi ya Bahari Zanzibar – Chuo Kikuu Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, Taasisi ya Sayansi ya Bahari Zanzibar – Chuo Kikuu Dar es Salaam ni pekee nchini kama si kwa Afrika ya Mashariki na Kati, inayotoa mafunzo ya elimu ya juu ya Sayansi ya Bahari. Kutokana na umuhimu wake, ndipo Serikali ilipoamua kuipanua taasisi hiyo, kwa kujenga majengo huko Zuyu Zanzibar, ambapo ujenzi ulianza mwaka 2006 kwa Kampuni ya China Railway Cooperative, ujenzi ambao ulikisiwa kugharimu Sh. 6.8 bilioni na ungekamilika baada ya miaka miwili tangu kuanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, Mradi huo haukukamilika kama ulivyopangwa na hadi sasa bado haujamalizika, ambapo gharama zilizopangwa zitakuwa zimeongezeka karibu mara dufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na juhudi za upanuzi wa taasisi hiyo, ukishirikiana na ule wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, kuchukua juhudi ya namna ya kutafuta fedha ili kukamilisha ujenzi huo, ikiwa ni pamoja na kufanya mazungumzo na taasisi mbalimbali za fedha (CRDB, NSSF na kadhalika) na taasisi hizo kimsingi kukubali kutoa mikopo kwa ajili ya kukamilisha Mradi huo kwa sharti la Serikali kudhamini, kwa bahati mbaya Serikali inakuwa ikikataa kudhamini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Taasisi ya Sayansi ya Bahari ni ya Serikali na mdhamini ni Serikali; inakuwaje Serikali ikatae kudhamini taasisi hii wakati Serikali hiyo hiyo imekubali kuidhamini TTCL? Naomba maelezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Mradi wa Ujenzi wa Majengo ya Taasisi ya Sayansi ya Bahari huko Zanzibar umechukua muda zaidi kuliko uliokubalika kimkataba ya wajenzi; ni hatua zipi Wizara inazochukua ili kuona Mradi huo unakamilika mara moja ili kupunguza gharama na utakamilika mwaka gain?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia Mheshimiwa Waziri, alieleze Bunge lako Tukufu ni kiasi gani mkandarasi anachodai kutokana na Serikali kukiuka mkataba wa kushindwa kumlipa ili kukamilisha ujenzi kwa muda uliopangwa, pamoja na hatua pande zote mbili zinazochukua ili kuhakikisha kuwa mjenzi haifikishi Mahakamani Taasisi?

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ninalotaka kujua ni kuwa, je, fedha iliyopangwa Sh.1,212,000,000 zitatosha kukamilisha ujenzi wa majengo yaliyokusudiwa? Kwa nini fedha iliyopangwa mwaka jana kwenye Mradi huu zinalingana na zile za mwaka huo? Je, kampuni hii haina uwezo wa kufikia kazi inayolingana na fedha zaidi ya hizo?

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi karibuni vyombo vya habari vilitoa taarifa kuwa, wazabuni wanaosambaza vyakula kwenye shule za sekondari, ambao wanadai kuwa hawajalipwa madeni yao, watagoma kupeleka vyakula mashuleni. Je, Mheshimiwa Waziri analifahamu hilo na kiasi gani cha fedha wanachodai na lini watalipwa ili wasisababishe shule kufungwa (baadhi)?

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii ina majukumu mengi na gharama zinazotakiwa ni kubwa, lakini fedha inazotengewa hazikidhi haja. Serikali iongeze fedha kwenye bajeti yake, angalau kwa asilimia 50 zaidi ya bajeti ya sasa kwa vile elimu ndiyo ufunguo wa maisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja.

**MHE. ARCHT. FUYA G. KIMBITA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninawapongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Mawaziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu, pamoja na Watendaji wote hapo Wizarani, kwa kutuletea bajeti nzuri, licha ya ufinyu wa bajeti; hongereni sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaipongeza Wizara kwa mapinduzi makubwa sana katika sekta hiyo muhimu; hongereni na *keep it up.* Mwenyezi Mungu awabariki sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nishauri mambo machache yafuatayo:-

(i) Ninashauri watoto wa shule za msingi wapatiwe chakula cha mchana mashuleni, kwani ipo tofauti kubwa kwa shule zinazowapatia chakula na zile ambazo hazitoi chakula. Msisitizo wa masomo ya sayansi ni muhimu sana.

(ii) Ninashauri Serikali iunge mkono zaidi jitihada za wananchi katika ujenzi wa majengo ya shule za sekondari, pamoja na kuchukua jukumu la ujenzi wa maabara katika shule zetu zote za sekondari. Serikali ijitahidi kusambaza walimu katika mashule yetu, pamoja na kuhakiki kwa haraka zaidi, madai ya walimu pamoja na madeni mengine ili kuondoa malalamiko yaliyopo. Msisitizo ni kuongeza Kidato cha Tano na Sita na kuongeza jitihada zaidi kwenye masomo ya Sayansi.

(iii) Ninashauri Serikali ijitahidi kujenga Vyuo vya Ufundi (VETA), kokote pale nchini ambako havipo na pale vilipo kuviimarisha ili mwanafunzi aelewe vyema. Ninaipongeza Serikali kwa kuongeza idadi ya watoto watakaopata mikopo ya elimu ya juu. Ninashauri utaratibu wa kutoa mikopo uwekwe wazi zaidi ili kuondoa malalamiko kidogo yaliyopo. Ninasisitiza umuhimu na ulazima wa nidhamu katika vyuo vyetu, maadili yameporomoka sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaunga hoja mkono.

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu Mawaziri, kwa kazi kubwa wanayofanya kwa umahiri mkubwa. Pia nampongeza Katibu Mkuu na Wataalam wote wa Wizara, kwa kazi wanayoifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Elimu ina tatizo kubwa la Idara ya Ukaguzi isiyo na vitendea kazi na ukaguzi haufanyiki kama inavyotakiwa na ndiyo chanzo cha kuvurugika kwa elimu katika ngazi ya msingi, sekondari na vyuo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Wizara iniambie ni lini Idara hii ya Ukaguzi itaimarishwa ili ukaguzi ufanyike ipasavyo kusimamia utendaji mzuri katika shule zetu?

Mheshimiwa Naibu Spika, je, Wizara ya Elimu ni lini itawekeza fedha za kutosha kuipatia Idara hii fedha, magari ya kutosha, kompyuta na watumishi ili wafanye kazi ya ukaguzi?

Mheshimiwa Naibu Spika, walimu wengi wamekuwa wakipata shida sana mara wanapotaka kwenda kusoma, wamekuwa wakizuiwa. Ninaomba walimu wanaotaka kwenda kusoma, wapewe fursa hiyo waweze kujielimisha zaidi ili wanaporudi kutoka masomoni, waweze kuwaelimisha wanafunzi vizuri zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, elimu ndio mshipa wa damu wa Taifa letu na wananchi kote nchini wameitikia wito wa Serikali yao wa kujenga Shule za Sekondari za Kata na kupanua shule za msingi katika kila kijiji.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na juhudi zote hizo, bado lipo tatizo la uhaba wa walimu katika Shule zetu za Sekondari za Kata. Mfano, Shule ya Busami ambayo ipo Kata ya Bunyambo, Wilaya ya Kibondo, yenye wanafunzi zaidi ya hamsini na ina mwalimu mmoja tu, ambaye pia ndiye Mkuu wa Shule. Naomba Wizara itusaidie kutatua tatizo hilo ili watoto wetu waweze kupatiwa haki yao ya kupata masomo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba Wizara ifikirie kusaidia walimu wetu kuwapatia japo sukari ili wanapokuwa wanaendelea na kazi, waweze kupata kiburudisho waweze kufanya kazi vizuri zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hayo machache,naomba kuunga mkono hoja.

**MHE. AL-SHAYMAA J. KWEGYIR**: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, napenda kumpongeza Waziri na Naibu Mawaziri, kwa kazi nzuri wanayoifanya kwa umakini mkubwa. Pia nawapongeza Watendaji wote kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa elimu ni haki ya kila mtu na ndio msingi wa maendeleo, lakini imekuwa ngumu kwa watu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ugumu huu upo kuanzia elimu ya awali, msingi, sekondari hadi vyuo vikuu na tatizo kubwa ni miundombinu kwa ujumla; haikidhi kabisa kwa watu wenye ulemavu. Je, Waziri anasemaje kwa hilo? Nina imani kubwa, nanyi na mtanipa maelezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitoe mfano wa Albino; kuna shule ipo Misungwi ambayo ni ya wasioona, watoto Albino wapo zaidi ya 150 na wazazi wanawapeleka kwa ajili ya usalama ili wasiuawe. Je, kuna dalili ya watoto hao kupata elimu ukizingatia wanapelekwa kwa ajili ya usalama ili wasiuawe? Tatizo lao kubwa ni kukosa uwezo wa kuona (*low vision*), shule kama hiyo nyingine ipo Kigoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, kikubwa kwa watu wenye ulemavu ni *inclusive education,* lakini bila walimu wa elimu maalum, inakuwa ni bure, kwani kuna uhaba mkubwa wa walimu hao. Chuo kilichopo hakitoshi (Patandi), kinahitaji kitazamwe angalau kukiboresha.

Mheshimiwa Naibu Spika, utakuta watu wenye ulemavu wengi, wanakata tamaa kutokana na hali ilivyo. Serikali imejitahidi sana kulipa uzito wa hali ya juu suala la elimu kwa ujumla. Upungufu kidogo haukosekani; kwa mfano, tatizo la walimu, malipo yao na wanahitaji kupatiwa nyumba.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina imani kubwa kuwa, hayo yote yatawezekana, kwa mshikamano mlionao ninyi Mawaziri na Watendaji wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, namaliza kwa kuunga mkono hoja.

**MHE. ABASS Z. MTEMVU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakupongeza kwa hotuba yako nzuri na kazi nzuri unayofanya, pamoja na Naibu Mawaziri; Mheshimiwa Mwantumu Mahiza na Mheshimiwa Kabaka, kwa ushirikano mzuri mnaoupata kutoka kwa Katibu Mkuu, Profesa Dienga na Watendaji wote wa Wizarani.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda na mimi nichangie katika hotuba ya bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Wizara itoe tamko ndani ya Bunge hili Tukufu, maana ya ujenzi wa Shule za Sekondari za Kata. Wanafunzi wengi katika Jimbo langu wamekuwa wakipangiwa kusoma mbali na Kata wanazoishi pia mbali na Kata za jirani.

Mheshimiwa Naibu Spika, matarajio yetu, wanafunzi wengi wakikosa nafasi katika Shule za Kata zao, hawatapangiwa Kata ya jirani na Kata wanayoishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, cha ajabu, wanafunzi wengi katika Jimbo la Temeke, naamini na Majimbo mengine, tatizo hili lipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Jimbo langu la Temeke, kuna tatizo la walimu, najua ni tatizo la Kitaifa lakini umefika wakati tutafute dawa ya kumaliza tatizo la walimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja mia kwa mia. Naomba kuwasilisha.

**MHE. BALOZI ABDI H. MSHANGAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Mawaziri na Wataalamu wote wa Wizara na Taasisi, kwa hotuba nzuri sana. Naomba ufafanuzi kwenye maeneo yafuatayo:-

(1) Elimu ya Msingi: Kiwango cha ufaulu Darasa la Saba ni cha chini sana Wilayani Lushoto. Tatizo sugu ni upungufu wa walimu. Tunashauri Wizara ianzishe Chuo cha Ualimu IIIA katika majengo ya Chuo cha Mabughai, Magamba, kwani vyuo vilivyopo havikidhi haja kwa vile ni vichache mno. Vile vile wale walimu wa ziada 580 Mkoa wa Kilimanjaro, angalau 200 wahamishiwe Wilaya jirani ya Lushoto, kupunguza upungufu uliopo Wilayani Lushoto.

(2) Elimu ya Sekondari: Mwaka huu wanafunzi wa Darasa la Saba wanaokaribia 18,000 watafanya mtihani. Tukifanikiwa ufaulu wa asilimia 75, wanafunzi 13,500 waendelee Form I nafasi zikiwepo. Idadi hiyo ya wanafunzi wa Form I Januari 2010, itahitaji vyumba vya madarasa 338, sawa na Sekondari 85 za mikondo minne katika Wilaya yenye Kata 32 tayari zipo 64. Tutajenga kukidhi mahitaji. Serikali ituwezeshe maabara na walimu wa kutosha. Nashauri Wizara iziiwezeshe shule za ‘A’ Level za kutwa katika Sekondari za Mlongwe na Malibwi, Kwai, Lushoto, Ubiri na Gare.

(3) Vyuo vya Ualimu IIIA: Mafunzo yawe *intensive* ya mwaka mmoja badala ya miwili na idadi ya vyuo iongezwe tuwe na Chuo kila Wilaya.

Mhehimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. DEVOTA M. LIKOKOLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napongeza jitihada zote zilizofanyika katika Sekta ya Elimu. Ninashauri yafuatayo:-

(1) Suala la Elimu ya Awali lipewe programu maalum ya kuboresha, kwani msingi wa mtoto ukiwa mzuri naye atakuwa raia mwema. Masomo ya Stadi za maisha kama kufundisha watoto kusalimu, kusema ahsante, samahani, pole na kadhalika, sasa hivi jamii yetu ina upungufu mkubwa wa maadili ya stadi za maisha, lakini watoto walioanza vizuri katika shule za awali wanakuwa na mzisingi mzuri na wanaiendeleza.

(2) Naishukuru Serikali kurudisha Idara ya Elimu ya Watu Wazima. Kimsingi, mchango wa Elimu ya Watu Wazima ni mkubwa sana hasa tukiangalia kuwa, watu wazima kama wataelimika, basi watoto pia wataelimika. Maana watu wazima wakielimika, watakuwa na uwezo wa kiuchumi na watoto wengi watasomeshwa na

wazazi wao. Naishukuru Serikali kwa mpango wa MUKEJA, ambao unasaidia sana katika nyanja zote za maendeleo na maisha ya Mtanzania. Vitabu vyao vinaelimisha kujua kilimo na uchumi, afya ya jamii, utunzaji wa fedha, siasa ya jamii na kiongozi cha mwalimu. Huu ni mchanganyiko mzuri kusaidia mwananchi kujitegemea na kuliendeleza Taifa.

(3) Mabweni kwa watoto wa kike ni muhimu sana. Mkoa wa Ruvuma, Wilaya ya Tunduru, maendeleo ya elimu hasa watoto wa kike ni tatizo kubwa. Naomba Serikali kwa kushirikiana na Mkoa na sisi Wabunge, hasa wa Viti Maalum Mkoa wa Ruvuma, tukutane kujadli hili. Tunduru elimu ya watoto wa kike ni tatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. DKT. JAMES A. MSEKELA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, pamoja na Naibu Mawaziri wake wawili, kwa kazi nzuri wanayoendelea kuifanya katika kupanua na kuboresha elimu kwa ujumla nchini Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Hata hivyo, napenda nitumie fursa hii kuihimiza Wizara na Serikali kwa ujumla, kuhusu makazi ya walimu katika shule zetu za msingi na sekondari ambazo ziko vijijini ambako hazitoshi. Pongezi sana kwa kuongeza na kupanua shule hizi, lakini bado hakika kuna mahitaji makubwa sana ya nyumba hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru na kuipongeza Wizara kuhusu kurejesha michezo mashuleni. Basi ni vyema, zoezi hili lifanyike kwa umakini zaidi ili kupata faida ya kuwa na hiyo michezo mashuleni.

Nakushukuru Mheshimiwa Naibu Spika, kwa fursa hii.

**MHE. ZAYNAB M. VULU:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua nafasi hii, kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Manaibu wake, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu wa Wizara na Watendaji wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali kwa juhudi zake katika kuendeleza Sekta ya Elimu nchini. Naishauri Serikali iongeze idadi ya walimu nchini ili kukidhi tatizo la walimu katika shule zetu za sekondari na msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakaguzi wa shule wasogezwe ili kuweza kukidhi na kuweza kukagua maendeleo ya elimu katika shule zetu. Vile vile wakaguzi hao wawezeshwe kwa kupewa vitendea kazi kama pikipiki na kadhalika, hata kwa mkopo ili waweze kufikia shule zote katika maeneo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vyema Serikali ikaweka mkakati wa kusaidiana na wazazi katika kuhakikisha huduma ya chakula kwa wanafunzi mashuleni inapatikana.

Hii itasaidia kutoa changamoto kwa wanafunzi kupenda shule na pia kuwa makini na kuzingatia masomo yote.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile, itasaidia watoto wa kike, kutokupata vishawishi kwa wanaume wachache, ambao huwafuata watoto hao kwa kuwalaghai na fedha kidogo, hatimaye kupata mimba.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala hili huwakumba zaidi, watoto wanaoishi kwa kujitegemea (kupanga nyumba za kuishi). Huenda mimba za utotoni zikapungua.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kuongeza vyuo vya ufundi katika wilaya zetu, litasaidia zaidi kuinua vipaji na hata uchumi kwa wale ambao watashindwa kwenda sekondari Kidato cha Tano na kuendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ishirikiane kwa karibu zaidi na Wizara ya Nishati na Madini na Wizara ya Maji na Umwagiliaji ili kuweza kuweka umeme uwe wa mionzi ya jua au hata wa kawaida na pia kuweka maji au kutega/kuvuna maji ya mvua. Ni vizuri mikakati hiyo ya Wizara ikaongeza bidii zaidi hata kwa kushirikisha wahisani mbalimbali; maji na umeme mashuleni ni muhimu zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MWAJUMA HASSAN KHAMIS:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kunipa afya njema na kuniwezesha kuchangia Wizara hii. Nakushukuru na wewe Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuliongoza Bunge hili kwa umakini mkubwa na pia namshukuru Waziri wa Wizara hii, pamoja na timu yake nzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa nianze na mchango wangu kupitia Wizara ya Elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama tunavyojua kwamba, Wizara hii ni muhimu sana na ni Wizara ambayo inategemewa na kila mtu kuliko Wizara zote.

Mheshimiwa, pamoja na mazuri yote hayo, lakini pia ina kasoro chache ambazo imezikumba Wizara hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa nianze na uvujaji wa mitihani. Uvujaji wa mitihani umekuwa ni changamoto kubwa sana katika mwaka 2008.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa au ningeomba nimuulize Mheshimiwa Waziri, kuhusu wanaohusika na uvujishaji wa mitihani; ni hao tu au kuna wengine ambao wanahusika? Pia kama ni hao ambao wameachishwa kazi na wengine kupelekwa uhamishoni mwa vituo vya kufanyia kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, bado ninaendelea na hatima ya matatizo ambayo yanaikumba Wizara hii.  Tatizo la uchache wa walimu katika shule za sekondari ni kubwa sana hasa Kidato cha IV.

Mheshimiwa Naibu Spika, shule nyingi zina uchache wa walimu hususan kwa upande wa masomo ya Sayansi na kwa upande wa masomo ya History na Geography, ambayo yanaingia pande zote mbili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ningependa kuiomba Serikali kupitia Wizara ya Elimu, kama ilivyosema kuwa italifanyia marekebisho, basi ilifanyie marekebisho haraka ili wanafunzi waweze kupata haki zao za kielimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuna tatizo ua upungufu wa maabara za masomo ya sayansi na lugha, pamoja na vifaa vingine vya kufundishia na kujifunzia na huduma za maktaba.

Mheshimiwa Naibu Spika, haya pia ni matatizo ambayo yanaikumba Wizara. Kwa kuwa Waziri ameshayatolea changamoto, matatizo hayo katika mwaka 2008/2009 na mimi ningependa kuyatilia mkazo zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ninaiomba Wizara ilifanyie utafiti haraka suala hili ili wanafunzi waweze kusoma kwa uangalifu mzuri na ulio bora zaidi.

**MHE. KHADIJA SALEH NGOZI**: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia moja.  Nianze kutoa pongezi kwa Mheshimiwa Waziri, Naibu Mawaziri, Katibu Mkuu na Wakurugenzi wote, pamoja na Watendaji wa Wizara nzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mitaala ya Elimu ya Kujitegemea; mitaala yetu hivi sasa inawaandaa vijana wetu kifikra kwa kazi ya kuajiriwa tena Serikalini. Ningeshauri mitaala hii ibadilishwe ili iwaandae vijana kujiajiri wenyewe kutoka sekta binafsi.  Somo la elimu ya kujitegemea liwafundishe stadi za kilimo, ufugaji, useremala, ujasiriamali, ualimu na kadhalika.  Kwa ujumla, elimu itolewayo ilenge kuwasaidia vijana kuingia katika soko la ajira na mahitaji halisi katika maeneo ya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimba mashuleni ni tatizo sugu.  Pamoja na adhabu zilizotolewa kwa watuhumiwa; watiaji wa mimba na watiwaji wa mamba, bado makosa yanaendelea kufanyika na madhara zaidi yanabaki kwa mtoto wa kike.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu, kama kosa kalifanya mwalimu kumpa mimba mwanafunzi, kusiwepo na kesi au kumpa mwalimu nafasi ya kujitetea; afukuzwe kazi mara moja na asiajiriwe popote pale, kwani hataacha mchezo wake.  Kama ni mwanafunzi, basi afukuzwe shule abaki mtoto wa kike aendelee kusoma.  Tutakuwa tumemwokoa mtoto na mama yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukumbuke kuwa, ukimsomesha mwanamke mmoja ni sawa na kuisomesha jamii nzima. Ahsante.

**MHE. BENEDICT N. OLE-NANGORO**: Mheshimiwa Naibu Spika, ninampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Mawaziri, Katibu Mkuu na Wataalamu, kwa Hotuba nzuri sana ya Bajeti ya 2009/2010.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru kwa kuwezesha Shule Maalum ya Kichina, inayojengwa Wilayani Kiteto katika Kijiji cha Partimbo, ambayo ujenzi wake umeanza sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna Shule nne za Sekondari za Kata (Njoro, Sunya, Kiperesa na Sesoit), zilizofunguliwa Machi, 2009. Wanafunzi wapo na hakuna shule kati ya hizo yenye mwalimu hata mmoja. Naomba shule hizi zipatiwe walimu sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, madai ya walimu yalipwe sasa, kwani hili linaathiri sana ufundishaji. TAMISEMI ipatiwe uwezo ili iweze kuratibu elimu ya sekondari katika Halmashauri mbalimbali nchini. Aidha, katika ngazi ya Wilaya, mbali na DEO, kuwepo na *District Secondary Education Officer (DSEO),* ambaye kazi yake ni Ukurugenzi wa Elimu ya Sekondari Wilayani.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua za makusudi zichukuliwe, kuboresha ufundishaji wa masomo ya *science*, kwani ndiyo yatakayoleta *sound transformation.*

**MHE. JOHN P. LWANJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongeza sana kwa kazi nzuri ya kuiongoza Wizara hii nyeti. Pongezi ziende kwa Mheshimiwa Waziri na Manaibu wake, kwa kufanya kazi kwa uwazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika shule za *High School* Mkoani Singida, Shule za Sekondari Mwanzi na Itigi, zimekidhi vigezo vya kuanzisha Kidato cha V na tayari Mwanzi Sekondari wameanza *registration* ya wanafunzi wa Kidato cha V, baada ya kupata kibali cha Kamishna wa Shule za Sekondari. Je, kwa nini Shule ya Sekondari Itigi haijapata kibali kama ya Mwanzi?

Sekondari zilizoteuliwa kuanzisha *High Schools* ziliteuliwa kulingana na majimbo ya uchaguzi. Sasa Shule ya Itigi iliyoko Jimbo la Manyoni Magharibi; wananchi wataelewaje wanaponyimwa fursa ya Shule hiyo kuanza kwa *High School* (Kidato cha V na VI) wakati Shule ya Mwanzi iliyopo Mashariki yao wamepata kibali ilhali shule hizo mbili zimekidhi vigezo vya kuanzisha Kidato cha V?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba majibu na ufafanuzi wa kina kuhusu hili; kulikoni?

**MHE. FATMA A. MIKIDADI:** Hongera kwa bajeti nzuri, tunaomba walimu wa msingi/sekondari.

Mahitaji ya Shule za Msingi 4,259; waliopo 3,243 na pungufu 964.

Mahitaji ya Shule za Sekondari 1,199; waliopo 452 na pungufu 741.

Mwisho, tunaomba msaada.

**MHE. JUMA SAID OMAR:** Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kutupatia uzima na afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wote wa Wizara, kwa kuwasilisha bajeti yao hapa Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, watahiniwa wengi wa Kidato cha Nne, walipata daraja la nne katika mitihani yao ya kumaliza elimu ya sekondari katika mwaka 2007 na 2008. Matokeo haya, yanachangiwa sana na misingi mibaya ya wanafunzi wanaomaliza elimu ya msingi. Shule nyingi hazina walimu wa kutosha na hivyo kusababisha masomo mengine kutofundishwa ipasavyo au kutokufundishwa kabisa wakati mtihani unaofanywa ni mmoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, malimbikizo ya madai ya walimu, yanawaathiri wao wenyewe pamoja na kuathiri utendaji wao wa kazi. Ni vyema Serikali ikaliona hili na kulipatia ufumbuzi unaofaa. Mishahara yao ilipwe kwa wakati, pamoja na posho nyingine, kuepukana na malimbikizo ya madeni ambayo ulipaji wake baadaye unakuwa ni vigumu na hivyo kuwa kero.

Mheshimiwa Naibu Spika, jitihada kubwa zimechukuliwa katika ujenzi wa madarasa katika Mpango wa MMEM na MMES, lakini juhudi kama hiyo haionekani katika ujenzi wa nyumba za walimu. Kujenga nyumba 1000 kwa mwaka, itachukua muda mrefu sana mpaka kumaliza tatizo la nyumba kwa walimu. Mkakati wa makusudi unahitajika.

Mheshimiwa Naibu Spika, maslahi ya walimu yaboreshwe ili yaweze kuwavutia vijana wengi wanaomaliza masomo yao na kufaulu vizuri, pamoja na kuwafanya walimu waliopo kazini, waendelee kuipenda kazi yao ya ualimu, badala ya kuvunjika moyo na kuamua kuacha kazi na kutafuta kazi nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili ubora wa elimu uweze kufikiwa, hapana budi Kitengo cha Ukaguzi wa Shule, kikapewa ofisi bora, pamoja na vitendea kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa masomo ya sayansi yanahitaji vitendo zaidi kuliko nadharia; ni vyema Serikali ikawa na mikakati itakayohakikisha kwamba, shule zote za sekondari zinapatiwa maabara zenye vifaa vyote vinavyohitajika katika masomo ya sayansi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa kumekuwa kukitokea migomo na maandamano yanayofanywa na wanafunzi katika baadhi ya Vyuo Vikuu hapa nchini, kwa madai mbalimbali yakiwemo mambo ya mikopo. Je, Serikali inajiandaa vipi sasa kulipatia ufumbuzi wa kudumu tatizo hili la migomo na maandamano ya wanafunzi?

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ina mipango gani itakayohakikisha kwamba, vifaa vya kujifunza na kusomea vinapatikana katika mashule yote hapa nchini kwani hili limekuwa ni tatizo la muda mrefu?

**MHE. NURU A. BAFADHIL:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, napenda kuipongeza Wizara kwa kutoa mkopo wa asilimia mia moja kwa wanafunzi wa masomo ya sayansi na pia kuongeza madaraja ya *Means Testing*. Angalizo; ujazaji wa *Means Testing* utolewe elimu, kwa vile wengine wanapoulizwa kipengele kile cha kazi wanaelezea baba anafanya kazi, lakini kumbe kazi hiyo kipato chake ni kidogo. Mfano, baba anafanya kazi lakini ni mlinzi wa makampuni ya ulinzi ambayo mshahara wake ni Sh.45,000. Je, mshahara huu anaweza kumsaidia mwanawe kuchangia?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba ufafanuzi toka kwa Mheshimiwa Waziri, kuhusu Jengo la Mwalimu House lililojengwa Dar es Salaam Wilaya ya Ilala. Jengo hili ni Kitega Uchumi cha Walimu. Miaka ya 2000 kurudi nyuma, walimu walikatwa sehemu fulani ya mishahara yao kwa ajili ya kuchangia ujenzi wa Jengo hilo, ambalo lilielezwa kuwa ni kitega uchumi cha walimu. Swali ninalotaka Mheshimiwa Waziri atolee ufafanuzi wakati wa majumuisho:-

Kuna walimu wengi waliokatwa mishahara yao na Chama cha Walimu Tanzania (CWT) katika Wilaya zao nikiwemo mimi. Je, gawio la faida itakayotokana na Jengo hili litawafikia vipi wale walimu ambao wamechangia katika Jengo hili kama walivyoambiwa na Viongozi wao wa CWT wa Mawilayani mwao wakati wakichangia fedha zao na wengine wamestaafu na baadhi yao wamefariki?

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kuchangia kuhusu Baraza la Mitihani la Taifa, japokuwa Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, wakati akijibu swali kuhusu uvujaji wa mitihani, alilieleza Bunge letu Tukufu kuwa, Serikali ina mpango wa kutafuta mashine za kisasa kwa ajili ya uchapaji wa mitihani ili kudhibiti uvujaji huo. Ushauri wangu ni kuwa, japokuwa udhibiti huu utakuwepo, lakini bado hatujaweza kudhibiti katika hatua za usahihishaji. Katika usahihishaji, mwanafunzi anapewa namba ya mtihani, namba ambayo na jina lake linajulikana. Kuna watu wanawatumia wasahihishaji namba ambazo wengine huzichezea.

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi langu; hata kama kila mwanafunzi atakuwa na namba yake ya mtihani, ingefaa ziwepo na *code number* ambazo zitaandikwa katika karatasi ya mtihani. Hizi *code number* zitakuwa ni kwa kila jina la namba ya mtahiniwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati wa kusahihisha kila karatasi itatambulika kwa *code number*. Baada ya kumaliza masahihisho, ndio inaangaliwa *code number* fulani ni

jina la mtu Fulani mwenye namba fulani ya mtihani. Hii kwa kiasi Fulani, itasaidia kidogo kudhibiti pia matokeo katika usahihishaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu upandaji madaraja kwa walimu; niishukuru Wizara inajitahidi kupandisha walimu madaraja; lakini Wizara inazo taarifa kuwa:-

(i) Kuna baadhi ya walimu wenye sifa na uzoefu sawa sawa lakini wametofautiana kimadaraja?

(ii) Kuna baadhi ya walimu wamerekebishiwa mishahara bila kupewa barua za kupandishwa madaraja?

(iii) Wapo walimu ambao hawamo katika orodha za upandishwaji madaraja na wametumikia daraja husika hata miaka saba.

Mheshimiwa Naibu Spika, walimu ni nguzo ya Taifa, tuwasaidie ili waijenge nchi kwa kupata wahitimu mahiri.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa pongezi kwa Mheshimiwa Waziri, Naibu Mawaziri wote wawili, Katibu Mkuu, Wakurugenzi wote na Wafanyakazi wote wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, kwa kazi nzuri wanayoifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii ni pana na kubwa sana, lakini ni kweli kazi imefanyika. Naamini wote wanajua na kufahamu na kukubali kuwa, Serikali yetu na uongozi wa Awamu ya Nne, wamefanya kazi nzuri, hasa kujenga shule za sekondari kila Kata.

Mheshimiwa Naibu Spika, hongera pia kwa Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete na Waziri Mkuu, Mheshimiwa Peter Pinda, kwa kutambua na kusukuma maendeleo ya elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia nitambue na kushukuru kuona Serikali ya Awamu ya Nne imetambua kuwa elimu ni kipaumbele namba moja. Sasa la msingi ni kuwa, kutokana na Wizara hii kuwa pana kuanzia chekechea hadi Chuo Kikuu, ualimu na kadhalika, ingawa bajeti imeongezeka, tunaishukuru Serikali kazi zote ziendelee vizuri, bajeti ijayo iongezeke. Ni kweli bajeti bado ni ndogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa madai ya walimu wa Shule za Msingi, Sekondari na Vyuo Vikuu, kwa njia moja au nyingine, tafadhali sana, natoa ombi langu kwa Waziri na Katibu Mkuu wa Wizara hii, madeni yote licha ya bajeti ndogo yakalipwe mara moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, bajeti hiyo ndogo, watafiti wa Vyuo Vikuu waangaliwe. Elimu hasa ya sayansi bila ya tafiti sio elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mikopo ya wanafunzi Vyuo Vikuu; naipongeza Wizara na Serikali, kwa kuamua kuwapatia mkopo wanafunzi wote watakaochukua masomo ya sayansi na elimu kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii itasaidia sana, watoto wote waliofaulu kwa darasa la kwanza na pili na hasa kwa wale ambao wazazi wao hawajiwezi, kuendelea na masomo bila matatizo. Pia, ni motisha tosha kwa watoto/wanafunzi kuwa na moyo wa kuchukua masomo ya sayansi na ualimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi langu kwa Mheshimiwa Waziri na Serikali, kwa kuwa Serikali yetu bado tunamjali sana mtoto wa kike; ombi langu ni kwa kuwa mtoto wa kike ambaye amechukua hasa masomo ya sayansi na amejitahidi kufaulu kwa daraja la tatu, naye afikiriwe kupewa mkopo kwa asilimia mia moja, kwani ingekuwa njia tosha, angalau ya kuhimiza na kushawishi wanafunzi hasa wasichana kuchukua masomo ya sayansi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba msaada mkubwa wa maabara (majengo na vifaa), vitolewe na Serikali kwa Shule za Sekondari za Kata. Ni kweli Mikoa yote, Wilaya na Kata tunajitahidi na bado tunawahimiza wananchi kujenga, lakini wanahitaji na kuomba mkono wa Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa pongezi kwa Waziri, Serikali ya Awamu ya Nne na kwa Rais wetu, kwa ujenzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma, ambacho kwa sasa kimechukua wanafunzi zaidi ya 7,000. Naomba Mheshimiwa Waziri, aangalie ukarabati wa majengo ya vyuo vingine kama SUA, University of Dar es Salaam, ambayo hali ya majengo ni mbaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru na ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. ATHUMANI S. JANGUO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nawapa pole Mheshimiwa Waziri na Wasaidizi wake, kwa mzigo mkubwa walionao wa kusimamia makundi nane ya Elimu na Taasisi kumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongeza pia kwa kazi nzuri na hotuba ndefu na safi. Nawapongeza pia kwa yafuatayo: Kuvuka lengo la mapato kwa asilimia 320 tena bila ya msaada wa TRA; Kusimamia vizuri matumizi yanayokaribia lengo (99.6%); na kutekeleza miradi ya maendeleo kwa kiasi cha asilimia 66.2. Hapa panahitaji maelezo ya sababu za kutokufikia lengo, kwani kwenye miradi ya maendeleo ndiko liliko tumaini letu wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na pongezi hizo, kazi ya Wizara bado kubwa, kwani kuna upungufu kwenye maeneo mbalimbali:-

Pamoja na kuajiri walimu 3,217 mwaka uliopita, unaambiwa kuwa pengo ni walimu 115,000, ambalo huenda likachukua miaka 15 kuliziba. Kule kwangu Kisarawe tuna upungufu wa walimu 150.

Baadhi ya shule nchini zina walimu wawili tu. Kwa mfano, katika Wilaya ya Kisarawe, kuna shule nne zenye walimu wawili kila moja na shule tano zenye walimu 5 – 7. Hawa hawawezi kumudu kufundisha madarasa saba ya shule ya msingi na manne ya sekondari.

Wizara imejitahidi kulipa madeni ya walimu yanayozidi shilingi bilioni nane mwaka jana na inahakiki madai mengine ya walimu yenye thamani ya Sh. 22.8 bilioni. Walimu wanadai kuwa madeni ya Serikali kwao ni Sh. 53.6 bilioni na kwamba, zoezi la Wizara la kuhakiki madeni lililipuliwa. Pengine Mheshimiwa Waziri, ungependa kuyachunguza madai haya.

Kuna upungufu makubwa wa majengo ya shule. Tanzania nzima bado inahitaji nyumba za walimu 127,000. Kule Kisarawe tuna upungufu wa nyumba 435 za walimu wa shule za msingi na 285 za walimu wa sekondari.

Wilaya yangu bado inahitaji majengo yafuatayo: Madarasa 237 ya shule za msingi; madarasa 55 ya shule za sekondari; vyumba 41 vya maabara za sekondari; na vyumba 12 vya bwalo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipimo cha ufanisi wa Wizara ya Elimu ni matokeo ya mitihani. Kwa miaka ya 2007/2008 na 2008/2009 upasishaji ulikuwa kama iffuatavyo:-

Mwaka 2007/2008 waliofanya Mtihani wa Darasa la IV walikuwa 1,017,967; waliofaulu ni asilimia 52.7. Haya si matokeo ya kujivunia. Waliofaulu Kidato cha IV ni asilimia 75.8. Isitoshe, tunaambiwa kuwa, theluthi mbili ya hao wa Kidato cha IV walishinda Daraja la IV. Kwa hiyo, waliofaulu Daraja la I – III ni theluthi moja, sawa na asilimia 25.27.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini niipongeze Wizara kuwa, matokeo ya mwaka 2008/2009 yanayooneshwa Uk. wa 159 ni mazuri. Hii ina maana kwamba, mwaka huo yalifanywa marekebisho yaliyoleta mafanikio zaidi. Pongezi.

Mheshimiwa Naibu Spika, niwapongeze kwa kuorodhesha changamoto kwenye Ibara ya 110 na kugawa majukumu ya kupambana na changamoto hizi kwa kila Idara na Taasisi. Ingekuwa bora kama mwishoni kungekuwa na Jedwali *(matrix)*, linaloonesha majukumu hayo, wanaowajibika na utekelezaji na tarehe za kukamilisha kila jukumu. Kwa yale ambayo utekelezaji wake ni wa kila siku na mengi ambayo hayawezi kukamilishwa ndani ya kipindi cha bajeti, yangeelezewa hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini wanafanya kazi nzuri. Nawatakia kila la kheri.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. ALHAJI DKT. JUMA A. NGASONGWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, nampongeza Mheshimiwa Prof. Jumanne Maghembe (Mb), Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, Manaibu wake ; Mheshimiwa Gaundentia Kabaka (Mb) na Mheshimiwa Mwantumu Mahiza (Mb), Katibu Mkuu Prof. Hamisi Dienga na Viongozi na Watumishi wote wa Wizara na taasisi zake, kwa kazi nzuri wanayoifanya katika kuendeleza Sekta ya Elimu, pamoja na Mafunzo ya Ufundi nchini mwetu. Aidha, wote hawa nawapongeza kwa maandalizi na hatimaye uwasilishaji hapa Bungeni wa Hotuba ya Makadirio na Matumizi ya Mwaka 2009/2010.

Mheshimiwa Naibu Spika, maendeleo ya elimu nchini mwetu kwa ujumla yanaridhisha na kazi nzuri imepangwa na Wizara na Serikali katika miaka mitatu hadi minne iliyopita. Kwanza, utekelezaji wa ujenzi na ufunguzi wa Sekondari za Kata ni wa kimapinduzi na haujawahi kutokea. Chuo Kikuu cha Dodoma ni mafanikio makubwa kwa Awamu ya Nne ya Serikali ya CCM, inayoongozwa na Mheshimiwa Rais Kikwete. Pia juhudi za Serikali za kulipa walimu malimbikizo yao, pamoja na kuboresha maabara ya masomo ya sayansi. Mipango ya ukarabati wa Vyuo Vikuu vya Serikali na uboreshaji wa ufundishaji katika Shule za Sekondari ni mzuri wa unaungwa mkono na watu wote wenye nia njema na Sekta ya Elimu nchini.

Mehshimiwa Spika, napenda kuelekeza maoni yangu kwanza katika uboreshaji wa elimu ya msingi na sekondari, kwa kupunguza upungufu mkubwa wa walimu. Nyumba za walimu hasa vijijini, tuzipe kipaumbele kikubwa maana bila nyumba bora za walimu, uhaba wa walimu vijijini utaendelea kuwa tatizo na kero. Kweli ubora wa elimu ni walimu. Suala la maabara katika shule za sekondari, lazima nalo lipewe kipaumbele cha juu na liwe jukumu la Serikali kuzijenga maabara hizo na kuziwekea vifaa na nyenzo stahiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, uboreshaji wa elimu ya sayansi ni muhimu sana hasa wakati/zama hizi za TEKNOHAMA. Matumizi ya kompyuta na kuwapa walimu kompyuta ni hatua muhimu sana katika zama hizi za karne ya ishirini na moja. Serikali imeanza vizuri na naiomba iendelee na juhudi hizi nzuri sana. Uamuzi wa Serikali wa kuipa Sekta ya Elimu sehemu kubwa ya keki ya taifa ni mzuri, muafaka wa sahihi kabisa. Kama Mwalimu Julius K. Nyerere, Baba wa Taifa letu, alivyotufundisha: Elimu ni ufunguo wa maisha; lazima tuziendeleze juhudi za kuwapa elimu nzuri na bora wananchi wetu kwa kasi zaidi sasa, kama uzoefu wa nchi za Asia (Asian Tigger Economies), inavyotuonesha kwa dhahiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la idadi ya vitabu vya kiada katika shule zetu lipunguzwe hadi kuwa viwili au vitatu tu. Tulijadili kwanza kabla ya kufikia uamuzi wa kuvipunguza kutoka *multi-text books advice* kwenda kwenye *single-or two-text book;* tusiliamulie kwa haraka. Kwa maoni yangu, hoja kuwa tuwe na kitabu kimoja cha kiada, siyo sahihi kabisa. Msingi wa kuamua kitabu kipi cha kiada kitumike shuleni nchini mwetu ni mitaala inayopaswa kutumika kwa wanafunzi na darasa husika. Aidha, ni muhimu kuongeza hapa kuwa mitaala pia inazingatia lengo na shabaha ya aina ya elimu, jamii inatarajia kupata au kufikia kwa watoto/wanafunzi wake. Fursa waipatayo

wanafunzi kujifunza kutoka vitabu vya kiada vingi ni nzuri sana kuliko yale anayojikita kwenye kitabu kimoja cha kiada. Wale wanaosema kuwa ufundishaji wa vitabu vya kiada tofauti katika shule mbalimbali kwa kila darasa ni suala la uendeshaji mbaya wa ufundishaji na siyo suala linalotokana na kuwa na vitabu vingi vya kiada.

Mheshimiwa Naibu Spika, haiwezekani nchi nzima tuwe na kitabu kimoja cha kiada cha hisabati au historia. Lazima mwalimu apate fursa ya kuwafundisha wanafunzi wake vitabu vya kiada vingi *(multi-text books).* Elimu finyu haiwezi kuwa jambo la kudhamiria, elimu pana ndiyo elimu sahihi. Katika hili la *multi-text books choice,* lazima wachapishaji na wachapaji wa vitabu vya kiada wakiwa wengi ni jambo bora maana ushindani unasaidia; kwanza, ubora wa kazi yenyewe ya kutoa vitabu vya kiada; pili, ushindani utaleta nafuu ya bei ya vitabu hivyo vya kiada. Kumpa mtu au taasisi moja ya kuandaa na kuchapisha vitabu vya kiada ni ukiritimba ambao haukubaliki, kwani hauwezi kuwa wa tija na siyo sahihi katika mazingira ya leo ya uchumi wa soko, ambao kanuni yake moja ya msingi ni ushindani. Ukiritimba wowote na wa sababu yoyote, haufai na haukubaliki.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Nawasilisha kwa heshima.

**MHE. MAIDA HAMAD ABDALLAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, kwa hotuba yake aliyoiwasilisha Bungeni leo tarehe 23 Julai, 2009 na ambayo inalenga maboresho mbalimbali katika Sekta ya Elimu, lakini msisitizo ni lazima ufanyike ili kukubaliana na changamoto zinazoendelea kujitokeza kila mara ndani ya Sekta hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongeza Waheshimiwa Naibu Mawaziri wa Wizara hii, Katibu Mkuu na Watendaji wa Wizara, kwa kazi nzito na ngumu wanazozifanya katika kuhakikisha kuwa elimu inafanikiwa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, naipongeza Serikali kuweza kufungua Shule zikiwemo za Sekondari kila Kata, ikiwa ni utekelezaji wa Mpango wa Elimu (MMEM) na (MMES). Naiomba Serikali iweke mkazo na mikakati zaidi ya kupata walimu wenye sifa, kutokana na upungufu wa walimu uliopo nchini. Pia kuweka mkazo wa kuongeza walimu wa masomo ya sayansi ili wanafunzi wa masomo hayo waweze kufanya vizuri, kwani hali iliyojitokeza ya kutokufanya vizuri ni kutokana na upungufu uliopo wa walimu hao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokuwepo kwa maabara nako kunachangia kwa kiasi kikubwa, kutokufanikiwa katika masomo ya sayansi. Serikali katika kipindi hiki cha msukosuko wa uchumi; ni vyema fedha zilizotengwa kwa ajili ya maendeleo ya elimu, ikajikita katika maeneo haya kwa kiwango kikubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo, Serikali iangalie kwa makini matatizo yanayowakabili walimu katika maeneo ya mijini na vijijini ili waweze kufanya kazi kwa

ufanisi zaidi; bila hivyo, kundi kubwa la walimu wanataka kukimbilia katika shule za binafsi kwa ajili ya kupata maslahi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi kuna kundi kubwa la walimu, ambao tayari wameshamaliza masomo kupitia vyuo mbalimbali, lakini suala la ajira limekwama kwa muda sasa. Ni vyema Serikali kudhibiti kwa kuwapatia ajira za ualimu mara tu baada ya kupitishwa bajeti hii, kwani upungufu wa walimu uliopo, unaathiri maendeleo ya elimu nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala utoro mashuleni, kama tunavyofahamu kuwa, tunaendelea kuweka mikakati ya kuhakikisha kuwa, kila mtoto anapata elimu ya awali hadi sekondari, lakini lipo suala la utoro ambalo limekithiri mashuleni. Naomba Maafisa Watendaji wa Kata, ambao ndio msingi wa kuhakikisha kuwa, wanafunzi wanafuatiliwa ipasavyo kuhusiana na mahudhurio mashuleni, kwa kuwafuatilia kule waliko na kuhakisha wanafunzi hao wamehudhuria shuleni. Je, Maafisa hawa wanatekeleza kazi hiyo kama kanuni za uandikishaji na mahudhurio mashuleni inavyowataka?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la wanafunzi wanaobeba mimba wakiwa shuleni; sasa hivi tumekuwa na kundi kubwa la wanafunzi wa kike wanaokatisha masomo kutokana na matatizo ya kubeba mimba mashuleni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, elimu zaidi itumike kuwaelimisha wasichana wakiwa shuleni hata na wale ambao wameacha shule. Pia Serikali iangalie uwezekano wa kuleta sheria Bungeni, inayowalenga wanafunzi kupeana mimba shuleni, wakiwemo wavulana na wasichana ili kuondoa kabisa kuwawezesha kumalisha masomo yao ya msingi na sekondari.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. GIDEON A. CHEYO:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, kwa hotuba yake nzuri, yenye taarifa muhimu kuhusu Sekta ya Elimu. Aidha, nawapongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara na Sekta nzima ya Elimu, kwa juhudi zao za kuendeleza na kuinua kiwango cha elimu nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuunga mkono hoja hii, napenda kuchangia maeneo machache kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutumia fursa hii, kuishukuru sana Wizara kwa kutoa kibali cha kufungua Kidato cha V katika Shule ya Sekondari ya Ileje Day na kupeleka fedha za kununulia vifaa vya kufundishia na kujifunzia, kama ilivyoelezwa kwenye Hotuba ya Waziri, aya ya 32(h). Wilaya yetu ya Ileje ina Shule za Sekondari za ngazi ya Kidato cha Nne 21. Wilaya yetu iko pembezoni, lakini inafikika na kukalika. Jiografia yake ni milima na mabonde. Shule ya Sekondari ya Ileje Day iko ukanda wa bondeni, tunahitaji kuwa na shule ya sekondari Kidato cha V ukanda wa milimani. Kwa

hiyo, pamoja na kupata Kidato cha V katika Shule ya Sekondari ya Ileje Day, tunaomba Wizara iendelee kufikiria ombi letu la Kidato cha V kwa Shule ya Sekondari ya Kafule, ambayo iko ukanda wa milimani. Naomba ombi hili lizingatiwe kwa mwaka kesho 2010.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Wizara kwa jitihada zake za kuongeza idadi ya walimu wanaohitimu katika Vyuo vya Elimu na kuwasambaza katika shule mbalimbali nchini. Hata hivyo, pamoja na jitihada hizo, bado upo upungufu mkubwa wa walimu katika shule zetu. Kwa Wilaya yetu, tuna upungufu wa walimu 132 katika shule za sekondari na walimu 213 katika shule za msingi. Kwa hiyo, naomba Wizara iendelee kutukumbuka katika mgao wa walimu kuweza kupunguza pengo lililopo. Viongozi na Wananchi wa Ileje, wataendelea kuweka mazingira mazuri ili walimu waweze kukaa na kutekeleza majukumu yao kwa utulivu, amani na furaha.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Wilaya yetu, mahitaji ya maabara kwa shule zetu ni 57, lakini sasa hivi kuna maabara mbili tu. Halmashuri ya Wilaya ya Ileje ni kati ya Halmashauri ambazo uwezo wake kimapato ni mdogo sana. Wananchi wanajitahidi kujenga madarasa na majengo mengine ya shule za msingi na sekondari, lakini uwezo wao una kikomo. Kwa hiyo, naomba na kushauri kwamba, Serikali iwapunguzie mzigo wananchi kwa kubeba jukumu la kujenga maabara katika shule zetu zote. Hatua hii itawahakikishia wanafunzi wote kupata fursa ya kujifunza masomo ya sayansi na kupata elimu bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya mchango huo mdogo, naunga mkono hoja hii na kuwatakia mafanikio mema.

**MHE. MUSSA A. ZUNGU**: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Lipo tatizo kubwa la shule kuzungukwa na biashara ya maduka, watoto wengi hupata fursa ya kuhamasika kufanya matendo maovu yanayofanywa na wafanyabiashara, naomba kauli ya kukemea zoezi hili.

**MHE. DKT. RAPHAEL M. CHEGENI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mheshimiwa Waziri anipatie ufafanuzi juu ya masuala yafuatayo wakati anahitimisha hoja hii :-

Kwa kuwa walimu walishafanyiwa uhakiki juu ya madai yao na stahili wanazodai Serikali na ni muda mrefu wamekuwa wakiahidiwa na serikali juu ya malipo yao. Je; ni lini Serikali itahakikisha stahili hizo zinalipwa? Ni vyema Serikali ikaheshimu uamuzi wake ili walimu hawa wasiendelee kupata usumbufu usiokuwa na lazima.

Kwa kuwa Bodi ya Mikopo ilitoa barua tarehe 6 Julai, 2009 ikielekeza suala la *Quota System* kwa vyuo hapa nchini, lakini leo Waziri wakati anawasilisha hoja yake, amesema kuwa wanafunzi wote watapata mikopo kama walivyoomba. Je, lipi ni sahihi ; lile la *Quota System* au kauli ya Mheshimiwa Waziri? Huku siyo kutoa maelezo na taarifa zenye kuwachanganya wanafunzi na wazazi?

Kuna vyuo vya SAUT wana uwezo wa kuchukua wanafunzi zaidi ya 4,000 lakini wameambiwa ni wanafunzi 600 tu watapewa mikopo; je, hii siyo kwenda kinyume na dira ya Serikali ? Naomba ufafanuzi wa kina juu ya haya yote, sambamba na msisitizo wa Serikali wa kudahili wanafunzi zaidi ya 6,500 UDOM. Je; ni ubaguzi wa vyuo kwa vyuo au tatizo ni nini?

Mheshmiwa Spika, Wanafunzi wa Kitanzania wanayo haki sawa popote walipo na wanapaswa kupewa uzito sawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitaunga mkono hoja baada ya majibu yenye ufafanuzi.

**MHE. MARGRETH AGNES MKANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naongezea mchango wangu kimaandishi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nafarijika kwa kazi nzuri inayofanywa na Kitengo cha Elimu Maalum pale Wizarani. Hata hivyo, kwa vile wanafunzi wenye ulemavu wanaongezeka; changamoto zinaongezeka. Naishauri Wizara, kitengo hiki kipandishwe kuwa Idara kamili. Ikiwa Idara, watendaji wataongezeka ili kuweza kushauri mipango mizuri zaidi ya Elimu Maalum; rasilimali zitaongezeka na watoto wenye ulemavu watafaidika na haki hii ya msingi (Elimu).

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni kuwa walimu wanaokwenda kujiendeleza kusomea Elimu Maalum kwenye Chuo cha Patandi, wengi wao wananyanyasika wanaporudi mahali pao pa kazi. Hawapandishwi mishahara, baadhi ya Maafisa Elimu (DEOs), huwahamisha na kuwapeleka kwenye Shule ambazo si za wenye ulemavu. Hivi kwa mtindo huu kweli Walimu Wataalam wenye ulemavu wataongezeka? Naishauri Wizara, kwa kuwa jukumu la kutoa sera, miongozo ni la Wizara, basi hilo litolewe maelekezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna tatizo la wanafunzi wenye ulemavu wasioona, Albino, wenye ulemavu wa viungo; vibyongo; mikono mifupi; wenye vibiongo mgongoni; hushindwa kujibu maswali ya mitihani kwa kazi inayostahili kwa muda unaopangwa. Hivyo, nashauri wanafunzi hawa waongezewe muda wa kujibu maswali ya mitihani katika ngazi ya elimu ya awali, msingi, sekondari hata elimu ya juu. Naomba Wizara itoe miongozo kuhusu ushauri huu, kwa sababu husababisha kufeli mitihani yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, naendelea kuunga mkono hoja.

**MHE. PINDI H. CHANA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuipongeza sana Elimu, napongeza sana suala la mikopo na ongezeko la bajeti ya mikopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunavyo Vyuo vya Elimu kama Chuo cha Kilimo SUA na Chuo cha Sayansi za Afya Muhimbili (MUHAS), ambacho ndio Chuo Kikuu cha Tanzania kinachozalisha Wataalamu wa Afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba eneo hili la Chuo Kikuu (MUHAS), lipewe *attention* ya kutosha. Eneo la Chuo Kikuu cha sasa pale Dar es Salaam ni dogo hivyo ni muhimu sana kupanua maeneo mengine kwa huduma ya MUHAS. Chuo cha Muhimbili, kimefanya jitihada kubwa sana za kuhakikisha kuwa ni eneo la Mlonganzila. Hivyo, kwa kupitia mchango wangu huu, naomba kujua Serikali ina mpango gani wa kuendeleza eneo la Mlonganzila ?

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, nikumbushe kuwa ni muhimu kukawepo huduma za maji katika shule zote za msingi, watoto wapewe huduma ya maji ya kunywa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Loans Board; 65,000, 67,000, watakaopewa mikopo, baadhi ya vyuo hivi sasa vimepandisha ada kwa mfano Tumaini kutoka 1.5 to 2m; UDSM kutoka 1.6 to 2.5m; SEKUCO Lushoto 1.6 to 2m; na KCMC pia.

Aidha, ongezeko lote hilo Bodi ya Mikopo haikushirikishwa au kuwasiliana na vyuo husika. Tungeomba ufafanuzi kwani uwekezaji katika elimu kwa wakati huu wa sasa wa *Globalization* ni muhimu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Wilaya ya Ludewa iko pembezoni sana ; hivyo ninaomba maabara katika Sekondari ya Kayao Kata ya Madope.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Vyuo vya Ufundi nchini kama VETA, ambavyo huchukua vijana wetu wengi bado ni vichache sana ; na kundi hili bado ni kubwa la vijana wanaomaliza Darasa la Saba na kushindwa kujiendeleza ; ningependa kujua mikakati ya kuanzisha Vyuo hivi katika Manispaa zote nchini ? Kuna vyuo vichache sana, ambavyo havikidhi, ningependa kujua mikakati ya Serikali kusaidia sekta binafsi ambazo zinawekeza katika eneo hili la kuanzisha Vyuo vya Elimu ya Ufundi.

**MHE. ROSEMARY K. KIRIGINI**: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa wakati nikichangia kwa kusema, muda wangu ulikwisha kabla sijamalizia kuchangia mambo mengi muhimu, nichukue wakati huu kuwasilisha baadhi ya mambo ambayo ningependa kupata ufafanuzi.

Kwa kuwa Chuo Kikuu Huria kimepanuka mno; na kwa kuwa mwaka hadi mwaka OC ya Chuo Kikuu Huria imekuwa ikishuka; na kwa sababu OC hii hutumika na Chuo kwa kulipa walimu wa muda jambo linalosababisha walimu hawa kuwa na malimbikizo ya madeni kutokana na OC hii ambayo ni ndogo na mbali na matumizi mengine pia hutumika kuwalipa walimu hawa wa muda; ningependa kupata maelezo toka kwa Waziri ni kwa nini OC hii haiongezeki kutokana na ukuaji na upanukaji wa Chuo hiki Kikuu Huria ?

Mheshimiwa Naibu Spika, Chuo Kikuu Huria kinahitaji kiasi cha fedha zipatazo Sh.170 bilioni ili kukamilisha ujenzi wa Makao Makuu ya kudumu huko Kibaha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ilivyofanyika kwa Vyuo Vikuu vingine, mfano Chuo Kikuu cha Dodoma; kwa nini Chuo hiki kisipewe *guarantee* ya Serikali ili kiweze kukopa kiasi hiki cha fedha toka kwenye taasisi za fedha mfano, NSSF, PPF na LAPF ili kiweze kukamilisha ujenzi wa Makao Makuu ya Chuo hiki Kikuu Huria?

Mheshimiwa Naibu Spika, ni dhahiri kabisa, Serikali imechelewa sana kuweka miundombinu ya kuunganisha Vyuo vya Elimu ya Juu na mtandao wa Kimataifa kupitia SEACOM, kutavifanya vyuo vyetu viwe nyuma sana kitaaluma kikiwemo Chuo Kikuu Huria cha Tanzania baada ya SEACOM kuunganishwa Julai, 2009.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru na ninaomba kuwasilisha.

**MHE. JOEL N. BENDERA**: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, napenda kuchukua nafasi hii, kumpongeza Waziri wa Elimu, Naibu Mawaziri, Katibu Mkuu na Wataalamu mbalimbali wa Wizara hii, kwa hotuba nzuri sana.

Ninayo mambo machache ambayo ninaomba sana yapatiwe majawabu katika Jimbo langu la Korogwe Mjini, mambo hayo ni kama ifuatavyo:-

Ninazo Shule za Sekondari 10 katika jimbo langu, lakini zote hazina maabara. Ninaomba msaada wa maabara, hata kwa kuanzia katika shule tatu na Chuo cha Ualimu Korogwe. Shule hizo ni Semkiwa Secondary School; Kilole Secondary School; na Old Korogwe Secondary School. Muhimu zaidi, Chuo cha Ualimu Korogwe.

Ninaomba sana msaada nilioahidiwa kujengewa bweni la wasichana katika Shule ya Sekondari Semkiwa. Wananchi wa Korogwe, wameanza mchakato wa kujenga bweni hilo. Hapa tunachoomba ni Wizara kutuunga mkono.

Idara ya Ukaguzi ni muhimu sana. Ninashauri iimarishwe kwa kupatiwa usafiri na kupatiwa wakaguzi wengi. Nimegundua kwamba, shule zilizopata matokeo mazuri ni zile zilizopandishwa mara nyingi. Kwa hiyo, kuwepo na msisitizo kwa idara hii kufanya kazi zaidi ili kuboresha taaluma.

Chuo cha Ualimu Korogwe, kimeanzisha jengo kubwa la maktaba. Jengo hilo, Chuo peke yake tutachukua muda mrefu kulimaliza. Tunaomba msaada kiasi chochote ili kuunga mkono juhudi za Chuo cha Wananchi wa Korogwe na Mbunge wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, imani yangu, maktaba hii itasaidia shule zote zinazozunguka Chuo cha Ualimu Korogwe zipatazo kumi. Maktaba ni chombo muhimu sana kwa kuboresha taaluma.

Chuo cha Ualimu Korogwe kiongeze udahili wa walimu wa Daraja la IIIA kama ilivyokuwa zamani. Hilo litasaidia sana kupunguza pengo la upungufu wa waalimu nchini.

Ninaomba sana, Wizara ipange tarehe zinazojulikana katika mwaka za mashindano ya UMISHUMTA, UMWETA na Vyuo, ikizingatiwa mambo ya msingi kwamba ratiba na siku za masomo zisiingiliwe. Aidha, hiyo itasaidia sana kupata msaada toka kwa wafadhili ambao wanaonesha nia ya kusaidia sehemu ya gharama, pamoja na kutangaza kwamba, mashindano hayo yameainisha, lakini yapo wazi.

**MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI**: Mheshimiwa Naibu Spika, katika kujadili Bajeti ya Wizara ya 2008/2009, Mheshimiwa Waziri, aliahidi kuhakikisha Wilaya ya Ludewa inajengewa Shule ya Ufundi Stadi (VETA). Kwa sasa maandalizi yote yamekamilika, pamoja na kupatikana ardhi ya kutosha iliyopimwa na kupata hati miliki. Je, lini Chuo hicho kitaanza kujengwa Ludewa?

Tatizo mojawapo linalorudisha nyuma maendeleo ya elimu hasa ya msingi ni kwa Kitengo cha Ukaguzi wa Shule kutokufanya kazi kama inavyostahili. Wakaguzi wapo, lakini hakuna bajeti inayotengwa kwa ajili yao ili kuwawezesha kufanya kazi kwa ufanisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Ofisi ya Ukaguzi ipewe au itengewe bajeti kama vile idara nyingine za Halmashauri. Kwa namna ya pekee, Wakaguzi Ludewa wapewe gari na kompyuta.

Shule mpya ya Sekondari ya Mount Masusa Wilayani Ludewa, imekumbwa na tatizo la kufiwa na aliyekuwa Mwalimu Mkuu wa Shule hiyo, ambayo kwa sasa ina mwalimu mmoja tu wa cheti. Ni karibu nusu mwaka, tangu Mkuu huyo wa Shule afariki na hadi leo hakuna *replacement.* Kwa vile shule ni mpya na watoto karibu 200 wanakosa msimamo au msingi na mwongozo wa maendeleo; naomba tupatiwe mwalimu mkuu mara moja.

Walimu wa MEMKWA, hasa Ludewa, wanajitolea kufundisha watoto wetu na wanatoa mchango mkubwa sana hapa nchini. Watoto ambao sasa wanafanyiwa utaratibu wa kuingizwa katika mkondo rasmi wa elimu ya msingi. Walimu hawa kwa Ludewa hawalipwi na Serikali za Vijiji husika. Naomba Serikali itusaidie Ludewa kutoa posho kwa walimu hawa, kwa vile vijiji havina uwezo.

Serikali inajali sana Vyuo Vikuu vipya na kupuuza vyuo vya zamani kama kile cha UDSM. Tunaacha mbachao kwa msala upitao.

**MHE. HALIMA J. MDEE**: Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia matamko mbalimbali, iliahidi kutoa udhamini utakaowawezesha wanafunzi wanaomaliza Shahada ya Sheria (LLB) kwa kusema shule ya sheria *(Law School)* ili kuwawezesha kutimiza matakwa ya kisheria ya kuweza kuajiriwa kama mtumishi wa Serikali (kama mwanasheria), hali kadhalika kupangiwa kama Wakili katika Mahakama Kuu ya Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika ahadi husika zilitoweka wakati Serikali ikitoa majibu ya barua ya *Tanzania Higher Learning Students Organisation (TAHLISO)* kwamba,

Serikali imeingia makubaliano baina ya Bodi ya Mikopo na Wizara ya Katiba na Sheria ili kuwawezesha wanafunzi wa Kitanzania maskini, kuweza kupata elimu husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala husika lilirudiwa katika Hotuba ya Bajeti 2008/2009, ambapo Waziri wa Katiba na Sheria, aliwahakikishia wanafunzi maskini wa Kitanzania, uhakika wa kuwepo kwa fungu husika litakalotolewa na Wizara ya Fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kinyume na matarajio ya wengi, fungu husika halikupatikana ; hali iliyopelekea wanafunzi wengi kushindwa kutimiza hitaji hilo muhimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, wanafunzi wanalazimishwa kulipa ada, malazi na vyakula, wengi wao wakiwa hawana kipato chochote kutokana na ukweli kwamba, wengi wao ni wanafunzi waliomaliza kipindi cha miaka minne masomo ya sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na uanzishwaji wa *Law School*, ambayo kimsingi imehodhiwa na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, inawalazimisha wanafunzi kutoka mikoa mingine ya Tanzania, kulazimika kuja Dar es Salaam kusoma, pasipo msaada wowote toka Serikalini.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nipate majibu toka kwa Mheshimiwa Waziri ni nini kilichopelekea Serikali kujitoa kabisa katika udhamini wakati ikijua fika itakuwa ni vigumu kwa watoto wengi wa Kitanzania kukidhi masharti husika ? Hali kadhalika, napenda kufahamu kama Serikali ina mipango yoyote ya ziada ili kutafuta ufumbuzi wa suala husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, tangu *Law School* ilipoanzishwa, na *Cohort* ya kwanza ni mwaka, miezi sita imepita na mpaka sasa imeshafika *Cohort* ya Tano na ya sita iko mbioni.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, hakuna matokeo yoyote ambayo yameshatoka kuonesha mustakabali au mafanikio ya *Law School*, kwani matokeo ya *Cohort* ya kwanza yaliyotarajiwa mwezi March, 2009 bado yanasubiriwa na hatima ya wanafunzi husika bado haijulikani.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kupata maelezo toka kwa Mheshimiwa Waziri ya mikakati ya utatuzi wa upungufu huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ilitangaza kuvifuatilia vyuo vya dini ili vitoe elimu bora na nafuu kwa Watanzania, hasa watoto wa maskini. Kinyume chake, kuna baadhi ya vyuo vya dini; mfano Tumaini University, baada ya tamko hilo, wamepandisha ada na bila hata kutoa *notice* kwa wanachuo. Kupandishwa huko, kumewafanya baadhi ya wanafunzi kushindwa kulipa ada na hata Bodi ya Mikopo wamesema hawatambui ongezeko hilo la ghafla.

Mheshimiwa Naibu Spika, je, Serikali inatoa maelezo gani kuhusu hali hiyo hasa ikizingatiwa kwamba wanafunzi wengi watashindwa kumudu gharama zilizoongezeka ghafla ?

Mheshimiwa Naibu Spika, ni muda mrefu sasa walimu wetu wanekuwa wakidai malimbikizo yao. Hali iliyopelekea Serikali kuunda Kamati Maalum kwa ajili ya kufanya uhakiki wa madeni husika. Uhakiki ambao umeshakamilika kwa sasa na kwa mujibu wa Waziri wa Utumishi, fungu husika limeshatengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa Mheshimiwa Waziri alieleze Bunge lako Tukufu, fungu husika liko katika Vote gani na ni shilingi ngapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. DKT. CHARLES O. MLINGWA**: Mheshimiwa Naibu Spika, narudia kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Mawaziri, Katibu Mkuu na Watendaji Wakuu wote, kwa kazi muhimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nyongeza ya mchango wangu:-

(a) Ningependa kuelezwa bayana ni lini au mwaka gani MUCOBS kitakuwa Chuo Kikuu kamili ? Hotuba yako haijabainisha wazi kuhusu hili. Sambamba na hili la kuwa Chuo Kikuu kamili nauliza ni vitivo vingapi na vya fani zipi vitaanza kujengwa katika kampasi ya Kizumbi ambayo ni kubwa kuliko kampasi zote za Chuo hiki?

(b) Ni lini walimu wataacha kuzomewa na udhalilishaji mwingine kama inavyojidhihirisha kwenye Gazeti la leo tarehe 24 Julai, 2009 la Taifa Letu ?

(c) Kwa mikoa iliyofanya vibaya katika matokeo ya Darasa la Saba mwaka 2008, kwa nini Mheshimiwa Waziri usiwatake walimu wote katika mikoa husika wakuletee sababu za hali hiyo badala ya kutegemea maelezo ya watawala peke yake ?

Mheshimiwa Naibu Spika, suala hili uwatake wabainishe sababu tatu za msingi na nyingine. Hii itakuwezesha kuelewa bayana kiini cha tatizo na hivyo kulitafutia ufumbuzi wa kweli na wa kudumu bila kuwanyanyasa walimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, walimu ni waumbaji wa mtu duniani, hivyo wathaminiwe na kusaidiwa ipasavyo.

**MHE. GOSBERT B. BLANDES**: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Mawaziri wote na Katibu Mkuu wa Wizara, kwa hotuba yao nzuri. Pia nawapongeza Naibu Mawaziri ; Mheshimiwa Kabaka na Mheshimiwa Mahiza, kwa kujibu maswali yao kwa ufasaha hapa Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jimbo langu la Karagwe halina walimu wa kutosha na kutokana na ongezeko la wanafunzi wa shule za msingi, karibu mara mbili katika miaka

mitatu iliyopita na kuendelea kupungua kwa walimu kiwango cha ufaulu kinavyozidi kuporomoka ni kwa sababu hiyo. Hitaji la walimu Wilayani Karagwe ni la msingi na la haraka sana. Hali ni mbaya zaidi katika upande wa Sekondari, mfano, Shule ya Sekondari ya Ihembe, ina mwalimu mmoja tu! Naomba walimu katika Shule za Sekondari Ihembe, Rugu, Nyakasimbi, Ruhinda, Nyakahanga, Kayanga, Ndama, Kihanga, Igurwa, Ruiche, Kiruruma, Nyabiyonza, Kawela, Nono, Kibondo, Bugene, Katembe, Chakaruru na Rwambaizi. Hali ya walimu kwenye shule hizi za sekondari inakatisha tamaa. Serikali ipeleke walimu wa kutosha haraka ili kutuondolea aibu inayoweza kutupata Jimboni Karagwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, shule zote za sekondari Jimboni Karagwe hazina maabara. Serikali ijenge na kuleta vifaa vya maabara haraka iwezekanavyo. Ikibidi tuanze na *Science Kits* zinazouzwa na wajasiriamali. Bila maabara, hatutapata wanasayansi.

Tatizo la kuvuja kwa mitihani limekuwa sugu. Tuna hatari kubwa mbele yetu ya kutengeneza Taifa la watu wasiojiamini na wasio na ujuzi. Hatutaweza kushindana na wenzetu katika ajira. Wizara ifanye kila linalowezekana, upuuzi huu ukomeshwe. Kama hali hii itajitokeza mwaka ujao au miaka ijayo, ninashauri Waziri wa Elimu ajiuzulu mwenyewe kwa misingi ya uwajibikaji. Pia, nashauri Baraza la Mitihani la Taifa, lipatiwe bajeti ya kutosha ili linunue vifaa vya kudhibiti wizi, vinginevyo tutazidi kuwalaumu bure.

Mishahara ya walimu bado ni midogo, lakini kibaya sana hailipwi kwa wakati; ni kwa nini? Tafadhali sana, Serikali iondoe kero hii moja kwa moja ya kulimbikiza mishahara ya walimu wetu. Kitendo cha kulimbikiza mishahara ya walimu kinawadhalilisha sana kwa kukopa mahitaji yao ya kila siku.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. HASSAN C. KIGWALILO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua nafasi hii, kuchangia Hotuba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, Mheshimiwa Prof. Maghembe. Ninampongeza Mheshimiwa Waziri, kwa hotuba na kwa kazi nzuri. Aidha, ninawapongeza Naibu Mawaziri; Mheshimiwa Kabaka na Mheshimiwa Mahiza, kwa kujibu maswali vizuri Bungeni na kwa ushirikiano wa dhati, wanaoutoa wakati nikifuatilia masuala mbalimbali ya elimu, yahusuyo Jimbo langu. Bila kusahau, ninawapongeza Katibu Mkuu, Wakurugenzi na Wataalam husika, kwa hotuba hii nzuri ambayo ninaiunga mkono kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaipongeza Serikali kwa jitihada zinazofanywa, kuendeleza Elimu nchini. Kikwazo kikubwa ni ufinyu wa bajeti. Hata hivyo, pawepo na utaratibu kwa kutumia kilichopo, kuboresha maslahi ya walimu wa ngazi zote. Kwa ushirikiano wa Halmashuri zetu, pawe na mwongozo wa jinsi ya kutoa motisha kwa maeneo yenye mazingira magumu kama Wilaya ya Liwale na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachukua fursa hii, kushauri kwamba, wale walimu waliohitimu mafunzo yao na wangependa kufanya kazi maeneo wanayotoka hasa yale yenye mazingira magumu, waruhusiwe kufanya hivyo. Kwa mfano, baadhi ya walimu wapya kutoka Liwale wamepangiwa kwenda nje ya Wilaya na Mkoa wa Lindi, kwa sababu zao za msingi wameniomba niiombe Wizara wabadilishiwe vituo na wapewe nafasi kufundisha Liwale kama walivyoomba.

Mheshimiwa Naibu Spika, baadhi ya walimu hao ni Imani Mtalika, Hydery Ndoka na Kondo A. Majorohu. Maombi yao niliyatuma Wizarani kupitia Naibu Waziri, Mheshimiwa Kabaka. Naomba vijana hao ambao wapo tayari kufanya kazi Liwale, eneo mojawapo lenye mazingira magumu waruhusiwe. Nitashukuru kwa hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutekeleza ujenzi wa Sekondari, Kata ya Liwale ina Sekondari 15, ikiwemo Liwale Day ambayo pia ni High School. Liwale Day ina walimu wanne tu wa O-Level, ina upungufu wa walimu 20 wa High School na A-Level ina walimu wanne tu na upungufu wa walimu sita. Sekondari nyingine ni kama ifuatavyo: Sekondari ya Barikiwa, Nangano, Kibutuka, RM Kawawa, Mlembwe, Ngunja na Banduka, ambazo zina walimu kati ya wawili hadi watatu na nyingine ni Sekondari za Mihumo, Anna Magowa, Milna, Mirui, Mkundi na Kiangara, ambazo zina mwalimu mmoja tu kila sekondari. Baadhi ya sekondari hizo zina nyumba mbili hadi tatu nzuri, zilizojengwa chini ya miradi mbalimbali kama TASAF. Hivyo, tatizo la nyumba za walimu kwa baadhi ya sekondari hizo halipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Elimu ina takwimu kamili za upungufu wa walimu wa kada mbalimbali katika Shule za Msingi, Sekondari hadi High School kwa kila Wilaya ikiwemo ya Liwale. Naomba zitumike kwa kutuletea walimu zaidi kwa Wilaya ya Liwale.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu madeni ya walimu, naomba uwekwe utaratibu maalumu wa kulipa madeni hayo ili tatizo hili lisijirudie mara kwa mara, kwani linapunguza ari ya walimu kufanya kazi zao vizuri. Baadhi ya walimu walio katika *contract*, hawatalipwa baadhi ya mishahara yao kwa kipindi walichoanza kufundisha. Nina mfano mmoja, kwa Shule ya Sekondari R.M. Kawawa, ambaye *details* zake zimetumwa Wizarani tukisubiri matokeo.

Mheshimiwa Naibu Spika, narudia kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, nampongeza Mheshimiwa Waziri na Watumishi wote wa Wizara, kwa kazi muhimu na ngumu wanayoifanya na kwa Hotuba nzuri. Nachangia katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, sera juu ya mikopo haijaeleweka vizuri. Kwanza, swali la msingi ni kama Mfuko huu unaweza kufika ukajiendesha? Nitafurahi kama jambo hili litafanyiwa utafiti na majibu yaoneshe dira iliyo sahihi. Tafakari ya mawazo inaonesha wazi kwamba, Mfuko utaendelea kuwa mzigo kwa Bajeti ya Serikali na ni chanzo cha matatizo mengi, pamoja na migomo. Aidha, ukomo wa bajeti haueleweki,

mfano, mwaka huu Wizara imelazimika kutegemea bajeti ya ziada ya kiwango cha bilioni 80, ambayo haina uhakika na kama hazitapatikana basi Wizara ijiandae kwa matatizo, pamoja na upotevu wa amani. Mawazo yangu yananielekeza kwamba, jambo hili tunalipa mfumo wa kisiasa zaidi kuliko ukweli wa kibajeti. Ukiacha siasa, Serikali ingesema ukweli tu kuwa uwezo wa kifedha basi na itangaze uwezo wa Serikali kila mwaka na itoe *bursary* badala ya mikopo isiyorudishika. Wale wanaopewa *bursary* ya Serikali, wafanya kazi ya Serikali kwa mkataba kwa takriban miaka mitano.

Mheshimiwa Naibu Spika, labda kwa idadi ya walimu tulionao, mtindo wa mafao uangaliwe upya. Inanisikitisha kuona kwamba, katika madai yanayodaiwa kuna udanganyifu mkubwa. Hotuba imesema madeni bilioni 22.6, za kweli bilioni 17, udanganyifu bilioni 5. Hali hii haikubaliki na inaonekana madai haya ni biashara mpya. Nashauri kipaumbele kipewe kwenye mishahara na mazingira mazuri ya kuishi, kwa mfano, nyumba nzuri na mishahara mizuri, ambayo mafao ya uzeeni kama pensheni, yatakuwa mazuri kuliko hizi *allowances* zinazodaiwa. Tutazame upya ajira ya walimu na tupunguze safari za likizo na matibabu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Utawala wa Elimu *(Education Administration)*; naipongeza Serikali kwa uamuzi wa kupeleka Sekondari ziwe chini ya Halmashauri. Ukweli ni kwamba, mazingira ya Halmashauri kutawala elimu, lazima pia yarekebishwe ili Idara ya Elimu katika Halmashauri ziimarishwe. Aidha, ajira ya Wakuu wa Shule za Sekondari ihamie Halmshauri ili wawajibike kwa Mkurugenzi wa Halmashauri. Kwa muda mrefu, *Headmasters* wanajiona ni huru na Mkurugenzi siyo mwajiri wao. Jambo hili litamkwe bayana na Waziri katika Mkutano huu wa Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, sanjari na hili, usafiri na fedha ya matumizi mengineyo (OC), iwekwe bayana kwa Idara hii muhimu zaidi wakati huu wa mpito kutoka Serikali Kuu – Halmashauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. JOSEPH J. MUNGAI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja na nawapongeza sana Waziri na Maibu Mawaziri, kwa uongozi wao mzuri wa Wizara hii muhimu sana. Nampongeza sana Waziri wa Elimu, kwa hotuba yake yenye maelezo mazuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mchango wangu, naomba nifafanue suala la lugha ya kufundishia kwa kuweka rekodi sawa kuwa, miaka saba ya kwanza, elimu ya msingi inatolewa kwa Lugha ya Kiswahili, ikifuatiwa na Kiingereza kufundishiwa elimu ya sekondari kwa miaka sita (Kidato cha I – VI). Kwa hiyo, ukweli huu ni kwamba, Lugha zote mbili; Kiswahili na Kiingereza, zinatumika kutoa elimu ya msingi na sekondari.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri, alieleze Bunge, wanafunzi wanafaulu vipi masomo ya Lugha za Kiswahili na Kiingereza katika Mitihani ya Kitaifa? Kwa maoni yangu ni muhimu sana wanafunzi wetu wafundishwe vizuri na

wafaulu vizuri masomo hayo ya kufundishia. Upo usemi kuwa, elimu ni ufunguo wa maisha. Mimi nasema lugha ya kufundishia ni ufunguo wa elimu. Tusijidanganye kuwa, kuongea kwa Kiswahili ni kukijua Kiswahili cha kufundishia au kujifunzia.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri suala hili la lugha za kufundishia na kujifunzia, liamuliwe kwa kuzingatia taaluma na mahitaji ya elimu na siyo utashi wa kisiasa. Kwa kutoa elimu ya msingi kwa Kiswahili, tunafanya jambo kubwa na nadhani ni Tanzania tu tunaofanya hivyo hapa Duniani. Ushauri wangu, teongeze ufasaha wa kufundisha masomo ya lugha na hisabati.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. BUJIKU P. SAKILA**: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutumia fursa hii, kwanza, kuwapongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Mawaziri na Watumishi wote wa Wizara hii, kwa kazi nzuri zinazoendelea kufanyika chini ya Wizara hii hapa nchini. Wizara hii ni ngumu, ina mambo mengi na imepambana na mabadiliko mengi mno ya kiuendeshaji ndani ya kipindi kufupi.

Ugatuaji wa uendeshaji na usimamizi wa Shule za Sekondari, limekuwa ni badiliko kubwa. Ninapongeza kwa utaratibu mzuri uliotumika katika zoezi hilo. Iwapo kutakuwa na upungufu utakaokuwa ukijitokeza kutokana na zoezi hili ni vyema uwe ukishughulikiwa mapema ili hali hiyo isije ikakatisha tamaa Walimu wa Shule za Sekondari.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na pongezi nilizozitoa kwa mambo mazuri yanayoendelea kutokea ndani ya Wizara hii chini ya Uongozi wa Mheshimiwa Prof. Maghembe, Naibu Mawaziri wake wote wawili; Mheshimiwa Gaudentia Kabaka (Mb) na Mheshimiwa Mwantumu Mahiza (Mb) na Katibu Mkuu wa Wizara hii. Napongeza pia kwa hotuba nzuri iliyotolewa na Mheshimiwa Waziri mbele ya Bunge hili, kwa uchapa kazi, usikivu, uvumilivu na ubunifu wa viongozi. Ninaamini kuwa, asilimia kubwa ya yaliyopangwa kwa fedha waliyoiomba yatatekelezwa. Hivyo, sina wasi wasi wowote na sina budi kutamka kuwa, ninaunga mkono hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya utangulizi, naomba kuendelea kuchangia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, madeni yana athari ya moja kwa moja kwa ubora wa elimu, kwa kuwa yanakatisha tamaa na kuvunja ari ya kazi kwa kujituma kwa wazabuni mashuleni; watoa huduma (maji na nishati mashuleni); wanafunzi; na walimu. Hivyo, mara kwa mara husababisha migomo mbalimbali, kitu kinachosababisha masomo kutokutolewa kikamilifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Serikali pamoja na juhudi kubwa na za kutia moyo zilizofikiwa na Wizara, Hazina ishawishiwe kutoa fedha hiyo mapema. Ni vyema nguvu za ziada zikatolewa na Serikali ikaitaka Wizara ya Fedha, kuona umuhimu wa

kutoa fedha hiyo mapema. Wizara hii ndiyo mara nyingi huiangusha mipango mizuri ya Wizara ya Elimu katika suala hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka jana ahadi nyingi zilitolewa kuhusu ujenzi wa Vyuo vya Ufundi (VETA), kimoja kila Wilaya. Mwendelezo wa ahadi hiyo, hauko wazi mwaka huu. Je, ahadi hiyo mbona imefifiishwa mwaka huu kulikoni?

Baada ya ujenzi na Chuo cha Ufundi Makete kutakuwa na ujenzi wa vyuo viwili tena katika Wilaya mbili zaidi. Ninafahamu wataalamu watakuwa wanakwenda kukagua maeneo yaliyotengwa kwa shughuli hiyo katika wilaya nyingine ikiwemo Kwimba. Naomba Wilaya ya Kwimba iwe moja ya Wilaya mbili zinazofuata.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba elimu ya lazima sasa iwe Kidato cha Nne, tutoke kwenye elimu ya msingi.

Gari kwa Shule ya Sekondari ya Wasichana Mwamashimba: Shule hii ni ya ‘A’ Level kwa wasichana, iko kilomita 100 kutoka Mwanza na kilomita zaidi ya 70 kutoka Makao Mkuu ya Wilaya. Imezungukwa na Shule nyingine sita za sekondari, kwa muda mrefu nimekuwa nikiiombea shule hiyo gari na leo natoa tena ombi hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitumie fursa hii kutoa nyongeza juu ya michango yangu ambayo tayari nimeiwasilisha. Katika nyongeza yangu hii, ninapenda kuchangia katika mambo mawili kama ifuatavyo:-

Kwanza, binafsi nashawishika kuamini kuwa, kazi ya Baraza la Mitihani ni nzuri na inaendelea kuwa bora kila mara. Dosari za mitihani kuvuja, huchafua sifa nzuri za Baraza. Ninaamini kuwa, Mkurugenzi Mtendaji wa Baraza, Dkt. Ndalichako, anafanya kazi nzuri sana. Kwa tathmini zangu, mama huyu ni mzalendo, shupavu na mchapakazi; ni dhahiri mtu anayeifahamu historia ya Baraza kabla na baada ya kufika mama huyo katika taasisi hiyo, hategemei kuwa atakuwa na marafiki wengi. Kwa mtu anayetaka kulitendea haki Taifa hili kupitia Taasisi hii, siyo ajabu akazungukwa na maadui ambao wangependa kumwangusha ili juhudi zake zisionekane. Kwa watu wanaowafahamu baadhi ya waliokuwa Watumishi wa Baraza hilo, maisha yao, majumba yao na kulinganisha na vipato vyao halali, mtu awaye yoyote, hasiti kuhisi kuwa kuna mchezo mchafu katika kukihujumu kituo cha kazi.

Hata hivyo, kwa lengo la kusaidia Bazara kugundua udhaifu na mianya ya mitihani kuvuja, Tume Teule yaweza kuundwa na ikaenda kuchunguza. Mimi sidhani kuwa ni busara kuunda Tume hiyo kwenda kumchunguza mtu mmoja kwa nini anafukuza watumishi na sababu zinajulikana! Iwapo wapo waliofukuzwa na wanaamini wameonewa, waagizwe kujitokeza wafuate utaratibu kudai haki zao. Iwapo wapo watu waliobadilishiwa vituo vya kazi na wanataka warudishwe Baraza, basi wajitokeze waseme ni kwa nini wanataka warudi Baraza wakati hawajafukuzwa kazi. Bila shaka wataeleza kuna nini walichokiacha Baraza na wanavikosa walikopelekwa. Namwomba Mheshimiwa Waziri, amtie moyo Mkurugenzi asije akavunjika moyo na kukata tamaa.

Wasichana wanaopata mimba mashuleni na kufukuzwa, kurudishwa kuendelea na masomo: kwanza, ninaomba kuuliza; je, tunaowarudisha tunataka wapate elimu ipi waliyoikosa? Je, ni kwa nini wafukuzwe shule? Nifahamuvyo, wanafukuzwa shule kama adhabu, baada ya kudhihirika kuwa wametenda kosa lisilokubalika katika jamii. Kwa kikundi hiki, wametenda tendo la ngono/wamezini! Je, shuleni kuna makosa mangapi yanayosabisha mwanafunzi kufukuwa shule? Kama lengo ni kumpa mtoto haki ya kupata elimu; je, ni kosa lipi linalosababisha wanafunzi wengi kufukuzwa shule na kumfanya akapoteza haki yake hiyo? Je, kwa wanafunzi wote wanaofukuzwa shule katika mwaka mzima; hii ya mimba inapoteza asilimia ngapi ya vijana?

Mheshimiwa Naibu Spika, bila shaka hakuna mtu ambaye angependa adhabu ziondolewe kwa makosa hayo. Ninashawishika kuamini kuwa, kinachowasumbua wengi ni kuona adhabu ya kufukuzwa shule ni kubwa mno na wanakimbilia kusema iondolewe badala ya kusema ipunguzwe. Ninaomba wote tukubaliane kuwa, kitendo hicho ni kosa linalostahili adhabu; ni vyema tukasema ni adhabu gani mwanafunzi huyo apewe ili atambue kuwa ametenda kosa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninashauri yafuatayo:-

(1) Muda wa kujifungua ukikaribia, mwanafunzi atakiwe kwenda nyumbani kujifungua.

(2) Atakiwe kurudi shuleni baada ya mwaka mmoja na nusu au miaka miwili baada ya kujifungua, akiangalia mtoto wake kipindi chote hiki, binti huyu anahesabika kuwa mwanafunzi.

(3) Baada ya kipindi hicho, arudipo shuleni aje kuanza alipokuwa ameishia na alazimike kuendelea na masomo mpaka pale atakapohitimu elimu inayotakiwa kisheria.

(4) Pamoja na sheria zilizopo, sheria itungwe ya mwanafunzi yeyote wa namna hii au mtu mwingine yeyote atakayekataa/kumkataza au kumsababishia asiendelee na masomo, achukuliwe hatua za kisheria. Hatua hii itaweka uzito wa adhabu ya kutokuwa shuleni kipindi cha kubaki nyumbani, kwa kipindi cha mwaka mmoja na nusu au miwili kama adhabu kwa kosa lililomsababishia mimba. Mazingira ya kupata ujauzito huo, mfano, kubakwa na kadhalika vikithibitishwa, vitaweza kurekebisha uzito wa adhabu.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo ninaloogopa ni kutoa ruhusa ya mwanafunzi huyo kurudi shuleni na kuendelea na masomo kwa kuondoa dhana ya adhabu. Hivyo, tutakuwa tunabariki kosa la mwanafunzi kutenda kitendo cha ngono/kuzini, hata baada ya kosa hilo kuthibitishwa. Ni vyema ikawa wazi, uwepo wa kosa na adhabu kwa kosa hilo mara linapothibitishwa, vitaweza kurekebisha uzito wa adhabu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vyema Serikali ikakili uzembe wa kushindwa kusimamia kwa dhati, sheria na kanuni mbalimbali zilizotungwa kumlinda msichana ili aendelee kupata haki yake ya elimu. Kama tu Serikali ingelisimamia, ninaamini tusingeshawishika kufika hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, huu ni mwendelezo wa mchango na ninayo masuala matatu tu ya kuongelea kama ifuatavyo:-

(a) Wapo vijana wa vyuo vikuu; UDOM ikiwa ni mfano mzuri, wanatarajia kuanza mafunzo yao kwa vitendo *(field)*, kutoka chuoni kwenda walikokubaliwa kwenda kufanya mazoezi hayo, wanastahili kupewa nauli. Kwa bahati mbaya, fedha hiyo hawakupewa. Je ; ni kitu gani kimetokea na fedha hiyo wasipatiwe ? Je, serikali imeandaa utaratibu upi wa kuwawezesha wanavyuo hawa kupata fedha hiyo ?

(b) Yapo malalamiko mengi yanatolewa na wanachuo wa Chuo Kikuu Huria. Makubwa ni kutokupata fedha yao. Rejea matatizo yaliyojitokeza kwa vijana hawa, walipokuwa Mpwapwa karibu na kuanza mitihani yao kwa kilichosababisha wakaja mpaka hapa Bungeni na hatimaye kufukuzwa na Jeshi la Polisi kwa mabomu ya machozi. Namwomba Mheshimiwa Waziri, aelezee kama tatizo hilo sasa limekwisha ; lilitokeaje na nini suluhisho lake ? Wanachuo hao wanasubiri maelezo ya Mheshimiwa Waziri.

(c) Matokeo ya mitihani kuchelewa sana kutolewa, kupotea na mara kadhaa kuwalazimisha wanachuo kurudia masomo na mitihani kwa gharama zao. Je, tatizo hilo linasababishwa na nini ; lini na kwa utaratibu gani Wizara imejipanga kulitatua tatizo hili ili kuwafanya wanachuo wapya wanaotarajia kujiunga na utaratibu huo wasikate tamaa na kuamua kujiunga na vyuo vingine ? Namwomba Mheshimiwa Waziri atoe maelezo.

Mwisho kabisa, nazipongeza shule mbiu za ‘A’ Level katika Jimbo langu, zinazoendelea kufanya vizuri katika masomo, nazo ni Shule ya Sekondari Ngudu na Mwamashimba. Naomba Wizara ikubali ombi langu na Wilaya ya Kwimba, kuipandisha Shule ya Sekondari ya Nyamilama kuwa ya ‘A’ Level mwakani. Namwomba Waziri au Naibu Waziri, akubali kutembelea Kwimba ili azitembelee shule hizo na nyingine Wilayani humo, kwa lengo la kuwatia nguvu walimu, wanafunzi na wananchi wanaozijenga shule hizo. Mawaidha yake na maelekezo yake, kwa uhakika yatakuwa changamoto chanya kwa maendeleo ya elimu katika Jimbo na Wilaya ya Kwimba.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mheshimiwa Waziri akubali na tunamkaribisha sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante na ninaunga mkono hoja.

**MHE. MBARUK K. MWANDORO:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua fursa hii, kutoa pongezi zangu za dhati kwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, Mheshimiwa Profesa Jumanne Maghembe (Mb), Naibu Mawaziri, Katibu Mkuu na Watendaji wengine wa Wizara na Taasisi zake, kwa hotuba nzuri na kazi nzuri kwa jumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na jitihada kubwa zinazofanywa na Serikali kuboresha elimu na mafunzo ya ufundi, bado jitihada kubwa zaidi zinahitajika katika

maeneo mengi.  Awali ya yote, tatizo la walimu bado ni kubwa nchini kote, hasa katika maeneo ya vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuipongeza Wizara, kwa kujielekeza katika kuchukua hatua thabiti za kupambana na upungufu wa walimu kwa ngazi zote.  Pamoja na jitihada hizi; ni muhimu kuboresha maslahi yao ikiwa ni pamoja na kuboresha mishahara yao, kulipa madeni yao na kuwapatia makazi bora.  Haya ni muhimu zaidi kwa maeneo ya vijijini na pembezoni kama Wilaya ya Mkinga.  Ipo haja ya upendeleo maalumu kwa maeneo ya pembezoni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na umuhimu wa maabara kwa masomo ya sayansi na kwa kuwa ujenzi wa maabara una gharama kubwa, ni vyema Serikali ikabeba jukumu la kujenga maabara pamoja na kuzipatia maabara hizo vifaa vyake.  Aidha, Serikali ifikirie kubeba jukumu la kuhakikisha upatikanaji wa umeme kwa maabara hizo na kuwashirikisha wananchi kuchangia ujenzi wa madarasa, madawati, nyumba za walimu, mabweni, maktaba, mabwalo, viwanja vya michezo na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Elimu kwa mtandao wa kompyta ni hatua nzuri.  Hata hivyo, ipo haja kubwa sana ya kuwa na maandalizi makini na kamilifu.  Kwanza, ni muhimu kuhakikisha matayarisho mazuri ya wakufunzi.  Pili, ipo haja kubwa ya kuhakikisha uwepo wa umeme katika shule mbalimbali, japokuwa kuna kompyuta ambazo zinatumia betri kavu *(dry cell batteries).*  Hatua nyingine muhimu ni pamoja na kuwa na utaalamu wa kutosha na spea za kutosha ili kuweza kukabili matatizo ya kiufundi mara yanapotokea.

Mheshimiwa Naibu Spika, nafarijika na najivunia kwamba, Wilaya yetu mpya ya Mkinga, imeibuka ya kwanza katika Mkoa wa Tanga, kwa kufaulisha na kuweza kuwachukua wanafunzi wote waliofaulu Darasa la Saba kwenda Kidato cha Kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuendeleza na kuboresha hali hiyo kwa uendelevu, tungependa kurudia rai kwamba, Wilaya hii iwe miongoni mwa maeneo ya pembezoni yanayostahili kupewa upendeleo maalum.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:**  Mheshimiwa Naibu Spika, pongezi kwa Mheshimiwa Waziri, Manaibu wake na Wataalamu wote wa Wizara, kwa kuandaa Hotuba ya Bajeti na kuileta tuijadili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa muda mrefu, walimu wamekuwa wanalalamikia madai yao bila kukamilishiwa.  Hili linaitia aibu Taifa, kwa kutambua Taifa lolote bila elimu hakuna maendeleo.  Pia linawakatisha tamaa walimu ya kufanya kazi kwa moyo na hasa kwa kuzingatia mazingira magumu wanayofanyia kazi.  Mbaya zaidi, linatia hofu kwa wale wanaosomea fani ya ualimu, kuchepuka kwenda kwenye fani nyingine na hivyo kero ya upungufu wa walimu Tanzania, kuendelea kuwa tatizo sugu.  Serikali iondoe aibu hii kwa Taifa, haipendezi kuwa na majadiliano yasiyokwisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo nililoliona miaka ya hivi karibuni la mitihani kuvuja na chanzo chake kikiwa ni Baraza la Mitihani ni la aibu. Tunategemea Taifa hili kujenga wataalamu wa aina gani ambao wamefaulu kwa kuoneshwa mitihani? Watoto wa watu wenye uwezo, ndio wanaoibiwa mitihani na wanainunua. Watoto wa maskini, ambao wanafaulu kihalali, wanakosa nafasi ya kusoma shule bora, wanapelekwa waliofaulu kwa viwango vya juu kwa kuiba mitihani. Hii sio haki kwa nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Baraza la Mitihani, hutoa vyeti feki kwa baadhi ya wanafunzi wanaomaliza Shule za Sekondari na kuwasababishia usumbufu mkubwa makazini na vyuoni. Wapo walioathirika *Psychologically,* kwa kufukuzwa vyuoni kwamba, wana vyeti feki. Baada ya wazazi wao kuhangaika kwa muda mrefu, Baraza linakiri kwamba, vyeti hivyo vimetoka kwa makosa, hivyo ni feki. Kweli chombo muhimu kama hiki kinafanya mambo haya? Waziri alieleze Bunge; hawa watoto ambao wengine wamepoteza dira ya maisha yao wakati wazazi wao wakiwasomesha kwa matarajio makubwa; Serikali inawasaidiaje?

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imekuwa inatoa/inatenga fedha kwa ajili ya kuwasomesha watoto yatima na wale wanaotokea kwenye familia duni, baada ya kutambuliwa na Serikali ya Kijiji, Kata, Tarafa hadi Halmashauri. Hata hivyo, fedha hizi hazitolewi kwa wakati, jambo linaloleta usumbufu mkubwa sana kwa watoto hawa. Wamekuwa wanarudishwa nyumbani mara kwa mara na hivyo wengine kukata tamaa na kuacha shule. Kwa sasa hivi, shule hizi zimerudishwa TAMISEMI, lakini bado Serikali Kuu ndio wanatoa fungu hilo na kupeleka kwenye Halmashauri. Kwa kuwa hii ni dhamira nzuri kwa Serikali kuinua watoto hawa maskini, basi fedha zitoke kwa wakati. Pia, napendekeza Serikali iangalie namna ya kuwasaidia watoto hawa mahitaji yanayowawezesha kufika shule, mfano *uniforms fully*, nguo za michezo na kadhalika. Kwa kweli wengi wanashindwa kufika shule, kwa sababu hata *uniforms* hawana na hata chakula, wanaishi kwa msaada wa wasamaria wema.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la elimu kwa watoto wenye ulemavu wa aina yoyote ni muhimu sana na watoto wa kawaida. Kwa sehemu kubwa, watoto hawa wanasaidiwa na taasisi sizizo za Serikali na Mashirika ya Dini. Tunaomba Serikali ilieleze Bunge hili, mpango unaopangika kwa watoto hawa wenye ulemavu.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala hili katika jamii mara nyingi linasahaulika na hata majengo ya shule hayazingatii uwepo wa watoto hawa kuanzia madarasa, maabara na *toilets.* Hakuna uangalizi kusaidia watoto hawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, upungufu wa walimu hapa nchini ni tatizo kubwa sana. Hili limepelekea viwango vya elimu kuanza kushuka badala ya kupanda. Mwaka 2007/2008, wanafunzi watahiniwa theluthi mbili kupata Division IV na zero ni aibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hizi ni ishara mbaya. Serikali imesaidia watoto wengi kuingia shuleni, lakini mazingira ya elimu hayajaboreshwa; walimu hakuna, vifaa hakuna, maabara hamna na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, shule nyingi za vijijini hasa za Kata, ndizo zenye matatizo haya, lakini cha ajabu wanapewa mtihani mmoja, sawa na wale wanaosoma shule kongwe zenye vifaa na walimu wa kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itueleze ni vigezo gani inavyovitumia kutoa mtihani mmoja kwa shule zote za sekondari wakati upungufu wa shule zote unajulikana? Je, wanafunzi hawa wa shule zenye upungufu wanatendewa haki?

Mheshimiwa Naibu Spika, kule Urambo Kata ya Msisya kuna Shule ya Msingi, ina walimu wanne ambao wameajiriwa na wazazi na wanalipwa na wazazi wenyewe. Hivi kweli ndani ya miaka 48 ya Uhuru; shule inakosa mwalimu hata mmoja aliyeajiriwa na Serikali. Wanafunzi wanachangia kila mwezi kupata mishahara ya walimu hawa. Hili ni tatizo na Serikali ilifuatilie kwa karibu.

**MHE. HERBERT J. MNTANGI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwapongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Mawaziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara hii, kwa kazi nzuri na Hotuba nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kupewa maelezo na kutoa ushauri katika maeneo yafuatayo:-

Bado wanafunzi wengi wanahofia masomo ya sayansi kwa kuogopa hisabati, physics na chemistry. Katika matokeo ya wahitimu ya Kidato cha Sita 2008/2009, licha ya matokeo ya wastani kwa wahitimu hao, wapo wanasayansi wamepata Division III kwa sababu ya kufeli somo moja tu la Hisabati. Kwa sababu hiyo, wamekosa nafasi kwenda Chuo Kikuu. Licha ya kupenda masomo ya sayansi, matokeo hayo yamewakatisha tamaa na sasa wanajiondoa katika fani hiyo ya sayansi. Je, Serikali haioni haja ya kuwasaidia vijana hao walioonesha moyo wa kuipande sayansi kwa kufanya yafuatayo:-

(a) Kuwapa muda maalumu wa marudio ya somo moja au mawili aliyofeli kwa kuweka programu ya miezi sita ili wakae na walimu bingwa wa masomo hayo na hatimaye kupewa mitihani maalumu ili wakifaulu waweze kuendelea na masomo ya Chuo Kikuu. Programu hiyo iwe maalumu kabla ya Vyuo Vikuu kufunguliwa.

(b) Kuwapokea wanafunzi hao na kuwaingiza Chuoni miezi mitatu kabla vyuo havijafunguliwa na kuwaandalia Programu Maalumu ya kuwawezesha katika somo moja au masomo mawili waliyofeli. Programu hizo ziwe maalumu kwa wanafunzi waliohitimu masomo ya sayansi pekee.

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha za MMES zinaelekezwa kusaidia ujenzi wa madarasa na ujenzi wa nyumba za walimu wa shule za sekondari. Kutokana na wingi wa Shule za Kata, zipo Shule za Sekondari zimejenga sasa zaidi ya vyumba vinne vya madarasa, lakini hawajapata msaada wa MMES kwa madarasa ila wamepata kwa ujenzi wa nyumba moja tu ya mwalimu. Kwa matokeo ya aina hiyo; je, Wizara inasema nini

juu ya hali hiyo kwa shule zilizokumbwa na hali hiyo, kwa mfano Shule ya Sekondari ya Zirai, Kata ya Zirai, Tarafa ya Amani, Wilaya ya Muheza?

Mgao wa fedha mara nyingi unafanywa kati ya Mwenyekiti wa Halmashauri na Afisa Elimu Wilaya. Taarifa zinafika katika Baraza la Madiwani, linalokutana mara nne kwa mwaka na wakati mgao umeshafanyika na fedha zimeshaanza kutumika, hivyo kukosa uwezo wa usimamizi bora wa mgao wa fedha hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu kubwa ya madai ya walimu ipo katika maeneo ya madai ya gharama za uhamisho. Sehemu nyingi Wilayani, Maafisa Elimu wa Wilaya, wametumia vibaya madaraka yao kwa kuhamisha walimu kiholela na wakati mwingine kwa upendeleo na chuki binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, bila kujenga mfumo mzuri wa upeo na ukomo wa madaraka ya Maafisa Elimu wa Wilaya kwa shule za msingi na sekondari katika maamuzi ya kufanya uhamisho ndani ya madaraka yao, basi madai ya mafao ya walimu yataendelea bila ukomo na badala yake kuendelea kuongezeka. Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi na TAMISEMI, lazima wasimamie eneo hili na kutoa miongozo thabiti, juu ya mamlaka ya uhamisho wa walimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri iwepo Programu Maalum ya upendeleo wa kujenga nyumba za walimu wa shule za msingi na sekondari maeneo ya vijijini. Siyo rahisi kumpeleka mwalimu wa ngazi ya Diploma au Degree kijijini, mbali sana ambapo hakuna nyumba, hakuna umeme, hakuna maji (mwalimu akaoge mtoni!), barabara na usafiri duni, tukategemea atakaa huko na kufundisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuwe na Programu Maalum ya upendeleo wa kuanza kujenga nyumba za walimu maeneo hayo ya vijijini, sambamba na kutoa motisha kwa kusaidia gharama za kodi za nyumba kwa walimu wanaoendelea kupanga nyumba binafsi maeneo ya mijini, ambapo nyumba bora na nyingi zinapatikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. PROF. IDRIS A. MTULIA**: Mheshimiwa Naibu Spika, natoa pongezi kwa Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi , Manaibu wake wawili, Katibu Mkuu na Naibu wake, pamoja na Watumishi wote wa Wizara, kwa kutuletea hotuba nzuri, inayotoa matumaini kwa wananchi wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa vile Wilaya ya Rufiji ina matatizo makuwa ya Elimu na iko nyuma sana kielimu, kKuna mahitaji makubwa ya nyumba za walimu, majengo ya maabara, maktaba na mabweni ya wanafunzi. Aidha, kuna upungufu mkubwa wa madawati.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali itupie macho Rufiji na iongeze ruzuku ya rasilimali fedha, kwa ajili ya kukidhi mahitaji niliyoyaorodhesha hapo juu, yaani nyumba za walimu, majengo ya maabara, maktaba, mabweni na madawati.

Upungufu mkubwa wa walimu katika Shule zetu kule Rufiji; Shule za Msingi walimu 500 wanahitajika na Shule za Sekondari tunahitaji walimu 100. Kwa mfano, Shule ya Kata za Mwaseni ina walimu wawili tu, Sekondari inayokwenda hadi Kidato cha Tatu. Shule ya Kata ya Ngorongo ina mwalimu mmoja tu!

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Wilaya ya Rufiji itangazwe kuwa *disaster area* kielimu, yenye mazingira magumu na walimu wote Rufiji wapate posho ya mazingira magumu.

(b) Wizara iendelee kuiruhusu Halmashauri ya Rufiji kuandikisha wanafunzi (Ex-Form IV) wengi zaidi, tuwafundishe kwenye Vyuo vya Ualimu ili wakimaliza masomo waje kufundisha Wiyala ya Rufiji.

(c) Hatua za haraka zichukuliwe za kukarabati Shule zote za Msingi zilizojengwa katika Vijiji vya Rufiji wakati wa kuhamia vijijini katika miaka ya 1970.

Mheshimiwa Naibu Spika, maendeleo ya elimu katika nchi yetu, yanapishana sana kati ya mkoa na mkoa na kati ya wilaya na wilaya. Wilaya ya Rufiji, inahitaji kutazamwa zaidi. Kwa vile ina maendeleo duni ya elimu, basi Wizara ikubali kupeleka rasilimali fedha nyingi na watu (watumishi) wengi wapelekwe Rufiji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara iwe na mpango wa kurekebisha hali mbaya ya *imbalance* ya maendeleo. Tafadhali, Kaskazini ya nchi ni Tanzania na Kusini na Pwani vile vile ni Tanzania; Maafisa Mipango wa Wizara wawe Wazalendo zaidi ili kila siku wakumbuke kuwa Tanzania ni nchi moja. Rufiji inalia, tafadhali tutazameni usoni na sisi tuendelee.

Tafiti zote duniani zimeonesha kuwa, lishe ya wanafunzi ni msingi mkubwa wa afya bora ya wanafunzi na kuleta ufaulu wa juu. Kwa vile Rufiji iko katika maendeleo ya elimu, Serikali, ikubali kuziweka Shule zote za Msingi za Rufiji katika mpango wa kupata chakula cha mchana shuleni. Hatua hii ya kuwalisha vijana mchana, itanyanyua ufaulu wa wanafunzi wetu kule Rufiji.

Rufiji ina vijana wengi sana Ex-Std. VII, inahitaji Shule ya Ufundi (VETA) ili pamoja na Chuo cha F. D. C. ziendelee kuwasomesha wanafunzi wetu waweze kuajiri wenyewe. Chuo cha VETA ni ukombozi kwa Rufiji.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, naunga mkono hoja. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tukirudi jioni nitakuwa na wachangiaji wawili tu, ambao watakuwa ni Mheshimiwa Benedict Ole-Nangoro na Mheshimiwa Zabein Mhita. Nafanya hivi ili Waziri aweze kujibu na halafu tuwe na muda mrefu zaidi kwenye Kamati, kwa sababu kwenye Kamati kwa mujibu wa taratibu zetu, naweza nikawaachieni dakika mbili tukaingia kwenye *guillotine stage*. Sasa *guillotine stage* siyo nzuri sana, kwa sababu inaweza ikawaachieni ninyi nyote mliosimama, najua mshahara

wa Waziri mmnautaka pamoja na gari lake. Kwa hiyo, inabidi tutoe muda mrefu angalau muweze kusema na Waziri aweze kujibu. Naona ndio maana tuwape wawili halafu tutoe nafasi ya nusu saa Waziri kujibu na Naibu wake dakika kumi na tano.

Ningependa pia kutoa maelekezo, tumesikia kwenye vyombo vya habari kuhusu nia na mpango wa hawa wanaojiita wanaharakati, kuandamana kwa sababu ya Muswada uliosomwa mara ya kwanza jana kuhusu CDFCF. Tunasema Bunge siyo sawa sawa na vitu vingine; ni *institution* yenye taratibu zake, zilizoandikwa Kikatiba na Kanuni zetu. Sasa napenda kuwaelekeza hawa jamaa zetu kwamba, hawatamwona Spika. Watapata matatizo wakimwona Spika, hapa hatuingii kwa mtindo huo. Eneo hili lote limekuwa *secured*, yaani linalindwa. Mbunge yeyote katika maeneo hafungwi, akitoka nje ya majengo haya anafungwa kama ana kosa. Hivyo hivyo mtu mwingine, hawezi kuingia kwa utaratibu anaotaka hapa ndani sijui kumwona Spika, haiwezekani.

Muswada ule umesomwa jana kwa mara ya kwanza, kwa hiyo, hatua zinazofuata naomba wazifuate kama kweli ni watetea haki. Kanuni yetu ya 83(1): "Muswada wowote wa sheria ambao umetangazwa kwenye gazeti, unaweza kuwasilishwa Bungeni kufuatana na orodha ya shughuli ili kusomwa mara ya kwanza na katika hatua hiyo, Katibu atasoma jina refu la Muswada wa Sheria unaohusika bila hoja yoyote kutolewa." Kwa ajili hii, ndiyo kitendo kilichofanyika jana.

Kifungu cha pili kinasema: "Hakutakuwa na mjadala wowote wakati wa Muswada wa Sheria kusomwa mara ya kwanza." Kama ilivyofanyika jana, kifungu cha 84(1): "Spika atapeleka Muswada wa Sheria kwenye Kamati inayohusika na Kamati itaanza kuujadili Muswada huo mapema iwezekanavyo." Kifungu kidogo cha pili: "Kamati iliyopelekewa Muswada itatoa matangazo au itatoa barua ya mwaliko kumwalika mtu yeyote afike kutoa maoni yake mbele ya Kamati hiyo, kwa lengo la kuisaidia katika uchambuzi wa Muswada huo, bila kuathiri masharti ya ibara ya 99(3) ya Katiba. Kamati iliyopelekewa Muswada itakuwa na uwezo wa kufanya marekebisho katika Muswada wa Sheria kwa kumshauri Waziri au Mbunge anayehusika na Muswada huo kufanyiwa mabadiliko. Vile vile Serikali itakuwa na uwezo wa kuishauri Kamati ya Kudumu ya Bunge kuhusu kufanya marekebisho au mabadiliko juu ya Muswada huo binafsi. Kama Muswada binafsi basi Serikali itamshauri Mbunge mwenye Muswada binafsi, kama Muswada ni wa Serikali, basi Kamati inamshauri Mbunge mwenye Muswada binafsi, kama Muswada ni wa Serikali basi Kamati inaishauri Serikali."

Sasa hawa ndugu zetu ambao wanataka kufanya maandamano, kwanza, hawafanyi ukweli. Pili ni tabia ambayo inaonekana kwamba, labda watu wana muda mwingi sana wa kupoteza. Taratibu tunazo; waje wote tutatoa Ukumbi wa Msekwa wakaseme maneno yao. Kwa hiyo, huo ndiyo utaratibu. Vinginevyo, siyo utaratibu wa Bunge na wala hautakubalika katika eneo letu.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, sina matangazo mengine, nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa kumi na moja.

*(Saa 7.00 mchana Bunge lilifungwa mpaka saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, wakati tunasitisha shughuli za Bunge mchana, niliwataja Mheshimiwa Benedict Ole-Nangoro na Mheshimiwa Zabein Mhita kama ni wachangiaji wetu wa mwisho katika hoja. Nitamwita pia Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi, aweze kuchangia mambo yaliyokuwa ya Utumishi. Mheshimiwa Ole-Nangoro.

**MHE. BENEDICT N. OLE-NANGORO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika hoja hii ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Mawaziri, Katibu Mkuu na Wataalam katika Wizara hii, kwa kutuandalia hotuba ambayo ni nzuri na inayoeleweka. Hotuba ambayo imetoa picha kuhusiana na hali halisi ya elimu katika nchi yetu sasa.

Pili, ningeliomba uniruhusu nimshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa mchango aliotupa katika Sekondari yetu ya Kiperesa na kusaidia kukamilisha shule na kuwezesha wanafunzi kuanza. Pia nimshukuru Waziri wa Elimu, kwa Shule ya Kichina inayojengwa katika Kijiji cha Kartimbo Wilayani Kiteto. Ujenzi umeshaanza na kwamba, shule hii itawahudumia wenyeji wa Kiteto. Kwa hiyo, ninashukuru sana kwa mchango huo wa Wizara ya Elimu. Nilimwomba Mheshimiwa Waziri wa Elimu kwamba, kuna shule nne za Kata ambazo zimefunguliwa mwezi wa tatu na hazina hata mwalimu mmoja, akatuahidi kwamba angetupatia walimu. Natarajia kwamba, baadaye ahadi hiyo ataiweka bayana atakapokuwa anahitimisha hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, elimu hakuna mtu atakayebisha kwamba, ndiyo msingi wa kila kitu; ni msingi wa maisha bora; msingi wa maendeleo; na ni msingi wa *social transformation.* Kwa hiyo, bila elimu hakuna kitu kitakachowezekana kwa mtu mmoja mmoja, kwa kaya, kwa jamii na kwa Taifa zima. Kwa sababu ya umuhimu huu wa elimu, mahitaji yameongezeka, kwani ongezeko la watu tangu uhuru limekuwa kubwa. Miundombinu ya elimu haikukua kufuatana na ongezeko hilo la watu. Kwa sababu hiyo, watu wengi tumekuwa tunanyang’anyana huduma ambazo zimebaki kuwa chache. Huduma nyingine ambazo ziliandaliwa kwa watu waliokuwa wachache zaidi ukilinganisha na idadi iliyopo katika Tanzania ya sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu ya uhaba wa huduma za miundombinu; vifaa vya kufundishia vya kutosha havipo na Walimu wa kutosha hawapo. Kwa sababu hizi, unakuta kwamba, elimu katika ngazi ya msingi, elimu ya sekondari na elimu ya juu katika maeneo haya yote inasongwa na matatizo ya kila aina. Nadhani wakati umefika wa kujaribu kutazama upya mambo kadhaa hasa tukianza na suala zima la usimamizi wa elimu, kwa sababu tumebaki na Wizara kila kitu kinafanyika Dar es Salaam. Kwa hiyo, kumekuwepo na *over centralization* ya *administration* ya elimu kama huduma ya muhimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu ya hii *over centralization,* matatizo yamekuwepo na mengine unashindwa kuelewa kwa kuwa kumekuwepo na *in-balances* za ajabu. Katika Wizara hii ambayo inahitajika iwahudumie watu wote, pamoja na kuwa na madeni kwa mabilioni ya shilingi, yanayodaiwa na walimu, bado muujiza umekuwepo katika Wizara hii kuwezekana pia kuwa na idadi kubwa na fedha nyingi za kuwalipa walimu ama watumishi hewa. Hiki ni kitu kisichoeleweka, hakieleweki kwa sababu ni wazi kwamba, kuna rasilimali nyingi zinazokwenda mahali pasipostahili. Kwa hiyo ni kweli kama rasilimali hazitoshi kwa huduma nyingine muhimu, kwa sababu huenda pia zinachangiwa na utumiaji wa rasilimali kulipa hawa watu ambao hawapo wakati huo huo, inapokuwa kwamba walimu hawatoshi na kweli ni haba katika maeneo mengi, bado kuna wengi wanaolipwa malipo hewa. Hili ni tatizo ambalo limekuwepo kwa muda mrefu na mimi ninadhani hili lipo kwa sababu usimamizi umewekwa mbali mno na maeneo ya huduma; kila kitu kinakuwa Dar es Salaam. Kwa hiyo, kinachofanyika Kiteto, kwenye vijiji vyake, kinachofanyika Shinyanga, kinachofanyika Bukoba si rahisi *administrators* walioko Dar es Salaam wakafahamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tukitaka kutatua nadhani tatizo hili ni sharti tuje na muundo mbadala wa kuweza kusogeza *administration* penye huduma. *Administration* ihamie ngazi za Halmashauri, labda kwa njia hii huenda mabovu mengi yanayofanyika yanaweza kupungua.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika maeneo mengi hasa yale yaliyo kame, utakuta kwamba shule ni chache na zipo mbalimbali. Umbali unakuwa ni sababu kubwa ya watoto kutosoma. Kama shule ipo kilomita 20, 30, 35 katika maeneo mengine, utamtazamiaje mtoto huyu atembee kilomita hizi zote na bado aende kuwa na nguvu za kuketi darasani kwa siku nzima na kumsikiliza mwalimu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hiki ni kitu ambacho hakiwezikani. Kama tutahitaji huduma iwafikie hawa watu ni lazima huduma ya elimu iendane na huduma ya mabweni, kwa sababu bila kuwa na mabweni watoto katika maeneo haya hawatasoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kama nilivyosema, iko *over centralized,* lakini hili linasababisha vitu vingine vingi. *Curriculum* ni hiyo hiyo moja inayofundishwa nchi nzima. Kwa hiyo, katika shule yenye walimu 80 na shule nyingine ya msingi ambayo haina hata walimu wawili, bado unawatazamia watoto hawa waketi na kufanya mtihani ule ule. Ninaelewa kwamba, kuna haja ya kubakiza *standards* katika ngazi fulani, lakini nadhani si halali kutazamia mtoto aliyekaa mwaka mzima, mwaka wa pili, wa tatu, miaka yote saba, bila ya kuwapata walimu kuja kuketi na kufanya mtihani sawa na ule ule unaofanywa na mtoto ambaye amekuwa na walimu kwa vipindi vyote, kwa miaka yote saba kwa shule ya msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili ni tatizo linalohitaji kutazamwa na kama Wizara itasimamia Sera na *Standards,* nadhani kunapaswa kuwa kuna *minimum standards* angalau zinazohitajika ili kila shule iweze kutarajiwa kutimiza masharti Fulani, lakini pia kufikia kiwango fulani cha elimu iwe ni darasa la nne, darasa la saba ama elimu ya

sekondari. Bila kufanya hivi, nadhani itakuwa hatuwatendei haki wale watu wanaoishi katika maeneo ya pembezoni.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la walimu limeongelewa sana na walimu ndiyo msingi wa elimu. Hatutarajii kunyanyua elimu, endapo walimu hatutawatazama kwa namna ya pekee. Wana madai mengi, lakini huduma nyingine nyingi wanazopaswa tu kupata stahili yao kama walimu, wengi hawapati. Ukipita kwenye kila shule, vijijini ukipita kwenye Halmashauri, madai ya walimu yamekuwa ni madai sugu na ni mengi kweli. Hakuna Halmashauri ambayo utapita usikute madai ya walimu yapo kwenye mabilioni na maadam tumeahidiwa kwamba, sasa wataanza kushughulikiwa. Hili lingepashwa kuwa ni *priority* ya kwanza katika kipindi hiki tunachokianza sasa ili walimu wafunge *chapter* hiyo ya madai, waanze mwaka huu wakiwa na moyo mpya, wakiwa na juhudi mpya, kwa kuwa watakuwa wameshatunukiwa upya kile wanachokidai ambacho ni maslahi yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni la vitabu. Hili suala linatatiza sana, vitabu havipatikani katika maeneo mengi, bado ni aghali kupita kiasi. Hili ni eneo lingine ambalo ningeliomba litazamwe na Mheshimiwa Waziri na angelitupa katika majumuisho yake kwamba, mkakati ni upi wa kuhakikisha kwamba, angalau vitabu vya lazima vinapatikana katika shule zote; ziwe za msingi ama za Sekondari za Kata zinazofunguliwa sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni wazo zuri na ni mpango mzuri kwamba, Shule za Kata nyingi zimefunguliwa. Shule hizi mbali na kuwa miundombinu bado haitoshelezi, kuna ambazo karibu zinamaliza mwaka sasa bila kuwa na mwalimu hata mmoja. Mratibu wa Shule katika ngazi ya Kata, amekuwa anakwenda shuleni na kuorodhesha wanafunzi waliokuwepo. Ukitazama upande wa taaluma, bado hatujajipanga na hii haitakuwa haki kwa wale watoto wakimaliza miezi mitano, sita, mwaka mzima bila kufundishwa, kwa sababu haitawezekana kwa siku za baadaye waweze kuja kufidia muda walioupoteza, muda waliokosa walimu na muda waliokosa kufundishwa. Hili lingalipashwa kuchukuliwa kama ni suala la dharura, kwa sababu maadam shule zimefunguliwa, inatarajiwa walimu pia wawepo. Huwezi kuwa na shule yenye wanafunzi, bila kuwa na walimu au mwalimu hata mmoja. Kwa hiyo, ningaliomba Wizara ijaribu kutazama hili na ichukuliwe kama ni suala la lazima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine, kama Taifa tukitaka kuondokana tulipo, tukawa Taifa lililoendelea, Taifa lenye *middle income* kama tunavyosema katika *Vision 2025* ni lazima tuwekeze zaidi katika elimu. Hatujawekeza vya kutosha katika elimu na *indicator* moja inayoonekana, siku Kenya wanapofungua shule zao kwenye vituo vya mpakani Namanga na kwingineko, ukiwakuta wanafunzi wanaotoka huku kwenda upande mwingine wanakwenda kwa maelfu na hii ni *indicator* moja inayoonesha kwamba, wanakwenda kutafuta kile ambacho hawajakipata kutoka huku kwetu. Ningeliomba kwamba, hili la uwekezaji pamoja na kuwa na uhaba wa rasilimali, tufunge mikanda lakini tuwekeze katika elimu, kwa sababu rasilimali nyingi tulizonazo hazitatunufaisha na hatutaweza kuendelea hata kama tuna rasilimali hizo mpaka tutakapokuwa na Taifa lilisoma, Taifa la watu wenye taaluma za kila aina. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ningelisisitiza pia kwamba, kwa upande wa *administration*, tujaribu kufanya *decentralization* na katika ngazi ya Halmashauri mbali na kuwa na Afisa Elimu anayesimamia Elimu ya Shule za msingi, tungelipashwa pia kuwa na Afisa Elimu ya Sekondari, ambaye kazi yake kubwa itapashwa kuwa ni kusimamia Elimu ya Sekondari katika Halmashauri. Najua kuna waliowekwa kama Waratibu, lakini nadhani jukumu la kuhamisha jukumu la Elimu ya Sekondari kwenda TAMISEMI, liendane pia na kuifanyia Wizara ya Elimu *over haul* ili staff wengi waliopo Wizarani wahamishiwe TAMISEMI, lakini zaidi waende Mikoani na wahamishiwe katika Halmashauri ili waweze kusaidia kuratibu na kujaribu kusimamia masuala ya elimu ya sekondari katika kila Halmashauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, tusipofanya hivyo, bado tutabaki na tatizo hilo hilo lenye *inbalances* za kila aina, kwa sababu ya usimamizi wa elimu kuwa mbali na huduma mahali ambapo huduma zenyewe zinatolewa. Nimalizie tu kwa kusisitiza kwamba, ili elimu ya msingi pia iweze kuwa nzuri, Wizara ijaribu kutafuta namna ya kuwawezesha Wakaguzi wa Shule waweze kufanya kazi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja. Nashukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Sasa nitamwita Mheshimiwa Zabein Mhita azungumze.

**MHE. ZABEIN M. MHITA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili nami kwa niaba ya Wananchi wa Jimbo la Kondoa Kaskazini, niweze kuchangia hoja iliyo mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya mwisho, nikiwa hasa na maana kwamba, kwa Kirangi tunao msemo unasema; *Kiheka nyuma charie mkindo;*, maana yake hata jambo la mwisho linakuwa na uzito wake, ndiyo maana nakushukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Haya ahsante. *(Kicheko)*

**MHE. ZABEIN M. MHITA:** Awali ya yote, naomba niwapongeze kwa dhati kabisa Mheshimiwa Waziri, Waheshimiwa Naibu Mawaziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu, Kaimu Kamishna, Wakurugenzi, Viongozi wa Vyuo Vikuu, Wakuu wa Taasisi zilizo chini ya Wizara ya Elimu na Watendaji wote wa Wizara hii, kwa kuandaa Bajeti nzuri, yenye mwelekeo wa kisayansi na yenye malengo ambayo yanatekelezeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile naipongeza Serikali kwa dhati kabisa, kwa mafanikio makubwa yaliyofikiwa katika Sekta hii ya Elimu. Katika maendeleo ya Elimu, kuna hatua kadhaa. Hatua ya kwanza kabisa ni ile ambayo inahusika na *access to education*, kwa maana ya kwamba, upatikanaji wa elimu. Hili tumeelezwa na

Mheshimiwa Waziri katika hotuba yake kwamba, watoto wanaostahili kwenda Shule za Msingi mpaka sasa hivi wamefikia asilimia 97.5 na wale wanaokwenda kupata Elimu ya Sekondari wanafikia asilimia 60, wakati mwaka 2004 *access to eduction* kwa *level* hiyo ya sekondari ilikuwa ni asilimia 42 tu.  Kwa hiyo, ndiyo maana nasema haya ni mafanikio makubwa sana, ambayo yametokana na Serikali yetu inayoongozwa na Chama cha Mapinduzi.  *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue fursa hii, niwapongeze kwa dhati kabisa, Wananchi wa Wilaya ya Kondoa na hususan Wananchi wa Jimbo la Kondoa Kaskazini, kwa jinsi walivyochangia katika ujenzi wa shule za sekondari.  Mwaka 2005, Jimbo la Kondoa Kaskazini kulikuwa na Shule za Sekondari nane tu.  Mwaka huu wa 2009, kuna shule 31 na hili ni Jimbo na siyo Wilaya, ongezeko la shule 23 zilizojengwa kwa michango ya wananchi, wakishirikiana na Halmashauri yao na vile vile wakishirikiana na Mbunge wao.  *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2005, waliofaulu mtihani wa kumaliza elimu ya msingi na waliojiunga na sekondari ilikuwa ni chini ya asilimia 40.  Kutokana na ongezeko kubwa la shule za sekondari, hivi sasa Wilaya ya Kondoa ni asilimia mia moja ya wanafunzi waliofaulu wanaingia Kidato cha Kwanza.  *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mchango mkubwa wa wananchi, lakini tuna tatizo kubwa la upungufu wa walimu.  Naomba nitoe mfano tu wa shule chache.  Mfano Shule ya Gubali Sekondari, ina walimu wawili,  Itaswi ina walimu wawili, Kwadelo ina wawili, Masawi mwalimu mmoja, Changa hakuna kabisa mwalimu na Kinyasi hakuna mwalimu.  Ninapata faraja kwa sababu nimeeleza ile hatua ya kwanza katika maendeleo ya elimu ni kwamba, ni *access to education.*  Hatua ya pili katika maendeleo ya elimu ni kuboresha elimu.  Sasa tumeelezwa na Mheshimiwa Waziri kwamba, Serikali inasomesha walimu wapatao 12,900 katika ngazi ya Stashahada na Shahada, ambao ametuambia kwamba, hivi karibuni walimu hawa wataanza kupangwa katika shule.  Kwa hiyo matumaini yangu ni kwamba, walimu hawa watakapoanza kupangwa, wataletwa katika Wilaya yetu ya Kondoa na ninawahakikishia walimu hawa kwamba, watakapofika Kondoa watakuta tumeandaa mazingira mazuri na hawatataka tena kuondoka na kuhama Kondoa.  *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, napenda niipongeze Serikali kwa jinsi inavyoshughulikia upatikanaji wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia.  Tumeelezwa hapa na Mheshimiwa Waziri kwamba, Wizara imepata msaada wa *US Dollars 11,000* milioni ambazo ni kwa ajili ya ununuzi wa vitabu vya sayansi.  Sasa bado mimi nina imani kwamba, kwa kuwa Wilaya ya Kondoa ina upungufu mkubwa wa vitabu, naamini vitabu hivi vitakapokuwa vinagawanywa, Mheshimiwa Waziri atatukumbuka Kondoa ili na sisi tuweze kupata vitabu hivyo kwa wanafunzi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, tumeelezwa pia na Mheshimiwa Waziri kwamba, Serikali ina Mkataba na *ADB* kutupatia dola 90 kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya maabara.  Hii inaonesha dhamira thabiti ya Serikali katika kuboresha elimu.  Mimi sina wasi wasi kabisa kwamba, elimu imeanza kuboreshwa na itaendelea kuboreka.

Namwomba Mheshimiwa Waziri, mtakapokuwa mnagawa vifaa hivyo vya maabara, tafadhali sana naomba mkumbuke Rumburia wako kule Kondoa ili na maabara yetu iweze kupata vifaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa kuna mpango mzuri kabisa wa Serikali, ambao ulikuwa na lengo la kuwapatia wanafunzi fursa sawa, kwa wale ambao wanatoka kwenye familia zenye kipato duni, kisichoweza kukidhi gharama za elimu ya sekondari. Mpango huu ulikuwa ni mzuri na wanafunzi hawa walikuwa wanalipiwa, ambao sasa mpango huu utaendeshwa na Halmashauri za Wilaya tangu mwaka huu wa 2009; wakati mpango huu ukiendeshwa, mwaka 2008, wanafunzi wa Kidato cha Pili, cha Nne na cha Sita ndiyo waliogharimiwa. Wanafunzi wa Kidato cha Kwanza, cha Tatu na cha Tano, hawakugharimiwa na idadi yao ni 322. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri, fedha hizo ambazo Wizara iliahidi kwamba ingezilipa, zipelekwe kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa ili ziweze kuwalipia deni hawa wanafunzi 322.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue nafasi hii, vile vile niipongeze Serikali yetu inayoongozwa na Chama cha Mapinduzi, kwa kuamua kuongeza idadi ya wanachuo ambao watapewa mikopo kwa ajili ya elimu ya juu. Huu mpango ni mzuri na kusema kweli Wananchi wa Kondoa wamenituma nimshukuru Mheshimiwa Waziri, kwa kuthubutu kuchukua hatua hii. Kwa sababu wanafunzi wengi ambao wanatoka katika familia ambazo hazina uwezo, walikuwa wakishindwa kulipa ada hiyo, sasa wamefarijika na wamerufahi sana. Naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri na Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba nichukue nafasi hii adhimu, niwashukuru kwa dhati walimu wote nchini, tukianza katika ngazi ya elimu ya awali mpaka Vyuo Vikuu, pamoja na Maafisa Elimu wao, Maprofesa wote, pamoja na Watafiti wote, kwa kazi nzuri wanayofanya ya kuleta maendeleo katika nchi yetu na bila kusahau walimu wa Jimbo la Kondoa Kaskazini.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba niseme kwamba, ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ahsante sana kwa kunisikiliza. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Sasa nitamwita Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, napenda kuunga mkono hoja na pia napenda nishukuru kupata nafasi ya kutolea ufafanuzi kwa baadhi ya hoja, ambazo zimeulizwa na ambazo zinagusa moja kwa moja katika Ofisi yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kwanza ambalo ningependa nilitolee ufafanuzi ni suala ambalo tuliombwa Utumishi na Hazina, tuache kushughulikia walimu na tuwaachie TAMISEMI na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi. Kimsingi, jukumu la kuwahudumia walimu kama ilivyo kwa watumishi wengine, linahusisha maeneo mbalimbali na Wizara mbalimbali. Maeneo ya uandaaji wa Sera, utekelezaji na masuala ya usimamizi wa Utumishi. Kutokana na mgawanyo huo, Wizara ya Elimu na Mafunzo

ya Ufundi, kazi yake ni kusimamia Sera zinazohusu maendeleo na uboreshaji wa Sekta ya Elimu na TAMISEMI ndiyo watekelezaji wa masuala yote ya kielimu, ambayo yanatolewa Sera au yanawekewa viwango na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi.

Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, kazi yetu ni kusimamia hizo Sera zinazohusu watumishi, ikiwa ni pamoja na kuratibu na kuhakikisha kwamba, watumishi wanalipwa mishahara inayostahili, lakini wanalipwa watumishi wale ambao wapo kazini. Kwa hiyo, kimsingi hapa ni muhimu kila mtu, kila Wizara kwa maana sisi Utumishi tufanye kazi yetu, Wizara ya Elimu wafanye kazi yao na TAMISEMI wafanye kazi yao. Watumishi wote kwa masuala yao yanayohusu malipo, huwezi ukaikwepa Wizara ya Fedha na Utumishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la pili ambalo nilipenda nilitolee ufafanuzi ni la mishahara; tofauti ya mishahara baina ya Maafisa Elimu wa Mikoa na Maafisa Elimu wa Wilaya kwamba, kwa nini baadhi ya Maafisa Elimu wa Mikoa mishahara yao ni midogo na Maafisa Elimu wa Wilaya ni mikubwa. Maafisa Elimu wa Wilaya wanalipwa mshahara wa madaraka *(Duty Post)* kama Wakuu wa Idara na wale Maafisa Elimu wa Mikoa ambao pia ni Wakuu wa Idara katika ile *clastor* ya huduma za jamii, basi wao wana mishahara mikubwa sana kushinda Maafisa Elimu wa Wilaya. Kama yeye ni Mkuu wa ile *clastor*, lakini siyo mkuu wa *claster,* anapata mshahara wa chini. Hata hivyo, tumepokea maombi kutoka Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, wakiomba kwamba, elimu iwe na *claster* yake katika Sekretarieti ya Mkoa na kwa kuzingatia kwamba, sasa hivi shule za sekondari zinapelekwa Wilayani. Hilo ombi tunalifanyia kazi na ni imani yangu kwamba, suala hilo litapatiwa ufumbuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine lilikuwa kwamba, Mheshimiwa Masunga aliuliza utaratibu ukoje kwa watumishi kwenda kutibiwa nje ya nchi. Watumishi wa Umma kama walivyo wananchi wengine wowote wa Tanzania, wanastahili kutibiwa nje ya nchi, endapo tu Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, itajiridhisha kuwa mhusika anastahili tiba hiyo na haipatikani hapa nchini. Pia utaratibu huu ulivyo ni kwamba, mtumishi anapotakiwa kwenda nje ya nchi, kama ikionekana labda upande wa hospitali unachelewa, mwajiri wake anaweza akamwombea kwenda kutibiwa nje na anachopaswa kufanya mwajiri ni kumlipia pesa za kujikimu kule, lakini gharama zote za matibabu akiwa nje, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii ndio ambayo inapaswa kumlipia.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo liliulizwa na Mheshimiwa Maneno ni suala la mwalimu anapofiwa na mkewe, mumewe au mtoto wake, utaratibu unakuwaje?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa Sheria ambazo tulikuwa nazo kabla ya marekebisho ya Sheria Namba 8 ya Mwaka 2002, ambayo tumeyafanya mwaka 2007 na Kanuni za Kudumu ambazo tumezikamilisha mwaka huu; Sheria ilikuwa haitamki wazi kwamba, haki za mototo na mke, sana sana ilikuwa inaruhusu kugharimia gharama za mazishi ambazo ni jeneza, sanda na kaburi kwa maeneo ambayo inabidi labda kuchimbwa kwa gharama au kununua eneo la kuchimbia, lakini suala la kusafirisha lilikuwa haliko wazi. Hata hivyo, tulivyofanya marekebisho ya Kanuni zetu ambazo

tumezikamilisha mwaka huu, suala la gharama za mazishi kwa watumishi pamoja na mke wake na watoto wake nalo limewekwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mtumishi akifariki mkewe au mtoto wake, atagharimiwa gharama za sanduku au jeneza, kaburi, nyuzi, mapambo yote, pamoja na usafiri. Kwa hiyo, kwa yale yaliyokuwa yanatokea huko nyuma, ilikuwa inategemea utu, uwezo wa sehemu ile; mwajiri mwngine anaweza kuwa na uwezo, walikuwa wanasafirisha. Waajiri wengine hawakuwa na uwezo huo, kwa hiyo sana sana walikuwa wanasaidia sanda, lakini masuala la kusafirisha, wengi walikuwa hawayawezi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo limezungumzwa hapa ambalo napenda tu nilijibu kama Waziri wa Utumishi, Waziri wa Elimu naye atakuja kulijibu tena kwa kirefu ni suala la Katibu Mtendaji wa *NECTA*, achukuliwe hatua kwa kuwaondoa watumishi wengi kazini kwa muda mfupi. Kwanza, inabidi yeye mwenyewe achunguzwe utendaji wake wa kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua alizozichukua Katibu Mkuu wa Baraza la Mitihani ni utekelezaji wa uamuzi wa Serikali katika kusafisha chombo hicho. Hivyo, wananchi na wadau wengine, wanatakiwa kuendelea kutoa ushirikiano ili hatimaye chombo hicho kiweze kufikia kiwango cha juu cha utendaji na uadilifu. Sote tumelalamika hapa kwamba, mitihani inavuja na kweli tuna ushahidi kwamba inavuja. Mheshimiwa Rais, alitoa maelekezo kwamba, Baraza la Mitihani liangaliwe upya na lisafishwe, kwa hiyo, hayo aliyoyafanya ni utekelezaji wa Agizo la Mheshimiwa Rais. Pia Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, tumeshirikishwa na pia tumetoa ushauri kwa baadhi ya maamuzi ambayo mnayaona. Kwa hiyo, tunaomba tumuunge mkono, lakini pia niwaombe Wabunge wenzangu, tuwashauri watumishi, pale inapotokea mtumishi anaona anaonewa, vipo vyombo ambavyo vimewekwa kwa ajili ya kushughulikia matatizo ya watumishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunayo Tume ya Utumishi wa Umma, Waziri yupo na mimi Waziri wa Utumishi nipo. Kwa hiyo ni vizuri wakati mwingine tukiambiwa vitu kama hivyo, tukanong'ona kwanza na Mawaziri, tukapata uhakika badala ya kuja kulizungumza hapa. Pia Sheria za Utumishi zinamkataza mtumishi kuomba apate *political influence*. Kwa hiyo, niwaombe watumishi, ukiona umeonewa nenda kwa kiongozi wa juu wa yule aliyekuonea, kama huridhiki kata rufaa Tume ya Utumishi wa Umma. Kama hauridhiki, nenda kwa Mheshimiwa Rais, yeye ndiye wa mwisho katika masuala haya na kama huridhiki basi unaweza kwenda Mahakamani. Maelezo zaidi ya nini kilichotokea, Mheshimiwa Waziri wa Elimu, atayatolea ufafanuzi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine lililozungumzwa ni la posho ya kufundishia.

Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu uliopo, posho ya kufundishia kama zilivyo posho nyingine, ziliondolewa na kujumuishwa kwenye mishahara kwa lengo la kuboresha mafao ya mwisho ya utumishi. Hata hivyo, walimu wameajiriwa kwa ajili ya kufundisha na wanapata mshahara kwa ajili ya kufundisha. Kwa hiyo, ndio maana

iliangaliwa na kuonekana hiyo posho iondolewe kama ilivyoondolewa kwa watumishi wengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA):** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, naomba nikuombe radhi sauti yangu sio nzuri, yawezekana hapa na pale nikakwama kwama.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwenye wingi wa rehema na mapenzi mema kwetu sote. Aidha, ninawaombea rehema na amani, wazazi wangu ambao wako mbele ya haki; Mwenyezi Mungu aziweke roho zao mahala pema Peponi. Amina.

Pili, nichukue fursa hii kuwashukuru familia yangu, watendaji wote wa ngazi zote na kwa ujumla wananchi ambao wamefanya kazi kubwa sana, kwa kushirikiana na Serikali za Mitaa na Serikali Kuu, kujenga madarasa ya shule za msingi na sekondari. Tunawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja za Waheshimiwa Wabunge ni nyingi sana, michango yao mingi imekuwa ni ya manufaa makubwa kwetu. Hata hivyo, nitazijibu hoja hizo kwa kadiri muda utakavyoniruhusu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja zangu nimezijumuisha na Mheshimiwa Waziri atataja majina ya waliochangia. Kwanza, nazungumzia juu ya mazingira magumu ya walimu ya kufanyia kazi na kufuata mishahara mbali na vituo vya vya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala hili limefanyiwa kazi kwa karibu sana, hivi sasa walimu walio wengi wanapokelea mishahara yao kupitia Benki ya NMB na kwamba, wanayo tarehe maalum. Nachelea kuitaja, wasije wakawa wanaviziwa viziwa huko njiani. Bado tunatambua umbali upo na mifano iko mingi; kwa kadiri Wizara itakavyokuwa inajaliwa, tutaangalia uwezekano wa kuwasogezea huduma hizo, posho, mishahara na nyumba.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waziri mwenye Dhamana ya Utumishi, amezungumzia juu ya posho na mimi nimetoa ufafanuzi juu ya mishahara. Nyumba za walimu ni moja kati ya vitu muhimu sana na hili ndilo linalotupa tabu sana, pale tunapowapangia walimu kwenda kufanya kazi kwenye shule mbalimbali. Inasikitisha kidogo kwamba, uwezo wa Serikali wa kuweza kujenga nyumba kwa kila shule kwa kadiri zinavyohitajika ni mdogo, lakini wananchi nao wameelekeza nguvu nyingi kwenye vyumba vya madarasa, lakini nyumba za walimu mchango umekuwa ni mdogo. Kwa pamoja tunasema, tumeweka kipaumbele, tutashirikiana kuhakikisha tunazijenga hizi nyumba, walimu wanastahili kupata makazi yenye heshima na hadhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na hoja ya Mheshimiwa mmoja, kuhusu shule ambayo alikuwa ameisimamia kwa karibu kwamba, ilikuwa haina Mwalimu Mkuu.

Napenda kumwarifu Mheshimiwa Makamba kwamba, Shule ya Mehezangulu, sasa imepatiwa Mkuu wa Shule anaitwa Kijangwa Mtunguja na Wizara imeshapanga kupeleka walimu wengine wanne na mgao wa namna hiyo umeendelea kwa shule zote za Kata. Jambo kubwa ambalo ninawaomba Waheshimiwa Wabunge, tushirikiane kutengeneza mazingira mazuri ya kuwapokea walimu; baadhi ya walimu tunapowapeleka katika mikoa, wanapofika kwenye vituo, ukarimu wanaoupata ni mdogo. Naomba tutambue walimu hawa ni vijana wenye umri mdogo sana, hawana uwezo mkubwa wa kustahimili mikiki mikiki, kwa hiyo, kutuachia jukumu hilo Serikali peke yetu, hatutaweza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Walimu kupangiwa vituo na kuondoka; sababu zinazowafanya waende kwenye vituo na kuondoka ni nyingi na muda ni mfupi. Mimi binafsi, nimeshuhudia mazingira magumu na mahali pengine mambo yanayotokea ukiyasikia, wewe kama mzazi utasema potelea mbali. Naomba niseme, tutambue kwamba walimu ni binadamu, tusiwafanyie mambo mengine ambayo hata kuyazungumzia hadharani ni vibaya. Sasa kuna mambo mengi; nyumba hakuna, mapokezi hafifu, lakini kuna *chemistry* za ajabu ajabu huko; basi haya yote yanawakwaza walimu. Naomba tu niseme, tuwaandalie mapokezi mazuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa Vyuo Vya Ualimu Shinyanga na Manyara ili walimu wazowee mazingira ya huko. Pendekezo la kujenga Vyuo Vya Ualimu katika mikoa iliyotajwa ni zuri na tunalipokea, tunawapongeza sana kwa ujasiri wao. Hata hivyo, tunaomba vyuo vyote vya ualimu itambulike kwamba, kama kikijengwa huko bado vitakuwa ni vya Kitaifa, lakini tunasema tumelipokea pendekezo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, wanafunzi waliochaguliwa kusoma katika Sekondari za kila siku, wapangwe katika shule za jirani. Madhumuni makubwa ya Shule za Kata, ilikuwa ni kuwapunguzia wanafunzi umbali mrefu na pia kuweza kupata huduma hii ya elimu karibu na makazi yao. Kwa baadhi ya mikoa imewezekana, na kwa baadhi imeshindikana hasa kutegemeana na Jiografia. Dar-es-Salaam ni moja ya Mkoa ambao Jiografia yake ni ngumu, idadi ya wanafunzi wanaofaulu kwa shule zilizopo kwenye mazingira ya mjini ni ndogo, shule nyingi zimejengwa pembezoni. Wazazi wa mikoa ya namna hiyo, wanahitaji kukaa pamoja na Serikali zao za Mitaa na kuangalia namna bora ya kuwasaidia. Si lengo la Serikali kuwapatia ugumu na vishawishi na hiyo ni bahati mbaya sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine ilikuwa ni elimu maalum, walimu hawatoshi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunakiri kweli idadi ya walimu hao ni wachache sana. Juhudi zinafanywa, tunacho Chuo cha Patandi, tunawashukuru sana wenzetu wa Chuo cha Sekuko na wao wanatoa taaluma hii na sisi tunafanya juhudi, kama ambavyo Mheshimiwa Mkanga jana alipendekeza. Hivi sasa mtaala umelegezwa kidogo na kwamba, walimu katika vyuo vyote watapata stadi za awali za namna ya kuwasaidia na kuwapatia taaluma wanafunzi wa elimu maalum katika madarasa jumuishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali isaidie watoto walemavu wa shule ya Kahororo, Bukoba; tumesikia, tutafanya hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, wingi wa wanafunzi unatiliwa mkazo kuliko ubora.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kugatua, Serikali imeelekeza nguvu zake zote sasa kwenye Idara ya Ukaguzi wa Shule. Maana yake ni kwamba, sasa kwa bajeti iliyoboreshwa zaidi, watapata uwezo wa kununua vitendea kazi, wataweza kuzifikia shule hizi kwa wepesi zaidi. Tuseme kwamba, nia sio kutoa bora elimu, nia yetu ni kutoa elimu bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine ilikuwa kwamba, Serikali ilikuwa na mpango gani wa kuleta Mpango wa MMEM na MMES na je, yamefikiwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, kidogo nimepata mshangao; hivi kweli wenye macho hawaoni; wenye masikio hawajasikia! Hivi hata ukipita barabarani asubuhi na jioni, hupishani na wanafunzi wanaotoka kwenye Shule za Kata? Hivi kweli hiyo haitoshi kuonesha mafanikio ya MMEM na MMES*?* Kila binadamu ana uamuzi wake; nasema malengo tumeyafikia na kwa uwezo wa Mungu, tutakamilisha yale yaliyobakia na yenye dosari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Maafisa Elimu wa Sekondari, wameshateuliwa na wamesharipoti. Kuna maeneo machache ambayo hawajaripoti kwa sababu mbalimbali, lakini naomba kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba, Maafisa hao wapo kazini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeweka umiliki wa Shule za Sekondari za Kata chini ya Halmashauri. Vipi Bodi?

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya Serikali kuzipeleka au kuzigatua, hivi sasa Bodi za Shule, bado zitabakia na Mamlaka zake na Serikali za Kata, yaani *Ward C*, zitakuwa na jukumu la kufuatilia utendaji wa kila siku kwa karibu, hakuna muingiliano. Bodi ina majukumu yake na mipaka yake na *Ward C* ina mipaka yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Arfi nimeshamjibu, Serikali ijipange kuanzisha *A-Level* katika MMEM. Katika MMES II, tumepanga kujenga hizo shule.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ijenge shule zaidi kwa ajili ya wanafunzi wenye vipaji. Shule zilizopo ni saba kwa ajili ya vipaji maalum na tumepokea ushauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali iingize somo la uraia kwenye Mitaala. Somo la uraia linaanzia darasa la tatu. Siku moja moja itabidi tuwapatie *tuition* Waheshimiwa Wabunge. Limeanzia darasa la tatu na linaendelea mpaka Vyuo Vikuu. Ndio maana sasa kumekuwa na uwezo mkubwa wa wanafunzi kuweza kujieleza, kujitambua na kujua haki zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitazungumzia suala la mimba. Tumepokea ushauri wa Wabunge, mwezi Septemba kutakuwa na mkutano wa wadau wote, wakiwemo Waheshimiwa Wabunge. Mwezi Novemba tutawasilisha kwenye Cabinet ili ifikapo mwaka kesho kabla hatujang'atuka, watoto wale tutakuwa tumewajua, wakipata ujauzito watarudi mashuleni.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie kidogo juu ya Baraza la Mitihani. Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana ya Utumishi ameeleza na mimi nipende kusema kwamba, tumepokea hoja zote mbili, tusingependa kugeuza Ukumbi huu uwe wa malumbano, tutaileta taarifa yenye mambo yote kwa maandishi. Yale yalikuwa ni maagizo na ninyi wenyewe Waheshimiwa Wabunge hapa, hata nilipoeleza hatua zilizochukuliwa, wapo waliodiriki kusema adhabu ni ndogo. Wale hawakuachishwa kazi na kamwe hawakufukuzwa kazi, wamepewa uhamisho tu. Siku zote mnasema hapa, watumishi wasiketi kwenye kituo kimoja kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie matibabu ya mwalimu. Mwalimu Richard Mpondo wa Shule ya Msingi Buhangija, ilikuwa ni haki yake kupata matibabu nje ya nchi na stahili yake ilishaelezwa kwenye barua na kwamba, salio lililobaki ni haki yake. Kwa kushirikiana na wenzetu wa TAMISEMI, tumelifanyia kazi, tunamwomba mwalimu huyo Jumatatu, Mungu akimfikisha salama, aende kwa Afisa Elimu wake, mambo yake yatakuwa mazuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie sababu za kuchelewa mishahara kwa walimu na kuingizwa kwenye orodha ya walipwaji. Sababu zipo nyingi, nitataja chache; moja ni walimu kuchelewa kuripoti kwenye vituo vyao. Pili, ni kubadili kituo cha kazi baada ya orodha ya awali kupelekwa mikoani. Tatu, kutojaza fomu za mkataba au kuajiriwa kwa usahihi; na nne ni ucheleweshwaji wa kupelekwa fomu alizojaza mwalimu Wizarani na mambo mengine mengi. Kwa hiyo, tunatambua kwamba, lipo tatizo na Jiografia ya nchi yetu ni kubwa, lakini kwa niaba ya Waziri wa Elimu, ninaomba kutoa wito na agizo kwamba, Wakuu wa Shule mara wanapowapokea walimu wapya, wawapatie fomu wazijaze na wasiwasubirishe. Umepelekewa walimu wanne, unasema mpaka wafike wanne la hasha; amekuja Juma Athumani, mjazie fomu yake ipeleke, hao wengine kwa kadiri watakavyoripoti utawapelekea.

Mheshimiwa Naibu Spika, vifaa vya kufundishia na kujifunzia; hili limezungumzwa sana, kila mwaka Wizara na Serikali hupeleka fedha za kununulia vitabu vya kujifunzia na kufundishia shuleni. Utaratibu wa Kanuni za Manunuzi unapaswa kufuatwa. Naomba niwaombe Walimu Wakuu na Wakuu wa Shule, wanunue vitabu kwa kadiri wanavyopatiwa fedha. Fedha zile ni kwa manunuzi ya vitabu na wanaponunua vitabu wawapatie wanafunzi. Si vyema kuviweka makabatini au kuacha kununulia vitabu ukafanyia mambo mengine. Kwa kuwa sasa shule zote ziko karibu nasi, naomba Waheshimiwa Wabunge, kwa pamoja tushirikiane kufuatilia kwa maana ni haki ya kila mwananchi kupata stahili hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na suala lingine ambalo limezungumzia juu ya masuala ya michezo. Michezo tunaithamini, tulizindua mwaka juzi na mwaka huu

UMISETA imefanyika na Disemba mwaka huu tutakuwa na UMITASHUMTA na mitaala inaonesha na stadi zote zipo, tunaomba tushirikiane. Tutamuunga mkono Rais, lakini ni wajibu wa Wizara hii kuhakikisha kwamba, michezo inafundishwa kwa ajili ya kujenga afya, kujenga mahusiano na baadaye kuweza kuibua vipaji mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nikushukuru sana kwa kutupa nafasi hii ili na sisi tuweze kufanya majumuisho ya hoja yangu, ambayo nimeitoa jana. Nawapongeza sana Waheshimiwa Wabunge, kwa michango yao ambayo imesheheni hekima, ushauri mzuri sana, na changamoto ambazo zinatukabili katika hatua hii ambayo tumefikia. Katika Wizara ya Elimu, kila siku tunalala na changamoto hizi na tunaamka nazo. Jana na leo nimejua hizi changamoto sio zetu wenyewe ni za Bunge lako Tukufu, ninakushukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni dhahiri hoja hii ilikuwa inangojewa kwa hamu kubwa, kwa sababu waliopata fursa ya kuzungumza hapa Bungeni ni Waheshimiwa Wabunge 32, waliochangia kwa maandishi ni Waheshimiwa Wabunge 141 na walioongea wakati wa Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na Mheshimiwa Waziri wa Fedha ni Wabunge 91. Nina uhakika kwamba, Bunge lako Tukufu na Waheshimiwa Wabunge, wataungana na mimi kumshukuru sana Mheshimiwa Diana Chilolo, kwa kutoa hoja kwamba, hoja hii ijadiliwe kwa siku mbili. Tunakushukuru sana, kwa sababu tumepata michango mingi. Michango hii itatusaidia sana na ahsante sana dada yangu Diana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa niwataje wale ambao walichangia katika hoja hii kwa kutoa hotuba hapa Bungeni nao ni: Mheshimiwa Omar Kwaangw' - Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma za Jamii, Mheshimiwa Susan Lyimo - Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Mchungaji Getrude Lwakatare, Mheshimiwa Fatma Fereji, Mheshimiwa Abdul Marombwa, Mheshimiwa Rosemary Kirigini, Mheshimiwa Thomas Mwang'onda, Mheshimiwa Magreth Agness Mkanga, Mheshimiwa Profesa Feetham Banyikwa, Mheshimiwa Joyce Masunga, Mheshimiwa Nuru Bafadhil, Mheshimiwa Nimrod Mkono, Mheshimiwa Suleiman Kumchaya, Mheshimiwa Fatma Mikidadi, Mheshimiwa Mohamed Missanga, Mheshimiwa Dokta Ali Tarab Ali, Mheshimiwa Kilontsi Mporogomyi, Mheshimiwa Ramadhani Maneno, Mheshimiwa Felister Bura, Mheshimiwa Mzee Ngwali Zubeir, Mheshimiwa Vedastusi Manyinyi, Mheshimiwa George Simbachawene, Mheshimiwa Lucy Owenya, Mheshimiwa Anna Lupembe, Mheshimiwa Dokta Charles Mlingwa, Mheshimiwa Maria Hewa, Mheshimiwa Benson Mpesya, Mheshimiwa Stephen Galinoma, Mheshimiwa Benedicto Ole-Nangoro, Mheshimiwa Zabein Mhita, Mheshimiwa Hawa Ghasia na Mheshimiwa Mwantumu Mahiza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wale ambao walileta michango yao kwa maandishi ni Mheshimiwa Mariam Reuben Kasembe, Mheshimiwa Juma Killimbah, Mheshimiwa Rita Louis Mlaki, Mheshimiwa Jackob Shibiliti, Mheshimiwa John Damiano Komba, Mheshimiwa Gaudence Kayombo, Mheshimiwa Kaika Telele, Mheshimiwa Ruth Blasio

Msafiri, Mheshimiwa Abdallah Omar Kigoda, Mheshimiwa Aziza Sleyum Ali, Mheshimiwa Anna Lupembe, Mheshimiwa Mgana Msindai, Mheshimiwa Lucas Selelii, Mheshimiwa Luhaga Mpina, Mheshimiwa Charles Keenja, Mheshimiwa Susan Lyimo, Mheshimiwa Raynald Mrope, Mheshimiwa Bernadeta Mushashu, Mheshimiwa Salum Hemed Khamis, Mheshimiwa Michael Lekule Laizer, Mheshimiwa Victor Mwambalaswa, Mheshimiwa Siraju Juma Kaboyonga, Mheshimiwa Mohamed Abdulaziz, Mheshimiwa Godfrey Zambi, Mheshimiwa Rajab Hamad Juma, Mheshimiwa Fred Mpendazoe, Mheshimiwa Halima Kimbau, Mheshimiwa George Malima Lubeleje na Mheshimiwa Shally Raymond.

Mheshimiwa Naibu Spika, wengine ni Mheshimiwa Suleiman Kumchaya, Mheshimiwa Faida Mohamed Bakar, Mheshimiwa Lucy Fidelis Owenya, Mheshimiwa Vita Rashid Kawawa, Mheshimiwa Grace Kiwelu, Mheshimiwa Mkiwa Kimwanga, Mheshimiwa Omar Ali Mzee, Mheshimiwa Emmanuel Luhahula, Mheshimiwa Aloyce Bent Kimaro, Mheshimiwa Hemed Mohammed Hemed, Mheshimiwa Hadija Al-Qassmy, Mheshimiwa Ezekiel Maige, Mheshimiwa Mudhihir Mohamed Mudhihir, Mheshimiwa Castor Ligalama, Mheshimiwa Magalle John Shibuda, Mheshimiwa Paul Kimiti, Mheshimiwa Charles Mwera, Mheshimiwa Ameir Ali Ameir, Mheshimiwa Said Arfi, Mheshimiwa Dokta Willibrod Slaa, Mheshimiwa Benson Mpesya, Mheshimiwa Dkt. Binilith Satano Mahenge, Mheshimiwa Dkt. Guido Sigonda, Mheshimiwa Dkt. Ibrahim Msabaha, Mheshimiwa Joyce Masunga, Mheshimiwa Brig. Jen. Hassan Ngwilizi, Mheshimiwa Cyril Chami, Mheshimiwa James Wanyancha, Mheshimiwa Diana Chilolo, Mheshimiwa Anthony Diallo, Mheshimiwa Mgeni Jadi Kadika, Mheshimiwa Masolwa Cosmas Masolwa, Mheshimiwa Profesa Philemon Sarungi, Mheshimiwa Fuya Kimbita na Mheshimiwa Josephine Gezabuke.

Mheshimiwa Naibu Spika, wengine ni Mheshimiwa Al-Shymaa Kwegyir, Mheshimiwa Abbas Mtemvu, Mheshimiwa Balozi Abdi Mshangama, Mheshimiwa Mwalimu Bujiku Sakila, Mheshimiwa Dkt. James Msekela, Mheshimiwa Mbaruk Mwandoro, Mheshimiwa Profesa Idris Mtulia, Mheshimiwa Magdalena Sakaya, Mheshimiwa Herbert Mntangi, Mheshimiwa Benedict Ole-Nangoro, Mheshimiwa Zaynab Vulu, Mheshimiwa Mwajuma Hassan Khamis, Mheshimiwa Fatma Mikidadi, Mheshimiwa Athumani Janguo, Mheshimiwa Hawa Ghasia, Mheshimiwa Hamza Mwenegoha, Mheshimiwa Juma Said Omar, Mheshimiwa Hadija Ngozi, Mheshimiwa Nuru Bafadhil, Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma, Mheshimiwa Gideon Cheyo, Mheshimiwa Dkt. Juma Ngasongwa, Mheshimiwa Elisa David Mollel, Mheshimiwa Maida Abdallah, Mheshimiwa Paul Lwanji, Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, Mheshimiwa Dkt. Raphael Chegeni, Mheshimiwa Balozi Dkt. Getrude Mongela, Mheshimiwa Margreth Mkanga, Mheshimiwa Pindi Chana, Mheshimiwa Rosemary Kirigini, Mheshimiwa Joel Bendera, Mheshimiwa Dunstan Mkapa, Mheshimiwa Profesa Raphael Mwalyosi, Mheshimiwa Mwaka Ramadhani, Mheshimiwa Mhonga Ruhwanya, Mheshimiwa Kilontsi Mporogomyi na Mheshimiwa Devota Likokola. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wengine ni Mheshimiwa Zaynab Vulu, Mheshimiwa William Shellukindo, Mheshimiwa Emmanuel Nchimbi, Mheshimiwa Daniel Nsanzugwanko, Mheshimiwa Christopher Chiza, Mheshimiwa John Pombe Magufuli,

Mheshimiwa Clemence Lyamba, Mheshimiwa Mwanawetu Zarafi, Mheshimiwa Aggrey Mwanri, Mheshimiwa Diana Chilolo, Mheshimiwa Zuleikha Haji, Mheshimiwa Halima Mdee, Mheshimiwa Anastazia Wambura, Mheshimiwa Dkt. Charles Mlingwa, Mheshimiwa Gosbert Blandes na Mheshimiwa Hassan Kigwalilo, Mheshimiwa Kheri Ameir. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wengine ni Mheshimiwa John Cheyo, Mheshimiwa Joseph Mungai, Mheshimiwa Hasnain Gulamabass Dewji, Mheshimiwa Ludovick Mwanzila, Mheshimiwa Jackson Makwetta, Mheshimiwa Richard Ndassa, Mheshimiwa Savelina Mwijage, Mheshimiwa Dkt. Mzeru Nibuka, Mheshimiwa Vuai Abdallah Khamis, Mheshimiwa Meryce Emmanuel, Mheshimiwa Martha Umbulla, Mheshimiwa Stephen Galinoma, Mheshimiwa Felix Kijiko, Mheshimiwa Mariam Mfaki, Mheshimiwa Tatu Ntimizi, Mheshimiwa Lolesia Bukwimba, Mheshimiwa Dkt. Lucas Siyame, Mheshimiwa Sijapata Nkayamba na Mheshimiwa Pascal Nakei; Mungu awalinde. *(Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba uniwie radhi nisome orodha hii ya Wabunge waliochangia.

**NAIBU SPIKA:** Kwa hiyo, una dakika thelathini.

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Ndani ya dakika thelathini?

**NAIBU SPIKA:** Eeh!

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Basi nitawataja kama muda utabaki.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge, walipokuwa wanachangia wameeleza na wanaonesha uelewa mkubwa wa hali ya elimu tuliyonayo sasa.

Ninapenda pia kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge, kwa kuwapongeza Viongozi wetu Wakuu; Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete, Mheshimiwa Makamu wa Rais na Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa kazi kubwa wanayofanya kuhimiza elimu na kuhakikisha kwamba, mipango yetu inafikiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa tulipofika, idadi ya wanafunzi wetu kwenye shule za msingi imefikia milioni 8.4, wale wa sekondari inakaribia milioni 1.5 na wale wa vyuo vikuu kwa mara ya kwanza mwaka huu watavuka *threshhold* ya wanafunzi 100,000. Haya ni mafanikio makubwa sana, kwa sasa katika upatikanaji wa elimu, sisi tulikuwa nyuma sana; sio Tanzania tena, Tanzania tumevuka hatua hiyo na sasa tunawashinda majirani zetu wengi ambao walikuwa wametupita mbele sana. Kwa hiyo, hili tujipongeze na tujiandae kwa changamoto zilizoko mbele yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kilichoko mbele yetu sasa ni kuhakikisha kwamba, elimu yetu inakuwa bora na hii ndiyo kazi yetu kubwa kama Bunge, kama Wizara ya Elimu, kama Serikali na kama Wananchi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hili tulifanye bila kujali itikadi zetu na bila kujali vyama vyetu, hii ni faida ya Wananchi wote wa Tanzania. Mimi nawashukuru sana kwa mawazo ambayo yametoka hapa, katika hizi siku mbili ambazo tumejadili hoja hii. Ahsante sana. (*Makofi*)

Tumezungumza juu ya tatizo kubwa sana la walimu na mimi nakubaliana na Waheshimiwa Wabunge kwamba, tuna tatizo kubwa sana. Halafu tuna tatizo la walimu kwenda kwenye maeneo ambayo wamepangwa au kufika kule na kuondoka. Hizi ni changamoto ambazo sote tunatakiwa tuzishughulikie na tuziondoe ili tuweze kwenda vizuri. Nilieza katika hotuba tuliyotoa hapa jana asubuhi kwamba, kwa mwaka wa 2009 na 2010, tutapeleka walimu 6946 kwenye shule za msingi; kama mliiona hotuba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma za Jamii, mtaona karibu tunafikia lengo kwenye shule za msingi, maana tumebakiza upungufu wa walimu 37 na kidogo hivi. Kwa hiyo, tunakwenda vizuri sana.

Tatizo letu kubwa liko kwenye sekondari, lakini mwaka huu tumefikia hatua kubwa sana, ambapo tutakuwa na walimu 7,656 wa stashahada au diploma, tunawapeleka wote sekondari; halafu tutakuwa na walimu 5331 wa shahada ya kwanza ya ualimu ambao tunawapeleka sekondari. Hii ni hatua kubwa sana. Kwa ujumla, katika mwaka mmoja sasa tuna uwezo wa kupeleka walimu 12,987 shuleni. Nawaomba Waheshimiwa Wabunge, tuweke mazingira mazuri kama alivyosema hapa Naibu Waziri ili walimu hawa tutakapowaleta huko, waweze kukaa na kuendelea na kazi zao. Hatua ya kuongeza walimu ni dhahiri kuna vyuo 17 vya elimu ya juu, vinatoa elimu ya ualimu; kuna vyuo 77 vya ualimu; sasa vyote hivi vinatoa elimu ya ualimu katika ngazi ya diploma; bado vyuo vipya vinafunguliwa, bado vyuo vipya vinajengwa na Wizara inatoa kibali vyuo hivi vijengwe. Tutakapofika mwaka 2011/2012 tutaweza kuwa tumefikia kiwango tunapeleka shuleni walimu 25,000 kwa mwaka mmoja. Kwa hiyo, hili tunapambana nalo na karibu vita hii tutaishinda. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, ambalo ni kubwa, tumekuwa tunasumbuliwa sana na tatizo la maabara katika shule za sekondari. Hili ni tatizo kubwa, limekuwa linatusumbua sote na kila mmoja wetu alipozungumza hapa, ametoa hili kama changamoto kubwa sana mwaka huu. Mungu siyo Athumani, Viongozi wetu Wakuu, wametukubalia na Benki ya Maendeleo ya Afrika imekubali kutupatia awamu ya kwanza ya Dola za Kimarekani milioni 90 za kununulia vifaa vya maabara. Mwaka kesho tukipata Dola za Kimarekani milioni 90 nyingine kwa ajili hii, suala hili tutaanza kuliangalia kwa nyuma kwamba hatua hii sasa tumepita. Kwa hiyo, ndugu zangu nawaomba, hizi ni hatua kubwa na muhimu katika maendeleo ya nchi yetu. Nawaomba mtuunge mkono tupate fedha zilizoko kwenye bajeti ili twende kuichapa kazi hii, tukikutana hapa mwaka kesho tutaongelea haya kama historia. *(Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala lingine hapa ambalo limeandikwa sana kwenye michango na jinsi lilivyoandikwa, inaonekana kama wote tunasema kitu hicho hicho kimoja lakini tunasema kwa lugha tofauti. Tunasema kitu kimoja na hiki kinahusu

vitabu wanavyosoma watoto wetu shuleni. Kwa sasa inayotumika ni sera ya vitabu vingi au *multi-text books*. Utekelezaji wa sera ya vitabu vingi ni kama wataalam tulionao wanachagua ama *text book* tatu au nne na kuvipendekeza kutumiwa mashuleni. Mathalani, kwa somo la *biology*, nasema hivi vitabu vinne vinafaa mvitumie shule. Wanaketi wanasema kitabu hiki kati ya hivi vitabu vinne tofauti, ndiyo kizuri kupita vyote na kwa sababu hiki ndiyo kizuri kupita vyote, sasa kinakuwa kitabu cha kiada. Hivi vitabu vingine vitatu vilivyobaki, tunavinunua tunaviweka kwenye maabara vinakuwa vitabu vya ziada. Nia yake hapa ni kwamba, mwanafunzi mmoja anayeitwa Jumanne Abdallah Maghembe, anaweza kuvipata shuleni vitabu vyote hivyo vinne. Anaweza kusoma kile cha kiada alichonacho na anaweza akaenda *library* akavikuta vitatu; kwa hiyo, mwanafunzi sasa anavyo vitabu vinne vinavyomfikia yeye aweze kuvisoma.

Katika kuchagua kile kitabu kimoja cha kiada, lengo ni kuwafanya vijana wote Tanzania, wawe na msingi, uelewa imara na unaofanana. Kwa kuwa tunatekeleza mtaala mmoja nchi nzima na wanafunzi wote wanafanya mtihani mmoja, kwa hiyo, tuwapelekee vitabu vinavyofanana ili kila mmoja awe na vitabu vyote vilivyopendekezwa. *(Makofi*)

Kitu kingine ni kwamba, kitabu cha kiada lazima kiwe na ubora wa hali ya juu, utakaowapa wanafunzi wetu uelewa wa kina wa somo hilo na kuwapa uwezo wa kushindana na kuwapiku wenzao wa mataifa mengine.

Mwisho kitabu cha kiada, lazima kiwasaidie vijana wetu kujenga utaifa wao na kuwaongezea ari ya kusoma zaidi, kujenga utamaduni wa kutafuta ukweli. Utekelezaji wa vitabu vingi kwa sasa hapa nchini, umekuwa na dosari kwa kuwa badala ya mwanafunzi mmoja kuweza kuvipata na kuweza kuvisoma vitabu vyote vilivyochaguliwa shuleni kwake, kila shule na kila wilaya inachagua itumie kitabu chake. Hivyo, watoto wa Ileje Sekondari wanatumia kitabu tofauti cha baiolojia na watoto wa Kiwanja Sekondari, japo shule zote ziko Wilaya ya Ileje. Aidha, katika ngazi ya Wilaya, watoto wanaosoma Wilaya ya Rombo wanatumia vitabu tofauti na wale wa Wilaya ya Iramba, Wilaya ya Dodoma Wilaya ya Mahenge, Wilaya ya Kilindi na Wilaya ya Kasulu, kila mmoja anatumia kitabu chake, lakini wote wanafanya mtihani mmoja. Ndiyo maana Mheshimiwa Rais, ametushauri kwamba, tuchague hivi vitabu, kuwe na kitabu cha kiada na tuwe na MMES awamu ya pili, ihakikishe kwamba, vile vitabu vyote ambavyo vimewekwa kama vitabu vya ziada kwa kila somo, vikae kwenye maktaba yetu; ndiyo msingi wake. Kila mmoja wetu aliyeeleza hapa, ameeleza kwa maana ya watoto kupata vitabu vingi zaidi vya kusoma na sio kila mtoto kusoma kitabu chake. *(Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kuishukuru sana Kamati ya Huduma za Jamii, kama ulivyoona Hotuba ya Kamati, ilisheheni mapendekezo mengi. Ninaiahidi Kamati na Bunge lako Tukufu kwamba, mapendekezo yaliyokuwa ndani ya Hotuba ile, tutayafanyia kazi na kila mara tutakapokuwa na Kamati, tutapitia mapendekezo haya ili Kamati ijue hatua tuliyofikia na pale ambapo tunapata matatizo. Walieleza hapa kwamba, mazingira ya vyuo vya elimu ya juu siyo mazuri; miundombinu imechakaa, kuna upungufu wa vitendea kazi, upungufu wa Wahadhiri na Maprofesa, uhaba wa maktaba, madarasa na mabweni ya kulala wanafunzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua hili tatizo na zifuatazo ni hatua mbalimbali zinazochukuliwa ili kutatua matatizo haya:-

(i) Niliwaeleza juu ya Mradi wa Maendeleo ya Elimu ya Juu. Utekelezaji wa Mradi wa Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu, unaofadhiliwa na Benki ya Dunia, ulizinduliwa mwezi Mei, 2009. Mradi huu utakaogharimu Dola za Kimarekani milioni 100 kwa awamu ya kwanza na milioni nyingine kwa awamu ya pili, unalenga kuboresha maabara na kuboresha miundombinu kwa baadhi ya vyuo. Pia utasomesha wanafunzi wengi kwenye fani za sayansi, teknolojia na ualimu.

(ii) Hivi sasa tunaandaa Mpango wa Maendeleo wa Elimu ya Juu kama ule wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi na kama ule wa Maendeleo ya Sekondari unaoitwa MMES. Mpango huu unatarajiwa kuwa tayari kuanza utekelezaji mwaka 2010/2011. Mpango huu utaibua mikakati mbalimbali ya kuboresha miundombinu, pamoja na kujenga mipya katika vyuo vyetu vya elimu ya juu. Nia ni kuboresha miundombinu, kupanua nafasi za udahili, kujenga mabweni, kumbi za mihadhara na kumbi za kulia chakula ili vyuo vyetu viwe vya kisasa na viwe maeneo mazuri ya kusoma.

(iii) Serikali itaendelea kutoa fedha za maendeleo kwa ajili ya ukarabati na ujenzi wa miundombinu mpya vyuoni. Katika mwaka huu wa fedha, shilingi bilioni 46 za fedha za ndani zimetengwa kwa ajili hiyo.

Kuhusu uhaba wa wahadhili katika vyuo mbalimbali, hatua zifuatazo zimechukuliwa:-

(i) Kutekeleza Mradi wa Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu, ambao umelenga kusomesha wanataaluma kwenye fani za sayansi, teknolojia na ualimu.

(ii) Serikali ikishirikiana na Vyuo Vikuu, ina mkakati wa kuwaajiri wanataaluma kwa mkataba kutoka nchi kama vile India, Urusi na Cuba ili kupungu uhaba wa wanataaluma wakati vyuo vinaendelea kusomesha wanataaluma wake wa ndani.

(iii) Tangu mwaka 2006/2007, Serikali inatenga fedha za kuvisaidia vyuo kusomesha wahadhili wasaidizi kwenye vyuo vikuu vya ndani.

(iv) Kuanzia mwaka 2008/2009, Serikali iliruhusu Bodi ya Mikopo kutoa mikopo ya kuwasomesha wahadhili wasaidizi na walimu wasaidizi ili wasome shahada za uzamili na uzamivu katika vyuo vikuu vya umma.

(v) Serikali inaingia ubia na mashirika nchini Ujerumani kwa ngazi ya uzamivu.

(vi) Kuvielekeza Vyuo Vikuu vya Dar es Salaam, SUA na MUHAS, kupanua udahili katika ngazi ya uzamili na uzamivu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali iweke mtazamo mpya wa namna ya kuendelea kutoa mikopo. Kutokana na idadi kubwa ya ongezeko la waombaji, Serikali inatafuta utaratibu mbadala wa kutoa mkopo wa elimu ya juu na rasimu ya mapendekezo imekamilishwa tayari kwa kujadiliwa na Uongozi wa Elimu wa Wizara ya Fedha.

Kamati yetu pamoja na mambo mengine, imeelekeza Serikali iendelee kutoa elimu kwa wadau wote kuhusu sera ya uchangiaji kwa gharama za elimu ya juu na Serikali inakubaliana na Kamati katika jambo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza Msemaji wa Upinzani, kwa hotuba yake na mawazo mbalimbali ambayo ameyatoa. Ametoa mapendekezo mengi na mengi ya mapendekezo haya tutayafanyia kazi. Itoshe kusema kwamba, mapendekezo yake yanayohusu madaraja katika Bodi ya Mikopo, tatizo la mitaala na upungufu wa mahali pa kulala, pamoja na maji katika Vyuo Vikuu, tumeyapokea na tutayashughulikia. *(Makofi*)

Aidha, alikuwa na hoja kuhusu hatima ya wanafunzi wa *University of Dodoma*, waliosimamishwa bila kusikilizwa. Wanafunzi 26 waliohusika na suala hili, walibainika kuwa ndiyo vinara wa vurugu zilizofanywa kuanzia Chuo cha Elimu au *College of Education.* Wanafunzi hao waliohusika na kusababisha uharibifu mkubwa wa milango ya mabweni katika Jengo la Chimwaga na hali kadhalika walihusika katika kuwapiga wenzao, hasa wasichana ili wawaunge mkono katika vurugu walizozianzisha. Suala hili lilihusisha Vyombo vya Dola, yaani Polisi na utaratibu uliowekwa na Chuo Kikuu. Kwa upande wa Chuo Kikuu, Kamati iliundwa mara moja, kuchunguza suala hili, wakati wa uchunguzi ililazimika kuwasimamisha masomo na kuwarudisha nyumbani kwao. Hatua hii pia ilitoa fursa kwa polisi kukamilisha uchuguzi wake. Hatua hizi zote zinachukua muda, taratibu zinakitaka chuo kuunda Kamati ya Nidhamu na kuwapa fursa wahusika kujitetea. Kamati hiyo imeshaundwa, baada ya kukamilika kwa taratibu za uchunguzi, wahusika wataitwa mbele ya Kamati hiyo muda si mrefu kutoka sasa na hatima yao itaamuliwa na Kamati hiyo.

Pamoja na hayo, ningependa kuwashauri wanafunzi na kuvishauri Vyuo Vikuu kwamba, vyuo vina taratibu za kutatua migogoro na taratibu hizo zimebainishwa katika idhini na sheria ndogo ndogo zinazopitishwa na Mabaraza ya Vyuo Vikuu. Napenda kuwashauri wanafunzi wote katika vyuo vyetu vya elimu ya juu kwamba, wafuate utaratibu, sheria na sheria ndogo ndogo ambazo zimeanzishwa na Mabaraza yao. Ni vyema wanafunzi wakafahamu kwamba, si vizuri wao kuchukua sheria mikononi mwao na kuwalazimisha wanzao kwa kuwapiga, kwani kama raia wengine, wanafunzi hawako juu ya sheria. *(Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, leo alizungumza Askofu juu ya madeni ya maji na umeme katika shule za sekondari.

**NAIBU SPIKA:** Askofu gani?

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara inatambua kuwepo kwa madeni ya umeme na maji kwenye shule, yenye jumla ya shilingi milioni 631. *(Kicheko)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, hii kengele inakupa wewe *alarm*. Umesema Askofu, sasa lazima ujibu ni Askofu wa wapi ndani ya Bunge hili?

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Anaitwa Askofu Mpesya. (*Kicheko*)

**NAIBU SPIKA:** *Is not official name*.

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara mwaka huu wa fedha, itaanza kulipa madeni ya mwezi Agosti, 2009. Kuanzia mwaka huu wa fedha, gharama za umeme na maji zimekasimiwa katika Halmashauri zilizoko pale shule zilipo. Hata hivyo, ushauri wa Mheshimiwa Mpesya kwa Wizara yangu, kuwasiliana na Wizara husika ili kurejesha umeme na maji mashuleni mapema iwezekanavyo, umechukuliwa na utafanyiwa kazi mara moja. *(Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, upungufu wa walimu katika shule umeelezwa kwa undani, tunayo hoja hapa ya Mheshimiwa Magalle Shibuda, kuanzisha ujenzi wa Chuo cha Ualimu Maswa. Tumepokea pendekezo hili lenye lengo la kuongeza walimu katika nchi. Hata hivyo, mpango wa sasa wa kuandaa walimu wa kutosha unazingatia mikakati ifuatayo:-

(i) Kupanua na kukarabati vyuo vilivyoko ili kuhakikisha matumizi mazuri ya rasilimali za vifaa; hii ni pamoja na kupanua Chuo cha Ualimu Shinyanga kilichopo katika Mkoa wa Mheshimiwa Mbunge. (*Makofi*)

(ii) Kushirikiana na Sekta Binafsi katika kuanzisha vyuo vya ualimu ili kukidhi mahitaji ya walimu ngazi ya msingi na sekondari. Hata hivyo, Wizara yangu itatuma wataalam katika Wilaya ya Maswa ili kushirikiana na Wilaya hiyo na kuona uwezekano wa kujenga chuo hicho.

Mheshimiwa Naibu Spika, kero na matatizo mbalimbali ya walimu kama vile kutolipwa kwa wakati fedha za likizo, matibabu, uhamisho na malimbikizo yanayotokana na ajira mpya, pamoja na kupandishwa vyeo. Hoja hii imetolewa na Mheshimiwa Anna Lupembe, Mheshimiwa Benson Mpesya, Mheshimiwa Godfrey Zambi, Mheshimiwa Victor Mwambalaswa, Mheshimiwa Lucy Owenya, Mheshimiwa Getrude Lwakatare, Mheshimiwa Diana Chololo, Mheshimiwa Paul Kimiti, Mheshimiwa Rajabu Juma, Mheshimiwa Siraju Juma Kaboyonga, Mheshimiwa Raynald Mrope na Waheshimiwa Wabunge wengine.

Serikali imefanya uhakiki wa madai katika Serikali za Mitaa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, kwa walimu na watumishi wasiokuwa walimu, katika shule za msingi, sekondari, vyuo vya ualimu, wakaguzi wa shule na ofisi za mhariri wa magazeti

wa kanda. Katika ngazi ya Serikali za Mitaa, madeni yaliyokusanywa yalibainika kuwepo kwa madai ya watumishi 175,045, yenye thamani ya shilingi 49,562,884,311.27. Katika ngazi ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, uhakiki ulibaini madai ya watumishi 25,440 yenye thamani ya shilingi 22,779.6 milioni. Aidha, katika utaratibu wa kawaida kwa mwaka wa fedha 2008/2009, Serikali imelipa madeni ya Watumishi ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi ya watumishi 10,417, yenye thamani ya shilingi bilioni 7.6 na madai mengine yenye thamani ya shilingi bilioni 1.2. Madai ya shilingi bilioni 6,349.2 kwa ajili ya kupandishwa vyeo yalilipwa na madai yote ya walimu yametengewa fedha kama nilivyosema katika bajeti ya mwaka 2009/2010 katika Wizara ya Fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ambavyo unaona katika meza yangu, hoja ambazo zimetolewa ni nyingi na ninawaomba Waheshimiwa Wabunge, wakubali tuwaletee majibu kwa maandishi kama kijitabu cha hoja na majibu yake haraka inavyowezekana; kwa sababu hakuna uwezekano wowote ambao tunaweza kuufanya kwa kuyajibu maswali haya.

Yako maswali machache, ambapo Waheshimiwa Wabunge waliniomba Kitabu cha Mwele Binti Taabani. Kitabu hicho kilifika kwa wataalam wetu wa Emack wamekiangalia, kimefika kwenye Taasisi ya Elimu ya Tanzania kimeangaliwa. Tafadhali sana, kipeleke tena kwenye *round* inayokuja Januari, 2009 ili kiweze kupatiwa tathmini 2010.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, nimeletewa maombi hapa ya eneo la Jamii ya Wamasai, wanaofanya ibada yao ya kimira katika Chuo cha Ufundi Arusha. Napenda kumhakikishia Mheshimiwa Elisa Mollel na Waheshimiwa Wabunge wa Mkoa wa Arusha kwamba, Serikali haina tatizo kwa viongozi wa mila kwenda kuabudu katika eneo hilo na tutasaidia kulihifadhi vizuri ili huduma hiyo iweze kuendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kutoa hoja. (*Makofi*)

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**Fungu 46 - Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi**

Kif. 1001 *Administration and General* …………………………Sh. 20,646,293,400

**MWENYEKITI:** Haya mimi sina matatizo kabisa, isipokuwa msichukue gari la Waziri tu. Tutatumia kifungu cha 104(1) kuongeza muda wa dakika 30. Tutatumia pia kifungu cha 104(2), zikibakia dakika kumi tulizoongeza tuna guillotine. Kwa idadi niliyonayo hapa, hamuwezi kufikiwa wote lakini nitawaandika wote.

Tutaanza na Mheshimiwa Daniel Nicodem Nsanzugwanko, Mheshimiwa George Lubeleje, Mheshimiwa Felister Bura, Mheshimiwa Jacob Shibiliti, Mheshimiwa Lucas Selelii, Mheshimiwa Dkt. Charles Mlingwa, Mheshimiwa Godrey Zambi, Mheshimiwa George Simbachawene, Mheshimiwa Balozi Dkt. Getrude Mongella, Mheshimiwa Felix Kijiko, Mheshimiwa Rosemary Kirigini, Mheshimiwa Aloyce Kimaro, Mheshimiwa Vedastusi Mathayo Manyinyi, Mheshimiwa Diana Chilolo tena utaanza wewe leo, maana wewe ndiye uliyesababisha. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Emmanuel Jumanne Luhahula, Mheshimiwa Esther Nyawazwa, Mheshimiwa Margreth Agness Mkanga, Mheshimiwa Grace Kiwelu, Mheshimiwa Susan Lyimo, Mheshimiwa Said Amour Arfi, Mheshimiwa Michael Lekule Laizer, Mheshimiwa Ramadhani Athumani Maneno, Mheshimiwa Dkt. Zaynab Gama, Mheshimiwa Dkt. Samson Mpanda, Mheshimiwa Alhaj Mohamed Hamisi Missanga, Mheshimiwa Josephine Genzabuke, Mheshimiwa Lucy Owenya, Mheshimiwa Charles Mwera, Mheshimiwa Dkt. Ali Tarab Ali, Mheshimiwa Yahya Kassim Issa, Mheshimiwa Prof. Raphael Mwalyosi na Mheshimiwa John Lwanji.

Sasa tunaanza na Mheshimiwa John Lwanji.

**MHE. JOHN P. LWANJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, naomba *statements* zetu ziwe *very brief* kwani hakuna hotuba, atakayetoa hotuba namgongea kengele.

**MHE. JOHN P. LWANJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sawa. Nilichangia kuhusu ufunguzi wa Shule za *High School* Mkoani Singida na kwamba, mwaka jana kulipendekezwa shule saba mkoani, kila Jimbo kuwe na *High School*. Sasa shule mbili za Itigi na Mwanzi ndiyo zilizokidhi vigezo vya kuweza kufungua Shule ya *High School*.

Juzi tumepata kibali cha shule moja ya Mwanzi, lakini mpaka sasa hatujafanikiwa kupata kibali cha shule ya Itigi wakati imekidhi vigezo vyote. Ninapenda kupata maelezo ni kwa nini?

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, shule tatu zilipitishwa kwa sababu zilikidhi kila kigezo. Hata hivyo, nyingine ambazo zimekidhi vigezo, zilikuwa zimekidhi vigezo wakati muda wa kupeleka wanafunzi wa kidato cha tano umeshapita. Namwomba Mheshimiwa Mbunge, avute subira kwa sababu mwaka unaofuata unakuja na hivyo shule hizo zitapata wanafunzi kwa kadiri ambavyo zimekidhi vigezo vinavyohitajika.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, ahsante sana. Mheshimiwa Diana Chilolo, ndiyo zawadi yake hiyo, karibu.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Katika mchango wangu wa maandishi, nilikuwa nimeiomba Serikali kwamba, wakati umefika sasa kuunda Tume kama iliyoundwa zamani enzi ya Marehemu Baba wa Taifa, iliyojulikana kwa jina la Tume ya Makwetta. Sababu ambazo zimenifanya kusema hivyo

au kuiomba Serikali ni kutokana na Muundo wa Wizara ulivyo sasa, una mabadiliko mengi sana na matatizo, kadhalika kero na changamoto nyingi ndani ya Wizara hii.

Si hivyo tu, ukizingatia mabadiliko ya Teknolojia yaliyopo sasa hapa duniani, kuna kila sababu ya Tume kuundwa hata msongamano wa Wabunge waliosimama hapa utapungua endapo Tume hiyo itakabidhiwa kazi ya kuipitia Wizara hii kwa kina kabisa ili tuweze kupata Wizara ambayo mambo yake yamepikika na yamejipanga vizuri kwa lengo la kuboresha Elimu.

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumshukuru sana Mheshimiwa Diana Chilolo, kwa mapendekezo yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa Wizara inapitia Sera zile za Elimu, yaani Sera ya Elimu na Mfunzo, Sera ya Ufundi na Ufundi Stadi, Sera ya Elimu ya Juu na kadhalika. Mwezi Septemba mwaka huu, tutawaita wadau wote waanze kujadili hii Sera na baadaye inakwenda kwenye Baraza la Mawaziri. Hatua ambayo tumefikia na kwa kuwa tumefika karibu kumaliza na wadau wamekuwa wakihusishwa wakati wote na hivi sasa tunangoja Sera hiyo ikamilike ili tuweze kubadilisha Sheria na kuitekeleza.

Ninamwomba Mheshimiwa Mbunge, avute subira mpaka mwezi Septemba na tutawaalika Waheshimiwa Wabunge ili muweze kushiriki katika mjadala huu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, ahsante. Mheshimiwa Margreth Mkanga karibu.

**MHE. MARGRETH A. MKANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi.

Jana nilihoji baada ya kutambua kwamba, kuna utaratibu ambao upo wa wanafunzi wasioona wa shule za sekondari ambao hawafanyi hesabu, kuja kuadhibiwa mwishoni kwa kushushiwa madaraja yao ya ufaulu kana kwamba hizo hesabu walikataa. Je, Serikali itaufuta lini mtindo huu?

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba, Mheshimiwa Mkanga alitoa mawazo haya na sisi tumeyapokea na kwa uhakika, tutayafanyia kazi na kutoa *report* mapema iwezekanavyo.

**MHE. DKT. SAMSON F. MPANDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwa kuwa mara nyingi tumeletewa *computer* nyingi kwenye shule zetu za sekondari; je na sisi Kilwa Kaskazini tumo katika watu watakaopata hizo *computer* au tutazisikia kwenye redio tu?

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samson Mpanda kwa swali lake.

Mheshimiwa Dkt. Mpanda, yuko kwenye Kamati ya Huduma za Jamii, kwa hiyo, anaelewa mambo haya kwa karibu sana kwamba, tunaandaa mpango wa kufundisha kwa kutumia TEHAMA. Mpango wa shule za msingi umeshaanza unaitwa Bridge IT na tunapenda kumhakikishia kwamba na kwenye Jimbo lake katika Pilot hii tuliyonayo utatekelezwa.

**MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Chuo cha Ualimu cha Kabanga Kasulu, kina umri wa miaka 29. Chuo hiki tangu majengo yake yametaifishwa kutoka kwa Kanisa Katoliki, hakijaongezewa jengo lolote wala *infrastructure* yoyote. Napenda kumuuliza Mheshimiwa Waziri kwamba; je, ana mpango wa kukifuta Chuo hiki?

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana rafiki yangu Mheshimiwa Nsanzugwanko, kwa swali lake.

Jibu kwa kweli ni hapana. Napenda kumhakikishia Mheshimiwa Nsanzugwanko kwamba, Chuo hicho ni muhimu na nimekitembelea na tutakifanyia ukarabati kadiri fedha zitakavyopatikana na kukiongezea udahili wa wanafunzi kadiri miundombinu itakavyopanuka.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu wa maandishi, nilitaka maelezo tu. Katika Chuo cha Ualimu Mpwapwa kuna nyumba 79 za Walimu na Shule ya Sekondari ya Mpwapwa kuna nyumba 21 za Walimu. Nyumba hizi zina hali mbaya sana, zimefanyiwa ukarabati mara ya mwisho mwaka 1986, sasa ni zaidi ya miaka 20 na Mheshimiwa Waziri ameshatembelea Chuo cha Ualimu Mpwapwa.

Je, Serikali ina mpango gani kuzifanyia ukarabati nyumba za Walimu kwa sababu wanaishi katika mazingira magumu sana?

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumshukuru sana Mheshimiwa George Lubeleje, kwa kazi nzuri anayoifanya. Katika Chuo cha Elimu Mpwapwa na Shule ya Sekondari kule Mpwapwa, yeye ni Mwenyekiti wa Bodi ya Taasisi hizi.

Napenda kumhakikishia kwamba, Serikali inafanya ukarabati katika Chuo kile na katika Shule ya Sekondari ile, hatua kwa hatua kutegemeana na jinsi tunavyopata rasilimali za kuhudumia Taasisi hizi.

**MHE. FELISTER A. BURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, leo asubuhi nilichangia juu ya watoto wa kike wanaokatizwa masomo yao, baada ya kupata ujauzito kama wanaweza kuendelea na masomo. Pia niliomba kujua kama Tume iliyoundwa ilishatoa mapendekezo Serikalini na kama mapendekezo haya tunaweza kuyapata na kuyajadili hapa Bungeni?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimetoa ufafanuzi kwamba, tutakaribisha *public hearing.*

Ni kweli ile Tume imewasilisha Taarifa yake Wizarani na imeshapitiwa. Kwa kuwa Wizara iko katika mchakato wa kufanya maboresho ya Sera na kwa utaratibu ni lazima tuanze kufanya marekebisho ya Sera, ndipo tuweze kubadilisha Sheria ya Elimu. Italetwa hapa Bungeni ili kipengele hicho cha ama kuruhusu, kuruhusu namna gani na kwa wakati gani, tutakiamua sisi wenyewe.

**MHE. JACOB D. SHIBILITI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Katika mchango wangu wa maandishi, nimezungumzia mambo mengi lakini nichukue hili moja.

Hii ni mara ya tatu, nasimama hapa kutokana na tatizo la Wakaguzi pale Misungwi, hatuna gari, yaani sijapata gari. Hilo gari liko wapi?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, tuliahidi kumpatia gari Mheshimiwa Shibiliti. Mazingira na jiografia ya eneo lake, hayahitaji gari ambalo kwa wakati huo tulikuwa nalo. Tulikuwa na *Double Cabin Hilux*, tuliona si hekima kumpelekea gari la namna hiyo.

Katika bajeti hii, Mwenyezi Mungu akituwezesha na mkituwezesha kuipitisha, tumemuahidi kumpatia gari *Hard Top* mpya.

**MHE. LUCAS L. SELELII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Mpango wa MMEM na MMES, upo utaratibu nchi nzima wa kutoa fidia ya ada na kutoa pesa ya vitabu.

Kwa Mkoa wa Taboa hasa katika Wilaya ya Nzega, fedha hizi za fidia ya ada na vitabu hazifiki na hata zikifika, hufika zikiwa zimechelewa na hata zikichelewa kufika basi hufika kidogo sana.

Hivi kwa utaratibu huo; Mpango huo umesitishwa au hizo pesa zimepunguzwa au kumetokea kitu gani chini ya Mipango hiyo yote miwili?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, hatujasitisha utaratibu wa kupeleka fidia ya ada. Fedha hizo zinapelekwa kwa kadiri Wizara inavyopokea kutoka Hazina.

Hata hivyo, hutofautiana kiasi, kiwango na muda wa kuzipeleka, kwani mlolongo wake ni mrefu. Namwomba Mheshimiwa Mbunge, awasiliane na Bodi ya Shule kama ni kwa Shule za Sekondari au Kamati ya Shule na yeye anaweza kufahamu. Pia kwa kuwa Mheshimiwa Mbunge ni Mjumbe katika Kamati ya Halmashauri ya Madiwani, huwa

zinajadiliwa zile fedha, kuarifiwa ni kiasi gani kimepatikana na zitagawanywa namna gani. Naomba ashiriki kwenye vikao.

**MHE. DKT. CHARLES O. MLINGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Manispaa ya Shinyanga, haina sekondari hata moja yenye Kidato cha Tano na Sita. Kwenye mchango wangu niliuliza nili ni Shule ya Sekondari ya Rajani, yenye sifa stahili ya kuwa na Kidato cha Tano na Sita itapewa hadhi hiyo ili vijana waweze kuingia Kidato cha Tano na Sita?

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Mlingwa, kwa swali lake.

Tutawatuma Wakaguzi katika shule hiyo na kupitia Bunge lako Tukufu, tutawataka Wakaguzi waende pale wakaikague na kama kila kitu kiko tayari, basi kwa mwaka mpya wa fedha, shule hiyo itafunguliwa.

**MHE. ALOYCE B. KIMARO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu bora ni pamoja na vitabu bora vya kiada, pamoja na Walimu bora.

Wizara inatambua kwamba, kuna upungufu mkubwa sana wa vitabu vya kiada mashuleni. Pia Wizara inatambua kwamba, Walimu Wakuu wa Shule hawanunui vitabu vya kiada na pia Wizara inatambua kwamba, *publishers* wana vitabu vyenye thamani zaidi ya shilingi bilioni 80 kwenye maghala yao.

Je, kwa nini Wizara isinunue hivyo vitabu na kusambaza mashuleni moja kwa moja?

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Kimaro, kwa swali hili na kwamba yeye ni jirani yangu kwenye Jimbo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha hizi zinakwenda shuleni moja kwa moja na ni mwaka huu kama tulivyosema, tulijaribu kupeleka vitabu vya baiolojia na hesabu kwenye shule za sekondari kwa shule 150 na utaratibu huo ulionesha kufanikiwa sana. Mwaka huu tutapeleka vitabu vyenye thamani ya Dola za Marekeni milioni 11 kwa utaratibu huo, yaani kwa masomo ya hesabu, bailojia, kemia na fizikia. Utaratibu wa zamani utaendelea kwa masomo mengine yaliyobaki.

**MHE. VEDASTUSI M. MANYINYI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Shule ya Sekondari ya Musoma Technical, pamoja na Songe, kwa muda wa zaidi ya mwezi sasa zimekatiwa umeme na kibaya zaidi, Shule ya Musoma Technical imekatiwa hata ule umeme unaopampu maji kuja shuleni. Kwa hiyo, hivi ninavyozungumza, maji pale shuleni hayapo. Mheshimiwa Waziri amesema, madeni yote na majukumu yote haya yatarudishwa katika Halmashauri.

Napenda kufahamu kwamba; je, shule hizi zitaendelea kusubiri mpaka mchakato wote wa urudishaji utakapokamilika ndipo zipate umeme?

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana ndugu yangu, Mheshimiwa Manyinyi, kwa swali lake. Shule hizo zitarudishiwa umeme mara moja.

**MHE. EMMANUEL J. LUHAHULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi karibuni kuna vijana waliomaliza Chuo cha Ualimu Grade A, walipangwa kwenda Wilayani Bukombe, kufika kule wale vijana wakarudishwa siku mbili zilizopita na wale vijana wameendelea kuhangaika sana. Wakati huo huo, Wilaya ya Bukombe ina shida sana, kwani ina upungufu wa Walimu na vijana wengi sana wa Bukombe wamemaliza Vyuo vya Ualimu ambao hawajaonekana na wanahitaji kurudi Bukombe.

Sasa sijui Mheshimiwa Waziri au Serikali wanasema nini kuhusiana na tatizo la hao Walimu ambao wamerudishwa hawajui wafanye nini lakini pia hata hao wa Bukombe kama wanaweza kurudi kule?

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Luhahula, kwa swali lake zuri.

Ni kweli kwamba, Walimu wa *Grade A* kwa maana ya wa Daraja la III A, walitangaziwa kwamba, kama majibu ya mitihani yao yatakuwa yamepatikana kabla ya tarehe 20, basi vijana hao waripoti mashuleni tarehe 20 Julai. Aidha, Walimu wengi hawakuona hii kadhia kwamba, kama majibu yametoka ya mitihani na wakaona kwamba wamefaulu ndiyo waende shuleni.

Bahati mbaya, majibu ya mtihani wa Cheti na Diploma hayakutoka kabla ya tarehe 20 na yatatoka wiki ya kwanza ya August; na kwa hiyo, wamearifiwa kwamba, wote warudi kuripoti mwezi Septemba.

Hata hivyo, tumetoa maelekezo kwamba, kama Walimu wameshakwenda kuripoti, DOs wa Wilaya hizo wawapokee na kuwapangia kazi; na Wizara yangu na Ofisi ya Waziri Mkuu TAMISEMI, tutashauriana juu ya hatua za kuchukua.

**MHE. ESTHER K. NYAWAZWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika majibu ya Mheshimiwa Waziri, alilihakikishia Bunge hili kwamba, watalipa madeni ya maji na umeme.

Shule ya Wasichana ya Bwiru tarehe 18 Julai, walitembelewa na Mama Kikwete, wamelalamika kuwa na deni la maji ambalo limefikia shilingi 11,707,770.10. Je, kama Waziri amesema kwamba ataanza kulipa mwezi wa nane; kwa sababu ni Serikali moja; kwa nini Waziri asiongee na Waziri wa Maji ili awarudishie wale watoto maji na wao Serikali kwa Serikali waendelee kulipana deni hilo?

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana dada yangu Mheshimiwa Nyawazwa, kwa swali hili.

Nimeeleza nilipokuwa najibu hapa kwamba, pamoja na kwamba, fedha zitatoka kwa ajili ya kulipa mwezi wa nane, tutashauriana na Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini ili umeme huo urudishwe mara moja.

**MWENYEKITI:** Watafanya kazi hiyo ndani ya Serikali ili maji yarudi na umeme urudi.

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itahakikisha kwamba, maji yanarudi mara moja.

**MHE. GRACE S. KIWELU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunamwomba Mheshimiwa Waziri, atupe hatima ya wanafunzi waliokuwa wakiishi Mabibo Hostel wa Chuo cha Ardhi, walioondolewa katika Hostel hizo wakati wale wenzao wa Chuo Kikuu cha Tiba Muhimbili waliondolewa na kupewa Hostel za Chole.

Sasa nini hatima ya Wanafunzi wa Chuo hicho cha Ardhi?

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba, Chuo cha Ardhi kilipokuwa Chuo Kikuu kinachojitegemea chenyewe, kilikuwa na wajibu wa kutafuta utaratibu kwa ajili ya wanafunzi wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wengi wa wanafunzi hawa, wanapewa mkopo na Serikali kwa ajili ya kutafuta malazi na chakula chao. Kwa hiyo, Chuo Kikuu cha Ardhi, pamoja na Bodi ya Mikopo, itawawezesha wanafunzi hawa ili waweze kujitafutia utaratibu wa kuishi.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. La kwangu ni kuhusu migogoro au migomo katika Vyuo vya Elimu ya Juu.

Namshukuru Waziri kwa jibu lake kuhusu University of Dodoma, lakini nilikuwa na swali kuhusu wanafunzi waliofukuzwa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na hawa ni wale Viongozi na mara zote kunapotokea migomo katika Vyuo vya Elimu ya Juu; hata kama kuna sababu za msingi; Viongozi wa Wanafunzi wamekuwa ndiyo wanaotolewa kafara. Nilitaka kujua sasa yule Rais wa DARUSO na wenzake hatima yao ni nini; kwa sababu mpaka leo bado hawajasikilizwa na wako nje; ukizingatia kwamba walikuwa mwaka wa mwisho kwa hiyo tayari Serikali imeshapoteza fedha nyingi kwa ajili yao?

Naomba Mheshimiwa Waziri, atoe ufafanuzi.

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wanafunzi hawa wana kesi iliyoko Mahakamani hivi sasa; na kwa sababu kesi hiyo ni kesi ya jinai, mpaka kesi itakapokwisha ndiyo wataweza kurudi chuoni.

**MHE. SAID A. ARFI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naomba na mimi nipate maelezo kutokana na kauli ya Mheshimiwa Waziri kwamba, malimbikizo na madeni ya Walimu yatalipwa mara baada ya kikao cha bajeti mwezi wa nane, lakini sioni mahali popote katika Vote 46 na pia katika Vote 56 ya Tawala za Mikoa; je, Serikali ina utaratibu mwingine wa kutumia fedha bila kuidhinishwa na Bunge?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Arfi, mimi nilisikia kwamba, ziko Hazina, lakini Mheshimiwa Waziri anaweza kujibu zaidi.

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha hizi zimetengwa na Serikali kwenye Vote ya Hazina na uhakiki wa Ofisi ya Controller and Auditor General ukishamalizika, Walimu hawa watalipwa fedha kutoka Hazina.

**MHE. MOHAMED H. MISSANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, sina tatizo na Mheshimiwa Prof. Maghembe na dada yangu Mwantumu Mahiza, lakini tatizo langu ni utendaji wa ovyo kwenye Baraza la Mitihani.

Majibu ya Waheshimiwa Mawaziri wawili; yaani Waziri wa Utumishi na Mheshimiwa Mwantumu Mahiza, hayakutosheleza haja yangu kwamba, kutatua tatizo la kuvuja kwa mitihani kwa kufukuza watu maelfu kwa maelfu kama siyo mamia hiyo siyo solution.

Haiwezekani watu wote katika waliofukuzwa, list ninayo hapa, wapo walinzi, madereva na hata wakata majani. Sasa huwezi kutibu donda ...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Missanga, usijadili ila uliza ni nini unachotaka.

**MHE. MOHAMED H. MISSANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sawa. Hatuwezi kufanya hivyo kwa kuwafukuza watu wengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu maelezo hayatoshelezi, pamoja na msaada wa Mheshimiwa Mporogomyi kumsaidia dada yake wanayetoka mahali pamoja, halafu ni mwanafunzi wake, bado mimi nakusudia kama hakuna maelezo mengine, Tume ya Bunge iende ikaangalie yote hayo. Pamoja na kumsafisha huyo anayetaka kusafishwa, lakini kubwa wabaini nini tatizo la kuvuja mitihani kila mara. Kwa hiyo, yeye ana majibu mengine au kama hana majibu mengine, mimi naendelea na utaratibu wangu wa kuleta hoja binafsi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa kifupi sana kwa sababu ya muda, tunataka angalau wafikie wengi.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya Mheshimiwa Mbunge tumeizingatia. Katibu Mtendaji wa Baraza la Mitihani hakuwa na utashi wa kuweza

kukaidi Agizo la Mheshimiwa Rais. Malalamiko ndani ya Baraza la Mitihani ni makubwa. Waheshimiwa Wabunge ninyi wenyewe mmekuwa mkihimiza tufanye maboresho. Baada ya Tume iliyosimamiwa na Prof. Maboko, mapendekezo yake yalifikishwa ngazi za juu na jawabu ni kusafisha. Katika kusafisha, utafagia kila kona. Kama hoja ni Katibu Mtendaji aondoke, utafika wakati wake, kwa hoja zitakazoonekana na kama mapendekezo, lakini siyo kumwondoa tu bila sababu za msingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamwomba Mheshimiwa Mbunge awe na subira, bado kazi inaendelea ndani ya Baraza la Mitihani na kamwe hatumlindi mtu, haki itatendeka. *(Makofi)*

**MHE. PROF. FEETHAM P. BANYIKWA:** Mheshimiwa Mwenykiti, ahsante kwa kuniruhusu niombe ufafanuzi. Katika mchango wangu, nilisema ya kwamba, kuna *High Schools* mbili zote ziko karibu na Makao Makuu ya Wilaya ya Ngara. Tarafa za Murusagamba na Tarafa ya Rulenge hawana *High School* hata moja. Naomba ufafanuzi ni lini Serikali Kuu itafanya utaratibu wa kuhakikisha kwamba Murusagamba wanapata *High School* na Tarafa ya Rulenge wanapata *High School* kwa sababu kuna malalamiko makubwa sana kuhusu Tarafa hizo mbili?

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba, jana tulipokrea maombi hayo. Napenda kumshukuru Mheshimiwa Prof. Feetham Banyikwa, kwa hoja yake. Mheshimiwa anaelewa utaratibu ambao tunajenga shule za sekondari na Serikali itashirikiana na Halmashauri yake, kuhakikisha kwamba, shule hizo kama wananchi wana utashi nazo, basi zitajengwa na zitakuwa tayari kwa matumizi.

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Katika mchango wangu wa maandishi, nilitaka kufahamu ni lini Wizara itatupatia walimu katika Shule yetu ya Busami, Kata ya Bunyambo, Wilaya ya Kibondo, yenye wanafunzi zaidi ya 50, Kidato cha Kwanza na cha Pili, ambapo shule hiyo ina mwalimu mmoja tu, Mwalimu Severino Mathew Matanyi; sasa nataka nijue ni lini Shule hiyo ya Busami itapelekewa walimu?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika orodha ya walimu ambao tumepokea, Shule zote za Kata zimepangiwa walimu wanne wanne, tunaamini watatosheleza. Hata hivyo, mazingira, jiografia na sarakasi huko si njema. Naomba mambo mengine tusiyapeleke kwenye vyombo vya habari, watoto wanatishika.

**MHE. CHARLES N. MWERA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwenye mchango wangu niliuliza kwamba, Serikali imekuwa ikigharimia wanafunzi wanaosoma sekondari wanaotoka katika familia duni, wenye vipato vidogo. Katika Wilaya yangu, wanafunzi ambao wako sekondari hawajalipiwa karo yao; ni lini watalipiwa?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiri kwamba, fedha hizo

zilichelewa kupelekwa. Tumepeleka hivi sasa kwa ajili ya Kidato cha Nne na Kidato cha Sita na mgawanyo wa hizo fedha umeelekezwa. Tumetoa maelekezo mara kadhaa na leo narudia kwamba, wanafunzi wote wanaolelewa na Serikali, hawatafukuzwa shule na nawaomba Wakuu wa Shule wanisikie, wanielewe, wasiwashike michango na wasiwabughudhi. *(Makofi)*

**MHE. DKT. ALI TARAB ALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, TENET sasa hivi ina miaka 10 na ipo katika juhudi ya kuunganisha mtandao wa Vyuo Vikuu vya Tanzania, pamoja na Taasisi za Utafiti katika Mtandao wa Kimataifa kupitia SICOM. Wizara imekuwa ikiisusia, haitoi ushirikiano kwa TENET na *Trust* ya TENET kwa nini?

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UIFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, napenda nimshukuru Mheshimiwa Dkt. Ali Tarab Ali, kwa mchango wake, jana tulimsikia. Jana hiyo hiyo Mheshimiwa Rais, alikuwa anauzindua ule Mkongo, *Marine Cable,* iliyoingia pale ya SEACOM. Shule zote pamoja na Vyuo Vikuu, vimefurahia sana *opportunity* hii imekuja na vitashirikiana na TENET kuhakikisha kwamba, tunatumia Mkongo huu ambao umefika. Sasa leo hii wakuu wetu wa vyuo wanakutana kuangalia ni jinsi gani wataunganisha *system* ambazo wanazo kwenye vyuo vyao ili kuweza kutumia rasilimali kama maabara kwa pamoja.

**MHE. LUCY F. OWENYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Elimu, imehamishia shughuli zote za usimamizi na uendeshaji wa shule za sekondari kwenda TAMISEMI. Tunaelewa kabisa, TAMISEMI wana shughuli nyingi sana na pia hawana wataalam, wataalam wako kwenye Wizara ya Elimu, ambako ndio pangekuwa pazuri pa kufanyia shughuli zote za sekondari. Swali langu; je, Serikali haioni kwamba inahamisha matatizo kutoka Wizara moja kwenda nyingine?

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Elimu, inatatua matatizo ambayo yanawakabili walimu kwa kukaa mbali na mamlaka ya maamuzi. Wataalam tulionao ni Walimu, Viongozi wa Wilaya ya Elimu, Viongozi wa Elimu wa Mikoa na kutakuwa na Viongozi katika Ofisi ya Waziri Mkuu na katika Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufindi. Kila Wizara ina kazi yake na kila ngazi ya utawala imepangiwa kazi vizuri, shule za msingi zinaenda vizuri, hakuna shaka na shule za sekondari zitaendeshwa vizuri.

**MWENYEKITI:** Wacha tujaribu! Mheshimiwa Dkt. Mongella, naomba kwa kifupi sana.

**MHE. BALOZI DKT. GETRUDE I. MONGELLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi mwalimu mstaafu, UTS6390. Nauliza kwa nini Waziri na Naibu Waziri hawakusikiliza ushauri wangu ya kwamba, Ukerewe Mawaziri hawafiki na watu wengine hawafiki. Walimu wa kutoka sehemu nyingine kama Kilimanjaro na mahali pengine, hawawezi kumudu mazingira. Nimewapa ushauri mzuri wa kukifanya Chuo cha Mrutunguru kilichojengwa mwaka 1952 kiwe Chuo Special kwa kutoa walimu wanaotoka katika sehemu za maji, ambako wanamudu mazingira na waongeze mkondo

wa sekondari. Kwa nini hawakunijibu pamoja na uzoefu wangu wa kuwa Mkaguzi Kanda ya Mashariki kuwa Mkuza Mitaala na Mwalimu wa Walimu? *(Makofi/Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU. B. MAHIZA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, tumepokea ushauri wake na utafanyiwa kazi. Katika kuboresha masuala ya maeneo ya Vivuko, katika bajeti ya wenzetu TAMISEMI, wamepanga kununua boti. Mimi mwenyewe nilikuwa tayari kwenda, aliniambia nisubiri wakati ukifika ataniambia. Mama Mkwe niambie kama tayari twende wote? *(Kicheko)*

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kupata nafasi na mimi niweze kupata ufafanuzi kutoka kwa Mheshimiwa Waziri. Swali langu au ufafanuzi wangu hautofautiani sana na jambo ambalo ametoka kulizungumza Mheshimiwa Dkt. Mongella.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi watoto wanaomaliza Vyuo vya Ualimu au vijana wanaomaliza Vyuo vya Ualimu wana umri wa miaka kati ya 18 na 20, labda na 22. Wakimaliza Vyuo, unaweza ukakuta mtoto anatoka Mkoa wa Rukwa anapangiwa kazi Mara, mtoto anatoka Mkoa wa Kagera anapangiwa kazi Lindi. Sasa inapokuja wakati wa likizo inakuwa tatizo. Pia wanapokwenda kule, inawachukua muda mrefu hata kupata mshahara, wanaishi kwenye mazingira ya kigeni na kwenye hali ngumu sana. Hivi kwa nini Wizara isione kwamba ni busara sasa watoto hawa wakapangwa kikanda kwenye maeneo ambayo wameyazoea na ikawa pia nafuu kwa Wizara hata kulipa nauli na mambo mengine kwa vijana hawa wakati wanakwenda likizo?

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, niseme tu kwamba, namshukuru Mheshimiwa Zambi, kwa suala lake. Najua kwamba, vijana hawa bado wadogo lakini sote sisi tumesoma na tulipokuwa tunasoma, tuliondoka kutoka Mwanza kuja Dodoma, kutoka Mbeya kwenda Mtwara na pia kutoka maeneo mengine mbalimbali. Mimi nilitoka Upare mpaka Tosamaganga na nilikuwa mdogo kuliko hawa Walimu na nia ilikuwa ni kujenga umoja wa kitaifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutaendelea kuhimiza kujenga umoja wa kitaifa kwa kadiri tunavyoweza. Hata hivyo tumezingatia kwa kiasi kikubwa, mawazo haya ambayo yamependekezwa na tutaendelea kuzungumza suala hili ili tuone tunafanyaje kwa lengo la kuongeza tija na kuhakikisha kwamba, Walimu wanakaa shuleni.

**MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nikichangia nilizungumza tena kwa masikitiko sana, namna ambavyo mafundi hawapati nafasi na heshima yao katika nchi hii. Nikasema kuhusu hawa watu waliomaliza FTC, wakafanya *Diploma in Technical Education*, baadae wakaenda kufanya *Advanced Diploma in Engineering* na baadae wengine wakafikia mpaka kwenye level ya *Degree*. Kwa nini Waraka Na. 11 wa Maendeleo ya Utumishi wa Mwaka 2002 umewaondoa hawa kuwa *Education Officers* na hivyo kuwazuia kupata haki ya kupandishwa madaraja na vyeo?

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeupokea mchango wa Mheshimiwa George Simbachawene na tutaufanyia kazi, tuone ni jinsi gani tunaweza kuwasaidia hawa Walimu ili kusaidia kuboresha elimu ya ufundi katika shule zetu.

**MWENYEKITI**: Mimi nilikuwa nashawishika kwamba, Mheshimiwa Simbachawene, ungetumia Kanuni ya 34 ya *Petition.* Watu wanasaini *documents* zako unaleta, Mbunge mmoja anasoma hapa, lingekuwa *dealt* kwa utaratibu. Soma Kanuni ya 34, *petition* katika Bunge. Mheshimiwa Kijiko.

**MHE. FELIX N. KIJIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Wakati nikichangia kimaandishi, nilieleza hali ambayo inawakabili wanafunzi wa Shule za Sekondari katika Mkoa wa Kigoma na hususan katika Wilaya ya Kibondo. Nilisema kuwa, *standard* ya elimu ambayo inapatikana kwa wanafunzi na *performance* ya matokeo ya mitihani inashuka kutokana na wanafunzi kutopata muda wa kusoma, hali ambayo inatokana na mkoa mzima kutokuwa na umeme, nikatoa mapendekezo kwamba, kwa shule nilizozitaja, Wizara inajipanga vipi kutoa *generators* angalau wanafunzi wapate muda wa kusoma usiku, kwa sababu ikifika 12 hawawezi kusoma wanakwenda kulala? Naomba kupata jibu.

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani ninaelewa kabisa anchoeleza Mheshimiwa Felix Kijiko na juhudi za Serikali za kupeleka umeme Kigoma zitaelezwa na Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini kesho katika hotuba yake. Kwa hiyo, tutakuwa na muda wa kulijadili na kuona ni jinsi gani linatatuliwa.

**MHE. ROSEMARY K. KIRIGINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuuliza ripoti kuu ya uchunguzi dhidi ya Watumishi kama ilivyoelezewa na Ofisi ya Rais, Menejementi ya Utumishi wa Umma na kama ilivyoandikwa kwenye Taarifa ya CAG imebainisha kwamba, Wizara hii iliipatisha Serikali hasara ya shilingi 1,413,000,000, kutokana na kulipa watumishi hewa. Nilitegemea Waziri wakati anafanya majumuisho, angeonesha *concern* yake lakini hakufanya hivyo. Naomba maelezo juu ya hili.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJEMENTI YA UTUMISHI WA UMMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili sasa hivi liko kwa wenzetu wa PCCB wanalifanyia kazi ili hatua zinazostahili ziweze kuchukuliwa.

**MHE. MICHAEL L. LAIZER:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nilipochangia kimaandishi, nilisema Longido ina mazingira magumu na jiografia ngumu. Niliomba gari kwa ajili ya ukaguzi wa shule, kwa sababu tatizo kubwa kule ni ukaguzi wa shule, niliomba katika magari yaliyopatikana Longido ihesabiwe. Sijui Mheshimiwa Waziri atanipa jibu gani?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba,

tunazo takwimu na taarifa za Wilaya zote ambazo hazina magari ya ukaguzi, tutazipatia tunaomba watupitishie bajeti.

**MWENYEKITI:** Hata mimi bila shaka nitapata?

**MHE. RAMADHANI A. MANENO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru. Wakati nachangia asubuhi, nilisema kuhusu Walimu wanaofundisha Watoto Maalum kwa maana ya wenye ulemavu walioko katika kituo kile cha Chalinze, wanazunguka kwenye Shule za vijijini, lakini wakati wanazungukia kuwatafuta hawa Watoto Walemavu na kuwapeleka kwenye kituo kwa ajili ya kuwafundisha, hawana usafiri wa aina yoyote ile. Kwa kuwa katika mchango wangu nimesema kuwa bajeti ni finyu hivyo; suala la gari ni tatizo; je, hata pikipiki haiwezekani? Nilikuwa naomba ufafanuzi.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, napenda kumuarifu Mheshimiwa Mbunge wa Chalinze kwamba, Walimu wale wamepatiwa pikipiki mbili na wanapatiwa posho. (*Makofi*)

**MHE. DKT. ZAINAB A. GAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza, Naibu Waziri nakushukuru kwa kunielimisha tofauti ya MUKEJA na Mpango wa Elimu kwa waliokosa Sekondari. Swali langu ni Mpango wa Elimu kwa Waliokosa Sekondari, watoto hawa wengi waliokosa Sekondari si kwamba walifeli ni kwa sababu shule zilikuwa hazitoshi na wazazi wao walikuwa hawana uwezo wa kulipa ada. Sasa hivi mpangu huu umewapa matumaini ya kwenda kusoma, kwa bahati mbaya umaskini ule bado unaendelea, ada ni ghali (Shilingi 240, 000), kwa maana ya Kitengo cha Elimu ya Watu Wazima. Je, Mheshimiwa Waziri yuko tayari kama ile Elimu ya Waliokosa kwa Shule za Msingi waliwapunguzia; kwa nini wasiwapunguzie hawa ili hata sisi Wabunge tuwasaidie kusoma kwa kuwalipia?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, naomba nimjibu Mheshimiwa Dkt. Zainab Gama, kama ifiuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijana wale ni kundi ambalo tunaliita MESKWA. Wanasoma kwa kutumia moduli; moduli moja ni Shilingi 10,000, kwa kuwa wako kwenye kikundi si lazima kila mmoja anunue moduli zote, wanaweza wakachangishana wakanunua. Hatua ya kwanza ni shilingi 70,000, ndiyo moduli zake maana hizo zitakuwa ni moduli saba. Kwa hiyo, wanaweza wakanunua kidogokidogo kwa kuchangishana na hivyo wakamaliza, sio lazima wanunue kozi nzima kwa siku moja.

**MHE. YAHYA KASSIM ISSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilikuwa napenda kujua kuhusu Chuo Kikuu cha Tunguu, ambapo kipindi hiki cha kwenda *field*, wengi wao walishindwa kutokana na upatikanaji wa fedha. Hivi karibuni nilipata taarifa kwamba, mmepeleka Wajumbe wawili ili kuzungumza na wanachuo wale. Kwa hiyo,

ninapenda Mheshimiwa Waziri anieleze ili wanachuo wajue msimamo ukoje kuhusu suala hilo.

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumjibu rafiki yangu, Mheshimiwa Yahya Kassim Issa, suala lake kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwanzoni kulikuwa na utata kidogo kuhusu wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Zanzibar pale Tunguu kwa fikra kwamba, wale wanafunzi watakuwa wameshamaliza masomo yao ya Sheria. Baada ya kupata maelekezo kutoka kwa viongozi wetu, tulituma timu pale ikaenda kuangalia Mtaala wenyewe ulivyo na utaratibu wa mafunzo kabla ya kuhitimu na kukuta kwamba, masomo yale yanafanywa ndani ya kozi ile ya Sheria katika Chuo kile. Kwa hiyo, wanafunzi wale watapewa mkopo kwa ajili ya kufanya kazi hiyo.

**MHE. PROF. RAPHAEL B. MWAYOSI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Sina shida ya kumwibia mshahara Profesa mwenzangu mstaarabu, lakini niliposoma ukurasa wa 91, nililazimika kumwandikia kutaka kujua kama Ludewa tutaanza kujengewa Chuo cha Ufundi mwaka huu kama alivyoahidi. Ahsante.

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba, Profesa Mwalyosi, Mbunge wa Ludewa, ameleta suala hili mara nyingi na kazi ya ujenzi wa Chuo hicho utaanza, baada ya eneo lile kufanyiwa *Survey* na utaanza mwaka huu.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu Kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 1002 – *Finance and Accounts ……………………………… Sh.* 625,455,800

*(Kifungu Kilichotajwa hapo juu Kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

*Kif. 1003 – Policy and Planning ………………………………… Sh.* 5,760,926,650

**MHE. SUZAN A. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu kidogo 210500 - *Personal Allowances in Kind*. Nilikuwa naomba ufafanuzi kuhusu kifungu hicho, kutokana na hali halisi kwamba, mwaka jana walikuwa wamepata shilingi 6 250,000, lakini mwaka huu ni zaidi ya shilingi bilioni tatu. Kwa hiyo, naomba maelezo ni kitu gani kimetokea hasa ukizingatia kwamba katika mishahara iko vilevile? Nilikuwa naomba maelezo ni kwa nini zimeongezeka kiasi hicho?

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu hiki kimepanda kwa ajili ya posho za nyumba za Wahadhiri wa Vyuo Vikuu na posho za nyumba za Watumishi wa Idara wenye stahili.

*(Kifungu Kilichotajwa hapo juu Kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 1004 – *Internal Audit Unit ……………………………………… Sh.* 274,524,900

**MHE. LUCAS L. SELELII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Kifungu hicho 1004, kifungu kidogo cha 210100 - *Basic Salaries Pensionable Posts*. Hizi pesa zimewekwa za mishahara, mimi naona kama hazitoshi. Ninavyoelewa mimi, Internal Audit sijui ndiyo hiyo hiyo ambayo imewekwa na Mkaguzi Mkuu au Mkaguzi Mkuu yuko kwenye kifungu gani kingine? Nimeangalia kwenye vifungu vingine vyote, Mkaguzi Mkuu simwoni; yeye amewekewa fungu gani?

**MWENYEKITI:** Mkaguzi Mkuu au *Internal Auditor?*

**MHE. LUCAS L. SELELII:** Kuna hiki kifungu cha *Internal Auditor*.

**MWENYEKITI:** Kifungu cha *Internal Auditor*, sasa wewe unauliza nani?

**MHE. LUCAS L. SELELII** Mkaguzi Mkuu, haonekani yeye anapata mshahara wapi?

**MWENYEKITI:** Yaani Mkaguzi Mkuu wa ndani?

**MHE. LUCAS L. SELELII:** Mkaguzi Mkuu wa Serikali.

**MWENYEKITI:** CAG?

**MHE. LUCAS L. SELELII:** Mkaguzi Mkuu wa Shule.

**MWENYEKITI:** Hapana hii ni *Internal Audit.* Mheshimiwa Waziri, hiki kifungu ni cha kufanyia nini?

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *Inspectors* wa shule wana mishahara yao na matumizi yao yako chini ya Ukaguzi wa Shule. Hii ni *inspectorate* ambayo ni 2002, haihusiki kabisa; ni ya *Internal Audit* pale Wizara.

*(Kifungu Kilichotajwa hapo juu Kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 1005 – *Procurement Management Unit ………………………….. Sh.* 645,178,200

**MHE. SUZAN A. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu kidogo cha 210100 - *Basic Salaries Pensionable Posts*. Nilikuwa naomba maelezo kutoka kwa

Waziri; kwa nini mishahara ya watu hawa wa Kitengo cha *Procurement* imeongezeka kwa zaidi ya shilingi milioni 456 ulinganisha na mwaka jana?

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu hiki kimejuisha mishahaara ya Watumishi wa Idara ya Ukaguzi wa Ndani na Mawasiliano na Habari na nyongeza za mishahara yao.

**MWENYEKITI:** Haiwezakani, kwa sababu Wakaguzi wa Ndani ndiyo kifungu tulichomaliza. Sasa hiki hapa ni *Procurement Management Unit?* Mheshimiwa Waziri wa Nchi.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJEMENTI YA UTUMISHI WA UMMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama walivyosema kwamba, mwaka huu *GFS Code* nyingi zimebadilika. Kwa hiyo, baadhi ya vifungu havikuweza ku-*pick* ilipokuwa inatakiwa. Mfano, ukiangalia hapa *Information, Education and Communication*, mwaka jana mshahara ulikuwa shilingi milioni 19

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, tukifika kwenye vifungu tunazungumzia fungu linalohusika. Hii ni 1005.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJEMENTI YA UTUMISHI WA UMMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kusema kwa nini imeongezeka kule juu; imetoka huku chini imekeenda juu, ndiyo maana akasema mishahara hii imejumuisha hao, ndiyo maana huku chini imepungua imezidi kule juu.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 1006 – *Information, Education and Communication …………* Sh. 58,773,000
Kif. 2001 – *Commissioner for Education ……………………………* Sh.7,156,363,900
Kif. 2002 – *Inspectorate……………………………….*Sh.12,096,007,820
Kif. 2003 – *UNESCO Commission……………………………..*Sh. 0
Kif. 3001 – *Basic Education………………………………………..*Sh. 6,976,864,600
Kif. 3002 – *Adult Education and Non Formal Education…………………*Sh.828,891,700

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 4001 – *Secondary Education……………………..*Sh.2,306,374,200

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 221000 - *Travel in Country*. Nilikuwa naangalia, ukianzia mwaka juzi ilikuwa ni shilingi bilioni nne, mwaka jana ikaenda kwenye shilingi bilioni mbili na mwaka huu inakuja shilingi bilioni moja. Sasa nadhani mahitaji yanaongezeka, lakini hizi pesa zimeendelea kupungua sana. Pengine Mheshimiwa Waziri atufafanulie; wataendelea kufanya kazi namna gani wakati pesa zinazidi kupungua kila mwaka?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa, umekipata kifungu chenyewe?

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Ndiyo nimekipata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha hizi zimepungua kwa sababu fedha za safari za Walimu zimekasimiwa kwenye Halmashauri zilizopo, ambapo shule zilipo. Kwa hiyo, fedha hizo ziko TAMISEMI.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 5001 – *Teacher Education* … … …Sh. 47,052,871,830

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu kidogo cha 220100 - *Offices and General Supplies and Services.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaelewa kwamba, sehemu ya Ualimu ni muhimu sana. Ukiangalia utaona kwamba, mwaka jana walikuwa na shilingi 5,000,000,000, lakini mwaka huu wamepewa shilingi 20,000,000,000 na kifungu hiki kinahusiana hasa na huduma kama za maji na umeme. Nilikuwa naomba kupata ufafanuzi ni kwa nini imepungua kiasi hiki na je, Kitengo hiki kitafanyaje kazi zake?

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu hiki fedha zimeshuka kwa kuwa zimegawanyika katika vifungu vipya mbalimbali ambavyo ni 2220700, 221200, 221300 na 229090.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 7001 – *Higher Education* … … Sh. 262,957,674,500

**MHE. DKT. ALI TARAB ALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na maombi tangu mwaka jana ya kwamba ...

**MWENYEKITI:** Kifungu gani?

**MHE. DKT. ALI TARAB ALI:** *Subvote 7002, item* 210100 - *Basic Salaries – Pensionable Posts*. Chuo Kikuu Huria kinalipa Walimu wa muda kupitia OC. Kulikuwa na maombi toka mwaka jana kwamba, walipwe fedha zao kupitia PE na tangu mwaka jana shughuli hiyo ilikuwa inashughulikiwa na Hazina ili wapate ufumbuzi. Je, kuna tatizo gani na ufumbuzi ukoje?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Ali Tarab Ali, hilo ni swali la kisera lili-*fit* kule kwenye mshahara wa Waziri hapa hapana.

**MHE. CHARLES N. KEENJA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *item* 270300 inahusu ruzuku kwa *academic institutions.*

**MWENYEKITI:** Tutajie *item* yenyewe sisi hatujaiona.

**CHARLES N. KEENJA:** *Item* 270300, inahusu ruzuku kwenda kwenye *academic institutions.* Chuo Kikuu cha Tiba na Sayansi za Afya, kilichukuwa eneo kubwa sana lililokuwa la KABIMITA na wakaahidi kulipa fidia kwa wananchi waliokuwa katika eneo lile, ilikuwa ni matatizo kulipata lile eneo, wananchi walikuwa wabishi kweli kweli ilibidi Waziri wa Ardhi aende kushughulikia suala hili. Je, fungu hili ndilo litakalotumika kulipa fidia wananchi wale na kama siyo ni fungu gani ambalo litatumika kwa ajili hiyo?

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba, fungu hili ni kwa ajili ya ruzuku kwa Vyuo Vikuu vyote vya Umma na sehemu ya fedha hizi, itaanza malipo ya mwanzo ya fidia kwa wananchi ambao wako kwenye eneo hilo la Mlonganzila.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 7002 - *Technical and Vocational Training Division* ............ Sh. 10,304,966,500

**MHE. SAID A. ARFI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu 7002, kifungu kidogo 221000 - Safari za Ndani. Mwaka uliopita, walikuwa wamepewa shilingi 8,374,012,900, wameomba shilingi 315,113,400, kiwango hiki kimepungua sana kutoka shilingi bilioni nane mpaka shilingi 300,000,000 na Vyuo vya VETA vinaendelea kupanuka. Je, kuna maelezo gani kuhusu tofauti hii?

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba, fedha iliyo chini ya kifungu hiki imepungua kwa kuwa Taasisi zilizopo chini ya Idara hii zimepewa bajeti yake moja kwa moja na zitapata ruzuku chini ya vifungu 270300, 270800. Taasisi hizo ni Mwalimu Nyerere *Academy* na Arusha *Technical College* na Baraza la Taifa la Ufundi NACTE.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**MIPANGO YA MAENDELEO**

Kif. 1001 - *Administration and General* … … Sh. 446,448,000

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 1003 - *Policy and Planning* … … Sh. 18,664,400,900

**MHE. DKT. ZAINAB A. GAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Subvote 1003, item 4397 - Support VETA.

Naomba anisaidie Mheshimiwa Waziri; hizi fedha pia zitasaidia ku-*support* ujenzi wa VETA ya Kanda ambayo mmechukua eneo kubwa pale Kibaha?

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hili swali zuri. Ujenzi wa Chuo cha Mkoa cha VETA kwa Mkoa wa Pwani, kimeanza kujengwa tayari kwa fedha ya msaada kutoka Serikali ya Korea ya Kusini. Kwa hiyo, siyo sehemu ya fedha hizi.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu kidogo 4371 - *Rehabilitation of Schools and Colleges.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni wazi kwamba, sasa hivi wamegatua madaraka ya Shule za Sekondari na za msingi kwenda TAMISEMI. Nilikuwa naomba kujua ni kwa nini sasa wanapewa fedha kwa ajili ya ku-*rehabilitate* shule wakati shule tayari zimekwenda TAMISEMI.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Naibu Waziri. Kwa mara ya kwanza, nimesikia neno kugatua leo. (*Makofi/Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha hizi ni kwa ajili ya kukarabati Shule za Mazoezi, ambazo ziko chini ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi.

**MHE. MOHAMED H. MISSANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu 1003, Subvote 4312. Katika mchango wangu, nilielezea kwamba, wenzetu kule SMZ wanao Walimu wa ziada takriban 3000 na nikasema kwamba pengine wangekuja huku.

**MWENYEKITI:** Hebu tusomee kifungu chenyewe kinasemaje?

**MHE. MOHAMED H. MISSANGA:** Kinasema *Education Sector Development Program* katika mambo ya *Policy and Planning.*

**MWENYEKITI:** Endelea sasa.

**MHE. MOHAMED H. MISSANGA:** Nilisema Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, wanao Walimu wa ziada takriban 3000 na iko tayari kuwaruhusu waje huku; na kwa kuzingatia tatizo kubwa la upungufu wa Walimu katika Shule za Msingi na Sekondari haingekuwa busara tukawaleta wenzetu ili kuja kujaza mapengo yaliyopo?

**MWENYEKITI:** Mwenyekiti wangu wewe. Hili swali ni zuri sana la kisera, ungeliulizia kule ingekuwa vizuri sana, lakini hapa hebu jaribu kujibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli tunatambua ziada ya Walimu Zanzibar, hata Mheshimiwa Waziri tumewahi kufanya mazungumzo naye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo lililopo, mahitaji makubwa ya Walimu tulionayo ni vijijini na katika mazungumzo wenzetu waliweka masharti. Kwa hiyo, tumeacha wazi pale ambapo Halmashauri zitatangaza nafasi za kazi, zikieleza kwamba zinahitaji Walimu, wenzetu walioko Zanzibar wako huru kuomba hizo nafasi kupitia Halmashauri.

**MWENYEKITI:** Hizi fedha zilizopo ni za nini?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA):** Kifungu hicho kimewekwa kwenye *Teachers Training Colleges*, maana kule nako wana mambo yao, ambayo yanahitaji kuboresha Wakufunzi, Miundombinu na kadhalika.

**MWENYEKITI:** Kwa hiyo, kama mkikuta kuna swali hali-*fit* kwenye vifungu vyote, ndio tunabana kwa mshahara wa Waziri, kwa sababu pale ni *very open*, huku kidogo kunabanwa na fedha zinazostahili.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 2001 - *Commissioner for Education* … … Sh. 1,045,299,000

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. *Item* 5492 - AIDS Education in Schools. Nimeona miaka miwili iliyopita mfululizo, walikuwa wanatengewa fedha na bahati mbaya au nzuri zilikuwa ni *forex*. Mwaka huu naona *Zero;* sasa sijui suala la elimu ya UKIMWI mashuleni litakuwa linafanyika namna gani?

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha hizi zinatolewa na Benki ya Dunia kwenye kifungu hiki kwa ajili ya ...

**MWENYEKITI:** Hazipo mwaka huu?

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mwaka huu hawajasema watatoa shilingi ngapi. Kwa hiyo, hatuwezi kuweka fedha humu.

**MWENYEKITI:** Anasema shughuli hiyo imeishia, ndiyo swali? Mheshimiwa ndicho unachouliza? Sasa kama hivyo ndivyo, ndiyo imekwisha hivyo hakuna maelezo.

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI**: Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni *Development Budget*, lakini fedha za Matumizi ya Kawaida, zimepangwa kwenye kifungu husika.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lediana Mng'ong'o, kama kifungu ni hicho hicho, huruhusiwi kwa mujibu wa kanuni.

**MHE. LEDIANA M. MNG'ONG'O:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni hicho hicho.

**MWENYEKITI:** Huwezi kuuliza swali tena.

**MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *Subvote* 6571, navutiwa sana na hii *Support to Environment Improvement*; nilitaka tu kuelimishwa hasa fedha hizi zinatumika kufanya nini katika Sekta ya Mazingira? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa fedha hiyo umeiona?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA)**: Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha hizo ni kwa ajili ya kuboresha na kuhifadhi mazingira katika maeneo mbalimbali.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, nilishawatolea taarifa kwamba, tutaongeza dakika 30 kwa mujibu wa Kanuni ya 104(1), kwa hiyo sasa tunaongeza.

**MHE. MARGRETH A. MKANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. *Subvote* 4382 - *Support to Special Education*. Mwaka huu ni sifuri kabisa na Elimu Maalum ina mahitaji mengi; kwa nini imekuwa hivi?

**MWENYEKITI:** Mmeiona Mheshimiwa Waziri? Hii ni *Support to Special Education* ilikuwa 0.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ifahamike kwamba, Shule za Sekondari na Msingi hivi sasa tumezigatua na kule ndiko ambako sasa kumekwenda mzigo mkubwa. Kwa hiyo, sisi pale tumebaki na masuala ya sera na kununua vifaa vya kufundishia na visaidizi tu.

**MWENYEKITI:** Kwa hiyo, wale mliokuwa mnasema fedha zibaki huku basi wameshagatua mpaka huko chini. (*Makofi/Kicheko)*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 2001 - *Commissioner For Education* … … Sh.1,276,500,000

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 3001 - *Basic Education* .. … … Sh. 3,889,082,000

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *item* 6341 - *Improvement of Primary Education*. Naona zimepangwa shilingi 123,000,000. Nilikuwa najiuliza kwamba; Sekta ya Elimu ilivyo kubwa nchini halafu katika ku-*improve* hiyo elimu tunapanga shilingi 123,000,000 zitafanya kazi gani hizi?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kiasi hicho kidogo cha fedha kimebaki pale kwa ajili ya shule zetu na mipango yetu ya kimaendeleo ndani ya Wilaya. Baada ya hapo, ukarabati na masuala mengine yote, yameshagatuliwa ndani ya Wizara.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 4001 - *Secondary Education* … … ... Sh. 550,000,000

**MHE. SAID A. ARFI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na maelezo ya Mheshimiwa Waziri, juu ya ugatuaji na fedha kupelekwa katika Halmashauri zetu, lakini nilikuwa natazama *Secondary Education.*

**MWENYEKITI:** *Item?*

**MHE. SAID A. ARFI:** *Subvote* 4001, kifungu kidogo 4390 - *Secondary Education Development Programme* (SEDP). Kwamba, mwaka jana zilitengwa zaidi ya shilingi 3,000,000,000 kwa ajili ya Maendeleo ya Elimu ya Sekondari na safari hii wametenga shilingi 550,000,000 tena fedha za kigeni. Pamoja na kugatuliwa huku juu *Primary Education,* kuna fedha ambayo imetengwa na kuna ugatuaji huo unaendelea. Sasa katika Maendeleo ya Shule za Sekondari wakati hakuna fedha za ndani tunategemea fedha za wafadhili; je, haya Maendeleo ya Shule za Sekondari yatapatikana?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha hizi bado zimebaki, tunazo shule chache ambazo ni za mazoezi ndiyo ambazo tumebakishiwa. Naomba pole pole, tuelewe namna ugatuaji ulivyofanyika na tumeshatengeneza kijarida ambacho tutawapatia Waheshimiwa Wabunge kitawasaidia kuelewa nini kimefanyika.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 5001 - *Teacher Education* … … ... Sh. 533,368,000

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 7001 - *Higher Education* … … … Sh. 96,813,318,100

**MWENYEKITI:** Sasa hapa mna mtego, mkirudia kifungu kilichosemwa, atakayekuwa anasema wa kwanza. Haya Mheshimiwa Dkt. Ali Tarab Ali anza. Muwe *careful* kama ameulizia kifungu hicho hamruhusiwi.

**MHE. DKT. ALI TARAB ALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kifungu kidogo cha 4391 – MUCHS Support.

Nafikiri sahihi ingekuwa ni MUHAS Support. Suala langu ni kwamba, MUHAS haipati, naona hakuna fedha hata moja iliyowekwa hapa kwa maendeleo ya MUHAS, Chuo ambacho sasa hivi kinahitaji udahili zaidi wa Madaktari kwa vile tuko nyuma sana kwa idadi ya Madaktari nchini. Je, kwa nini Chuo hiki kisipate fedha ili kuweka miundombinu kidahili wanafunzi wengi zaidi tupate Madaktari wengi zaidi nchini? Ahsante sana.

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika eneo hili kuna matatizo ya uchapishaji. Fedha kwa ajili ya Chuo cha Tiba na Sayansi za Afya Muhimbili, ziko chini ya kifungu 6364, zimeandikwa Tanzania Cultural Fund. Hilo ni kosa la uchapaji namba moja. Sasa labda ningesema tu na hii nyingine ambayo iko hapa.

**MWENYEKITI:** Kwa hiyo, ina maana *page* yote mlitakiwa kuleta *addendum*?

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Kuna matatizo haya, maana pale pia kuna mahali pameandikwa IJMC Project Rehabilitation University. Haya ni makosa ya uchapaji, Mradi huu ni kwa ajili ya ukarabati wa Chuo cha Ushirika na Stadi za Biashara Moshi.

**MWENYEKITI:** Sasa ili kwenda vizuri, tumeshamjibu Mheshimiwa Dkt. Ali Tarab Ali kwamba, hilo ni kosa, iko *somewhere* huku. Haya tuje kwa Mheshimiwa Mpesya, maana bila ya kuleta kikaratasi lazima twende hivyo hivyo.

**MHE. BENSON M. MPESYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Vote ndogo ya 4398 - *Open University College*, fedha iliyotengwa ni shilingi 2,000,000,000. Nilitaka kujua tu kwamba, hizi fedha ni kwa ajili ya ujenzi wa Makao Makuu pale Kibaha?

**MWENYEKITI:** Umeiona Mheshimiwa Waziri nayo imekosewa hivyo hivyo.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI**: Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha hizo zimetengwa kwa ajili ya maendeleo ya kitaaluma kwa Chuo hicho.

**MHE. MASOLWA COSMAS MASOLWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Elimu ya Juu, item 2225, Mradi wa Taasisi ya Bahari ya Sayansi (*Institute of Marine Science Project).*

Je, fedha zilizotengwa zitatosha kukamilisha ujenzi huo ambao umeanza zamani na unasuasua sasa hivi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri umeiona?

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo hiki kinapewa fedha za ujenzi na Serikali hatua kwa hatua. Mwaka huu tumetenga shilingi bilioni 2.2 na fedha hizi ni sehemu ya kazi hiyo, sio kazi yote na mwaka kesho tutatenga fedha nyingine kwa kadiri zitakavyopatikana.

**MHE. ROSEMARY K. KIRIGINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, niko katika Subvote 4398 - Open University College.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka tu Waziri anipe maelezo.

**MWENYEKITI:** Tukija katika vifungu hivi, matumizi ya fedha zile hayawezi kuwa mawili au matatu, ni yale tu aliyoyasema Waziri kama ulimsikiliza basi huwezi kuruhusiwa.

**MHE. ROSEMARY K. KIRIGINI:** Ndiyo Mwenyekiti, lakini nataka ...

**MWENYEKITI:** Naomba usibishane na Kiti ndio utaratibu. Kama ni kifungu, niliwaeleza toka mwanzo kuwa akiuliza mwenzio kuhusu kifungu ujihadhari pale hatukupi nafasi, kwa sababu matumizi ya fedha ni yale tu, basi hayawezi kuwa zaidi ya hapo. Kwa hiyo, ndiyo maana tunakwenda kwa namna hiyo.

**MHE. ESTHERINA J. KILASI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, niko kifungu hicho hicho cha 4391, lakini maswali yako tofauti. Hakueleza ufafanuzi wa Chuo Kikuu cha Muhimbili kwamba, hizo fedha ambazo amesema zimekosewa kutaipiwa, zitakuwepo fedha za kukarabati Hosteli ya Muhimbili ambayo alipoitembelea aliona jinsi ilivyoharibika.

**MWENYEKITI:** Matumizi yake ni yale yale yaliyotajwa ingawa zimehama.

**MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilidhani *Cultural Fund* imehamishiwa kwenye Wizara yake, lakini ameshanijibu nashukuru ahsante.

**MHE. LEDIANA M. MNG'ONG'O:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kifungu kidogo 6389 - *Tanzania Education Authority*. Katika miaka miwili mfululizo, wamekuwa wanapata fedha zinazofanana na ukilinganisha kwamba kama zilikuwa ni za mwaka jana, lazima thamani yake ilikuwa imepungua; je, kuna sababu?

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamuelewa sana dada yangu, Mheshimiwa Lediana Mng'ong'o, *concern* yake kwa ajili ya Bajeti ya TEA. Bajeti hii haitoshi, lakini kwa mwaka huu ndio fedha ambazo tumepata na tunategemea kwamba, kwa michango iliyotoka hapa, basi Serikali mwaka kesho itaweza kutuongezea fedha kidogo katika kifungu hiki.

**MHE. ESTHER K. NYAWAZWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu kidogo 4376, naomba nieleweshwe hii NUFU-UDSM ni nini?

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, huu ni msaada kutoka Serikali ya Norway.

**MWENYEKITI:** NUFU yenyewe ndiyo nini?

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** *Norwegian Support.*

**MHE. DKT. ZAINAB A. GAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimefilisiwa.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 7002 - *Technical and Vocational Training Division* ........ Sh. 6,583,400,000

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *Item* 6359 - *National Council for Technical Examination* (NACTE Project).

Nilikuwa naona zimetengwa shilingi bilioni moja, lakini unaposoma NACTE Projects nilitaka Waziri atueleze ni Projects gani hizi?

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, imeandikwa NACTE Project, ambayo Mheshimiwa Godfrey Zambi aliitaja ni moja tu.

**MHE. LEDIANA M. MNG'ONG'O:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu 4381 - Mwalimu Nyerere Memorial Academy. Tatizo langu ni lile lile kama nililouliza kwanza; kwa nini miaka miwili mfululizo wanapata fedha zinazofanana? Kwa nini hawaongezewi wakati vitu vimepanda bei na wengine wanaongezewa? Naomba nieleweshwe.

**MWENYEKITI:** Kwamba, vitu vimepanda bei kwa nini?

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hata mimi namuelewa Mheshimiwa Lediana Mng'ong'o, lakini huu ndio uwezo wa Serikali. Kwa hiyo, fedha hizi zitatumika mwaka huu. Najua kwamba, Waziri

wa Fedha popote alipo, atakuwa amesikia. Kwa hiyo, labda mwaka kesho watatuongezea fedha kidogo.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

*(Bunge lilirudia)*

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI**: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa taarifa kwamba, Kamati ya Matumizi, imeyapitia Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, kwa mwaka 2009/2010, kifungu kwa kifungu na kuyapitisha bila ya mabadiliko. Hivyo, naomba kutoa taarifa kwamba, sasa Bunge lako Tukufu liyakubali Makadirio hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kwa Mwaka 2009/10 yalipitishwa na Bunge)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, napenda kuchukua nafasi hii, kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Manaibu wake wote wawili na Wataalamu wa Wizara hii, kwa kazi nzuri waliyoifanya. Tunachokiomba, kama Elimu ni Msingi wa Maendeleo, basi kila mtu ajitahidi kuongeza nguvu angalau tuweze kufikia kiwango cha elimu inayofaa.

Waheshimiwa Wabunge, wakati tuko kwenye vifungu, nilikuwa nashawishika kumwambia Mheshimiwa Simbachawene, atumie kifungu cha 34, kwa sababu kifungu hiki hakijatumika hata siku moja katika kukaa kwangu ndani ya Bunge hili.

Mheshimiwa Simbachawene, amefikiwa na watu fulani wenye malalamiko yanayolingana. Kwa hiyo, unaweza ukaandika wakaweka sahihi zao na ikawa imewasilishwa na Mbunge yeyote isipokuwa yule anayehusika na hicho kitu. Kwa hiyo, ukileta hapa unasoma na sahihi zao, lazima waoneshe hiki kifungu kinaeleza moja kwa moja na kinachukuliwa nafasi yake ni ya mapema sana asubuhi. Sahihi zisizopungua 10, kwa hiyo, hiyo ndiyo sasa nashawishika. Maana kama watu wana hoja fulani, hiki kifungu kinaanza kutumika.

Halafu Mheshimiwa Alhaj Missanga, alikuwa na maelezo pale niliomba atumie kifungu cha 50. Kifungu cha 50 kinakupa nafasi ya kuandika maelezo yako vizuri na yakasoma vizuri yakaingia kwenye Hansard. Kwa sababu ukitumia kifungu cha utaratibu kulalamika, kazi ya kifungu kile siyo kulalamika ni kwamba, tumekosea utaratibu. Aidha, Mbunge amekosea au Kiti kimekosea utaratibu, ndio unasema kuhusu utaratibu. Kama ni malalamiko niliyosikia, ulianza kuyaeleza kifungu cha 50 kinatumika. Kwa hiyo, ningeomba sana ungetumia kifungu hicho cha 50.

Baada ya kusema hayo, Waheshimiwa Wabunge kama tulivyokubaliana, kesho ni Jumamosi lakini tutaanza saa 3.00 na Wizara ya Nishati na Madini, ambayo itaendelea saa 3.00 mpaka 7.00 na saa 9.00 mpaka saa 11.00, halafu tutaahirisha mpaka Jumatatu tunaendelea na Wizara hii.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hivyo, naomba niwashukuru sana kwa kazi kubwa mliyoifanya katika muda wa siku mbili, kujaribu kuboresha Wizara hii ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi. Kama alivyosema Waziri, tunategemea maswali mengine mtajibiwa kwa maandishi, kwa sababu kweli kabisa haikuwezekana kujibu yote hapa, maswali zaidi ya 200 na maana yake, kama wasingejirudia wengine basi kila Mbunge hapa amechangia. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri, timiza ahadi yako ya kuwajibu kwa maandishi.

Baada ya kusema hivyo, naomba kuahirisha Kikao cha Bunge mpaka kesho saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 2.02 usiku Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Jumamosi, Tarehe 25 Julai, 2009 Saa Tatu Asubuhi)*